

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 23 Mei, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Tukae, Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI: Hati za Kuwasilisha mezani.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MHE. KHALIFA SALUM SOLEIMAN (K.n.y. MHE. ATASHASTA J. NDITIYE - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n. y. MHE. ESTHER N. MATIKO - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MWENYEKITI: Ahsante, Katibu!

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mgimwa, kwa niaba yake Mheshimiwa Kabati.

Na. 254

**Kupandisha Hadhi Barabara Inayounganisha Wilaya
ya Mufindi na Wilaya ya Kilombero**

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MHE. MAHMOUD H.
MGIMWA) aliuliza:-**

Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alipokuwa Waziri wa Miundombinu aliahidi kupandisha hadhi barabara ya kutoka Mtiri – Ifwagi – Mdaburo, Ihanu, Isipi – Mpangatazara – Mpalla Mlimba ambayo inaunganisha Wilaya ya Mufindi na Wilaya ya Kilombero pia Mkoo wa Iringa na Morogoro.

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi barabara hiyo muhimu kwa uchumi wa Wilaya ya Mufindi na Taifa kwa ujumla ambayo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi imeshindwa kuihudumia wakati wote?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mtili – Ifwagi – Mdaburo, Ihanu, Isipi – Mpangatazara – Mlimba ni barabara ya Wilaya inayohudumiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaifanya kazi ahadi hiyo ya Serikali ya kuipandisha hadhi barabara hii na barabara nyingine nchini kwa kuzingatia vigezo viliivyoainishwa kwenye Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007 na Kanuni za Menejimenti ya Barabara za mwaka 2009. Baada ya taratibu za kisheria kukamilika, Wizara yangu itamjulisha Mbunge pamoja na kutangaza barabara zilizopandishwa hadhi kwenye Gazeti la Serikali.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali tu madogo ya nyongeza. Kwa kuwa tumekuwa tukikaa katika vikao vya Bodi za Barabara mara nyingi sana hasa katika Mkoa wetu wa Iringa, barabara nyingi sana za Halmashauri zetu tunakuwa tukipeleka lakini hazipandishwi daraja. Je, ni vigezo gani sasa vinatumika maana utakuta sehemu nyingine barabara zinapandishwa lakini sehemu nyingine barabara nyingi hazipandishwi madaraja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza pesa kwenye Halmashauri kwa sababu Halmashauri nyingi barabara zake ni mbovu sana ili Halmashauri hizi ziweze kutengeneza barabara zake kwa kiwango? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vya kupandisha hadhi barabara vimeainishwa katika Sheria ya Barabara pamoja na Kanuni zake kama ambavyo nilisema katika jibu langu la swali la msingi. Vigezo hivyo havijabadilika na kama tutataka kubadilisha tutakuja Bungeni kuvibadilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza fedha; fedha nazo tumekubaliana kwamba Mfuko wa Barabara unagawa asilimia thelathini zinaenda kwenye Halmashauri na asilimia 70 zinaenda kuhudumia barabara za *trunk road* za mikoa. Sasa kama tunadhani kwamba *formular* hii kwa sasa labda haitufai bado ni suala la kuamua sisi Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge hili Tukufu ili tuweze kubadilisha zile sheria ambazo tulikubaliana wenyewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa wa Ushetu, jiandae Mheshimiwa Mbatia.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona ili nami niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa hitaji la Mufindi Kaskazini linafanana na Ushetu na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliahidi kupandisha hadhi barabara hii inayounganisha mikoa mitatu; Mkoa wa Geita, Shinyanga na Tabora kwa kuititia maeneo ya Mbogwe, Mwabomba, Nyankende, Ubagwe, Uloa hadi Kaliua. Je, Serikali itaipandisha hadhi lini barabara hii? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizo ni barabara tatu tofauti lakini zinazoungana na kwa hiyo nadhani tufuate tu utaratibu. Kwa hapa itabidi mikoa yote mitatu kwa vipande vyake ifuate taratibu za kuomba kupandisha hadhi hizo barabara. Kama tayari zimefuata taratibu hizo basi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba

maombi yake yatashughulikiwa kama ambavyo tumeongelea kwa barabara ambayo inaanzia Mtili – Ifwagi – Mdaburo na kuendelea. Utaratibu huo tutaufuata na maombi hayo tutayapitia kwa pamoja na zile zitakazotangazwa tutakuja kuwajulisha rasmi baada ya kutokea kwenye Gazeti la Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa swali la msingi linaulizia ahadi ya Serikali na Mheshimiwa Dkt. Magufuli alivyokuwa Waziri wa Ujenzi aliahidi kukamilisha barabara ya Kawawa – Nduoni – Bakula – Marangu Mtoni ambayo ni barabara muhimu sana kwa ajili ya utalii, inajulikana kama utalii *road*. Alipokuwa anafanya kampeni wakati wa uchaguzi aliahidi pia kwamba itakamilika na imeshajengwa nusu tu kwa lami. Sasa ni lini Serikali itakamilisha barabara hii kwa maendeleo ya utalii na Serikali iweze kupata mapato. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ni lini, anataka kujua.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri kivuli wa Wizara hii nadhani anafahamu na tumejadili, ingawa katika kipindi kifupi kidogo hakuwepo lakini nadhani anafahamu kwamba tumekuwa tukijadili utekelezaji wa ujenzi wa barabara mbalimbali na tunesema kwamba kwanza tuzikazanie zile ambazo zina madeni ili tuondokane na madeni na baada ya hapo tutauendelea na hizi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hizi zingine kipaumbele cha uhamasishaji wa utalii nacho tulikiweka. Kwa hiyo, nimshukuru alitusaidia kuweka hiki kipaumbele na hivyo mara tutakapomaliza barabara hizi ambazo zina mikataba ya muda mrefu zitafuata hizi barabara zinazohamasisha utalii na vile vile zinazohamasisha viwanda.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami niulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa tatizo ambalo lipopo kule Mufindi linafanana kabisa na kule Kilolo; barabara nyingi za Kilolo zimekuwa zikiahidiwa na hasa na Mheshimiwa Waziri. Sasa je, ni hatua gani ambazo inapaswa tuchukue endapo Mheshimiwa Waziri ameahidi kwa upande wa Serikali lakini utekelezaji haujafanyika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ni dhamira, kwa hiyo tunapotoa ahadi tunaonesha dhamira ya kutaka kutekeleza hicho kitu. Hatua inayofuata baada ya kuwa na hiyo dhamira ni kutafuta fedha na mara fedha zitakapopatikana hii ahadi yetu tutaitekeleza.

MWENYEKITI: Ahsante, umejibu vizuri. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Malocha.

Na. 255

Ujenzi wa Barabara ya Kibaoni – Kasanga Hadi Mlowo - Songwe

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

Barabara ya kutoka Kibaoni – Kasansa – Muze – Illemba – Kilyamatundu – Kamsamba hadi Mlowo Mkoani Songwe inaunganisha Mikoa mitatu ya Katavi, Rukwa na Songwe; wananchi wa mikoa hiyo wamekuwa na maombi ya muda mrefu kutaka barabara hiyo itengenezwa kwa kiwango cha lami ili kuboresha maisha na kukuza uchumi wao na Taifa kwa ujumla:-

Je, ni lini barabara hiyo itatengenezwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kibaoni – Kasansa ambayo ni kilometra 60.57 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania Mkoa wa Katavi. Barabara ya Kasansa – Kilyamatundu ambayo ina urefu wa kilomita 178.48 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania Mkoa wa Rukwa; na barabara ya Kamsamba – Mlowo ambayo ina urefu wa kilomita 130 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni kiungo sana kati ya mikoa hii mitatu ya Katavi, Rukwa na Songwe kwani inapita katika Bonde la Ziwa Rukwa ambalo ni maarufu sana kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Hali ya barabara hii ni nzuri kwa wastani ila inapitika kwa shida wakati wa masika katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kufahamu umuhimu huo itaanza ujenzi wa Daraja la Momba ambalo ni kiungo muhimu katika barabara hiyo na katika mwaka wa fedha 2016/2017 ndiyo tuaanza ujenzi huo wa barabara ya Momba. Kwa sasa Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) upo katika hatua za mwisho za kupata mkandarasi wa kujenga daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga sh. 2,935,000,000 kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuanza ujenzi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018 zimetengwa sh. 3,000,000,000 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja la Momba kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kazi za kuifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara hiyo uanze na hatimaye ujenzi kwa kiwango cha lami ufanyike.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Malocha, ajiandae Mheshimiwa Oran na Mheshimiwa Mgumba.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Barabara hii nimekuwa nikiulizia mara kwa mara na hii ni kutokana na umuhimu wake. Katika llani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 ukurasa wa 62 inaeleza kuwa itafanyiwa upembuzi yakinifu na hivi sasa ni miaka miwili sioni dalili ya kutenga pesa kwa ajili ya kufanya usanifu katika barabara hiyo. Je, ni lini sasa Serikali itatenga pesa kwa kuanza kazi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Mawaziri wote wawili ni wapya, yawezekana hawajatambua vyema umuhimu wa barabara hii. Naomba Mheshimiwa Waziri afanye ziara ya kutembelea barabara hii toka Mlowo hadi Kibaoni ili ajionee fursa zilizopo katika barabara hiyo. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, Wabunge wako wengi kwenye suala hili.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu sana umuhimu wa barabara hii na pengine hukupata fursa ya kufahamu Waziri wangu alishapita katika sehemu ya kipande cha hiyo barabara; nami nilikusudia kupita lakini kwa bahati mbaya kulikuwa na dharura. Nimhakikishie sasa hivi baada ya Bunge nitapita katika barabara hiyo na nitaanzia Tunduma. Kwanza kuanzia Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe kuanzia Vwawa, Tunduma na nitafuata hii barabara mpaka inakoishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuahidi nitafuata hiyo na tumempa *commitment* na fedha

zimetengwa, tunaanza na ujenzi wa Daraja la Mombasa na mara tutakapomaliza Daraja la Mombasa tutatenga fedha ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kama ambavyo nilijibu katika swali la msingi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Oran.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kama ilivyo kwa Jimbo la Kwela, kuna barabara mbili ambazo ziliahidhiwa na Mheshimiwa Rais; Barabara ya Mbalizi kwenda Makongorosi ambayo inaunganisha Mbeya na Mkoa mpya wa Songwe. Pia kuna barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete mpaka Njombe ambayo vile vile inaunganisha Mikoa ya Mbeya na Njombe ziliahidhiwa na Rais kwamba zitajengwa kwa kiwango cha lami. Je, ni lini hizi barabara zitajengwa kwa kiwango cha lami pamoja na kulipa fidia wale wote ambao ni waathirika. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba serikali imeshaanza kuchukua hatua za dhati kabisa za kujenga barabara ya kutoka Isyonje – Makete na hiyo barabara yote tumeshaanza hatua na kwamba wakandarasi wameshatafutwa na nadhani anafahamu Mheshimiwa Mbunge na hasa nikijua amemuulizia vile vile Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Miundombinu ambaye naye yupo katika barabara hiyo. Nimhakikishie Serikali itatekeleza kile ambacho imekusudia na imeanza kukitekeleza.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mgumba, Mheshimiwa Mwakasaka na Mheshimiwa Kuchauka wajiandae.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa matatizo yanayowakabili watu wa

Kwera yanafanana kabisa na matatizo yanayotukabili watu wa Morogoro Kusini Mashariki na Morogoro Vijijiini kwa ujumla, kuna Barabara ya Bingwa – Mkuyuni – Kisaki mpaka kuelekea Rufiji kule Mloka kuelekea Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara na pia kuelekea katika Mbura ya Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii iliahidiwa kuwekwa kiwango cha lami tangu Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Waziri wa Ujenzi aliyekuwa katika Serikali ya Awamu ya Nne ambaye sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli; na kwa kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umeshamalizika, je, Mheshimiwa Waziri, ni lini barabara hii itaanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami ili kuinua hali ya kiuchumi ya wananchi hawa? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba hii barabara baada ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, anafahamu kwamba tumeanza kujenga. Hata hivyo, nakubaliana naye kwamba kipande ambacho tumeanza kujenga mpaka sasa ni kifupi. Nimhakikishie, tutaendelea kuongeza kasi ili hatimaye barabara hii ifike Kisaki kama ilivyokusudiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakasaka, wajiandae Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa Boniphace na Mheshimiwa Silinde.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Matatizo yaliyopo Kwera yako sawasawa kabisa na matatizo ambayo yapo kwenye Manispaa ya Tabora kwenye barabara ile ya Mambali ambayo inapita Misha, Kata ya Kabilia, Kata ya Ikomwa mpaka kutokea Bukene. Barabara hii kwa kiwango kikubwa eneo kubwa lipo eneo la halmashauri na haijapandishwa daraja pamoja na maombi

ya muda mrefu. Hata hivyo, kwa kuwa Halmashauri ya Tabora uwezo wa kuitengeneza barabara hii kwa lami unaonekana haupo kabisa, Serikali ina mpango gani kuhakikisha barabara hii inawekwa kiwango cha lami ili iweze kuwa endelevu katika uchumi wa Mkoa wa Tabora? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwakasaka ni mjumbe wa Kamati yangu ya Miundombinu. Tumeliongea sana hili katika Kamati na naomba tu nirudie kumhakikishia, kama ambavyo tulikuwa tumeongea katika Kamati, kwamba Serikali muda si mrefu itakamilisha kupitia maombi yote ya barabara ambazo zimeombwa kupandishwa hadhi na matokeo ya maombi hayo yatatangazwa kwenye Gazeti la Serikali hivi karibuni.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka, wajiandae Mheshimiwa Boniphace na Mheshimiwa Silinde.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Nimekuwa nikisimama hapa mara nyingi naongelea Barabara ya Nangurukuru – Liwale na Barabara ya Nachingwea – Liwale. Majibu ninayoyapata ni kwamba barabara hizi zitajengwa katika kipindi hiki cha miaka mitano, lakini barabara hizo sasa hivi hazipitikia kutokana na mvua za masika zilizokatika sasa hivi. Je, nini *commitment* ya Serikali kwa kuwaokoa hawa Wanaliwale ili waweze kupata barabara inayopitika masika na kiangazi? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kuchauka ni Mjumbe wa Kamati yangu ya Miundombinu na kwa kweli michango yake tunaithamini sana katika Makati hiyo; na amekuwa akiongelea mara nyingi barabara hizi zote

pamoja na ile ya kwenda Nangurukuru. Nimhakikishie Mheshimiwa Kuchauka, yale ambayo tumekuwa tukiyajadili katika Kamati ya Miundombinu, Serikali ina dhamira ya dhati ya kuyatekeleza. Hata hivyo, nimwombe, wala sio dhambi, pitia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ataona nini Serikali iliahidi kwa ajili ya barabara hizi na nimhakikishie tutatekeleza kile ambacho tumeahidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Boniphace na Mheshimiwa Silinde ajiandae.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kujua, kuna barabara ya Nyamswa – Bunda ambayo mwezi wa 12 mwaka jana alifika Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Waziri na kuitembelea barabara hii na kuahidi kwamba ikifika Februari mwaka huu mkandarasi atakuwa *s/te*. Kwa bajeti inayoendelea sasa hivi, hiyo barabara ilitengewa billioni nane. Sasa napenda kujua; ni lini mkandarasi atakuwa *s/te* kwa ahadi ya Waziri, kwa maana ya kwamba hii barabara ni ya muda mrefu kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi toka mwaka 2000?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara anazoziongelea ni kweli zipo katika mpango na fedha zimetengwa na tenda zimetangazwa. Nimwombe tu Mheshimiwa Getere kama ambavyo nimekuwa nikimwomba ofisini, maana amefuatilia sana ofisini, naomba tu yale masuala ya kutaka kupigana ayapunguze, lakini nimhakikishie kwamba kile ambacho nilimuahidi ndani ya ofisi tukiwa pamoja na Katibu Mkuu, tutayatekeleza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silinde, subiri hapo hapo Mheshimiwa Waziri.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nauliza kwa kifupi tu. Barabara hii aliyouliza Mheshimiwa Malocha, mimi na yeze tumekuwa tukiiuliza kila

mwaka na huu ni mwaka wetu wa saba hapa Bungeni na ni *commitment* ya Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Kikwete aliyepla na Rais wa sasa aliyepla madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali imekuwa ikitenga fedha kwenye barabara hii, lakini zimekuwa hazitoki na mwaka huu tumeona pamoja na lile daraja. Sasa nataka *commitment* yake, endapo na mwaka huu stori zitakuwa zilezile za miaka saba iliyopita, ni hatua gani atachukua kama Waziri ili hii barabara ikamilike?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Silinde amekuwa akiuliza mara nydingi na jibu letu muda wote limekuwa hilo hilo, kwamba tutajenga daraja hilo, lakini ameona mwaka huu tumetenga fedha na mwaka ujao na ameshiriki kuzipitisha, nikupongeze pamoja na Wabunge wote. Namuahidi kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano daraja hili litajengwa, lisipojengwa kwa kweli nitamruhusu anikate kichwa. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa barabara zimetuchukulia muda mwangi. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Gulamali kwa niaba Mheshimiwa Munde

Na. 256

Uanzishwaji wa VETA Katika Kila Wilaya Nchini

MHE. MUNDE T. ABDALLAH (K.n.y. MHE. SEIF K. S. GULAMALI) aliuliza:-

Serikali ina mpango wa kujenga vyuo vyaa ufundi katika kila wilaya nchini:-

(a) Je, shirika lisilo la Kiserikali linaweza kujenga chuo hicho katika Kata ya Chuma, Chakola Makao Makuu ya Tarafa ya Manonga na kuikabidhi Serikali?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga chuo hicho ili kiweze kutoa msaada katika Wilaya za Igunga na Nzega?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika Lisilo la Kiserikali linaweza kujenga chuo cha ufundi stadi katika Kata ya Chuma, Chakola, Makao Makuu ya Tarafa ya Manonga na kuikabidhi Serikali. Ili Serikali iweze kupokea chuo hicho, ni vema kabla ya kuanza ujenzi mawasiliano yafanyike katи ya taasisi hiyo kuititia Halmashauri ya Wilaya ya Igunga na Mamlaka ya Ufundı Stadi (*VETA*) ili kwa pamoja masuala yote ya kisheria yaweze kuzingatiwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inashauri kwamba wakati juhudhi mbalimbali za kutafuta fedha na wafadhili wa kujenga vyuo hivyo vya wilaya zinaendelea, wananchi wa Wilaya ya Igunga waendelee kutumia vyuo vya ufundi stadi vilivypo Mkoani Tabora ambavyo ni Chuocha *VETA* Tabora kilichopo Mjini Tabora na Ulyankulu kilichopo Wilayani Kaliua, pamoja na Chuocha Maendeleo ya Wananchi (*FDC*) Nzega na vyuo vingine vilivjosajiliwa na Mamlaka ya Ufundı Stadi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Munde, wajiandae Mheshimiwa Mwalongo na Mheshimiwa Shonza.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo hayaridhishi kabisa, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; Mheshimiwa Waziri haoni Serikali kushindwa kumalizia majengo haya na kutoa majibu haya ni kuwavunja moyo

wafadhili tuliowabembeleza na kuwaomba watujengee majengo haya? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; wafadhili kujenga majengo na kuyamalizia au kutoyamalizia ni jambo la kawaida kabisa kwenye nchi yetu; na kwa kuwa Serikali imesema kwamba haiukufuata sheria wakati majengo yale yamesimamiwa na *Engineer* wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga. Je, Mheshimiwa Waziri haoni anawanyima haki wananchi wa Igunga kwa kukosa kuwa na *VETA* yao ambayo wameihangaikia kutafuta wafadhili, bado tu kumalizia lakini wanasema kwamba sheria haikufuatwa wakati *Engineer* wa halmashauri ndiye aliyesimamia majengo haya? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nadhani hakunisikia vizuri katika jibu langu. Nimesema kwamba shirika linaweza likajenga chuo na kuikabidhi Serikali, lakini kwa sababu katika swalii la msingi haikuzungumzwa kwamba chuo hicho kimeshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosisitiza ni kwamba, kwa sababu mwisho wa yote hicho chuo itabidi kiendeshwe kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo, ndiyo maana tunasisitiza kabla ya wadau wetu wa maendeleo kuanza kufanya shughuli ya ujenzi, ni vema kuwasiliana na taasisi husika ili kile wanachokifanya kiendane na viwango na kiweze kuwa na tija kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, sijasema kwamba wao wamejenga bila kufuata sheria. Katika jibu langu la msingi nilisema kwamba ni vema kabla ya kujenga yawe yanafanyika mawasialiano kuititia halmashauri na *VETA* ili kwa pamoja kuweza kuzingatia masuala ya kisheria. Kwa misingi hiyo, ninachosema ni kwamba, kwanza hicho chuo hatujakitembelea na hatuwezi kukiamuru kama ilivyo, lakini niseme tu kwamba nazidi kuwaomba wadau wa maendeleo, wanapofanya shughuli yoyote ya kimaendeleo

kuhusiana na Wizara fulani, ni vema kushirikisha Wizara husika ili kile kinachofanyika kiwe na tija ili fedha zao zisipotee bila utaratibu ambao pengine usingkuwa wa lazima.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwalongo, wajiandae Mheshimiwa Shonza na Mheshimiwa Nassari.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa hitaji la vyuo vya ufundu kwenye nchi yetu liko juu sana na uwezo wa Serikali unaonekana kwamba ni mdogo kuwezesha kujenga vyuo vya *VETA* nchi nzima kwa wakati mmoja. Je, Serikali iko tayari kutumia fursa tulizonazo kwenye shule zetu za sekondari kujenga karakana ya fani angalau moja kila shule ya sekondari ili kuwezesha vijana wengi kupata elimu ya ufundu na kurejesha elimu hiyo katika shule za sekondari?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kuititia Sera yetu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ya Mwaka 2014, Wizara inaanjalishwa kwa umakini uwezekano wa kuongeza nafasi za udahili kwa wanafunzi wa vyuo vya ufundu ili kuwezesha wanafunzi wengi zaidi kupata fursa hizo. Kisera ni kwamba tungehitaji kuona mwanafunzi akisoma moja kwa moja mpaka kidato cha nne na kwa misingi hiyo kuna mambo mbalimbali ambayo yanaangaliwa ili kwa pamoja tuone kwamba ni jinsi gani tutaweza kuangalia mafunzo ya kawaida na vilevile mafunzo ya ufundu ili kuwezesha fursa hizo kupatikana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shonza, ajiandae Mheshimiwa Nassari.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo liliopo Manonga linafanana kwa ukaribu kabisa na tatizo liliopo katika Mkoa wa Songwe na kwa kuzingatia kwamba Mkoa wa Songwe ni mpya, lakini mpaka sasa Wilaya za Mbozi, Ileje, Mombasa pamoja na Songwe hazina vyuo vya ufundu. Je, ni lini Serikali

itajenga vyuo vya ufundi katika wilaya hizo ili kuwasaidia vijana wa Mkoa wa Songwe kuweza kuondokana na tatizo la ukosefu wa ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninavyofahamu ni kwamba Wilaya ya Songwe ni miongoni mwa maeneo ambayo yamo kwenye mpango, nafahamu kuna kiwanja kilishatengwa eneo la Makutano, kwa hiyo, muda ukifika tutafanya hiyo shughuli ya ujenzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nassari.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami kwa kifupi tu ni kwamba, mwezi wa kwanza mwaka huu nilikuwa nchini Uswisi na kuna wadau nilizungumza nao na wakaonesha nia kwamba wako tayari kutujengea chuo cha ufundi pale kwenye Jimbo letu la Arumeru. Swali langu kwa Wizara; naomba *commitment* ya Serikali, kwamba wadau watakapokuja na watakapokuwa tayari kutujengea ninyi mtakuwa tayari kutusaidia utaalam na vifaa pale ambapo chuo kitakamilika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Nassari na naomba niunganishe na maeneo yote ambayo wamejenga Vyuo vya VETA kwa kutumia taasisi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, katika kujenga vyuo vya ufundi kuna njia mbili za kuviendesha; kuna njia ya kwanza, watu wanajenga wenyewe na wanaendesha wenyewe katika sura zote za vifaa na Walimu. Njia ya pili, kujenga na kuikabidhi Serikali ili iweze kuviendesha. Sasa tatizo

ninaloliona ni kwamba halmashauri zinashirikiana na wadau kujenga hivyo vyuo lakini baadaye wanakuwa hawawezi kuflikia muafaka katika kupeleka Walimu pamoja na vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe tu toka mwanzo, ni vema ushirikiano uanzie toka mwanzo ili tujue wadau watakoju ka kusaidia ujenzi wa chuo hicho wajibu wao utakuwa ni nini na upande wa Serikali wajibu wetu utakuwa ni nini ili suala hilo litekelezwe kwa ukamilifu kama inavyostahili.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamad Salim Maalim.

Na. 257

Stahiki za Uhamisho kwa Askari Polisi

MHE. HAMAD SALIM MAALIM aliuliza:-

Miongoni mwa stahiki za askari polisi anapohamishwa kutoka mkoa mmoja kwenda mwengine ni nauli ya askari huyo na wategemezi wake pamoja na fedha za kusafirishia mizigo:-

Iwapo mwajiri atashindwa kumlipa askari huyo stahiki zake zote hizo, je, askari huyo atapaswa kuhama kwa gharama zifi na kuripoti mkoa wake mpya aliopangisha?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI aliujibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi hutoa uhamisho kulingana na mahitaji pale Inspekte Jenerali wa Polisi anapoona kuna umuhimu wa kuongeza nguvu eneo fulani ambalo ni tete kwa wakati huo. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 59(5)(a) ya Kanuni za Jeshi la Polisi (*PGO*). Askari

anayehamishwa atalipwa mafao yake kama ilivyoelekezwa katika Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, Toleo Na. 259 iwapo hakuhamishwa kwa makosa ya kinidhamu. Aidha, askari anayeomba kuhama eneo moja kwenda eneo lingine kwa sababu zake binafsi hatalipwa mafao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelezo hayo, inapotokea dharura ya askari kuhitajika kwenda kutoa huduma eneo lingine, askari husika atatekeleza amri ya uhamisho haraka wakati stahili zake zinafanyiwa kazi kwa mujibu wa taratibu za fedha. Kwa taratibu za Kijeshi, askari hawezi kusubiri malipo katika mazingira ambayo anakwenda kuokoa maisha ama kulinda maslahi ya Taifa katika eneo husika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hamad.

MHE. HAMAD SALIM MAALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, maswali ya barabara yametuchukulia muda mwingu sana. Mheshimiwa Hamad.

MHE. HAMAD SALIM MAALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa askari wengi hufanya kazi mbali na walikozaliwa na hulazimika kuwa pamoja na familia zao, je, askari hawa wanapohamishwa na wanachotegemea ni mshahara tu, pamoja na familia zao na mizigo yao, watahamaje kufika maeneo waliyohamishiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa kila mwaka Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani hupitishwa ikiwa na stahiki zote za askari polisi na sasa hivi askari wengi wamehamishwa, zaidi ya miaka mitatu hawajapata stahiki zao, ni lini Jeshi la Polisi litawalipa askari hao wanaodai stahiki zao za uhamisho?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyeekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kuwa na *concern* na maisha ya askari wetu. Hata hivyo, niseme tu kwamba askari anapohama kuna taratibu za Kijeshi pale alipokuwa anakaa ama pale ilipokuwa familia ipo huruhusiwa kukaa mpaka pale atakapokuwa amepewa fedha za kuhama na kuweza kuhamisha vifaa vyake.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kuhusu uwepo wa madai; katika mwaka wa fedha huu uliokwisha tumetumia zaidi ya bilioni tano kulipa madeni yaliyokuwa ya askari polisi wetu na tumetumia zaidi ya bilioni saba kulipa zilizokuwa stahili za askari wetu wa Magereza.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kinachotokea na kwa nini anaendelea kuona bado wapo wanaodai, ni kwa sababu uhitaji wa kuhama wa askari ni mkubwa kufuatana na mazingira na maeneo ambako anaweza akahitajika tofauti na watumishi wengine wa umma.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, kwa niaba yake Mheshimiwa Oran.

Na. 258

Mapigano Bainya Wakulima na Wafugaji

MHE. ORAN M. NJEZA (K.n.y. MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE) aliuliza:-

Hivi karibuni kumetokea mapigano baina ya wakulima na wafugaji ambayo yamesababisha baadhi ya Watanzania kupoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa maisha:-

Je, Serikali imejipangaje kupambana na janga hilo?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na migogoro kati ya wakulima na wafugaji katika maeneo kadhaa ndani ya nchi yetu ambayo yamesababisha Watanzania kupoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na hali hiyo Serikali kupitia Jeshi la Polisi inaendelea kushauriana na Mamlaka zinasosimamia matumizi bora ya ardhi, kutenga maeneo yatakayotumiwa na wakulima na wafugaji ili kuepusha migogoro na kutoa elimu kwa wakulima na wafugaji juu ya mazingira bora ya matumizi ya ardhi. Aidha, Jeshi la Polisi hufanya doria na misako na kukamata wale wanaovunja Sheria punde panapokuwepo na mwingiliano wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo yanayosababisha migogoro.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Oran Njeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa ajili ya matatizo ya migogoro ya wafugaji na wakulima, maeneo mengi yanahitaji sasa hivi kuwe na vituo vidogo vya Polisi. Je, Serikali au Wizara inatupa *commitment* gani kuwa kutakuwa na vituo vya Polisi katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa wananchi wamekuwa wakijitolea kujenga vituo vya Polisi kama ilivyokuwa kwa kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mbeya ambao wamejenga kwa asilimia karibu zaidi ya 50. Je, Serikali inawaahidi nini wale wananchi wa Mbalizi kuwaunga mkono kuwalamizia kile kituo chao cha Polisi? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpe pole Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete kwa kupatwa na msiba na ndiyo maana hajaweza kuwepo kuuliza swali. Mungu ampe moyo wa ustahimilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la nyongeza alilouliza Mheshimiwa Oran; moja kituo cha Mbeya ambacho wameshafanya kazi kubwa sana nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amefanya hamasa kubwa sana na najivunia kwamba nilikwenda kumuunga mkono wakati wa kampeni. Kwa kuwa amefanya kazi kubwa sana na sisi kama Wizara tuna bajeti ambayo tumetenga kwa ajili ya umaliziaji wa majengo ambayo yameshafikia hatua kubwa. Hivyo, tutafanya ziara, tutajionea na tutaweka wataalam ili waweze kukadiria na kwenda kwenye utekelezaji wa umaliziaji ili nguvu ya wananchi isiweze kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa vituo karibu na maeneo ambayo yanakuwa na migogoro ya mara kwa mara, Serikali inaendelea kufanya utaratibu wa kuweza kuwepo vituo hivyo lakini pale ambapo vituo hivyo havipo tutaendelea kufanya doria ili kuweza kuhakikisha kwamba tunawahakikishia wananchi usalama wao punde panapokuwepo na migongano ya aina hiyo hata kama bado hatujaweka vituo vya Polisi.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mkundi.

Na. 259

Kujenga Mazingira ya Vivutio vya Utalii - Ukerewe

MHE. JOSEPH M. MKUNDI alijibu:-

Kisiwa cha Ukerewe kina vivutio vingi vya utalii vinavyoweza kuiingizia nchi yetu pesa nyingi za kigeni

vikiwemo mapango ya Handebezyo, Makazi ya Mtemi Rukumbuza, Jiwe linalocheza la Nyaburebeka huko Ukara na kadhalika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kuimarisha na kujenga mazingira na kuvitumia vivutio hivyo ili kuongeza pato la Taifa na wananchi wa Ukerewe?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sura ya Nne aya ya 4.2.7 ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021) unasisitiza pamoja na mambo mengine upanuzi wa wigo wa vivutio vya utalii na utalii utokanao na vivutio vya urithi wa utamaduni (*The heritage tourism*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kuzihusisha Halmashauri husika inakamilisha orodha ya vivutio vyote vya utalii ikiwa ni pamoja na vivutio vya malikale nchini ili kuweka utaratibu wa kuvisajili, kuviboresha na hatimaye kuvitangaza na kuviuza kwa watalii wa ndani na wa nje. Zoezi hili linatengemea kukamilika mwaka wa 2017/2018. Vivutio vya mapango ya Handebezyo, Makazi ya Mtemi Rukumbuza na Jiwe linalocheza la Nyaburebeka vilivyoko katika kisiwa cha Ukara katika Halmashauri ya Ukerewe ni miongoni mwa vivutio hivyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mkundi, ajiandae Mheshimiwa Lucy Owenya.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na majibu hayo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Jumapili tulikuwa na semina inayohusu mambo ya utalii, na

kwenye jarida hili kulikuwa na taarifa ambazo zilikuwa na upungufu juu ya vivutio hivi. Sasa Je, Waziri yuko tayari kutembelea visiwa vya Ukerewe na kushuhudia vivutio hivi ili awe Balozi mzuri na mwenye taarifa zilizo sahihi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, suala la ukuzaji na uendelezaji wa vivutio hivi mbali na kuvitangaza inategemea zaidi ubora wa miundombinu ya kuvifika vivutio hivi; na kwa kuwa Halmashauri zetu hazina uwezo wa kutosha wa kuboresha miundombinu hii, sasa Serikali iko tayari kuboresha miundombinu ya kufikia vivutio hivi hasa Jiwe linalocheza la Nyaburebeka la Kisiwani Ukara? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niko tayari kabisa kutembelea vivutio hivyo pamoja na Mbunge, Mheshimiwa Mkundi bila wasiwasi wowote na tutapanga safari hiyo mwezi Agosti mwaka huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba vivutio vyote vya utalii vinakuwa vizuri zaidi kama vinafikika na raia na watalii wanaotaka kuvitembelea. Wakati tutakapotembelea tutafanya tathmini ya vivutio hivyo na kuona ni namna gani juhudii hizi zitakamilika ili vivutio hivyo vifikike.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Owenya, wajiandae Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Dkt. Sware.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Jimbo la Hai kuna kivutio cha Bwawa moja ambalo lina maji ya moto linaitwa Chemka. Wageni wamekuwa wakienda kule, lakini wanafika kwa kutumia kama vile njia za panya, lakini Serikali kama Wizara bado hawajakitambua kivutio kile na barabara ya kwenda kule ni mbaya sana. Swali langu, je, Serikali mpo tayari kwenda

kukitembelea kituo kile cha maji ya moto na kukifanya *official* ili Serikali nayo iweze kupata mapato? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu. Mnatazamana, nani sasa?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu anazungumzia juu ya kivutio ambacho kiko kwenye Wilaya ya Hai...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri swali lake uko tayari kwenda kutembelea ndiyo hilo tu, mjibu uko tayari yamekwisha tuendelee na wengine.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Tuko tayari kwenda kukagua lakini nilitaka kuweka nyongeza...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sware, wajiandae Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Kandege.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kilometra 180 tu kutoka hapa kuelekea Kondoa – Irangi kuna malikale nzuri, kuna michoro ya mapangoni na miundombinu ya barabara imeimarika. Sasa nataka kujua Wizara hii husika itatengeneza vipi yale mazingira ya kule ili kuimarisha utalii pamoja na mafunzo katika mapango ya michoro ya kale Kondoa – Irangi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi vivutio vyote vya utalii ambavyo vinaangukia kwenye eneo la *heritage tourism* vyote tumeefanya utaratibu wa kuviorodhesha halafu baadaye tunavisajili. Kuvisajili maana yake ni pamoja na kuangalia viwango vyake vya ubora na kuona kama kweli vinakidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa tumepokea taarifa hizo kutoka kwenye Wilaya mbalimbali, baadaye hatua inayofuata ni kuvitembelea na kuvihakiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bashungwa, jiandae Mheshimiwa Kandege.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza. Hata Wilaya ya Karagwe tuna vivutio vingi vya malikale likiwemo eneo ambalo Chief Rumanyika alikaa. Je, Wizara imeweka vivutio vya malikale hizi kwenye orodha ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kivutio kinachohusu makazi ya Chifu Rumanyika ni moja tu kati ya vivutio vinavyohusu Machifu wetu wote nchi nzima kila eneo na kila Wilaya. Kwa hiyo, mpango wa Serikali ni kama nilivyoeleza hapo awali kwamba ni kuviorodhesha, kuvisajili, kuvikagua na kuona ubora wake na hatimae kuviuza kwa kuangalia sifa zake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kandege.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swalii la moja. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameonesha utayari wa kutembelea vivutio mbalimbali na kimsingi hajakuwa na ziara hivi karibuni ya kutembelea Nyanda za Juu Kusini ili akajionee maporomoko ya pili Afrika ya Kalambo pamoja na Ngome ya *Bismark* iliyoko Kasanga. Je, katika mwezi huo Agosti aliojipanga atatembelea na Nyanda za Juu Kusini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ni lini kama uko tayari.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukanda wa Kusini ni eneo ambalo sasa hivi

kama Taifa tunaliangalia kuwa ni eneo la kupanua shughuli za utalii nchini kwa maana ya kufanya kwamba utalii sasa unakwenda kila eneo nchi nzima na si upande wa Kaskazini peke yake. Kwa hiyo, kwa ufupi jibu ni kwamba; kipindi hicho kitakapofika tutatembelea pia Ukanda wa Kusini ikiwa ni pamoja na maporomoko ya Kalambo.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, swali linauliza na Mheshimiwa Kapteni Mkuchika.

Na. 260

Mafunzo ya JKT Kwa Vijana

MHE. KAPT. GEORGE H. MKUCHIKA aliuliza:-

Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Mwaka 1964 (*The National Service Act. 1964*) imeweka ulazima wa Vijana Watanzania wanaomaliza kidato cha sita kuijunga na mafunzo ya Jeshi la kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria.

(a) Je, katika miaka mitatu iliyopita ni vijana wangapi waliomaliza kidato cha sita kila mwaka na kati yao wangapi walijiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa?

(b) Je, waliojiunga ni asilimia ngapi wa waliotakiwa kuijunga?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Newala Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa ya mwaka 1964 imeweka ulazima wa vijana wa Tanzania wanaomaliza kidato cha sita kuijunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria.

Hata hivyo, mwaka 1994 Serikali iliyasitisha kwa muda mafunzo hayo na kuyarejesha mwaka 2013 na yameendelea kutolewa hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za vijana waliohitimu kidato cha sita na kuhuduria mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014, vijana waliomaliza kidato cha sita ni 41,968, kati yao waliojiunga na mafunzo ya Jeshi la kujenga Taifa ni 31,692, ambayo ni sawa na asilimia 75.5.

Mwaka 2015, vijana waliomaliza kidato cha sita ni 40,753, kati yao waliojiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa ni 19,990, ambao ni sawa na asilimia 48.8.

Mwaka 2016, vijana waliomaliza kidato cha sita ni 63,623, kati yao waliojiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa ni 14,747, ambao ni sawa na asilimia 23.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizopo zinaonesha kupungua kwa idadi ya vijana wanaojiunga na mafunzo hayo muhimu ya Jeshi la Kujenga Taifa. Hali hii imesababishwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kugongana kwa tarehe za kuanza mafunzo ya vijana kwa mujibu wa Sheria na kufunguliwa kwa vyuo mbalimbali hapa nchini ambapo mihula ya mafunzo huanza.

Hali hii imewafanya vijana wengi walioteuliwa kuijunga na vyuo kukosa nafasi za kuijunga na mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria. Changamoto nydingine ni uhaba wa miundombinu, rasilimali watu na fedha. Hata hivyo Serikali inaendelea na juhudzi za kupata suluhi ya changamoto zilizopo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkuchika. Mheshimiwa Mkuchika!

MHE. KAPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasubiri ruhusa yako.

MWENYEKITI: Nilishakuita.

MHE. KAPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ambayo si mazuri sana kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. Hata hivyo, kabla sijauliza maswali yangu mawili ya nyongeza, nataka niwapongeze Waheshimiwa Wabunge vijana wa Bunge la 10 ambaao kwa hiari yao walijiunga na mafunzo ya Jeshi la kujenga Taifa, walionesha kwamba kuongoza ni kuonesha njia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Baba wa Taifa alituandalia akafanya JKT kama ndio jando, mahali pa kuwafunda, kuwaandaa vizuri vijana wa Tanzania kimaadili, kiuzalendo na kiulinzi; na kwa kuwa sasa inaonekana vijana wengi hawaendi tumeporomoka kutoka asilimia 75 mpaka mwaka huu 23. Je, kwa kutokuwapeleka hawa vijana JKT, Serikali haioni kwamba inachangia kuwaunda vijana ambaao hawana maadili, legelege, ambaao hawana uzalendo katika nchi yao? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa changamoto zilizoelezwa na Wizara nimezipitia zote ziko ndani ya uwezo wa Serikali. Je, Serikali inaweza kuliahidi Bunge hili kwamba itaunda kikosi maalum cha kuitipia changamoto hizi, kuziondoa na kuhakikisha kwamba vijana wote wanakwenda Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria na kwamba hata kama ikibidi kuomba pesa walete maombi hapa Bungeni; kwa sababu Watanzania tuna uzoefu wa kushughulikia matatizo mbalimbali kaa *UPE*; na kama mwaka wa jana tulivyopeleka watoto wote kutoka darasa la kwanza mpaka *form four* wamekwenda bila malipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba vijana ambao hawapati fursa ya kujunga na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kweli hawawezi kuwa sawa kimaadili na kiuzalendo kama wale ambao wamepitia Jeshi la Kujenga Taifa. Hata hivyo, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba Serikali ina nia na dhamira kubwa ya kuhakikisha kwamba vijana wote wanaomaliza kidato cha sita wanajiunga na Jeshi la Kujenga Taifa, lakini tunakabiliwa na changamoto kama nilivyozirodhesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mkuchika, kwamba wakati umefika wa kuunda kikosi kazi cha kupitia changamoto zote hizi au tuseme kufanya mikutano na wadau wote kwa sababu moja ya tatizo kubwa ni mihula ya masomo. Wale wanaanza Chuo Kikuu wanaanza mwezi Septemba jambo ambalo linasababisha tusiweze kuwachukua vijana hawa wote wengine wanakuwa wameshaanza masomo. Kwa maana hiyo ni kukaa pamoja kuangalia ni jinsi gani tunaweza tukafanya marekebisho ya mihula hii, aidha vyuo vikuu au muda ule wa kumaliza *form six* ili vijana wote waweze kupitia JKT angalau kwa miezi mitatua ambayo inatolewa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nydingine kubwa ni changamoto ya rasilimali fedha. Jambo hili limekuwa ni kikwazo kikubwa, tutaendelea kuomba bajeti mwaka hadi mwaka ili kuziondoa na wakati huo huo tunajipanga ili JKT liweze kujitegemea. Nadhani hiyo ndiyo njia nzuri zaidi ya kuhakikisha vijana wote wanapita huko.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lwakatare, ajiandae Mheshimiwa Bulembo.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu aliyojatoa Mheshimiwa Waziri, takwimu zinaonesha ukweli kwamba

changamoto alizozizungumza zinasababisha kupeleka vijana wachache ukilinganisha na idadi ya vijana wanaomaliza kidato cha sita. Nataka kujua, kutokana na ufinyu huo, ni vigezo gani hivi sasa wanavyovitumia katika kuteua vijana wa kwenda kwenye mafunzo haya na wale wasiokwenda watawafanyaje sasa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hakuna vigezo maalum vinavyotumika isipokuwa tunachofanya ni *random selection*. Kwa maana hiyo katika kila shule wanachaguliwa vijana wachache kwa utaratibu wa *random*. Kwa hiyo, wale wote ambaao wanachaguliwa ni wale waliopatikana kwa utaratibu huo; hakuna vigezo maalum kwa sababu wote wanastahili kuchukuliwa, lakini ni kwa sababu ya muda na rasilimali fedha ambazo nimezizingumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba kwa wale ambaao hawajapata fursa ya kwenda huko, kwa sasa hivi hakuna utaratibu wowote uliopangwa, ni matumaini yetu kwamba uwezo ukiongezekwa wa kuweza kuwachukua hata wale ambaao wamemaliza vyuo vikuu, basi tutafanya hivyo wakati ukifika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bulembo, wajiandae Mheshimiwa Mlata na Mheshimiwa Selasini.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Je, Serikali haioni umuhimu wa kugeuza Kambi za JKT kuwa vyuo vya VETA ili pamoja na mafunzo ya Kijeshi, vijana pia hasa wale wa kuitolea waweze kupata mafunzo ya ufundi? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa sasa, hususani kwa wale vijana

wanaoingia kwa kujitolea yana awamu mbili, kuna mafunzo ya Kijeshi ya miezi sita ya kwanza na baada ya hapo kuna mafunzo ya Stadi za Kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Jeshi la Kujenga Taifa linafanya utaratibu wa kupata usajili wa *VETA* ili waweze kutoa vyeti hivyo kwa wale wanaomaliza pale JKT. Kwa hiyo ni kwamba, Stadi za Kazi zinatolewa, zitaendelea kutolewa na usajili unatafutwa ili hatimaye vijana wanaomaliza pale siyo tu wawe wamemaliza JKT bali pia waweze kupata vyeti vya *VETA*. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlata, ajiandae Mheshimiwa Selasini.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba changamoto kubwa ni kutokana na ratiba za wanafunzi wanaomaliza *form six* kwenda Chuo Kikuu muda ni mdogo na wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne mpaka kuja kuingia cha tano waliofaulu ni miezi nane. Je, anaonaje kuleta sheria hapa ili tuje tubadilishe wawe wanaenda JKT wakati wanasubiri kwenda *form five*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati nawasilisha bajeti yangu, kwamba wazo hili liliuja ni wazo zuri, tulikubali kwamba totalichukua tukalifanyie kazi kwa sababu kuna wadau wengi wakiwemo Wizara ya Elimu, tupitie nao kwa pamoja tuone uwezekano wa jambo hili. Kwa maana hiyo baada ya mazungumzo na wadau tutaweza kulitolea uamuzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mimi ni muumini wa msemo unaosema kwamba mbwa mzee hafundishwi Sheria. Baadhi ya vijana

hatutaweza kuwafundisha uzalendo kwa kwenda tu JKT. Enzi za mwalimu kulikuwa na program za kwata mashulenii, tulikuwa tunafundishwa kwata kwa kutumia Bunduki za mbao. Pia kulikuwa na elimu ya kujitegemea ambapo vijana walikuwa wanafundishwa uzalishaji na stadi mbalimbali ambazo zinafundishwa sasa kwenye VETA. Je, Wizara iko tayari kushirikiana na Wizara ya Elimu, kwata ikarejeshwa mashulenii, vijana wakafundishwa ukakamavu kuanzia ngazi za chini na wakati huo huo elimu ya kujitegemea ikarejeshwa mashulenii kama zamani? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Mwambie siku hizi watu wote wanajifundisha IT.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni wazo zuri, wanafunzi kufundishwa mapema masuala ya kijeshi pamoja na elimu ya kujitegemea ni wazo zuri. Hata hivyo, kama nilivyosema tupo katika mchakato wa kuunda kikosi ambacho kitapitia changamoto zote; na kwa sababu kitajumuisha pia watu wa Wizara ya Elimu suala hili litazingatiwa ili tuone uwezekano wake.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis.

Na. 261

Uvuvi Haramu

MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS aliuliza

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuzuia uvuvi haramu nchini?

(b) Je, ni meli ngapi zilizokamatwa kwa sababu za uvuvi haramu kuanzia mwaka 2010 – 2015 ?

(c) Je, ni watu wangapi wametiwa hatiani na hukumu zao zikoje?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamisi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na wavuvi haramu, Wizara imeanzisha na kuimarisha vituo 25 vya doria kwenye maziwa makubwa, mwambao wa Bahari ya Hindi na mipaka ya nchi. Vituo hivyo viro katika maeneo ya Tanga, Dar es Salaam, Kigoma, Musoma, Kagera, Mwanza, Mtwara, Mafia, Kilwa, Horohoro, Kipili, Kasanga, Sota, Sirari, Kasumulo, Mbamba Bay, Tunduma, Kabanga, Kanyigo, Rusumo, Ikola, Geita, Buhingu, Namanga na Murusagamba. Kuwepo kwa vituo hivyo kumeongeza uwezo wa kukabiliana na uvuvi na biashara haramu kupitia operesheni mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi za Serikali, tatizo la uvuvi haramu na biashara ya magendo kwenye mialo, masoko na mipaka ya nchi bado ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia, imeanzisha Kikosi Kazi cha Kitaifa *Mult Agency Task Team* ambacho kinafanya kazi ya kudhibiti uhalifu wa mazingira ikiwemo kudhibiti uvuvi haramu hususan matumizi ya mabomu katika shughuli za uvuvi. Wajumbe wa Kikosi kazi hiki ni kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Baraza la Taifa la Mazingira. Wajumbe kutoka Taasisi nyingine wataongezeka kadri itakavyoonekana inafaa. Kikosi kazi hiki kipo chini ya uratibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani. Aidha, Wizara imeendelea kufanya maboresho ya Sera, Sheria

na Kanuni za uvuvi ili kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa kwenye maji ya ndani na ya Kitaifa (*Inner and territorial waters*) uvuvi unaofanyika ni wa kutumia mitumbwi, boti, mashua, jahazi na ngalawa na siyo meli. Kuanzia mwaka 2010 – 2015 jumla ya vyombo 2,795, injini za mitumbwi 118, magari 297 na pikipiki 33 vilikamatwa kwa sababu za uvuvi haramu na utoroshwaji haramu kwenye maji hayo. Aidha, katika Bahari Kuu kuanzia mwaka 2010 hadi 2015 hajjawahi kukamatwa meli ya uvuvi. Meli ya Uvvi *Tawariq1* ilikamatwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi tajwa jumla ya watuhumiwa 3,792 walikamatwa na kesi 243 zilifunguliwa mahakmani. Aldha, jumla ya shillingi 158,559,323 zilikusanya ikiwa ni faini kutokana na makosa mbalimbali na watuhumiwa 11 wamefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu, nawaomba Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe katika Halmashauri waendelee kutoa elimu kwa wavuvi kuhusu madhara ya uvuvi haramu na kuhimiza Halmashauri zao zidhibiti uvuvi haramu kwenye maeneo yao. Pia, jamii za wavuvi na wadau wote washirikishwe katika kusimamia rasilimali za uvuvi na matumizi endelevu kwa ajili ya kuwapatia wananchi ajira, chakula na uchumi wao na Taifa kwa ujumla. Ni njia hii Taifa linaweza kudhibiti uvuvi haramu hapa chini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fakharia.

MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake marefu lakini yametoa elimu kwa Watanzania. Naomba kuuliza maswali mawili madogo.

Kwa kuwa katika kupambana na uvuvi haramu baharini na katika maziwa yetu, jambo linaloonekana ni kwa mvuvi anaevua uvuvi wa haramu kwa sababu anapatikana

na nyavyu zenyе macho madogo; na yeye ndiye hutiwa hatiani. Kuna usemi unaosema mkamatwa na ngozi ndiye mwizi. Sasa swali, je, Serikali inasemaje kwa wale wenye viwanda nya kutengeneza nyavyu, wanaoleta, wanaouza, ambao wao ndio *source* kubwa ya kutufanya huu uvuvi haramu kutokana na vifaa wanavyovileta, kuliko huyu mvuvi ambaye ameuziwa akaenda akaifanya hii kazi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Wizara italeta lini Bungeni Sheria ambayo itaweza kuwadhibiti hawa waletaji, wenye viwanda pamoja na wauzaji ili tuweze kuwadhibiti kisheria pamoja na hawa wanaozitumia nyavyu hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nitambue kweli jitihada za Mheshimiwa Mbunge za kufuatilia masuala ya uvuvi. Si mara ya kwanza yeye kuuliza maswali katika Bunge hili, lakini amekuwa akiwasiliana na Wizara kuonesha *concern* yake kuhusiana na masuala mbalimbali ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kuhusu kwamba ni kwa nini wavuvi tu wanaokamatwa na nyavyu ndio wanachukuliwa hatua za kisheria. Nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba kwa sababu kutumia nyavyu ambazo haziruhusiwi kisheria ni kosa la kisheria, yoyote yule atakayehusika kwa namna moja au nyingine katika utengenezaji, uuzaji, usafirishaji, utumiaji wa nyavyu hizo anakuwa amekiuka sheria vile vile, kwa hiyo hakuna ambaye ataachwa.

Mheshimwia Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kuna kiwanda ambacho kinatengeneza nyavyu ambazo haziruhusiwi, kama kuna mfanyabiashara atafanya, kama kuna dalali, mtu yoyote atakayejihuisha kwa namna moja au nyingine sheria itachukua mkondo wake. Ni kweli kabisa

si wavuvi tu ndio wanakamatwa lakini tayari tumeshakamata bidhaa za kutengenezea nyavu kama hizo, lakini vile vile hata wafanyabiashara ambao wanahuksika wameshachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili kwamba lini tutabadiilisha sheria yetu ya uvuvi ya mwaka 2003 ili sasa kushughulikia kwa utaratibu zaidi makosa mbalimbali yanayopelekea watu kujihusisha na uvuvi haramu. Nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Wizara inafanya utaratibu wa kupitia sheria ile; lakini si sheria ile tu, tunaanza kufikiria sasa kama nchi kwamba suala la uvuvi haramu ni zaidi tu ya uvuvi, inahusisha vile vile mambo ya ugaidi, lakini vile vile inahusisha uhujumu uchumi. Kwa hiyo ikiwezekana sheria nyangi zitarekebishwa ili hili suala tuweze kulishughulikia kwa mapana zaidi na kwa ufanisi zaidi.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kumuuliza swali moja Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Taasisi ya Hifadhi ya Bahari Mafia, imeshindwa kazi yake ya msingi ya kuzuia uvuvi haramu na uhifadhi na hivi sasa inauza visiwa na maeneo Wilaya Mafia. Je, Sasa Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuondoa uongozi wa juu pale na kubadilisha kuleta uongozi mwingine? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tulielezea kwamba hakuna visiwa ambavyo vimeuzwa Mafia isipokuwa sheria tu zimefuatwa kukodisha Kisiwa cha Shungimbili kwa miaka 20 kwa Mwekezaji wa Hoteli. Vile vile kama kuna ushahidi wowote ule ambao utaonesha kwamba, maafisa anaowazungumzia wameshindwa kufanya kazi yao au wamejihusisha na vitendo ambavyo ni kinyume na sheria, lakini vile vile na maadili ya kazi yao, naomba Mheshimiwa Mbunge atuletee na sisi bila kusita tutachukua hatua.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Yosepher Komba.

Na. 262

Tatizo la Maji Mkao wa Tanga

MHE. YOSEPHER F. KOMBA aliuliza:-

Tatizo la Maji Mkao wa Tanga ni kubwa licha ya kuwa na vyanzo vingi vya maji, viongozi wa Serikali kwa nyakati tofauti wamekuwa wakitoa ahadi mbalimbali lakini hakuna hatua za makusudi za kutatua tatizo la maji:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka maji kupitia mradi wa Manga/Magoroto ambao uliana tangu mwaka 1970?

(b) Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya uchakavu wa miundombinu hasa mabomba na mipira katika mradi wa Kicheba na Kwemhosi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji Magoroto ulijengwa mwaka 1977 na ulilenga kuhudumia wakazi wapatao 8,000 katika Mji wa Muheza na maeneo yanayozunguka Mji wa Muheza. Hivi sasa mradi huu unahudumia wakazi wapatao 30,834 walioko katika Mji wa Muheza; idadi hii ni kutokana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu mradi huu hautoshelezi mahitaji katika Mji wa Muheza. Ili kuondoa tatizo, mradi wa dharura utakaogharimu shilingi bilioni 2.6 unaendelea kutekelezwa

kwa kutoa maji eneo la Pongwe. Taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea na kazi inatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji katika Kijiji cha Kwemhosi ulitekelezwa na Serikali kwa gharama ya shilingi milioni 225 na ulikamilika mwezi Juni, 2013. Mradi huu unafanya kazi kama ulivyosanifiwa, ila kwa sasa mradi huo umeharibiwa kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha. Aidha, Mradi wa maji wa Kicheba ulijengwa mwaka 1999 na Kanisa Katoliki ambapo hivi sasa miundombinu yake imechoka. Mradi huu utaendelea kukarabatiwa na Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya watumiaji maji katika eneo la Kicheba, kadri fedha zitakavyopatikana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Komba.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mradi wa dharura ambao anaouongelea Mheshimiwa Waziri hatua za awali zilanza tangu 2015, mradi ambao unatoka Pongwe kuleta maji Muheza. Hata hivyo, nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini mradi huu utakamilika ili uweze kupunguza adha ya maji kwa wananchi wa Muheza Mjini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ameongelea Mto Mnyodo. Kuna madhara makubwa yametokana na mvua zinazoendelea kunyesha, vyanzo vingi vya maji vimeharibika, lakini Waziri amejibu hapa kwamba wanategemea upatikanaji wa fedha ndipo watarekebisha vyanzo hivi vya maji. Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie, kwa sababu hili ni suala la dharura la uharibu wa vyanzo vya maji, ni lini hiyo fedha itapatikana ili kutengeneza vyanzo hivi ili wananchi waendelee kupata maji safi na salama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Komba tukubaliane tu, si kwa nia mbaya lakini ni kweli kwamba Mheshimiwa

Mbunge wa Jimbo la Muheza amekuja ofisini mara tatu na nilimuagiza aje pamoja na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji ya Tanga, tukafanya utaratibu, sasa hivi tuko kwenye utaratibu wa manunuizi. Ni kweli kwamba mradi unaanza utekelezaji mwezi Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lini utakamilika, baada ya kukamilika kwa taratibu za manunuizi na kumpata mkandarasi, ndani yake sasa baada ya kusaini mikataba ndipo tutajua ni lini sasa mradi utakamilika; lakini shughuli imeshafanyika na mradi unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 2.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uharibifu, mvua imenyesha sana Tanga na taarifa ninayo, Kamati ya Ulinzi na Usalama na nimeshaipata ile nyaraka ya uharibifu uliotokea kwenye maeneo mengi. Kwa hiyo, sasa hivi taarifa hiyo, kwanza itapelekwa kwa Mheshimiwa Jenista kwenye ile Kamati ya Maafa, lakini wakati huo hu na sisi tutachukua hiyo nakala, baada ya kupata taarifa ya Mheshimiwa Jenista na sisi tutafanya kazi ili tuhakikishe tumekarabati miradi hiyo kwa haraka ili wananchi wapate huduma ya maji. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi hilo tunalifanyika kazi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa suala la maji linahitaji Waheshimiwa Wabunge wengi na muda wetu umekwisha. Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Hussein, Mheshimiwa Devota Minja, tunaanza na hao.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Napenda niulize swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri shemeji yangu. Hivi tunavyoongea mradi mkubwa wa maji katika Mji wa Bunda unakaribia miaka 10 bila wananchi wa Bunda kupata maji safi na salama, yaani kama mihula ya Mheshimiwa Rais ni mihula miwili. Tatizo kubwa...

MWENYEKITI: Sema moja tu, usianze tena hadithi hapa.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni mkandarasi, mkandarasi yule ni mwizi, ana madeni, kila pesa mnayoiweka Serikalini kwa ajili ya kukamilika mradi ule ili wananchi wa Bunda wapate maji safi na salama...

MWENYEKITI: Ameshakuelewa, Mheshimiwa Waziri majibu. Mheshimiwa Waziri jibu kwa kifupi wako wengi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 tumetenga bilioni 1.6 kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kutengeneza chanzo cha maji. Tumeendelea na shughuli ya kufanya ununuzi wa makandarasi, tukapata makandarasi wabaya, kwa hiyo tumetangaza tena. Hata hivyo, kuhusu hao wakandarasi hao wanaoendelea Mheshimiwa Bulaya nimuahidi kwamba nitaenda huko niende nikawaone. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hussein, Mheshimiwa Devota Minja na Mheshimiwa Adadi wajiandae.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swalii. Mheshimiwa Waziri wa Maji nimewahi kuonana naye mara nyangi sana kuhusu mradi wa maji kutoka Nyamtukuza kwenda mpaka Bukwimba. Mradi ule umepangiwa 15,000,000,000 mpaka sasa hivi Serikali imeshatoa bilioni 3.5 lakini cha ajabu hata kijiji kimoja hakijawahi kupata maji. Je Serikali ina mpango gani ili kuweza kukamilisha mradi huo wa maji ili wananchi wa Nyang'wale waweze kupata maji safi na salama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Hussein tumeweka utaratibu kuhakikisha kwamba miradi yote ambayo ilianza tunaikamilisha kwanza kabla ya kuingia kwenye miradi mipyaa. Sasa hivi tunaendelea kuzunguka kubaini mahali popote pale ambapo pamehujumiwa Mheshimiwa Mbunge taratibu za kisheria zitafuatwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Devotha Minja, ajiandae Mheshimiwa Adadi.

MHE DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kukuniona. Licha ya Mkao wa Morogoro kuwa na mito mingi na hatimaye kuweza kulisha Mikoa mingine kama Pwani, Dar es Salaam na Mkao wa Tanga lakini Mkao wa Morogoro hauna maji safi na salama. Sasa ni lini Serikali itahakikisha Manispaa ya Morogoro hususan katika Kata za Bingwa, Kiegea A na B, Mkundi, Kingolwira na Kihonda zinapata maji safi na salama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu, ye ye anataka kujua ni lini tu, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umgawiliaji.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza swali lake linazungumza kiujumla kwamba Mkao mzima hauna maji salama hili si kweli, si kweli kabisa. Ni kweli kuna upngufu wa maji lakini huwezi kusema Mkao mzima hauna maji salama, watu wangekuwa wameshakufa. Kwa hiyo, kazi ziko na kuna miradi inayoendelea na eneo analolizungumza pale Manispaa ya Morogoro tunao mradi mkubwa wa kupanua mradi ule ambaou upo. Tutaongeza ukubwa wa lile bwawa la Mindu tutaongeza mtandao; hivi sasa kazi imeshaanza kwa awamu ya kwanza ya kupeleka hayo maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge anayasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepeata fedha kutoka Benki ya Ufaransa ya kuweza kuweka miundombinu ya kutosha kabisa kuongeza upatikanaji wa maji, huu wa sasa mara mbili zaidi. Kwa hiyo, Serikali inatambua tatizo hilo na inalifanya kazi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge asiwe na shaka, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kazi.

MWENYEKITI: Ahsante ameshakuelewa. Mheshimiwa Adadi.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali moja la nyongeza. Matatizo ya maji salama na safi Muheza ni makubwa sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa juhudini ambazo wanafanya jinsi walivyoweza kubuni mradi wa kutoa maji Pongwe mpaka Muheza. Mradi huo upo karibu kuanza, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, ukombozi mkubwa ambao tunautegemea Wilayani Muheza ni maji yale yatakayotoka Zigi mpaka Mjini Muheza na vitongoji vyake. Sasa huu mradi upo kwenye mkopo wa Benki kutoka India wa dola milioni mia tano na ni mradi mmojawapo kati ya miradi 17 ambayo inategemewa kuanza. Sasa nataka kujua, kwa sababu wananchi wa Muheza wana shauku kubwa sana wa huu mradi. Huu mradi unaanza lini ili wananchi wa Muheza waweze kujua? Nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri au unajibu mwenyewe Waziri.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwatoe wasiwasi Wananchi wa Muheza, ni kweli fedha imeshapatikana ya kuweza kujenga mradi mkubwa kutoka Mto Zigi kupeleka Mji wa Muheza. Taratibu ambazo tunazifanya sasa, kwanza tunakwenda kusaini mkataba wa *financial agreements*, wa fedha, tunasaini mkataba ule halafu tunaanza kufanya manunuzi ya kupata Mhandisi Mshauri atakayekwenda kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya kuhakikisha kwamba maeneo yote ya Muheza pale yanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tumepanga kulifanya katika mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie wananchi wa Muheza watakwenda kupata maji safi na salama.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

Na. 263

Manufaa kwa Mradi wa Maji kwa Jamii

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza:-

Serikali hutumia gharama kubwa katika utafiti wa maji na ujenzi wa miundombinu ya maji, lakini baadhi ya miradi inayokabidhiwa kwa mamlaka za maji za mji na jumuiya ya watumia maji (*COWUSA*) zinasusua na kutonufaisha jamii kama ilivyokusudiwa:-

Je Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha miradi ya maji inanufaisha jamii kama iliyokusudiwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji mijini na vijjini. Katika kuhakikisha miradi hiyo inanufaisha jamii kama iliyokusudiwa Wizara imeandaa na inatekeleza uundaji, usajili wa vyombo vya watumia maji na kuvijengea uwezo kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi. Katika kuhakikisha mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira zinatoa huduma endelevu mamlaka hizo zinasimamiwa na bodi ambazo zinajumuisha wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji huo kumekuwa na changamoto mbalimbali katika miradi hiyo ikiwemo uchakavu wa miundombinu ya maji, wizi wa vifaa vya maji pamoja na watumiaji maji kutolipia huduma hiyo zikiwemo taasisi za Serikali. Hali hiyo ya baadhi ya taasisi za Serikali kutolipa madeni yao kumepelekea mamlaka nyingi kushindwa kugharamia matengenezo ya miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na wizi wa maji pamoja na uchakavu wa miundombinu Wizara inaendelea kurekebisha Sheria za Maji ili ziweze kutoa adhabu kali kwa wezi wa maji na wahujumu wa miundombinu ya maji. Vilevile mamlaka za maji na usafi wa mazingira mijini zinaendelea kukarabati miundombinu ya maji iliyochakaa, kufunga dira za maji kwa wateja wote ili kubaini matumizi yao halisi na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu ya maji. Aidha, Wizara imeanza kuchukua hatua za kutumia nishati ya jua kwenye mitambo ya maji hususani vijijini kwa ajili ya kupunguza gharama za uendeshaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komanya, jiandae Mabula.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali yenye mikakati mizuri. Naomba nitumie muda wangu kuuliza swalii moja tu la nyongeza. Mamlaka ya Maji ya Mji wa Mwanuzi Wilayani Meatu inasuasua kwa kuwa chanzo chake cha bwawa kimejaa matope na kuathirika na mabadiliko ya tabianchi sambamba na chanzo cha *New Sola Zanzui* kilichopo Wilaya ya Maswa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira imefanikiwa kupata sh. 230,000,000,000 ikiwa ni mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kutoa maji Ziwa Victoria na kuyaleta Mkoa wa Simiyu na usanifu bado unaendelea. Je, Serikali haioni haja katika usanifu huo ikajumuisha kupeleka bomba kuu katika Makao Makuu yote ya Mkoa wa Simiyu ikiwemo Wilaya ya Meatu na Maswa kwa awamu ya kwanza kwa sababu Wilaya hizi zimeathirika kiasi kikubwa na ukame na ziko katika *phase two* na fedha ya *phase two* haijapatikana?

MWENYEKITI: Ahsante. Suburi Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri wa Mazingira

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia na kuuliza swali na kwa umakini anaouonesha katika kufuatilia shida za maji za wananchi wa Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe habari njema kwamba baada ya kupatikana sh. 250,000,000,000 siyo 230,000,000,000 za awamu ya kwanza sasa tunaanza utaratibu wa kupata fedha nyingine zaidi za awamu ya pili ambazo zitapeleka maji sasa katika maeneo yote aliyoyataja pamoja na mkoa mzima na mikoa mingine ambayo inakabiliwa na ukame mkubwa unaotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, Serikali inatamka rasmi kwamba, inatambua changamoto ya maji na ina mipango ya kuyapeleka kwa wananchi wote wanaokabiliwa na ukame katika eneo hilo kwa kuitia mradi huu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, baada ya majibu hayo watu wa Kanda ya Ziwa bado mna maswali? Mheshimiwa Mabula, ajiandae Mheshimiwa wa Kishapu.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa inaonekana utaratibu wa usambazaji maji unakuwa mgumu sana na ziko mamlaka za maji kwa mfano mamlaka ya *MWAUWASA* pale jiji la Mwanza; Serikali ina mpango gani kuziwezesha mamlaka hizi ili ziweze kuwa zinatatua changamoto za maji zinakabiliana nazo kwenye maeneo zilizopo? Hii itakuwa msaada mkubwa sana kwa Halmashauri hizi lakini pia kwa wananchi wenywewe. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawekeza, inaweka miundombinu ambayo ndio imekuwa chanzo cha maji. Kwa mfano tuna bomba la *KASHWASA* likishapita kwenye maeneo mamlaka Halmashauri na kwa sababu tunaendelea kutenga bajeti kila mwaka kile ndio chanzo chao cha maji. Kwa hiyo wanaweza wakatumia ile fedha; na tayari matoleo

yanawekwa kila sehemu wanaweza wakaunganisha pale wakaendelea kusambaza maji ili wananchi wapate maji safi na salama.

MWENYEKITI: Mheshimiwa wa Kishapu, ajiandae Mheshimiwa Mwijage.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *wabeja* sana. Kwa niaba ya wananchi Shapu wa Jimbo la Kishapu, kwanza naomba nitoe shukrani za dhati kwa Wizara kwa kutekeleza mradi kabambe wa maji ya ziwa victori katika Jimbo la Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nije na *scenario* tofauti baada ya mradi huo kufika katika Mji Mdogo wa Muhunze, Mbunge wa Kishapu kushirikiana na viongozi wa Kishapu tumeshafanya mkakati kabambe wa kutafuta mkandarasi ambaye anaweza kutupatia fedha kwa vigezo vile ambavyo Serikali inaweza ikaridhia. Je, Mheshimiwa Waziri je, yuko tayari kukaa na uongozi wa Kishapu ukiongozwa na Mbunge wa Kishapu ili tumweleze kuwa tumeshapata fedha ambazo zinaweza zikayasambaza maji katika Jimbo lote la Kishapu katika vitongoji vyote vya Kishapu iwapo utaridhia tena kwa masharti yale ambayo Serikali inaya... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Inatosha Mheshimiwa ameshakuelewa. Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakubaliana naye kama kuna mwekezaji ambaye anataka kuja kuwekeza katika sekta ya maji na iko ndani ya sera yetu ya maji, maji ni shirkishi ni Serikali pamoja na washirika wa maendeleo mbalimbali. Kwa hiyo, sisi tunamkaribisha yeye aje tuzungumze tuweze kuona namna gani tunaweza kwenda naye katika jambo hili.

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu sahihi. Mheshimiwa Mwijage.

MHE. SEVERINA S. MWIJAGE. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa mradi wa Shinyanga – Kahama uko karibu sana na Bukoba, ni lini Serikali itafanya upembuzi yakinifu kuunganisha maji kuanzia Wilaya ya Muleba, Bukoba Mjini na Wilaya zingine zilizopakana kwa sababu tunapata matatizo ya maji na sisi tuko karibu na mradi huo, ni lini Serikali itaunganisha maji kuwapa watu wa Bukoba?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza maji Bukoba tayari, mradi tumeshakamilisha na wananchi wanapata maji. Kazi iliyopo sasa hivi ni kuendelea kutanua mabomba ili yale maji yaweze kufika kwenye maeneo mengi. Kwa hiyo, kwa Mji wa Bukoba maji tayari tunayo.

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa, maswali yetu yamekwisha, sasa ni kipindi cha wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 15 wa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii wakiongozwa na Meja Jeneral Gaudence Milanzi, Katibu Mkuu. Ndugu Aloyce Nzuki, Naibu Katibu Mkuu; Jaji mstaafu Thomas Mihayo Mwenyekiti wa Bodi ya *TTB*. Pia wameambatana na wageni 42 ambaao ni Wakurugenzi, Mameneja, Wakuu wa Vitengo, Taasisi na Maafisa waliopo chini ya Wizara hiyo. (*Makofii*)

Mgeni mwengine ni Mke wa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, ambaye ni Ndugu Kudra Maghembe. (*Makofii*)

Pia tuna wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambaao wamekuja kutembelea Bunge. Wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni wanafunzi 65 na walimu watano wa Chuo cha Biashara Nganganya kutoka Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Waziri kivuli, Mheshimiwa Esther Matiko wa Wizara hii ya Maliasili anaomba kuwatambulisha Ndugu zake na wageni wake Magreth Matiko, Doroth na Benjamini Nkone. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kupunguza nyaraka zilizoko mezani mwenu hapa ukumbini ili mpate nafasi ya kuweka nyaraka nyingine ambazo huwa zinasambazwa humu ndani.

Tangazo lingine, Waheshimiwa Wabunge wenyewe Imani ya Kikristo. Waheshimiwa Wabunge wote wanatangaziwa kuhudhuria ibada katika eneo la *Chapel* yetu ya Pius Msekwa ghorofa ya pili. Aidha, Wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma pamoja na kwaya ya Safina kutoka Kanisa Kuu la Anglikana Dodoma watajumuika nasi, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. (*Makofii*)

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mwongozo wa Spika!

MWENYEKITI: Mwongozo, Mheshimiwa Bilago!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongozo wa Kanuni ya 68(7) lakini ikisomwa na 147, sitaisoma kwa sababu ya kiokoa muda juu ya jambo lilitokea mapema leo hapa Bungeni. Wakati Mbunge wa Kishapu alipopewa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza alikushukuru kwa lugha ya Kisukuma. Sasa nataka nipate Mwongozo wako kama lugha hizi za makabila mengine na mimi ikiwemo ya kwangu ya Kiha inaruhusiwa kutumika ndani ya jengo hili. Naomba Mwongozo wako. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ni kweli anachosema Mheshimiwa Bilago, lugha za humu ndani ni Kiingereza au Kiswahili, lakini wakati anauliza swali lake kuhusu mambo ya maji, mimi nikafikiri anataja kijiji ambacho kina shida ya maji. (*Kicheko/Makofi*)

Katibu!

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Maliasili na Utalii

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyeekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyeekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na utalii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa 2016/2017. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kunipa nguvu ya kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Mwanga na kuiongoza Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, naungana na Watanzania wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyeekiti wa tano wa Chama cha Mapinduzi, kufuatia uchaguzi wa viongozi wa Chama chetu

uliofanyika mwezi Julai, 2016 hapa Dodoma. Ni dhahiri Watanzania wana imani na matumaini makubwa ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi, chini ya Uenyekiti wake. Wizara yangu inaaahidi kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa kwa kuzingatia ahadi zilizomo kwenye llani ya CCM ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri. Maelekezo wanayotoa yanawezesha kuhakikisha maliasili na malikale zinahifadhiwa ipasavyo na utalii unaendelezwa ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenye viti wa Bunge kwa kuendesha shughuli za Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuishukuru na kuipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayoongozwa na Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Nditiye kwa ushirikiano, maoni na ushauri wakati wa kupitia Mipango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na Mpango wa Maendeleo ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Maoni na ushauri wa Kamati umesaidia sana katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, Wizara itazingatia ushauri huo katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo langu la Mwanga wanaendelea kuniunga mkono kwa dhati katika utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana wananchi na wapiga kura wote kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu na nawaomba waendelee kuniunga mkono ili kuliletea Jimbo letu maendeleo endelevu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pongezi kwa Wabunge wapya waliojunga na Bunge lako Tukufu. Hivyo nampongeza Mheshimiwa Juma Ali Juma, Mbunge wa Jimbo la Dimani Zanzibar, kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo hilo. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa; Profesa Palamagamba John Kabudi, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo, Mheshimiwa Salma Rashidi Kikwete, Mheshimiwa Dkt. Catherine Ruge na Mheshimiwa Mchungaji Getrude Pangalile Lwakatare kwa kuteuliwa kwao kuwa Wabunge wa Bunge letu Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee natoa pole kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na familia, ndugu na marafiki wote kwa kuondokewa na walloukuwa Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Namwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu, azipumzishe roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imepewa jukumu la kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili na malikale, kuendeleza ufugaji nyuki na utalii. Wizara inazingatia Sheria; katika kuimarisha mifumo ya usimamizi na uendeshaji; ukusanyaji mapato; maendeleo na ustawi wa wananchi; na utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa yenyе mitizamo chanya katika uhifadhi wa maliasili. Jukumu hili linatekelezwa kwa ushirikiano na wadau wakiwemo wananchi, sekta binafsi, asasi za kiraia na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda Mrefu mwaka 2011 hadi 2025 na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016 hadi 2021; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 na Hotuba ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph

Magufuli, alipokuwa anazindua Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umuhimu wa Maliasili, Malikale na Utalii; Sekta ya Maliasili, Malikale na Utalii ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii ya Tanzania. Sekta hii inachangia katika kuzalisha ajira na mapato ya Serikali, uhifadhi wa mazingira na kutunza mifumo ya ikolojia kwa manufaa ya binadamu na viumbe wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utalii ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi hasa katika Sekta za Kilimo, Mawasiliano, Miundombinu, Usafirishaji, burudani na uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa watalii. Aidha, katika mwaka 2016/2017 watu 500,000 walijiriwa katika Sekta ya Utalii na wengine 1,000,000 walijijari wenyewe katika sekta hiyo. Vilevile, sekta ilichangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa na kulipatia Taifa letu asilimia 25 ya fedha zote za kigeni

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imejaliwa kuwa na maeneo makubwa ya kuvutia ya uhifadhi wa wanyamapori na misitu yenye aina tofauti ya miti na wanyamapori ambao wamekuwa ni kivutio kikubwa cha utalii hapa duniani. Rasilimali hizo zina mchango mkubwa katika kuweka mizania ya bioanuwai (mimea na wanyama) na kuzuia mtawanyiko wa vimelea hatari vyta magonjwa. Aidha, Sekta ya Misitu imechangia asilimia 3.9 kwenye pato la Taifa. Ukichanganya asilimia 3.9 na zile asilimia 17.5 za utalii, utaona kwamba sekta hii inachangia zaidi ya asilimia 21 ya pato ghafi la Taifa na hivyo ni sekta muhimu sana kwa ulinzi na uendelezaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa Wizara hii kiuchumi, kijamii na ikolojia, natoa rai kwa wananchi na viongozi wa ngazi zote kutambua wajibu wao wa kulinda, kuendeleza na kutumia maliasili na malikale zilizopo kwa njia endelevu kwa faida ya kizazi hiki na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitoe taarifa ya Utekelezaji wa kazi za Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 na Mpango na Bajeti wa Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 135.8 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ambapo shilingi bilioni 118 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 17.7 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2016/2017 ulizingatia vipaumbele sita ambavyo vinafafanuliwa katika sekta ndogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kubwa la Sekta ndogo ya Wanyamapori ni uhifadhi wa wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Utekelezaji wa jukumu hilo unazingatia Sera ya Wanyamapori ya 2007 na Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 Sura 283. Aidha, Matumizi ya maeneo ya Wanyamapori yamezingatiwa na kugawanywa katika makundi ya uvunaji na yasiyo ya uvunaji. Maeneo ya uvunaji yako kwenye Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori na maeneo ya wazi. Maeneo yasiyo na uvunaji ni Hifadhi za Taifa na zinaangaliwa na Shirika la hifadhi za Taifa, *TANAPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Idara ya Wanyamapori ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori, Sura 283. Aidha, marekebisho ya Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282; Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura 284; na Sheria ya Taasisi za Utafiti wa Wanyamapori za Taifa, Sura 260; na Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Sura 549 yanaendelea. Vile vile, maandalizi ya Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Wizara inatekeleza mkakati wa kupambana na ujangili na

biashara haramu ya wanyamapori na mazao ya misitu kwa mwaka 2014 - 2019. Wizara pia imeanzisha Kikosi Kazi cha Kudhibiti Uhalifu wa Kijinai katika Tasnia ya Misitu na Wanyamapori (*Wildlife and Forest Crimes Task Force*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wizara iliendesha jumla ya siku 349,102 ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa zilizowezesha kukamatwa kwa jumla ya watuhumiwa 7,085 na meno ya tembo 129 na vipande vya meno 95 vyenye uzito wa kilo 810. Vilevile, silaha za kivita 48, silaha za kiraia 150, risasi 1,058, magobore 406, silaha za jadi 22,307, roda 120,538 zilikamatwa pamoja na pikipiki 189, balskeli 214, magari 20, ng'ombe 70,831 na samaki kilo 4,043.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia doria hizo, jumla ya kesi 2,097 zilifunguliwa katika Mahakama mbalimbali hapa nchini. Jumla ya kesi 802 zilikamilika ambapo kesi 262 zenye watuhumiwa 472 walifungwa jela jumla ya miezi 42,153. Aidha, kesi 43 zenye watuhumiwa 79 zilimalizika kwa wahusika kuachiwa huru. Vilevile, kesi 276 zenye watuhumiwa 469 walilipa faini ya jumla ya sh. 452,141,862/= na kesi 966 zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Wizara ilianzisha Kikosi Kazi Maalum, kutumia teknolojia ya ndege zisizo na rubani (*drones*) na mbwa maalum wa kunusa (*sniffer dogs*) kwa ajili ya kuimarisha doria dhidi ya ujangili na biashara haramu ya nyara za Serikali. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wajumbe wa kikosi kazi hicho, Jeshi la Polisi, Kamati za Ulinzi na Usalama na wananchi waliota ushirikiano katika kufanikisha kazi hii maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na viongozi wengine ambao wamefanya juhudini kubwa katika kukamilisha na kuhakikisha kwamba ujangili hapa nchini unatokomezwa, napenda kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba na *Inspector Generally* wa Polisi Bw. Joseph Mangu kwa ushirikiano

mkubwa na kazi kubwa waliyofanya kuhakikisha kwamba majangili hawana mahali pa kukaa hapa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania ulianzishwa chini ya Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori, Sura 283 kwa lengo la kuwezesha uhifadhi wa wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Katika mwaka 2016/2017, Mfuko umetumia shilingi bilioni 6.7 kuwezesha utekelezaji wa kazi za kiuhifadhi na miradi ya maendeleo zikiwemo doria na kazi ya Kikosi cha upambanaji na ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Ndogo ya Wanyamapori inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ujangili ambao tunaendelea kuutokomeza; uvamizi wa mifugo katika hifadhi; migogoro ya mipaka baina ya wananchi na hifadhi; na upungufu wa miundombinu muhimu hasa katika hifadhi zilizopo ukanda wa Magharibi na Kusini mwa nchi yetu. Aidha, Wizara inakabiliana na changamoto hizo kwa kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo kuanzisha mfumo wa Jeshi (Usu); kuimarisha mbinu za kupambana na ujangili; na kuboresha miundombinu katika maeneo mbalimbali ya uhifadhi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, Wizara inatarajia kupitia Kanuni tatu za nyara, uwindaji wa kitalii na usimamizi wa mikataba ya *CITES*; kuhakikisha na kukusanya nyara zote za Serikali zilizopo kwenye Vituo vya Polisi, Halmashauri za Wilaya, Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro. Aidha, itakarabati ghalbala kuu la nyara (*Ivory Room*) na kuweka vifaa vya kisasa kulinda ghalbala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia, inaendelea kutoa elimu ya ushiriki wa wananchi katika usimamizi na maeneo ya Jumuia za Hifadhi za Wanyamapori kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathirika na wanyama wakali na waharibifu na kukiwezesha Kikosi Kazi Maalum kupambana na ujangili katika kutekeleza majukumu

yake. Aidha, Wizara inaendelea na juhudzi za kukamilisha uendeshaji wa Mapori ya Akiba ya Kipindimbi huko Nachingwea, Mavuj, Litumbandyosi na Gezamasoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Hifadhi za Taifa, *TANAPA* lilianzishwa mwaka 1959 kwa Sheria ya Hifadhi za Taifa sura 282. Shirika limepewa dhamana ya kusimamia na kuendeleza maeneo yaliyoanzishwa kisheria kuwa hifadhi za Taifa. Aidha, Shirika linasimamia hifadhi 16 zenye jumla ya eneo la kilometra za mraba 57,365.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 kwa upande wa maduhuli Shirika lilikusanya jumla ya shilingi bilioni 173.2 na kuchangia shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuendeleza utalii. Katika mwaka 2016/2017, Shirika limetekeleza majukumu yake kwa kuweka *beacons* katika mipaka ya hifadhi ambapo jumla ya *beacons* 1,518, zimebekwa. Aidha jumla ya kilometra 2,571 za barabara zilizopo katika hifadhi zimekarabatiwa pamoja na kuimarisha mifumo ya kuondoa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika limeanzisha na kutangaza bidhaa mpya za utalii ambazo mkienda kutalii kama tulivyozungumza wakati wa semina mtazikuta kule pamoja na *canopy walkway* katika hifadhi ya Ziwa Manyara, *paragliding* katika hifadhi ya Kilimanjaro na kuendesha balskeli katika hifadhi za Kilimanjaro na Arusha. Aidha, utalii wa kupiga kambi katika kasoko au kreta ya Kibo umefunguliwa na unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo ya Ngorongoro ilianzishwa na sheria, Sura 284. Mamlaka ina jukumu la kusimamia eneo la kilometra za mraba 8,292 kwa ajili ya kuhifadhi, kuendeleza utalii na wafugaji wenyeji. Eneo hilo lilianzishwa likiwa na idadi ya wenyeji au wakazi takribani 8,000 mwaka 1959 na idadi hiyo sasa imefikia wakazi 90,000 mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Mamlaka lilikusanya shilingi billioni 82 kutokana na watalii

487,840 waliotembelea hifadhi hiyo. Aidha, Mamlaka imeweka *beacons* 387 kwenye mipaka yake na maeneo ya Oldeani, Karatu, Mbulumbulu, Lositete, Piyaya, Ndutu na Lemuta. Zoezi hilo lilitifanyika kwa ushirikiano mzuri wa vijiji vinavyozunguka hifadhi, Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya za Karatu, Ngorongoro na Monduli na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka imenunua magari manne ya doria na imekamilisha ujenzi wa Kituo cha Doria pamoja na kukamilisha ukarabati wa Kambi ya Mary Leakey katika eneo la Laitori. Hifadhi itatekeleza mradi wa maji kwenye eneo la Oletakule, Mbitini na Olduvai; na Ngorongoro itafanya Sensa ya kuwatambua wakazi wote na mifugo yao pamoja na kubaini wakazi halali ili kuwapatia vitambulisho, kuweka mifugo alama na kuwapatia wananchi na mifugo yao maji katika maeneo yote wanapokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, Mamlaka inakadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 88.3 kutokana na watalii wanaotarajiwa kufikia 631,520.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapor Tanzania (*TAWA*) ilianzishwa na tangazo la Serikali Na.135 la Mei, 2014 chini ya Kifungu Na. 8 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapor Na. 283 ikisomwa pamoja na marekebisho yaliyotolewa katika tangazo la Serikali Na. 20 la Januari, 2015. *TAWA* ilanza kazi zake rasmi mwezi Julai, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Mamlaka ya *TAWA* ni kusimamia uhifadhi wa wanyamapor kwenye mapori ya akiba 28, mapori tengefu 42 na maeneo ya wazi yenye mazalia ya wanyamapor, mtawanyiko na shoroba. Aidha, Mamlaka inashirikiana na jamii katika kusimamia maeneo 22 ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapor na maeneo manne ya ardhi oevu yenye umuhimu wa Kimataifa (*Ramsar Sites*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Mamlaka imekusanya jumla ya shilingi billioni 28.8 sawa na asilimia 78 ya lengo. Jumla ya watalii 47,272 walitazamiwa kutembelea eneo hilo pamoja na wawindani 491.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ilifanikiwa kubaini mtandao wa ujangili wa Kakakuona na kuwakamata watuhumiwa wanne mjini Morogoro kwa kupatikana na magamba ya Kakakuona wanaokadiriwa kufikia 670 wenye thamani ya Shilingi billioni 1.4. Aidha, kwa kushirikiana na *INTERPOL* pamoja na *Lusaka Agreement Task Force*, Mamlaka imewakamata vinara wa ujangili huo kutoka Mataifa ya Uganda, China na Austria. Katika matukio mengine, kobe 342 walikamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ilifanya jumla ya siku doria 935 katika maeneo mbalimbali na illazimika kuua jumla ya wanyama 31 ili kuwanusuru wananchi na mali zao na kuepusha madhara yanayoweza kusababishwa na wanyama wakali na waharibifu. Aidha, Mamlaka imesimika jumla ya *beacons* 3,493 katika mipaka yake inayozunguka mapori, sawa na asilimia 33 na kazi hiyo bado inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 19 Mei, 2016 Wizara ilisitisha kwa miaka mitatu utoaji wa vibali vyta kukamata na kusafirisha wanyamapori hai nje ya nchi yetu kutokana na kubainika uwepo wa ukiukwaji mkubwa wa taratibu za kisheria. Aidha, tamko rasmi la Serikali la usitishaji huo lilitolewa katika Bunge lako Tukufu tarehe 25 Mei, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanyamapori hai kutoka Tanzania wamekuwa wakikamatwa katika nchi mbalimbali za ughaibuni wakiwa wametoroshwa. Aidha, hii siyo mara ya kwanza ya taarifa za wanyama wa Tanzania kutolewa nje, kuibiwa kwa aibu. Lengo la katazo hili ni kutoa fursa kwa Wizara na wadau kufanya mapitio ya taratibu za biashara hiyo ili kukidhi mahitaji ya wadau na mahitaji ya Kimataifa na maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya uhakiki wa wanyamapori hai waliopo kwenye mazizi ya wafanyabiashara hao na waliouzwa nje ya nchi. Uhakiki huo ulihusisha mazizi 92, bustani za wanyamapor 17, maeneo ya uzalishaji 18 na ranchi tatu zenyе jumla ya wanyamapori hai 29,730 wenye thamani ya Dola za Marekani 1,602,632. Tathmini hiyo inalenga kutoa kifuta jasho kwa wafanyabiashara walioathirika na katazo hili kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapor Tanzania (*TAWIRI*) ilianzishwa kwa Sheria, Sura 260 kwa lengo la kusimamia, kufanya na kuratibu utafiti wa wanyamapor hapa nchini. Taasisi ina wajibu wa kutoa ushauri kuhusu uhifadhi endelevu wa wanyamapor kwa kutumia matokeo ya utafiti wa kisayansi. Aidha, *TAWIRI* ina wajibu wa kufanya sensa ya makundi mbalimbali ya wanyamapor ili kuwashauri Wahifadhi na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Taasisi imeendelea kufanya utafiti wa uhifadhi wa wanyama mbalimbali pamoja na mbwa mwitu waliokuwa hatarini kutoweka katika mfumo wa ikolojia wa Serengeti ambapo makundi 25 ya mbwamwitu yenyе jumla ya mbwamwitu 300 yalifuatiliwa na kurekodiwa. Taasisi iliendelea kufanya utafiti wa mwenendo wa magonjwa ya Kimeta, Kifua Kikuu na Homa ya Vipindi (*brucellosis*) na magonjwa mengine yanayoambukiza kati ya wanyamapor, mifugo na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, Taasisi itaendelea kusimamia na kuratibu utafiti wa wanyamapor ikiwa na miradi ya utafiti wa mbwamwitu na jinsi mfumo ya ikolojia wa Serengeti unavyofanya kazi na manufaa yake kwa jamii. Aidha, itafanya sensa ya wanyamapor katika sehemu mbalimbali ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Vilevile, Taasisi itaendelea na mradi wa ujenzi wa jengo la maabara ya kisasa ya utafiti wa nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Taaluma y a Wanyamapor; Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kupitia Vyuo vya Usimamizi wa Wanyamapor, Mweka; Chuo cha Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapor, Pasiansi; na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu, Sekamaganga ili kupata wataalam wa wanyamapor na kada mbalimbali za uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kuu la Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki ni uhifadhi wa misitu iliyopo ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa ikiwa ni pamoja na makundi ya nyuki ya aina zote. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Misitu ya mwaka 1998 na Sera ya Ufugaji Nyuki ya mwaka huo huo na Sheria ya Misitu, Sura 323 na Sheria ya Ufugaji Nyuki, Sura 224.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina misitu yenyeh hekta milioni 48.1 ambayo asilimia 93 ni Misitu ya Mataji Wazi au *woodlands* na asilimia saba ni misitu iliyofunga ikiwepo misitu ya asili na misitu ya kupandwa. Mahitaji halisi ya mazao ya timba kwa sasa yanakadirwa kuwa meta za ujazo milioni 62.3 kwa mwaka. Hata hivyo, kiasi kinachoweza kuvunwa hivi sasa ni meta za ujazo milioni 42.8 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Misitu hiyo inasimamiwa na Serikali Kuu kwa maana ya hekta milioni 92.2, hekta milioni 3.4 inasimamiwa na Serikali za Mitaa; na Serikali za Vijiji zinasimamia hekta milioni 21.6 na watu binafsi wanasmamia hekta milioni 3.4. Eneo liliobaki la hekta milioni 0.5 ni misitu iliyopo kwenye ardhi huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Ufugaji Nyuki, Serikali Kuu na Serikali za Vijiji kwa pamoja zinasimamia hifadhi 46 za nyuki zenyeh hekta 143,936.8 na katika ya hizo, hifadhi 26 ni za Serikali za Vijiji na hifadhi 20 ni za Serikali Kuu. Ufugaji nyuki unafanya katika mikoa yote hapa nchini lakini uzalishaji mkubwa wa mazao ya nyuki unafanya katika Mikoa ya Tabora, Kigoma, Dodoma, Singida,

Shinyanga, Rukwa, Arusha, Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kuu la Idara ya Misitu na Nyuki ni kutayarisha na kusimamia sera, sheria, kanuni na miongozo ya misitu na ufugaji nyuki. Katika mwaka 2016/2017, Wizara ilifanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Misitu na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki. Aidha, Wizara inaendelea kukusanya maoni ya wadau kwa ajili ya mapitio ya Sheria za Misitu na Sheria ya Ufugaji Nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeratibu utekelezaji wa dhana ya usimamizi shirikishi wa rasilimali za misitu na nyuki katika Wilaya 67 za Tanzania Bara. Aidha, imeanzisha na kuzijengea uwezo Kamati za Maliasili za Vijiji ili kuziwezesha kutambua rasilimali zao za vijiji zilizopo na kupanga mipango ya uvunaji katika misitu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *TFS*. Wakala huo ulianzishwa kwa Sheria ya Wakala, Sura 245 na kupewa jukumu la kusimamia na kuhifadhi rasilimali za misitu na ufugaji nyuki. Wakala unasi mamia misitu ya hifadhi za Serikali Kuu na misitu iliyopo kwenye maeneo huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Wakala umekamilisha mipango ya Usimamizi wa Misitu ya Hifadhi 56 ambayo inatumika kusimamia misitu husika. Aidha, tathmini kwa ajili ya kuandaa mipango ya usimamizi inafanyika kwenye misitu ya hifadhi 28 katika Mikoa ya Kagera, Tabora, Katavi, Lindi, Pwani na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala unaendelea kuondoa wavamizi kwenye hifadhi za misitu 14 katika Wilaya saba. Ilibainika kuwa vijiji 228 vipo ndani ya hifadhi za misitu na kati ya hivyo, vijiji 157 vimesajiliwa. Hatua za kutatua tatizo hili zinafanya na Kamati ya Wizara tatu ambayo inaendelea kufanya kazi vizuri na ripoti yake ya kwanza ilipokelewa na Mawaziri wiki iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala umepanda miti hekta 7,532, kupalilia hekta 26,671, kupunguzia miti hekta 5,038 na kufanya *pruning* katika mashamba ya hekta 2,859. Aidha, Wakala umeanzisha mashamba mawili mapya ya hifadhi. Hifadhi hizo ni za Misitu wa Nishati kule Morogoro na Mpepo kule Mbinga. Vilevile, Wakala umepanua shamba la miti la Wino-Ifiga kufikia hekta 17,000 kwa kuongeza eneo la Mkongotema la hekta 5,000 katika Wilaya ya Madaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala umetekeleza makubaliano yanayohusisha nchi za Zambia, Msumbiji, Kenya, Madagascar, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kudhibiti biashara haramu ya usafirishaji wa mazao ya misitu nje ya nchi. Kupitia makubaliano hayo, Serikali ya Msumbiji imerekebisha Sheria yake ya Misitu ambapo kuanzia Machi, 2017 imezuia usafirishaji wa magogo nje ya nchi. Udhibiti wa biashara baina ya Zambia na Kenya pia umeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Wakala ulikusanya shilingi bilioni 72.4 kwa kutumia mashine za *EFD* kukusanya maduhuli katika vituo vyake 46.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la mahitaji ya malighafi ya misitu hususan magogo kwa ajili ya mbao limesababisha ugumu wa kiasi kikubwa katika kugawa mgao kidogo wa magogo ambayo yanakuwa tayari kila mwaka. Kwa kipindi kirefu Wizara imekuwa ikuza malighafi kutoka katika mashamba ya miti kwa njia ya kutoa vibali. Utaratibu huu umesababisha malalamiko mengi kutoka kwa wadau na makundi mengi ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wakala umefanya mapitio ya njia za kugawa malighafi kutoka katika mashamba ya miti ya Serikali. Aidha, Wakala umefanya tathmini ya viwanda vya misitu nchini kwa lengo la kujua idadi na uwezo wa viwanda hivyo na idadi ya watu wanaoajiriwa kila mwaka na viwanda hivyo. Matokeo ya mapitio hayo yanaonesha kuwa utaratibu wa vibali kwa kiasi kikubwa unasababisha kutoa vibali kwa wadau wasio na sifa za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira hayo, yameibuka makundi ya walanguzi wa vibali ambao huuza vibali hivyo kwa wale waliowekeza kwenye viwanda vya uchakataji wa magogo. Matokeo yake ni kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na kuathiri mlaji wa mwisho; kufungwa kwa viwanda vingi na vijana wengi kuachishwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hiyo, kuanzia mwaka 2017/2018, vibali vya uvunaji kutoka kwenye mashamba ya Serikali vitatolewa kwa waliowekeza kwenye viwanda kama malighafi ya misitu. Viwanda vitakavyohusika ni viwanda vikubwa, vya kati na wajasiriamali wadogo wenye misumeno maarufu kama *dingdong*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala utatekeleza mikakati mbalimbali ili kukabiliana na changamoto zilizopo ikiwemo kusimamia rasilimali za misitu na nyuki kwa kushirikiana na wadau; kuongeza kasi ya upandaji wa miti katika mashamba mbalimbali ya Serikali; na kuhamasisha upandaji na matumizi ya nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, Wakala utapanda miti katika hekta 8,800, kupallilia mashamba ya hekta 29,505, kupogolea hekta 6,263 na kupunguza miti hekta 3,500. Aidha, *TFSitaanzisha* mashamba mapya matatu huko Buhigwe (hekta 800), Makere (hekta 30,000) yote hayo yakiwa Mkoani Kigoma; na Shamba la Biharamulo lenye ukubwa wa hekta 30,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2017/2018, Wakala unakadiria kukusanya shilingi bilioni 118.4. Aidha, Wakala utafunga mfumo wa kielektroniki katika vituo vyake vyote kukusanya maduhuli na kutoa mafunzo kwa wakusanya maduhuli ili kuboresha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Mbegu (*TTSA*); Serikali ilianzisha Wakala wa Mbegu wa Tanzania na umepewa jukumu la kuzalisha na kusambaza mbegu bora

za miti na vipandikizi vingine mbalimbali, vingine kwa ajili ya uendelezaji wa mashamba ya miti ya Serikali, mashamba ya wananchi na kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Wakala ulikusanya tani 14 za mbegu na kuuza tani saba kwa shilingi milioni 648.4. Katika mwaka ujao, Wakala umekadiria kukusanya tani 20 na utauza tani 17 za mbegu bora za miti zenye thamani ya shilingi milioni 850.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (*TAFORI*), ina jukumu la kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaaluma kuhusu matumizi ya teknolojia bora za uendeshaji wa misitu. Katika mwaka 2016/2017, Taasisi ilikamilisha utafiti wa umri sahihi wa kuvuna miti ya Misindano ya aina ya *pinus* na misaji unaozingatia uwekezaji (*economic rotation age*). Aidha, utafiti kuhusu uzalishaji wa miche bora ya miti ya Misaji, Mkongo, Mvule na Mkangazi kwa kutumia teknolojia ya tishu unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Sekta ndogo ya Utalii ni kuendeleza utalii nchini na kuhakikisha kuwa utalii unachangia ipasavyo katika kukuza pato la Taifa. Sekta ya Utalii inaongozwa na Sera ya Utalii ya mwaka 1999 na Sheria ya Utalii, Sura 29 ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya utalii yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2016 mapato yalifkia dola za Kimarekani bilioni 2.07 kutokana na watali waliofikia nchini kwetu 1,284,279 ikiliganishwa na dola za Marekani bilioni 1.9 zilizopatikana katika mwaka 2015. Aidha, juhudii kubwa zimefanywa ili kupanua wigo wa vivutio vya utalii kwa kuhamasisha wananchi kuanzisha na kuendeleza miradi ya utalii wa utamaduni ambapo hadi sasa jumla ya miradi ya utamaduni 66 imeanzishwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Idara ya Utalii imefanya mapitio ya Sera ya Utalii na kufanya zoezi la kupanga huduma za malazi na chakula (*Hotels, lodges*

& Restaurants) katika madaraja ya ubora wa viwango kati ya nyota moja hadi nyota tano. Katika zoezi hilo, huduma 203 zilizojengwa baada ya mwaka 2010 zilikaguliwa katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kati ya hizo, huduma 53 zilipata nyota ambapo mgawanyo wake ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyota tano, hoteli moja; nyota nne, hoteli mbili; nyota tatu, hoteli 13; nyota mbili, hoteli 31; na nyota moja hoteli sita. Aidha, huduma za malazi 18 ambazo hazikufikia kiwango cha kupata nyota zilipewa hadhi ya kuthibitishwa (*approved facilities*). Katika tathmini hiyo, huduma 132 ambazo hazikufuzu kwa kiwango kinachotakiwa, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kitaaluma kuziwezesha kufikia kiwango cha nyota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, maendeleo ya Sekta ya Utalii nchini bado yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti katika kutangaza, mfumo wa malipo wa fedha taslimu badala ya kadi za kibenki kama *Visa, Amex na Mastercard*. Idadi ndogo ya huduma za malazi, mtazamo hasi wa jamii kwa wahudumu wanaoshiriki katika tasnia ya ukarimu na huduma hafifu zitolewazo, gharama za juu za huduma za utalii na Shirika la Ndege la Tanzania kutokuwa na safari za moja kwa moja kutoka masoko makuu ya utalii; mabadiliko ya tabianchi yanayotishia uwepo na ubora wa vivutio vyetu vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, Wizara itaweka msisitizo katika kutangaza katika masoko yetu makuu ya utalii ya Marekani, Uingereza, Ujeruman, Ufaransa na Italia pamoja na nchi ambazo zimeendelea hivi karibuni kama Uyahudi, China na Urusi. Wizara pia itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Utalii na Kanuni za kusimamia Vyuo vinavyotoa Mafunzo ya Utalii na Ukarimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepokea kwa furaha kubwa uanzishwaji upya wa Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*) katika mwaka 2016/2017. Hatua hii imeanza kuzaa matunda kwa ndege za *ATCL* kutua katika viwanja

vya Mtwara, Songea, Songwe, Tabora, Kigoma, *KIA* na Arusha. Hatua hii imepunguza nauli za ndege za ndani kwa watalii kwa zaidi ya asilimia 50 kwa vituo vipyta ya Kigoma na Tabora. Mategemeo yetu ni punguzo la gharama za *Destination Tanzania* tutakapopokea *Dreamliner* na *ATCL* kuruka kutoka Ughaibuni ikiwa na watalii kuwaleta Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu ya pili ya utekelezaji, Wizara itaendelea kupanga huduma za malazi kwa madaraja ya ubora katika Mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Tanga na Mwanza na Mara na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa watoa huduma 500 katika fani ya Utalii na Ukarimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Bodi ya Utalii imeendelea kufanya mapitio ya Mkakati wa Utangazaji wa mwaka 2012 – 2017. Bodi ya Utalii kuititia Onyesho la Kimataifa la Utalii liliofanyika nchini Ujerumani mwezi Machi, mwaka huu pamoja na vivutio vingine ilionesha kielelezo cha nyayo za zamadamu wa Laetoli za miaka milioni 3.6 iliyopita pamoja na picha za wanyama na ndege wa wakati huo wa kale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kielelezo hicho kiliwavutia watu wengi kutembelea banda la Tanzania ili kujua chimbuko la historia ya mwanadamu. Aidha, banda letu lilipata zawadi ya kuwa mshindi wa kumi bora katika mabanda ya Afrika. Napenda niwapongeze sana Makumbusho ya Taifa na *TTB*kwa mafanikio haya makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Bodi imeratibu Ziara ya Waandishi wa Habari kutoka Kituo cha Televisheni cha *China Anhui* chenye watazamaji zaidi ya milioni nane katika lengo la kuvutia watalii kutoka China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Ndogo ya Malikale imepewa majukumu ya kuandaa, kusimamia na kudurusu Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya urithi wa utamaduni wa

Taifa. Sekta ndogo ya Malikale inajumuisha Idara ya Mambo ya Kale na Shirika la Makumbusho la Taifa. Idara hii imepewa jukumu la kutayarisha na kusimamia Sera, Sheria, kanuni na Miongozo ya kuendeleza na kutangaza urithi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka uliopita, hatua kubwa ilipigwa kwa eneo hili. Wizara imegundua nyayo nyingine za zamadamu na wanyama wa kale zenye umri wa miaka milioni 3.6 katika eneo la Laetoli, Mkoani Arusha. Ugunduzi huo umefanya maeneo yenye nyayo kufikia matatu. Vilevile, Wizara imebaini uwepo wa Jiwe la Mbaji na unyayo unaofanana na wa binadamu katika eneo hilo. Utafiti pia umebaini uwepo wa mapango ya Matiri yaliyopo Kindimba Juu na Kindimba Chini ambayo yalitumika kujificha kwa wananchi wetu wakati wa Vita vya Maji Maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wananchi wote, washirika wa maendeleo, asasi za kiraia na wadau wote wa Sekta ya Maliasili, Malikale na Utalii kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha katika utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka 2016/2017. Kwa namna ya pekee napenda niwashukuru viongozi wote wa Wizara ya Maliasili akiwemo Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Ramo Makani; Meja Jenerali Milanzi, ambaye ni Katibu Mkuu; Naibu Katibu Mkuu Dkt. Nzuki na Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishukuru sana familia yangu kwa kipekee hasa mke wangu mpenzi na watoto wetu kwa upendo na kuniunga mkono katika harakati za kuendeleza Wizara ya Maliasili na Utalii. Napenda niseme wazi kwamba hata katika harakati za kupambana na Faru John, familia yangu ilisimama nami imara kweli kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kuzishukuru nchi, mashirika na taasisi mbalimbali kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Nachukua fursa hii kuzitaja nchi hizo kama ifuatavyo:-

Serikali za Canada, China, Finland, Korea Kusini, Marekani, Norway, Ubelgiji, Ujeruman, Uswisi na Jumuiya ya nchi za Ulaya, Mashirika na taasisi ikiwemo pamoja na AWF, AWHF, BTC, FAO, FZS, GEF, GIZ, ILO, ICCROM, ICOM, ICOMOS, IUCN, KFW, NORAD, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, World Bank na WWF.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika 2017/2018, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya sh.148,597,946,000/= kwa matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kati ya fedha hizo, sh. 96,794,662,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 51,803,284,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha sh.58,572,687,000/= Fedha za Mishahara na sh.38,221,975,000/= kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Fedha za Maendeleo zinajumuisha sh.34,803,284,000/= ambazo ni fedha za ndani na sh.17,000,000,000/= ambazo ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge wote kwa kunipa heshima ya kuniskiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya www.mnrt.go.tz

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba yangu ya bajeti iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo kwenye kitabu chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofii)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Ahsanteni.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII MHESHIMIWA
PROF. JUMANNE ABDALLAH MAGHEMBE (MB) WAKATI
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018 -
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, Kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na mwenyekiti wa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii**, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

2.0 PONGEZA NA SHUKRANI

2. **Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kunipa nguvu ya kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Mwanga na kuongoza Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa heshima na unyenyekevu namshukuru Mheshimiwa Dr. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara ya Maliasili na Utalii.

3. **Mheshimiwa Spika**, Naungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa tano wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kufuatia uchaguzi wa viongozi wa Chama uliofanyika tarehe 23 Julai, 2016 mjini Dodoma. Ni dhahiri Watanzania wana imani na matumaini makubwa na uongozi wa Chama Tawala chini ya uenyekiti wake. Wizara yangu inaahidi kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa kwa kuzingatia ahadi zilizomo kwenye llani ya CCM ya mwaka 2015.

4. **Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri. Maelekezo wanayotoa yameweza kuhakikisha maliasili na malikale zinahifadhiwa ipasavyo na utalii unaendelezwa ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa.

5. Mheshimiwa Spika, Mafanikio ya viongozi wetu wa Kitaifa katika kuboresha miundombinu, usafi wa anga na kuhifadhi mazingira zimeimarisha usimamizi wa maliasili, malikale na kuchochea maendeleo ya utalii nchini. Jithada hizo zimeiletea sifa Tanzania katika jumuiya ya kimataifa kuwa nchi yenye dhamira ya dhati ya kujiletea maendeleo. Viongozi wengi kutoka mataifa mbalimbali duniani wamefika nchini na kusaini makubaliano ya ushirikiano katika nyanja za uhifadhi wa bioanuwai na kuendeleza utalii. Baadhi ya makubaliano hayo yamefanyika na nchi za Morocco, Uturuki, Ethiopia na Afrika Kusini. Kauli mbiu ya '**HAPA KAZI TU**' itaendelea kuongoza utendaji wa Wizara kwa kuzingatia maslahi ya Taifa na wananchi wake.

6. Mheshimiwa Spika, Nakupongeza wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb) na Naibu Spika Mheshimiwa Dr. Tulia Ackson (Mb) na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa weledi mkubwa. In-Shaa-Allah Mwenyezi Mungu azidi kuwapa nguvu za kuendelea kuongoza Bunge letu Tukufu.

7. Mheshimiwa Spika, Nitumie fursa hii kuishukuru na kipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayoongozwa na Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye (Mb) kwa ushirikiano, maoni na ushauri walioutoa wakati wa kupitia Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Maoni na ushauri wa Kamati umesaidia sana katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, Wizara itazingatia ushauri wa Kamati katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

- 8. Mheshimiwa Spika**, Wananchi wa Jimbo langu la Mwanga wameendelea kuniunga mkono kwa dhati katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wananchi na wapiga kura wa CCM wote kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo. Naendelea kuwahimiza tuzidi kushirikiana na kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo katika jimbo letu la Mwanga.
- 9. Mheshimiwa Spika**, Napenda kuungana na waheshimiwa wabunge wenzangu kutoa pongezi kwa wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu. Nampongeza Mheshimiwa Juma Ali Juma, Mbunge wa jimbo la Dimani, (CCM) Zanzibar kwa kuchaguliwa na wananchi wa jimbo hilo. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi, Anna Killango Malecela, Abdallah Majura Bulembo, Salma Rashidi Kikwete na Mchungaji Getrude Pangalile Lwakatare kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kuwa wabunge. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Dr. Catherine Nyakao Ruge kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum. Nawaahidi ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao muhimu ya Bunge.
- 10. Mheshimiwa Spika**, Kwa namna ya pekee natoa pole kwako na Waheshimiwa Wabunge pamoja na familia kwa kuondokewa na waliokuwa Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani (CCM) na Mheshimiwa Dr. Elly Marko Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA). Namuomba Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahala pema peponi, **Amina**.
- 11. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara yangu imeondokewa na watumishi na askari wa Wanyamapori ambao wamepoteza maisha wakati wakitekeleza majukumu yao. Aidha, kutokana na majanga na maafa hasa tetemeko la Kagera na mafuriko katika maeneo mbalimbali, Watanzania wenzetu wamepoteza maisha, kujeruhiwa na kupoteza mali. Vilevile, wanafunzi 32,

walimu wawili na dereva wa Shule ya Msingi Lucky Vicent waliofariki katika ajali iliyotokea tarehe 6 Mei, 2017 wilayani Karatu. Naungana na Watanzania wenzangu kumuomba Mwenyezi Mungu awajaalie nafuu waliopata majeraha na awapumzishe peponi wote waliopoteza maisha. Pia natoa pole kwa familia na wote walioguswa na matukio haya.

3.0 MAJUKUMU YA WIZARA

- 12. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imepewa jukumu la kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili na malikale, kuendeleza ufugaji nyuki na utalii. Wizara inazingatia sheria; kuimarisha mifumo ya usimamizi na uendeshaji; ukusanyaji mapato; maendeleo na ustawi wa wananchi; na utekelezaji wa mikataba ya kimataifa yenye mtizamo chanya katika uhifadhi. Jukumu hili linatekelezwa kwa kushirikiana na wadau wakiwemo wananchi, sekta binafsi, asasi za kiraia, na washirika wa maendeleo. Pamoja na Hotuba yangu ya Bajeti nimeambatisha Sheria zetu zinazotuongoza katika kuhifadhi, kulinda na kuendeleza misitu, wanyamapori, malikale na utalii pamoja na majarida muhimu yanayotoa elimu na ufahamu wa maliasili zetu.
- 13. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda Mrefu (2011/2012 – 2024/2025) na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021); Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015; Hotuba ya Mheshimiwa Dr. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2016 na maagizo mbalimbali ya Serikali.
- 14. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaundwa na Idara za Misitu na Nyuki; Wanyamapori; Mambo ya Kale, na Idara ya Utalii. Aidha, zipo Idara mbili na vitengo sita vya Uratibu. Mashirika chini ya Wizara ni pamoja na; Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Shirika la Makumbusho ya Taifa (NMT). Aidha, Mamlaka zilizo chini ya Wizara ni pamoja na;

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA).

15. Mheshimiwa Spika, Wizara inajumuisha pia Wakala za Mbegu za Miti (TTSA), Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT); Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI); na Bodi ya Utalii Tanzania (TB). Pamoja na Taasisi hizo, Wizara inasimamia vyuo vinavyotoa mafunzo na kufanya utafiti katika fani za maliasili na utalii. Vyuo hivyo ni Chuo cha Afrika cha Usimamizi wa Wanyamapori (CAWM - Mweka), Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi (PWTI), Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi kwa Jamii, Likuyu Sekamaganga (CBCTC), Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI), Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) – Moshi na Chuo cha Ufugaji Nyuki (BTI)- Tabora. Wizara pia inayo mifuko ya uhifadhi ambayo ni Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania (TWPF), Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) na Mfuko wa Mambo ya Kale (AF).

4.0 UMUHIMU WA MALIASILI, MALIKALE NA UTALII

16. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maliasili, Malikale na Utalii ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii ya Tanzania. Sekta hii huchangia kuzalisha ajira na mapato ya Serikali, uhifadhi wa mazingira na kutunza mifumo ikolojia kwa manufaa ya binadamu na viumbe wengine. Aidha, Sekta hii ni muhimu kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia, biashara, viwanda na uhifadhi wa mila na desturi za Mtanzania.

17. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi hasa katika sekta za kilimo, mawasiliano, miundombinu, usafirishaji, burudani na uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa watalii. Aidha, katika mwaka 2016/2017 sekta ya utalii imetoa ajira takriban 500,000 za moja kwa moja. Vilevile, zaidi ya watu wengine milioni moja wamejiajiri katika sekta hii kwa namna mbalimbali. Sekta hii pia inachangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa na kulipatia Taifa wastani wa asilimia 25 ya fedha zote za kigeni.

18. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania imejaaliwa kuwa na maeneo makubwa ya kuvutia ya uhifadhi wa wanyamapori. Maeneo hayo yana aina tofauti ya wanyamapori ambao wamekuwa ni kivutio kikubwa cha Utalii. Takriban asilimia 90 ya watalii wanaoingia nchini wanakuja kwa lengo la kuona vivutio vya wanyamapori katika hifadhi za Taifa na kufanya uwindaji wa kitalii katika mapori ya akiba. Aidha, wanyamapori wana mchango mkubwa katika kuweka mizania ya bioanuwai (mimea na wanyama) na kuzuia mtawanyiko wa vimelea hatari vya magonjwa.
19. **Mheshimiwa Spika**, Misitu ni moja ya nguzo muhimu za maendeleo ya uchumi kutokana na mchango wake kwenye Pato la Taifa. Rasilimali za misitu na nyuki zinakadiriwa kuchangia asilimia 3.9 (mwaka 2016) kwenye Pato la Taifa. Sekta ya Misitu inachangia kwa takriban asilimia tatu ya ajira rasmi nchini na asilimila sita ya ajira islyo rasmi (watu milioni tatu). Aidha, misitu inachangia zaidi ya asilimia 90 ya nishati ya kupikia inayotumika nchini ambayo inatokana na kuni na mkaa. Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, ukuaji wa shughuli za misitu kwa mwaka 2016 umeongezeka hadi asilimia 3.4 kutoka asilimia 2.6 (mwaka 2015).
20. **Mheshimiwa Spika**, Misitu inahifadhi bioanuai, kurekebisha tabia nchi (hali ya hewa na mvua), kuhifadhi udongo na kutunza vyanzo vya maji kwa matumizi mbalimbali. Mathalan maji huchangia takriban asilimia 60 ya umeme wote unaozalishwa nchini. Aidha, uharibifu wa misitu huleta kupungua kwa maji katika mito kama Malagarasi na Ruaha, kuhatarisha uendelezaji wa miradi ya umeme (kama Stieglers Gorge), hifadhi za Taifa kama vile Ruaha na miradi mikubwa ya umwagiliaji. Vile vile, ufugaji nyuki unaofanyika katika misitu una mchango mkubwa katika uhifadhi wa misitu, ukuaji wa uchumi, lishe, tiba na huduma ya uchavushaji wa mazao.
21. **Mheshimiwa Spika**, Kupitia sekta ya Malikale, wananchi wanajifunza kuhusu mifumo ya kihistoria kama kilimo cha umwagiliaji na kufua zana za chuma. Maeneo haya na aina za masalia ya malikale zinazopatikana humo

ni muhimu sana katika kuhifadhi kumbukumbu na kulitambulisha taifa ndani na nje ya nchi.

22. Mheshimiwa Spika, Kutohana na umuhimu wa Wizara hii kiuchumi, kijamii na kikolojia, natoa rai kwa wananchi na viongozi wa ngazi zote kutambua wajibu wao wa kulinda, kuendeleza na kutumia maliasili na malikale zilizopo kwa njia endelevu na kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

5.0 UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 NA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

23. Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe taarifa ya Utekelezaji wa kazi za Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

24. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017 Bunge lako tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi 135,797,787,000 ambapo shilingi 118,051,105,000 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 17,746,682,000 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

25. Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka 2016/2017 umezingatia vipaumbele sita ambavyo ni kuhifadhi maliasili na malikale; kuendeleza sekta ya utalii; kuboresha mifumo ya ukusanyaji maduhuli; kuwashirikisha wadau; kujenga uwezo wa Wizara; na kudumisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu katika Hotuba hii umefafanuliwa kwa kila sekta ndogo.

5.1 Sekta Ndogo ya Wanyamapor

26. Mheshimiwa Spika, Jukumu kuu la Sekta ndogo ya Wanyamapor ni uhifadhi wa wanyamapor ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Utekelezaji wa jukumu hilo

unazingatia Sera ya Wanyamapor ya 2007 na Sheria ya kuhifadhi wanyamapor Sura 283.

27. Mheshimiwa Spika, Matumizi ya maeneo ya Wanyamapor yamegawanyika katika makundi ya uvunaji na yasiyo ya uvunaji. Matumizi ya uvunaji yanahusisha biashara ya wanyamapor hai na uwindaji ambao hufanyika kwenye Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu, maeneo ya Jumuuya za Hifadhi za Wanyamapor na maeneo ya wazi. Matumizi yasiyo ya uvunaji yanahusisha utalii wa picha, kuona, kupanda mlima, utafiti na mafunzo. Matumizi hayo hufanyika ndani ya hifadhi za taifa, Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu, Maeneo ya Jumuuya za Hifadhi za Wanyamapor na maeneo mengine yenye wanyamapor.

28. Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya wanyamapor inajumuisha Idara ya Wanyamapor, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapor Tanzania, Shirika la Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapor Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapor Tanzania, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapor Mweka, Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapor Pasiansi na Kituo cha Elimu ya Uhifadhi kwa Jamii, Likuyu-Sekamaganga.

5.1.1 Idara ya Wanyamapor

29. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Wizara iliendelea na mapitio ya sheria zinazosimamia sekta ndogo ya wanyamapor. Kazi ya kufanya uchambuzi wa maeneo yanayohitaji marekebisho katika Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapor Sura 283 imekamilika. Taratibu za kufanya marekebisho ya Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282; Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro Sura 284; Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapor Tanzania Sura 260; na Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapor, Mweka Sura 549 zinaendelea. Aidha, maandalizi ya Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapor Tanzania yanaendelea.

30. Mheshimiwa Spika, Kanuni za Uchimbaji wa Madini Ndani ya Mapori ya Akiba zimekamilika na kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa Tangazo Na. 88 la tarehe 10 Machi, 2017. Aidha, kanuni za Jeshi Usu, Maeneo Kinga (buffer zones), Shoroba na Mtawanyiko wa Wanyamapori zinaandaliwa.

31. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya wanyamapori na mazao ya misitu kwa kuanzisha Kikosikazi cha Kudhibiti Uhalifu wa Kijinai katika Tasnia ya Misitu na Wanyamapori (Wildlife and Forest Crimes Task Team). Kikosi hiki kinateneza operesheni za kiintelijensia na kuratibu kazi zinazofanyika kwenye kanda za kiikolojia nchini.

32. Mheshimiwa Spika, Juhudi za kulinda wanyamapori dhidi ya ujangili na biashara haramu zimeendelea kuimarishwa. Katika mwaka 2016/2017, Wizara (Idara ya Wanyamapori, TANAPA, NCAA na TAWA) iliendesha jumla ya siku-doria 349,102 ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Matokeo ya doria zilizofanyika ni kukamatwa kwa jumla ya watuhumiwa 7,085 kwa makosa mbalimbali. Meno ya tembo 129 na vipande 95 vyenye uzito wa jumla ya kilo 810.03 vilikamatwa.

33. Vielelezo vilivyokamatwa kuhusiana na matukio ya ujangili ni pamoja na silaha za kivita 48, silaha za kiraia 150, risasi 1,058, magobore 406, silaha za jadi 22,307 na roda 120,538. Vielelezo vingine ni pikipiki 189, baiskeli 214, magari 20, ng'ombe 79,831 na samaki kilo 4,043.

34. Mheshimiwa Spika, Jumla ya kesi 2,097 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali na kesi 802 zilimalizika. Kesi 262 zenye watuhumiwa 472 zilimalizika kwa wahusika kufungwa jela jumla ya miezi 42,153 na kesi 43 zenye watuhumiwa 79 zilimalizika kwa wahusika kuachiwa huru. Kesi 276 zilimalizika kwa watuhumiwa 469 kulipa faini ya jumla ya shilingi milioni 452.1. Aidha, kesi 966 zinaendelea katika Mahakama mbalimbali nchini.

35. Mheshimiwa Spika, Hatua mbalimbali zimechukuliwa katika kuimarisha doria dhidi ya ujangili na biashara haramu ya nyara za Serikali kwa kuanzisha kikosi kazi maalum, kutumia teknolojia ya ndege zisizo na rubani (drones) na mbwa maalum wa kunusa (sniffer dogs). Katika mwaka 2016/2017, doria maalum za kiintelejensi zilifanyika katika kanda zote za kiikolojia na kubaini wahalifu 906 wa ngazi mbalimbali za ujangili ambapo 384 wamekamatwa na kufikishwa mahakamani.

Taarifa za kiintelejensi zinaonesha kuwa majangili wakubwa sasa wanakimbilia nje ya nchi kujificha. Aidha, majangili wengine wanasalimisha silaha kwa hiari yao. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wajumbe wa kikosi kazi, Jeshi la Polisi, kamati za ulinzi na usalama za wilaya na mikoa, na wananchi waliota ushirikiano katika kufanikisha kazi hii maalum.

36. Mheshimiwa Spika, Dhana ya ushirikishaji jamii katika uhifadhi wanyamaporì ilianzishwa kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanashiriki katika uhifadhi na kunufaika kwa mujibu wa Sera ya Wanyamaporì ya mwaka 2007. Hadi Machi 2017, jumla ya WMAs 38 zimeanzishwa ambapo 22 zenye ukubwa wa jumla ya kilometra za mraba 30,623 zimetangazwa katika Gazeti la Serikali kwa nyakati tofauti. Kwa mfano, Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamaporì ya Ngorongo, Utete na Mwaseni (JUHWANGUMWA) iliyoko Wilayani Rufiji ilitangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 204 la tarehe 01 Julai 2016.

Aidha, WMAs 16 zipo katika hatua mbalimbali za uanzishwaji ambazo zinajumuisha Ziwa Natron, Mpimbwe, Yaeda Chini, Mchimalu, Ndonda, ISAWIMA na Ubende. Vilevile, Wizara ilifanya mikutano ya uhamasishaji kwenye WMAs za Ziwa Natron katika Wilaya ya Longido na Mpimbwe katika Wilaya ya Mlele.

37. Mheshimiwa Spika, Kupitia WMAs zilizoanzishwa, jamii kwenye maeneo husika zimenufaika kwa kupata ajira, elimu, miradi ya kijamii na kuungeza kipato. Pamoja na mafanikio

hayo, baadhi ya WMAs zimekuwa na migogoro minge. Chimbuko la migogoro hiyo ni mgawanyo wa mapato, kutokuheshimu katiba, mikataba na wawekezaji, na ugomvi wa mipaka. Wizara kwa kushirikiana na Kamati za Wilaya za Ushauri wa Masuala ya Maliasili na wadau wengine imeendelea kufuatilia ustawi wa WMAs kwa kuzijengea uwezo na kutatua migogoro ya usimamizi. WMAs zenye migogoro ambayo inaendelea kutatuliwa ni pamoja na Mbomipa, Ikona, Burunge na Ngarambe -Tapika.

38. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuwalinda wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu. Hadi Machi 2017, Wizara imeendesha siku-doria 4,089 kwenye Wilaya 39 (Geita, Illemela, Magu, Misungwi, Muleba, Nyamagana, Nyang'hwale, Kondoa, Chemba, Rombo, Songwe, Igunga, Manyoni, Uyui, Nzega, Mwanga, Monduli, Tunduru, Iringa, Lindi, Sengerema, Ngara, Mbarali, Mbinga, Masasi, Nanyumbu, Nachingwea, Serengeti, Bunda, Kyerwa, Kilolo, Karatu, Bahi, Ikungi, Simanjiro, Kilombero, Mbulu, na Sihala).

39. Mheshimiwa Spika, Jumla ya shilingi milioni 567.5 zimelipwa kwa wananchi ambapo shilingi milioni 505.4 ni kifuta jasho na shilingi millioni 62.6 kifuta machozi. Malipo hayo yamefanyika kwa wananchi wa wilaya 27 ambazo ni Mvomero, Itigi, Iringa, Manyoni, Singida, Magu, Mbinga, Tunduru, Wanging'ombe, Kilosa, Chemba, Morogoro, Dodoma, Newala, Nachingwea, Bunda, Namtumbo, Masasi, Monduli, Babati, Kilombero, Chamwino, Simanjiro, Itilima, Moshi, Busega, na Mbulu.

40. Pamoja na malipo kufanyika, Wizara imeendelea kupokea maombi mapya ya kifuta jasho na kifuta machozi kutoka wilaya mbalimbali. Uhakiki wa matukio unaendelea kufanyika mara taarifa zinapopokelewa na baadaye wananchi kulipwa kwa mujibu wa sheria. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu ya jinsi ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwemo pilipili, madebe, kufuga nyuki na matumizi ya ndege zisizo na rubani.

41. Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kifuta Machozi na Kifuta Jasho za mwaka 2011 zinaelekeza wananchi kulipwa kiasi cha fedha cha kuwafariji kama kifuta machozi endapo wanyamapori watasababisha kifo au majeraha kwa binadamu na kifuta jasho kwa uharibifu wa mazao na mifugo. Aidha, kanuni zimeelekeza kufanyika uhakiki wa matukio husika kabla ya kuwalipa waathirika.

42. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendesha mafunzo kwa watumishi 661 kuhusu ukakamavu, uongozi na ukusanyaaji wa taarifa za kiintelijensia zinazohusu uwindaji haramu na biashara haramu ya nyara za Serikali. Watumishi hao ni kutoka Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapor Tanzania (139), Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (388), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (117) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (17).

5.1.2 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapor

43. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapor Tanzania (TWPF) ulianzishwa chini ya Sheria Sura 283. Lengo la Mfuko ni kuwezesha uhifadhi wa wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mfuko ulitumia shilingi bilioni 6.7 kuwezesha utekelezaji wa kazi za kiuhifadhi na miradi ya maendeleo.

44. Mheshimiwa Spika, Kazi zilizotekeliza ni pamoja na doria, kukiwezesha Kikosi Kazi Maalum cha kupambana na ujangili (Wildlife and Forest Crime Task Team); kuwezesha mapitio ya kanuni mbalimbali, usimamizi wa WMAs na uhakiki wa madhara yanayosababishwa na wanyamapor wakali na waharibifu. Aidha, Mfuko umewezesha kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathirika kutokana na madhara ya wanyamapor wakali na waharibifu; uhamasishaji na utoaji elimu ya uhifadhi; utekelezaji wa mikataba ya kimataifa; uhifadhi wa spishi ya chura wa Kihansi na uendeshaji wa bustani za wanyamapor za Ikulu, Tabora na Ruhila (Songea).

45. Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya wanyamapori inakabiliwa na changamoto za kuendelea kuwepo ujangili; uvamizi wa mifugo katika hifadhi; kuendelea kuwepo migogoro ya mipaka baina ya wananchi na hifadhi; upungufu wa miundombinu muhimu katika hifadhi zilizopo ukanda wa Magharibi na Kusini; upungufu wa rasilimali watu na fedha, vitendeakazi, na teknolojia duni. Aidha, kumekuwa na ongezeko la silaha haramu za kivita; uelewa mdogo wa jamii kuhusu manufaa ya uhifadhi wa wanyamapori; na mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa wanyamapori; ongezeko la wakazi na mifugo ndani ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro; na ongezeko la muingiliano katika shughuli za kibinadamu na wanyamapori.

46. Mheshimiwa Spika, Wizara inakabiliana na changamoto hizo kwa kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo kuanzisha mfumo wa Jeshi Usu; kuimarisha mbinu za kupambana na ujangili; kuboresha miundombinu kwa kufungua na kukarabati barabara za ndani na nje ya hifadhi, viwanja vya ndege, nyumba za watumishi, na vituo vya taarifa kwa watalii; na kuongeza watumishi na vitendea kazi. Aidha, Wizara, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kutoa elimu ya uhifadhi kwa umma na kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa maduhuli.

47. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/2018, Wizara inatarajia kupitia Kanuni tatu za nyara, uwindaji wa kitalii na usimamizi wa mkatuba wa CITES; kuhakiki na kukusanya nyara za Serikali zilizopo kwenye vituo vya Polisi, Halmashauri za Wilaya na Mahakama. Aidha, itakarabati ghala la nyara "Ivory Room" na kuweka vifaa vya kisasa vya ulinzi.

48. Mheshimiwa Spika, Wizara pia, itaendelea kufuatilia na kutoa elimu ya ushiriki wa wananchi katika usimamizi wa maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapor (WMAs) na kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathirika na wanyamapor wakali na waharibifu. Kikosi kazi maalum cha kupambana na ujangili kitawezeshwa kutekeleza majukumu yake. Aidha, Wizara itaendelea na

juhudii za kukamilisha uanzishaji wa mapori ya akiba ya Kipindimbi (Nachingwea), Mavuji (Kilwa), Litumbandyosi (Mbinga) na Gezamasoe (Songea); na kutatua migogoro katii ya mapori ya akiba, WMAs na wananchi.

5.1.3 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania

49. **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ilianzishwa mwaka 1959 kwa Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282. Shirika limepewa dhamana ya kusimamia na kuendeleza maeneo yaliyoanzishwa kisheria kuwa Hifadhi za Taifa. Aidha, Shirika linasimamia hifadhi 16 zenyenye jumla ya kilometra za mraba 57,365.8.
50. **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuendesha doria dhidi ya ujangili, jitihada zilielekezwa katika kupunguza na kuepusha migogoro kwenye maeneo ya hifadhi. Shirika linaendelea na kazi ya kuweka **beacons** katika mipaka ya hifadhi zake. Jumla ya **beacons** 1,518 katii ya 2,171 sawa na asilimia 70 tayari zimebekwa.
51. **Mheshimiwa Spika**, Jumla ya kilometra 2,571.2 za barabara zilizopo katika hifadhi za taifa zimekarabatiwa kwa kuwekewa changarawe (morrum) na kuimarisha mifumo ya kuondoa maji. Aidha, barabara katika hifadhi sita zimeimarishwa kwa kuongeza jumla ya makaravati 27. Vilevile, njia za miguu zenyenye urefu wa kilometra 143.5 zimekarabatiwa katika Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro, Udzungwa na Arusha.
52. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Shirika limeboresha ukusanyaji wa mapato kwa kuendelea kutumia mfumo wa kieletroniki. Jumla ya shilingi bilioni 173.2 ikiwa ni asilimia 94.5 ya lengo la mwaka zimekusanywa. Aidha, Shirika limechangia shilingi bilioni 4.9 kwa ajili ya kuendeleza utalii ikiwa ni asilimia tatu ya mapato ghafi kwa mujibu wa sheria.
53. **Mheshimiwa Spika**, Bidhaa mpya za utalii za ‘canopy walkway’ (Hifadhi ya Manyara), ‘paragliding’ (Hifadhi ya Taifa

Kilimanjaro) na kuendesha balskeli (Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro na Arusha) zimeanzishwa na kutangazwa. Aidha, utalii wa kupiga kambi katika kasoko (kreta) ya Kibo umefunguliwa na unaendelea kutangazwa.

54. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Shirika limenunua magari 50; silaha 85; mitambo ya kutengeneza barabara ('roller compactor, 'water bowser' na lori); gari la wagonjwa (kwa ajili ya Hifadhi ya Kilimanjaro), na kuweka mfumo wa kisasa wa mawasiliano ya redio za upepo. Aidha, Shirika limesanifu jengo la kituo cha kisasa cha kutoa habari kwa wageni katika Hifadhi ya Taifa Arusha; kujenga jengo la mapokezi katika uwanja wa ndege Seronera; malango mawili na daraja; mabanda mawili ya kulaza wageni (Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara); na vyoo 17 katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro. Vilevile, Shirika limejenga nyumba 16 za watumishi katika hifadhi saba.

55. Mheshimiwa Spika, Shirika limechangia shughuli za maendeleo ya jamii kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi. Miradi ya kielimu ni majengo ya maktaba mbili, maabara tano, madarasa 12, ofisi tisa, mabweni mawili, nyumba za walimu tatu na madawati 13,250. Aidha, miradi ya kiafya ni ujenzi wa nyumba tatu za wauguzi na zahanati mbili. Kwa upande wa huduma za maji Shirika limechangia kuchimba malambo mawili, kununua mtambo wa kusukuma maji kwa kutumia nishati ya upepo na kuchimba kisima kirefu kimoja. Vilevile, Shirika limewezesha vikundi 20 vya wavuvi kupata jumla ya taa 200 zinazotumia nishati ya juu.

56. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, kazi za kipaumbele zitakazoteklezwa ni pamoja na kukamilisha mapitio ya Sheria, kuimarisha usalama na kudhibiti ujangili hasa wa tembo na faru ndani na nje ya Hifadhi za Taifa. Shirika litaendeleza utaratibu wa mabadiliko ya mfumo wa Jeshi Usu kwa kutoa mafunzo kwa takriban asilimia 60 ya askari waliobakia. Kazi nyingine ni kuendelea kutatua migogoro ya mipaka katika Hifadhi za Taifa Arusha, Ruaha, Saadani, Mahale na Serengeti, na kukamilisha zoezi la uwekaji **beacons** katika mipaka ya hifadhi hizo.

57. **Mheshimiwa Spika**, Ujenzi wa vituo vya kutolea taarifa katika Hifadhi za Taifa Serengeti na Udzungwa utakamilishwa; na ujenzi wa kituo cha taarifa za utalii uthaanza katika Hifadhi ya Taifa Arusha. Aidha, Shirika litajenga vyoo 11 na vituo vitatu vya kupumzikia wageni na mabanda ya wabeba mizigo katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro; hosteli ya wanafunzi katika Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara; na nyumba ya malazi nafuu kwa ajili ya watalii katika Hifadhi ya Taifa Kitulo. Vilevile, itajenga nyumba 30 za watumishi, kukarabati nyumba sita na kujenga ofisi saba katika hifadhi mbalimbali.
58. **Mheshimiwa Spika**, Jumla ya kilometa 3,000 za barabara zitafanyiwa ukarabati katika hifadhi mbalimbali. Daraja moja litakalounganisha Hifadhi ya Taifa Mahale na mji wa Kigoma litajengwa. Shirika litajiimarisha katika shughuli za utangazaji wa vivutio vya utalii na kutangaza kuititia vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na wadau. Shirika pia litaendelea kuweka mabango kwenye viwanja vya ndege na barabara kuu. Mabango hayo yatakuwa na ujumbe wa aina mbalimbali wa kutangaza vivutio vilivyopo katika Hifadhi za Taifa.
59. **Mheshimiwa Spika**, Shirika litaendelea kutekeleza miradi ya ujirani mwema yenye ghamama ya shilingi bilioni 1.1 kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi. Miradi itakayotekelawa itahusu elimu ambapo vyumba vya madarasa 30, nyumba sita za walimu, bwalo la chakula, miradi ya afya (nyumba mbili, vyoo viwili na zahanati moja) vitajengwa. Miradi mingine itakayotekelawa ni kuanzisha vitalu viwili vya miche ya miti, kuchimba kisima cha maji, kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji viwili, kujenga Kituo cha Polisi, na kuwezesha vikundi viwili vya Benki ya Ushirika ya Jamii kujiedhesha.
60. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/2018, TANAPA inatarajia kupata watalii 930,583 ambao watakanza hifadhini kwa siku 1,620,225. Kutokana na watalii hao, Shirika linakadiria kukusanya shilingi bilioni 205.1 Aidha, makadirio ya matumizi

ni shilingi bilioni 142.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 25.3 kwa miradi ya maendeleo.

5.1.4 Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro

61. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) inasimamia eneo la Kilometa za mraba 8,292. Eneo hilo lillianzishwa kwa Sheria Sura 284, kwa ajili ya kuhifadhi, kuendeleza utalii na wafugaji wenyeji. Idadi ya wenyeji imeongezeka kutoka takriban wakazi 8,000 mwaka 1959 hadi zaidi ya wakazi 90,000 mwaka 2016. Idadi ya makazi ya kudumu nayo imeongezeka sambamba na ongezeko la wakazi wa eneo hilo.

62. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, juhudzi za kupunguza migogoro ya ardhi zilielekezwa katika uwekaji **beacons** kwenye mpaka ya Hifadhi. Zoezi hilo liliifanyika kwa kushirikiana na vijiji husika; Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya za Karatu; Ngorongoro na Monduli; na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kazi hiyo imekamilika kwa asilimia 70 ambapo **beacons** 387 zimebekwa kwenye mpaka wa Hifadhi na maeneo ya Oldeani, Karatu, Mbulumbulu, Lositete, Piyaya, Ndutu na Lemuta.

63. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imenunua magari nane ya doria, imekamilisha ujenzi wa kituo cha doria cha Masamburai, na inaendelea na ujenzi wa vituo vya Mang'ola Juu, Bonde la faru na Engaruka. Aidha, Mamlaka inakamilisha ujenzi wa jengo la kitega uchumi katika Jiji la Arusha na jengo la makumbusho katika Bonde la Olduvai. Vilevile, ukarabati wa kambi ya Mary Leakey umekamilika.

64. Mheshimiwa Spika, Hadi mwezi Machi 2017, jamii inayozunguka Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro iliwezeshwa kwa kugharamia ujenzi wa nyumba ya walimu yenye uwezo wa kuishi familia mbili katika Shule ya Msingi Makao (Meatu); madarasa mawili na jengo la ofisi ya Shule ya Sekondari Lake Natron Monic (Ngorongoro); na nyumba ya waalimu na kituo cha watoto yatima-Ebenezer (Ngorongoro). Vilevile, Mamlaka imechangia shughuli za maendeleo ya Shule ya

Wasichana Slahamo (Karatu). Mamlaka pia imenunua madawati 2,000 kwa ajili ya shule za msingi za Tarafa ya Ngorongoro.

65. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeanzisha mfumo mpya wa kielektroniki wa kukusanya maduhuli unaoitwa "NCAA Safari Portal" wenyewe ufanisi zaidi. Mfumo huo umeondoa adha kwa wadau na mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali. Katika bajeti ya mwaka 2016/2017, Mamlaka ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 82.1. Hadi kufikia Machi 2017, Mamlaka ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 81.9 sawa na asilimia 99.6 ya makadirio. Mapato haya yametokana na watalii 487,840 walitetembelea hifadhi ambapo watalii 298,458 ni wa kutoka nje ya nchi na 189,382 ni wa ndani. Kutokana na mapato hayo Mamlaka imechangia shilingi bilioni 10.2 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni asilimia 15 ya mapato ghafi na shilingi bilioni 2.4 zikiwa ni asilimia 3 ya mapato ghafi kwa ajili ya maendeleo ya utalii.

66. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Mamlaka itaendelea kulinda maliasili dhidi ya ujangili kwa kuendesha siku-doria 54,780 na kutekeleza mkakati wa usalama wa chakula kwa wenyeji. Aidha, itaendelea kutekeleza mradi wa maji kwenye eneo la Oletakule, Mbitin na Olduvai. Vilevile, Mamlaka itaendelea kutekeleza agizo la Waziri Mkuu la tarehe 6 Desemba 2016 kwa kuhesabu wakazi na mifugo; kubaini wakazi halali ili kuwapatia vitambulisho; kuweka mifugo alama na kuwapatia wananchi maji na chumvi kwa ajili ya mifugo.

67. Mheshimiwa Spika, Mamlaka itafanya mapitio ya mradi wa kuboresha mifugo Kakesio (IRAMAT) ikishirikiana na Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), na kuendelea kutoa huduma ya chanjo kwa mifugo. Aidha, Mamlaka itakamilisha majadiliano na wenyeji kuhusu kuimarisha uhifadhi ambayo yameanza toka Mei 2016 kwa kushirikiana na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro na Mkoa wa Arusha. Vilevile, Mamlaka itaendelea kutoa huduma ya elimu na afya kwa wenyeji.

68. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Mamlaka itaendelea kuweka *beacons* kwenye mpaka wa hifadhi; kujenga kituo cha askari maeneo ya Nasera Rock; kununua vitendea kazi kama mahema, sare, "GPS" na gari moja kwa ajili ya kikosi cha mwitikio wa haraka (rapid response team). Mamlaka pia, itapeleka watumishi 300 waliobaki kwenye mafunzo ya jeshi usu.

69. Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea kushirikiana na wananchi kuzuia wanyamapori wakali na waharibifu kwenye Wilaya za Karatu na Monduli kuititia mpango wa ujirani mwema. Aidha, Mamlaka itaendelea kulinda maeneo nyeti ya uhifadhi ya kasoko (kreta), msitu wa nyanda za juu kaskazini, ardhioevu za Ndutu na maeneo ya malikale.

70. Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea kuboresha barabara za ndani ya kasoko ya Ngorongoro, barabara kuu kutoka lango la Loduare hadi mpaka wa Hifadhi ya Taifa Serengeti na barabara nyingine ndani ya hifadhi. Aidha, Mamlaka itaendelea na majadiliano na UNESCO ili itoe kibali cha kuifanya marekebisho makubwa barabara ya Loduare-Golini bila kuathiri matakwa ya kiikolojia.

71. Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na muingiliano mkubwa kati ya binadamu na wanyamapori, na hivyo kuathiri uhifadhi, maisha ya wenyeji na utalii. Athari hizo ni pamoja na kuongezeka kwa magonjwa yanayotokana na muingiliano kati ya binadamu, wanyamapori na mifugo; matukio ya watu na mifugo kujeruhija na kuuawa na wanyamapori. Kutokana na hali hiyo, Mamlaka itafanya mapitio ya Mpango wa Kuendesha, Kusimamia na Kuendeleza Hifadhi.

72. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Mamlaka inakadiria kukusanya jumla ya bilioni 88.3 kutokana na watalii 631,520 wanaotarajiwa kutembelea Hifadhi. Kati ya hao, watalii 391,397 ni kutoka nje na 240,123 ni kutoka ndani.

5.1.5 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania

73. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA) ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 135 la tarehe 9 Mei 2014 chini ya Kifungu cha 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Sura 283 ikisomwa pamoja na marekebisho yake yaliyotolewa katika Tangazo la Serikali Na. 20 la tarehe 23 Januari 2015 na kuanza kazi rasmi tarehe 1 Julai, 2016.

74. Mheshimiwa Spika, Jukumu la Mamlaka ni kusimamia uhifadhi wa wanyamapori kwenye Mapori ya Akiba 28, Mapori Tengefu 42 na maeneo ya wazi yenye mazalia ya wanyamapori, mtawanyiko na shoroba. Maeneo haya yana jumla ya kilometra za mraba 222,031. Aidha, Mamlaka inashirikiana na jamii katika kusimamia maeneo 22 ya jumuiya za hifadhi za wanyamapori yenye ukubwa wa kilometra za mraba 30,623 na maeneo manne ya ardhiorevu yenye umuhimu wa kimataifa (Ramsar Sites) yenye ukubwa wa kilometra za mraba 48,684.

75. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 Mamlaka imefanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 28.8 ikiwa ni asilimia 78.48 ya lengo la mwaka ambalo ni shilingi bilioni 36.7. Hadi kufikia Machi 2017 jumla ya watalii 47,272 walitembelea maeneo ya vivutio vinavyosimamiwa na Mamlaka sawa na asilimia 98 ya lengo la kupokea watalii 48,200 kwa mwaka 2016/2017 ambapo watalii wa picha walikuwa 46,781 na uwindaji wa kitalii walikuwa 491.

76. Mheshimiwa Spika, Mamlaka kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ilifanikiwa kubaini mtandao wa ujangili wa kakakuona na kuwakamata watuhumiwa wanne mjini Morogoro kwa kupatikana na magamba ya kakakuona wanaokadirwa kufikia 670 wenyewe thamani ya shilingi bilioni 1.4. Aidha, kwa kushirikiana na INTERPOL pamoja na "Lusaka Agreement Task Force," Mamlaka imewakamata vinara wa ujangili kutoka mataifa ya Uganda, China na Austria. Katika

matukio hayo wanyamapori hai waliokamatwa ni pamoja na kobe 342. Watuhumiwa hao wamefikishwa katika vyombo nya sheria hapa nchini. Vilevile, katika ukaguzi uliofanyika kwenye vituo nya mipakani, bandarini na viwanja nya ndege raia wa kigeni 29 walikamatwa kwa makosa ya kukusudia kutorosha nyara za Serikali nje ya nchi. Watuhumiwa hao walikiri makosa yao na kulipa faini jumla ya shilingi milioni 43.

77. Mheshimiwa Spika, Ili kuepusha madhara yanayoweza kusababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu, jumla ya siku-doria 935 zilifanyika katika maeneo mbalimbali. Kutokana na doria hizo Mamlaka illazimika kuua jumla ya wanyamapori 31 (tembo 2, fisi 10, mamba 3, nyani 2, simba 3, kiboko 3, nyati 5 na tumbili 3) ili kuwanusuru wananchi na mali zao.

78. Mheshimiwa Spika, Ili kupunguza migogoro ya mipaka kati ya wananchi na mapori ya akiba, Mamlaka imesimika jumla ya **beacons** 3,493 katika mipaka inayozunguka mapori ya akiba. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 33 ya lengo la **beacons** 10,710.

79. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeanzisha kikosi maalum cha mwitikio wa haraka cha kupambana na matukio ya ujangili (Rapid Response Team). Kikosi hicho kimepatiwa mafunzo maalum na kimeanza kazi katika Mapori ya Akiba Rungwa, Kizigo, Muheesi, Rukwa, Lwafi, Lukwati na Piti. Aidha, kikosi maalum cha mbwa wa kunusa (sniffer dogs) kimeundwa na kuanza kazi katika viwanja nya ndege na bandari. Hadi Machi 2017 Kikosi kimebaini matukio 21 yenye watuhumiwa 34 waliokuwa wanasafirisha nyara za Serikali kinyume cha sheria. Nyara hizo ni vipande 81 nya meno ya tembo vyenye uzito wa jumla ya kilo 216.90. Nyara nyingine ni meno tisa ya kiboko, nyama ya nyati, mkia wa tembo na ngozi ya nungunungu.

80. Mheshimiwa Spika, Tarehe 19 Mei, 2016 Wizara ilisitisha kwa miaka mitatu utoaji wa vibali nya kukamata na kusafirisha wanyamapori hai nje ya nchi kutokana na

kubainika uwepo wa ukiukwaji mkubwa wa sheria na taratibu. Aidha, tamko rasmi la Serikali la usitishwaji huo lilitolewa katika Bunge lako Tukufu tarehe 25 Mei, 2016. Wanyamapori hai kutoka Tanzania wamekuwa wakikamatwa katika nchi mbalimbali za ughaibuni wakiwa wametoroshwa. Lengo la katazo hilo ni kutoa fursa kwa Wizara kufanya mapitio ya taratibu za biashara hiyo ili kukidhi mahitaji ya wadau na maslahi mapana ya Taifa.

81. Mheshimiwa Spika, Kufuatia katazo hilo, Wizara imefanya tathmini ya wanyamapori hai waliopo kwenye mazizi ya wafanyabiashara na kuhakiki vibali viliviyotolewa na thamani yake; idadi ya wanyamapori waliopo na idadi ya waliouzwa nje ya nchi. Uhakiki ulihusisha mazizi 92, bustani za wanyamapori 17, maeneo ya uzalishaji 18 na ranchi 3 zenyе jumla ya wanyamapori hai 29,730 wenye thamani ya Dola za Marekani 1,602,632. Wanyamapori hao ni wadudu (6,629), ndege (8,961), vyura (1,566), mijusi/kobe/hyoka (12,132) na mamalia (442). Tathmini hiyo inalenga kutoa kifuta jasho kwa wafanyabiashara walioathirika na katazo hilo.

82. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeweka mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto zilizopo. Mikakati hiyo inahusu kubadili mfumo wa kiutendaji kwenda Jeshi Usu; Kuimarisha ushirikiano na wadau katika ulinzi wa rasilimali za wanyamapori; Kuimarisha miundombinu; Kushirikisha sekta binafsi (Public Private Partnership) kuwekeza katika mapori ya akiba (hoteli, loji, kambi za kitalii); Kuendelea kutoa elimu kwa umma; Kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa maduhuli na kuboresha ukusanyaji wa taarifa za kiintelijensia ikiwemo matumizi ya teknolojia ya kisasa.

83. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Mamlaka itaimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za wanyamapori na kuendesha siku-doria 373,065 ndani na nje ya mapori ya akiba. Aidha, Mamlaka itaendelea kuhakikisha usalama wa maisha ya watu na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kuendesha siku-doria 9,450.

84. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza shughuli za maendeleo, Mamlaka inakusudia kujenga nyumba 11 za Watumishi katika Mapori ya Akiba ya Mkungunero, Uwanda, Maswa, Liparamba, Swagaswaga, Lukwati, Piti, Moyowosi, Selous na Mpanga-Kipengere. Aidha, Mamlaka itajenga maghala ya kuhifadhiya silaha katika Mapori ya Akiba Maswa na Uwanda. Vilevile, itafidia familia zilizokutwa ndani ya Pori la Akiba Mpanga-Kipengere wakati likianzishwa na kujenga lambo kwa ajili ya mifugo nje ya Pori la Akiba Mkungunero. Mamlaka pia, itakarabati na kufungua barabara mpya zenyenye kilometra 2,020 na kununua vitendea kazi kwa ajili ya doria.

85. Mheshimiwa Spika, Mamlaka itakamilisha maandalizi ya miongozo yake ya uendeshaji (Mpango Mkakati, Mwongozo wa Matumizi ya Fedha, Kanuni za Utumishi na Muundo wa Mamlaka). Vilevile, watumishi 300 watahudhuria mafunzo ya Jeshi Usu na 130 watahudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika masuala ya uhifadhi, upelelezi, intelijensia na utawala bora.

86. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori itaendelea kutekeleza jukumu la uhifadhi wa wanyamapori na kuendeleza utalii. Kutokana na juhudhi za uhifadhi zilizofanyika, Mamlaka inalenga kupokea watalii 50,610 pamoa na kukusanya shilingi billioni 42.2.

5.1.6 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania

87. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) ilianzishwa kwa Sheria Sura 260 kwa lengo la kusimamia, kufanya na kuratibu utafiti wa wanyamapori nchini. Taasisi inawajibika kutoa ushauri kuhusu uhifadhi endelevu wa wanyamapori kwa kutumia matokeo ya utafiti wa kisayansi.

88. Mheshimiwa Spika Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Taasisi imeendeleza utafiti wa mbwamwitu; magonjwa

yanayoambukiza baina ya wanyamapor, mifugo na watu; ufugaji nyuki; na kufanya sensa za wanyamapor.

89. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kufanya utafiti wa uhifadhi wa mbwa mwitu waliokuwa hatarini kutoweka katika mfumo ikolojia wa Serengeti. Katika mwaka 2016/2017, makundi 25 ya mbwamwitu yenyе jumla ya mbwamwitu wapatao 300 yamefuatiliwa. Kati ya hayo, makundi sita yalihamishwa kutoka Pori Tengefu Loliondo na kuachiwa ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti. Matokeo yanaonesha kuwa idadi yao inaongezeka na hivyo, kuboresha uthalii kwa kuongeza vivutio ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti.

90. Mheshimiwa Spika, Taasisi iliendelea kufanya utafiti wa mwenendo wa magonjwa yanayoambukizwa kati ya wanyamapor, mifugo na binadamu. Magonjwa hayo ni pamoja na kimeta, kifua kikuu na homa ya vipindi (brucellosis). Utafiti umeonesha kuwa ugonjwa wa kimeta unaendelea kuwa tatizo kubwa kwa wanyama na binadamu katika jamii za wafugaji. Mlipuko wa kimeta uliotokea kati ya Septemba na Novemba 2016 uliathiri eneo la Mto Kilombero ndani ya Pori la Akiba Selous, Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro na Kata ya Seleta wilayani Monduli. Matokeo ya mlipuko huo ni maambukizi kwa watu 10 na mmoja kati yao kufariki; vifo vya viboko 153, nyumbu 109, swala granti 21 na sungura mmoja. Taasisi imeendelea kushiriki katika kudhibiti milipuko hii ikiwemo kuteketeza na kuzika mizoga na kutoa elimu kwa jamii ili kujikinga na maambukizi ya kimeta ambayo hujitokeza zaidi wakati wa ukame.

91. Mheshimiwa Spika, Kutokana na athari kubwa zinazosababishwa na muingiliano baina ya binadamu, wanyamapor na mifugo, natoa tahadhari kwa wananchi na viongozi katika ngazi zote kuepuka kuingiza mifugo na kufanya makazi katika maeneo yaliyohifadhiwa. Utafiti umebaini kuwa magonjwa makubwa na hatari duniani kama Ebola na homa ya mafua ya ndege yametokana na muingiliano baina ya binadamu, wanyamapor na mifugo.

92. Mheshimiwa Spika, Taasisi ilitoa mafunzo ya njia muafaka za ufugaji nyuki kwa wafugaji wa maeneo ya vijiji wapatao 574 kutoka wilaya sita kwa nadharia na vitendo katika mashamba ya nyuki ya Taasisi na mashamba ya vikundi nya ufugaji nyuki kwenye vijiji husika. Wafugaji nyuki 300 walitembelea Kituo cha Njiro na kupewa ushauri kuhusu ufugaji bora wa nyuki. Taasisi imeendelea na ujenzi wa jengo la maabara ya utafiti wa nyuki lilloko Njiro, Arusha. Ujenzi huo umefikia asilimia 65.

93. Mheshimiwa Spika, Taasisi ilifanya sensa katika kipindi cha kiangazi cha mwaka 2016 katika mifumo ikolojia ya Serengeti na Tarangire - Manyara, ili kutathmini idadi, muingiliano na mtawanyiko wa wanyamapori, mifugo na maboma. Matokeo yalionesha kuwepo kwa takriban ng'ombe 46,000; mbuzi na kondoo 1,520 ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti. Aidha, takriban ng'ombe 22,000; na mbuzi na kondoo 5,200 walibainika kuwepo ndani ya Pori la Akiba Maswa.

94. Mheshimiwa Spika, Katika mfumo ikolojia wa Tarangire – Manyara jumla ya spishi 29 za wanyamapori zilihesabiwa na idadi ya wanyama walirekodiwa kwa wingi ni pundamilia (21,464), nyumbu (13,235) na swalapala (5,721). Ikilinganishwa na sensa zilizopita, spishi saba hazikuonesha mabadiliko ya idadi (nyumbu, pundamilia, swalapala, kongoni, pofu, swala granti na mbuni), spishi nne zilionesha mwenendo wa kuongezeka idadi (twiga, swala-tomi, tohe, na ngiri). Aidha, ng'ombe walikadiriwa kuwa 331,000, kondoo na mbuzi 228,000 na punda 4,000. Ikilinganishwa na sensa zilizopita idadi ya mifugo imeongezeka. Kutokana na tathmini hizo imeonekana kuna idadi kubwa ya mifugo katika maeneo hayo na hivyo, kuleta changamoto katika uhifadhi.

95. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi inakabiliwa na changamoto za ufinyu wa bajeti; upungufu wa wataalam (waliopo ni asilimia 62 tu ya mahitaji); upungufu na uchakavu wa vitendeakazi na

miundombinu hususan magari na majengo. Mkakati wa kukabili changamoto hizo ni kuibua vyanzo vipyta vya mapato na kuboresha vilivyopo; kuongeza ikama na hatimaye kuajiri wataalam na kusomesha waliopo ili kuongeza ufanisi; na kununua vitendeakazi.

96. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Taasisi itaendelea kusimamia na kuratibu utafiti wa wanyamapori nchini kote, kuendelea na mradi wa utafiti wa mbwamwitu, kuendelea na utafiti wa magonjwa ya wanyamapori (hasa kimeta, homa ya vipindi na kifua kikuu), kuendelea na utafiti wa ustawi wa urejeshwaji wa chura wa Kihansi na utafiti wa nyuki nchini hasa mahusiano ya nyuki na mimea. Pia Taasisi itaendelea na utafiti kuhusu jinsi mfumo ikolojia wa Serengeti unavyofanya kazi na manufaa yake kwa jamii.

97. Mheshimiwa Spika, Taasisi pia itafanya sensa za wanyamapori katika sehemu mbalimbali ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Sensa zitakazofanyika ni sensa ya mamba nchi nzima, sensa ya viboko nchi nzima na sensa ya wanyamapori katika mfumo ikolojia wa Selous-Mikumi. Aidha, Taasisi itawaendeleza kimasomo watumishi wake katika ngazi mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kitaaluma kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi. Vilevile, Taasisi itaendelea na mradi wa ujenzi wa jengo la maabara ya kisasa ya utafiti wa nyuki.

5.1.7 Vyuvo vya Taaluma ya Wanyamaporı

98. Mheshimiwa Spika, Ili kuhakikisha kuwepo kwa wataalam wa wanyamaporı wa kutosha katika kada mbalimbali, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kupitia Chuo cha Usimamizi wa Wanyamaporı Mweka, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamaporı Pasiansi na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu-Sekamaganga.

5.1.8 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka

99. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori (CAWM) Mweka kilianzishwa mwaka 1963 kwa Sheria Sura 549. Majukumu makuu ya Chuo ni kutoa mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapori na uendeshaji wa utalii, kufanya utafiti unaolenga usimamizi wa wanyamapori na utalii na kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu ndani na nje ya nchi.

100. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 563. Aidha, Chuo kimetekeleza shughuli za maendeleo kwa kununua magari mawili; kujenga nyumba ya mtumishi; kukarabati chanzo cha maji; kukarabati jengo la utawala; kuweka mtambo wa kuchemsha maji unaotumia nishati ya jua kwenye mabweni ya wanachuo; kujenga nyumba ya kuhifadhia jenereta; na kukamilisha ukarabati wa bwalo la chakula na lango kuu.

101. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, Chuo kinakabiliwa na changamoto za uhaba wa fedha; upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali; na uchakavu wa miundo mbinu na vitendea kazi. Chuo kinakabiliana na changamoto zilizotajwa kwa: kushirikisha wadau wa maendeleo; kuendelea kutangaza kozi za muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi; kuimarisha utafiti na huduma za ushauri wa kitaalamu; pamoja na kuandaa mpango wa biashara wa Chuo.

102. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Chuo kitadahili wanafunzi 560 kwa ajili ya kozi mbalimbali na kukamilisha mtaala kwa ajili ya kuanzisha shahada ya uzamili. Aidha, Chuo kitaendelea kujenga uazio; kujenga nyumba mbili na kukarabati nyumba tano za watumishi; kukarabati mabweni ya wanafunzi; kukarabati jengo la mafunzo (training block); kuanza ujenzi wa vyumba vya miyadhabara na kununua magari mawili kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

5.1.9 Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori, Pasiansi

103. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori, (WTI) Pasiansi ilianzishwa mwaka 1966 na kupata usajili wa NACTE mwaka 2002. Jukumu lake ni kutoa mafunzo kwa askari wanyamapori nchini katika ngazi ya Cheti cha Awali na Cheti cha Uhifadhi Wanyamapori kwa kuufuata mfumo wa Jeshi Usu. Vilevile, Taasisi huendesha mafunzo ya muda mfupi.

104. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Taasisi ilidahili wanachuo wa kozi ya Cheti cha Awali na Cheti cha Uhifadhi Wanyamapori 441 na kozi fupi kwa wanachuo 88. Aidha, Taasisi imetekeleza na kukamilisha miradi ya ujenzi wa jiko awamu ya kwanza, stoo na bwalo lenye uwezo wa kutumiwa na wanachuo 260; ukarabati wa mfumo wa majitaka; ukarabati wa nyumba moja ya mtumishi yenye vyumba vitatu na ujenzi wa kambi ya mafunzo (bweni, jiko, vyoo na mabafu).

105. Mheshimiwa Spika, Taasisi inakabiliwa na changamoto za uchakavu na uhaba wa miundombinu hususan bweni la wasichana, maktaba, zahanati na mfumo wa maji katika mabweni; upungufu wa vitendea kazi hasa magari madogo na vitabu vya rejea; upungufu wa watumishi katika nyanja za TEHAMA, maktaba, masijala na ugavi.

106. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Taasisi ina mpango wa kudahili wanachuo 441, kuendesha kozi fupi kwa wanachuo 200; kukamilisha ujenzi wa Kantini awamu ya pili; kuendesha mafunzo kwa wakufunzi kuhusu mbinu za ufundishaji; na kuongeza vitendea kazi.

5.1.10 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu-Sekamaganga

107. Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, (CBCTC) Likuyu-Sekamaganga

kilianzishwa mwaka 1995. Lengo kuu la kuanzisha kituo hiki ni kuzijengea uwezo jamii zinazoishi katika maeneo yenyе wanyamaporи ili ziweze kushiriki kikamilifu katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili hizo. Kituo kinatoa mafunzo kwa askari wanyamaporи wa vijiji na viongozi wa Serikali na wajumbe wa kamati za maliasili za vijiji.

108. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Kituo kimetoa mafunzo kwa washiriki 75. Aidha, Kituo kimekamilisha mapitio ya mtaala wa kozi za askari wanyamaporи wa vijiji na viongozi wa serikali na wajumbe wa kamati za maliasili za vijiji.

109. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, kituo kinakabiliwa na changamoto za uchakavu wa miundombinu hasa vyoo vya wanafunzi, nyumba za watumishi, jengo la utawala, maktaba, mabweni pamoja na upungufu wa vifaa vya mafunzo. Aidha, kuna uvamizi wa eneo la Kituo unaofanywa na wanakijiji kwa ajili ya kilimo. Hatua za kukabiliana na changamoto hizo ni kuandaa mpango wa biashara wa Kituo. Vilevile, Kituo kitaimarisha uhusiano na vijiji jirani ili kukabiliana na uvamizi wa ardhi.

110. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Kituo kitatoa mafunzo kwa wanavijiji 100. Aidha, Kituo kitaendelea na hatua za kupata usajili wa NACTE ili kuanzisha kozi ya cheti cha awali cha waongoza watalii vijijini. Vilevile, Kituo kitaendelea kuboresha miundombinu.

5.1.11 Miradi ya Maendeleo

111. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza miradi mitatu katika sekta ndogo ya Wanyamaporи kwa lengo la kuimarisha uhifadhi. Miradi hiyo inajumuisha:

5.1.11.1 Mradi wa Kilombero and Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management (KILOWEMP)

112. Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania Ubelgiji katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Rufiji. Lengo la mradi huu ni usimamizi endelevu wa ikolojia ya ardhioevu ya Bonde la Kilombero na Mto Rufiji kwa kuboresha maisha ya wananchi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mradi umenunua vitendeakazi na kujenga uwezo kwa WMAs za ILUMA na JUHIWANGUMWA, umeweka alama za mipaka ya maeneo kwa upande wa ILUMA na kugharamia mafunzo ya watumishi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi utaendelea kutekeleza majukumu yake katika maeneo hayo.

5.1.11.2 Mradi wa Kujenga Uwezo katika Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili

113. Mheshimiwa Spika, Mradi unalenga kujenga uwezo wa Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili kwa kununua vitendeakazi na kuimarisha miundombinu. Mradi unatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani, katika mwaka wa fedha 2016/2017 hakuna fedha zilizotolewa. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi umetengewa shilingi bilioni 34.1 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu na kununua vitendea kazi katika Mapori ya Akiba, Kikosi Dhidi ya Ujangili, TANAPA na NCAA.

5.1.11.3 Sustainable Natural Resources Management in Tanzania

114. Mheshimiwa Spika, Mradi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Ujerumanii katika Halmashauri za Wilaya ya Ngorongoro na Serengeti. Lengo la mradi ni kuweshesha jamii kushiriki katika usimamizi endelevu wa maliasili. Mwaka 2016/2017, kazi zilizotekeliza ni kuiweshesha TAWA pamoja na Kitengo cha Kupambana na Ujangili kutekeleza majukumu yake. Katika mwaka wa

fedha 2017/2018, Mradi utaendelea kuiwezesha TAWA na Kitengo cha Kupambana na Ujangili; kuimarisha miundombinu; na kuziwezesha jamii katika Wilaya za Ngorongoro na Serengeti kuimarisha uhifadhi.

5.2 Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki

115. Mheshimiwa Spika, Jukumu kuu la Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki ni uhifadhi wa misitu iliyopo ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa na makundi ya nyuki ya aina zote. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Misitu, 1998 na Sera ya Ufugaji Nyuki, 1998 na Sheria ya Misitu Sura 323 na Sheria ya Ufugaji Nyuki Sura 224.

116. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa ya tathmini ya rasilimali za Misitu (NAFORMA) iliyotolewa mwaka 2015, Tanzania ina misitu yenye hekta milioni 48.1. Kati ya hekta hizo, asilimia 93 ni misitu ya mataji wazi (woodland) na asilimia saba ni misitu iliyofunga. Hii ni sawa na meta za ujazo za miti bilioni 3.3. Kati ya meta hizo, meta za ujazo bilioni 3.2 sawa na asilimia 97 ipo katika misitu ya asili na meta za ujazo bilioni 0.1 sawa na asilimia tatu katika misitu ya kupandwa. Mahitaji halisi ya mazao timbaok kwa sasa yanakadirwa kuwa meta za ujazo milioni 62.3 kwa mwaka. Hata hivyo, kiasi kinachowenza kuvunwa ni meta za ujazo milioni 42.8 tu hivyo kusababisha upungufu wa meta za ujazo milioni 19.5 kwa mwaka.

117. Mheshimiwa Spika, Misitu hiyo yenye hekta milioni 48.1 inasimamiwa na Serikali Kuu yenye hekta milioni 19.2 sawa na asilimia 40; Serikali za Mitaa hekta milioni 3.4 sawa na asilimia saba; Serikali za vijiji hekta milioni 21.6 sawa na asilimia 45; na watu binafsi wanasimamia hekta milioni 3.4 sawa na asilimia saba. Eneo liliobaki lenye ukubwa wa hekta milioni 0.5 sawa na asilimia 1 ni misitu iliyopo kwenye ardhi huria.

118. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa sekta ndogo ya Ufugaji nyuki Serikali kuu na Serikali za Vijiji kwa pamoja zinasimamia hifadhi 46 za nyuki zenye hekta 143,936.78. Kati

ya hizo, hifadhi 26 zenyе hekta 74,323.78 ni za Serikali za vijiji na 20 zenyе hekta 69,613 ni za Serikali Kuu. Aidha, ufgaji nyuki unafanyika katika mikoa yote nchini. Hata hivyo, uzalishaji mkubwa wa mazao ya nyuki unafanyika katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Dodoma, Singida, Rukwa, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya na Ruvuma.

119. Mheshimiwa Spika, Ufugaji nyuki ni muhimu katika uhifadhi wa misitu, ukuaji wa uchumi, lishe, tiba na huduma ya uchavushaji wa mazao. Takwimu za soko la asali zinaonesha kuwa mahitaji yanaongezeka ndani na nje ya nchi ukilinganisha na uzalishaji na upatikanaji wake. Tanzania imeendelea kuwa mionganoni mwa nchi tano za Afrika zinazoruhusiwa kuuza asali yake katika soko la Ulaya. Takwimu za usafirishaji wa mazao ya nyuki nchi za nje ni wastani wa tani 278.6 za asali na tani 347.3 za nta. Aidha, ufgaji nyuki una fursa ya kuzalisha mazao mengine yanayotumika kwa urembo, tiba na malighafi za kutengeneza bidhaa nyingine viwandani

120. Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya misitu na nyuki inajumuisha Idara ya Misitu na Nyuki, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania, Mfuko wa Misitu Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Chuo cha Misitu Olmotonyi, Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi na Chuo cha Ufugaji Nyuki, Tabora.

5.2.1 Idara ya Misitu ya Nyuki

121. Mheshimiwa Spika, Jukumu kuu la Idara ya Misitu na Nyuki ni kutayarisha na kusimamia sera, sheria, kanuni na miongozo ya Usimamizi wa Misitu na Ufugaji Nyuki. Katika mwaka 2016/2017, mapitio ya Sera za Taifa za Misitu na Ufugaji Nyuki yamefanyika ambapo rasimu ya awali na mkakati wa utekelezaji wake vimeandaliwa. Aidha, Sheria ya Misitu Sura 323 imefanyiwa mapitio kwa lengo la kuainisha vifungu ambavyo vinatakiwa kufanyiwa marekebisho ili kuboresha usimamizi wa misitu nchini. Kazi inayoendelea sasa ni kukusanya maoni ya wadau.

122. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali za mitaa na wadau mbalimbali wa misitu, imeratibu utekelezaji wa dhana ya usimamizi shirkishi wa rasilimali za misitu na ufugaji nyuki katika wilaya 67 za Tanzania bara. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kuanzisha na kuzijengea uwezo Kamati za Maliasili za vijiji katika kupanga matumizi bora ya ardhii kwenye maeneo yao, kutambua misitu iliyopo, kupanga mipango ya uvunaji misitu yao, mafunzo ya usimamizi wa fedha na utawala bora.

123. Mheshimiwa Spika, Wizara inakabiliwa na changamoto ya uvamizi mkubwa wa maeneo ya misitu kwa ajili ya shughuli za kilimo, malisho ya mifugo, uchimbaji wa madini, makazi, ukataji haramu wa miti kwa ajili ya nishati, mbaao na nguzo za ujenzi. Misitu imeendelea kuwa chanzo kikuu cha nishati, ambapo ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa umekithiri. Aidha, majanga ya moto na uvunaji usio endelevu kwa ajili ya ujenzi hasa kwenye misitu ya asili unachochea kwa kasi kutoweka kwa bioanuwai. Takwimu zinaonesha eneo la misitu linalokadiriwa kufikia hekta 372,000 hupotea kila mwaka. Uharibifu huu unahatarisha utulivu wa hali ya hewa, hasa upatikanaji wa mvua kwa wakati na kuvuruga misimu ya kilimo na shughuli nyingine za kibinadamu.

124. Mheshimiwa Spika, Katika kukabiliana na changamoto hizi, Wizara itaratibu utekelezaji wa mkakati wa uhifadhi na kupanda miti kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hasa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Asasi zisizo za kiserikali na jamii kwa ujumla. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wengine katika kutafuta na kuhimiza matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza utegemezi wa misitu kama chanzo kikuu cha nishati.

125. Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya ufugaji nyuki inakabiliwa na changamoto ya uzalishaji mdogo wa mazao ya nyuki. Teknolojia duni inayotumika na baadhi ya wafugaji katika kufuga, kuvuna, kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki inaathiri ubora na ushindani katika masoko ya ndani

na nje. Katika kutatua changamoto hizi, Wizara inaendelea kutoa elimu na uwezeshaji katika uvunaji, uchakataji na ufungashaji wa mazao ya nyuki ili kuongeza uzalishaji na kukidhi viwango vya ubora.

126. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Wizara itakamilisha kazi ya kuhuisha Sera za Taifa za Misitu na Nyuki na mikakati ya utekelezaji wake. Aidha, Wizara itakamilisha uandaaji wa Programu ya Taifa ya Misitu kwa kipindi cha 2018-2023 na kufanya mapitio ya Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya 2001. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaandaa mkakati wa kupunguza uharibifu wa misitu unaotokana na matumizi ya mkaa.

Mikakati mingine itakayoandaliwa ni mkakati wa ugani na mkakati wa kukabiliana na moto katika maeneo ya misitu. Wizara pia itaandaa mpango wa utafiti wa ufugaji nyuki ili kuimarisha shughuli za ufugaji nyuki.

127. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma ili kuimarisha uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki. Baadhi ya njia zitakazotumika kutoa elimu ni maonesho na maadhimisho maalum ya Siku ya Kupanda Miti na Kutundika Mizinga Kitaifa, Siku ya Misitu Duniani, Siku ya Mazingira Duniani, na wiki ya Utumishi wa Umma.

5.2.2 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

128. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ulianzishwa kwa Sheria Sura 245 na kupewa jukumu la kusimamia na kuhifadhi rasimali za misitu na ufugaji nyuki. Wakala unasimamia misitu ya hifadhi ya Serikali Kuu yenye hekta milioni 16 na misitu yenye hekta milioni 2.7 iliyopo kwenye maeneo huria. Misitu hiyo inajumuisha misitu ya Hifadhi za Mazingira Asilia yenye hekta 239,669; Misitu ya Hifadhi lindimaji yenye hekta milioni 1.4 na hifadhi za mikoko zenyе hekta 115,000. Wakala pia unasimamia mashamba 19 ya miti yenye hekta 308,442 na Hifadhi za Nyuki 20 zenyе hekta 69,613.

129. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017 Wakala umekamilisha mipango ya usimamizi wa misitu ya hifadhi 56 na inatumika katika kusimamia misitu husika. Mipango ya usimamizi wa misitu ya hifadhi ya Kikale na Rungo (Rufiji), Sayaka (Magu), na Kome (Sengerema) ipo katika hatua ya kuidhinishwa. Aidha, tathmini kwa ajili ya kuandaa mipango ya usimamizi imefanyika kwenye misitu ya hifadhi 28 katika mikoa ya Kagera, Tabora, Katavi, Lindi, Pwani na Tanga. Vilevile, mipango ya uvunaji kwenye maeneo ya misitu katika ardhi huria imeandaliwa kwenye Wilaya za Kilwa, Liwale, Nachingwea, Tunduru, Songea, Namtumbo, Lindi, Masasi, Ruangwa na Nanyumbu.

130. Mheshimiwa Spika, Katika kuzuia uharibifu wa uoto wa asili, vyanzo vya maji na bioanuwai, Wakala umeendelea kuwaonda wavamizi kwenye hifadhi. Hadi Machi 2017, wavamizi wameondolewa katika misitu 14 iliyopo katika Wilaya za Kilosa, Kilindi, Biharamulo, Sikonge, Uyui, Kaliua, Bagamoyo na Tunduru. Aidha, Wakala umeendelea kutoa elimu kuhusu madhara ya uharibifu wa misitu kwa mazingira.

131. Mheshimiwa Spika, Katika juhudzi za kutatua migogoro iliyopo baina ya wananchi na hifadhi za misitu, Wakala iliunda kamati ya kutatua migogoro, kuainisha aina na idadi ya migogoro iliyojitokeza na kushirikisha wadau katika kutatua migogoro hiyo. Utambuzi na uhakiki wa vijiji vilivyojasiliwa kwenye maeneo yallyohifadhiwa kinyume na Sheria ya Misitu umefanyika. Kutokana na utambuzi huo imebainika kuwa vijiji 228 vipo ndani ya hifadhi za misitu na kati ya hivyo, vijiji 157 vimesajiliwa. Hatua za kukabiliana na changamoto hizo zimechukuliwa kwa kuainisha mipaka ya hifadhi na kuhuisa ramani za maeneo husika.

132. Mheshimiwa Spika, Katika jitihada za kushughulikia migogoro ya mipaka na kuondoa mifugo katika hifadhi, Serikali iliunda Kamati yenye wajumbe kutoka wizara za Maliasili na Utalii; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati hii ina jukumu la kutambua na kutoa mapendekezo ya kutatua migogoro ya

mipaka na matumizi yasiyoruhusiwa kwenye hifadhi. Kamati hiyo imeshafanya kazi katika Mikoa mitano ya Katavi, Morogoro, Tabora, Geita na Kagera. Aidha, adhabu mbalimbali kwa mujibu wa sheria na elimu kwa umma juu ya manufaa ya uhifadhi inaendelea kutolewa kwa wananchi.

133. Mheshimiwa Spika, Kazi ya kuainisha mipaka yote ya hifadhi za misitu, kuhakiki na kuweka *beacons* na mabango ya utambulisho wa mipaka inaendelea. Hadi kufikia Machi 2017, jumla ya *beacons* 4,039 zimewekwa katika misitu 154. Aidha, kazi ya kuweka *beacons* kwenye misitu iliyosalia inaendelea. Mabango 633 yamewekwa ikiwa ni pamoja na kusafisha njia za kuzuia moto zenye urefu wa kilometra 700. Vilevile, jumla ya kilometra 2,125 za mipaka ya hifadhi za misitu 54 zimerekebishwa. Pia, kilometra 1,886 za mipaka ya misitu zimesafishwa na kuchimba mashimo mwelekeo (*directional trenches*) 433 katika misitu mbalimbali.

134. Mheshimiwa Spika, Wakala umeendelea kusimamia misitu ya Hifadhi Mazingira Asilia 12 yenye bioanuwai nyngi na viumbe ndwele (*endemic species*) na adimu duniani. Hifadhi hizo ni Amani, Nilo, Magamba, Uluguru, Mkingu, Kilombero, Mlima Rungwe, Chome (Shengena), Udzungwa Scarp, Minziro, Mlima Hanang na Rondo. Misitu hii ni muhimu katika kukuza shughuli za utalii ikolojia na inawezesha wananchi wanaozunguka misitu kunufaika kupitia ajira, biashara na huduma za kijamii. Kazi zilizotekelizwa ili kuimarisha hifadhi hizo ni kusafisha barabara zenye urefu wa kilometra 89 na kufungua njia vinjari kilometra 40. Aidha, kambi tano za kupumzikia wageni zimejengwa kwenye hifadhi tano. Vilevile, njia asili (nature trails) kilometra 10 zimeanzishwa kwenye misitu ya Hifadhi za Mazingira Asilia Rondo na Mlima Hanang.

135. Mheshimiwa Spika, Ili kukabiliana na upungufu wa malighafi ya mazao ya misitu, katika mwaka 2016/2017 Wakala umepanda miti hekta 7,532. Kazi nyngine zilizofanyika ni kupalilia hekta 22,671; kupunguzia miti hekta 5,038 na kupogolea hekta 2,859. Aidha, Wakala umeanzisha

mashamba mawili mapya ya Hifadhi ya Msitu wa Nishati Morogoro (hekta 12,950) na Mpepo wilayani Mbinga (hekta 2,300). Vilevile, shamba la miti Wino-Ifinga limepanuliwa kwa kuongeza eneo la Mkongotema (hekta 5,000) Wilaya ya Madaba na hivyo kufanya shamba hilo kuwa na hekta 17,000.

136. Mheshimiwa Spika, Sekta ya misitu imeendelea kutoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya viwanda nchini. Ili kuchochaea kasi ya maendeleo ya uchumi na ukuaji wa viwanda, jumla ya meta za ujazo 971,734 zilivunwa kutoka katika mashamba nane yenye miti iliyofikia umri wa kuvunwa na kuuzwa kwa wavunaji 1,652. Kutokana na mauzo hayo hadi Machi, 2017 Serikali imekusanya mapato ya shilingi bilioni 40.3.

137. Mheshimiwa Spika, Katika kudhibiti uvunaji na biashara haramu ya mazao ya misitu, Wakala ulifanya jumla ya siku-doria 20,737 katika maeneo ya misitu, maeneo ya uvunaji, usafirishaji wa mazao ya misitu na kwenye masoko. Kupitia doria hizo mazao yaliyovunwa kinyume cha sheria yanayojojumuisha magunia 32,312 ya mkaa, vipande vya mbao 50,791, nguzo 622, na milango 556 ilikamatwa na kutaifishwa kwa mujibu wa sheria.

138. Mheshimiwa Spika, Wakala umeendelea kutumia vizuia kama moja ya mikakati ya kusimamia usafirishaji wa mazao ya misitu. Katika ukaguzi uliofanyika kwenye vizuia 116, magari 9,753 (sawa na asilimia 15.4) ya magari 63,213 yaliyokaguliwa yilibainika kukiuka sheria za kusafirisha mazao ya misitu. Hali hii inaonesha kuwa asilimia 84.6 ya wasafirishaji wa mazao ya misitu wanazingatia sheria. Aidha, Wakala umeendelea kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara 1,125 kuhusu taratibu za kufanya biashara ya mazao ya misitu kwa mujibu wa sheria.

139. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha usimamizi wa biashara ya mkaa, magilio 15 ya mkaa yameanzishwa kwenye wilaya za Kilosa, Mvomero, Mkinga, Korogwe, Kilindi, Gairo na Muheza. Wakala umeanzisha Magilio hayo ili kudhibiti uvunaji na uchomaji holela wa mkaa na

kuwatambua na kuwaunganisha wavunaji na wafanyabishara. Aidha, kuititia utaratibu huu wavunaji wataunganishwa na kushiriki kupanda miti kuititia vikundi. Hatua hii itaongeza uwajibikaji wa jamii na itapunguza uharibifu wa misitu na kurahisisha usimamizi na utoaji wa huduma za ugani.

140. Mheshimiwa Spika, Wakala umetumia fursa ya ushirikiano wa Kikanda kuingia makubaliano ya kudhibiti biashara haramu ya usafirishaji wa mazao ya misitu. Makubaliano hayo yamehusisha nchi za Zambia, Msumbiji, Kenya, Madagascar, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Katika mwaka 2016/2017, mikutano mbalimbali ya kuweka mikakati ya usimamizi wa pamoja wa mazao ya misitu ilifanyika. Aidha, kuititia mikutano hiyo, Serikali ya Msumbiji imerekebisha Sheria yake ya Misitu ambapo kuanzia Machi, 2017 imezuia usafirishaji wa magogo nje ya nchi.

141. Mheshimiwa Spika, Wakala umeendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa wafugaji nyuki 488. Elimu iliyotolewa ilihusu mbinu za ufugaji nyuki ili kuongeza tija na kuboresha bidhaa zinazozalishwa. Wilaya zilizonufaika na mafunzo hayo ni Misenyi, Magu, Biharamulo, Bahi, Chamwino, Babati, Ikungi, Same na Handeni.

142. Mheshimiwa Spika, Sampuli 63 za asali kutoka kwa wafugaji nyuki katika wilaya 25 zimefanyiwa uchambuzi wa kimaabara kubainisha ubora wake. Uchambuzi huo umebaini kuwa asali ya Tanzania inakidhi viwango vya ubora kwa soko la ndani na nje. Aidha, Wakala umeendelea kusimamia manzuki 82 zinazotumika kuzalisha mazao ya nyuki. Manzuki hizo pia zinatumika kama shambadarasa kwa wananchi na wadau wa nyuki. Jumla ya tani 7.8 za asali na kilo 340 za nta zimezalishwa katika manzuki hizo.

143. Mheshimiwa Spika, Katika kuboresha mazingira ya kazi, Wakala umejenga majengo mawili ya ofisi, nyumba 12 za watumishi na kukarabati nyumba 75. Aidha, magari 14, boti mbili na mitambo miwili ya kutengeneza barabara

imenunuliwa. Vilevile, Wakala umesafisha jumla ya kilomita 1,329 za barabara, na kutengeneza nyingine kilomita 99.

144. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Wakala uliimarisha mfumo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa kutumia mashine za EFD katika vituo 46. Mfumo huo umechangia kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ambapo hadi Machi, 2017 shilingi bilioni 72.4 sawa na asilimia 76 ya makisio zilikusanywa. Aidha, katika kuboresha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, Wakala unashirikiana na Wizara ya Fedha, Wakala wa Mtandao Serikalini na TAMISEMI kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji maduhuli. Mfumo huo wa kukusanya maduhuli yatokanayo na mazao ya misitu umeanza kufanyiwa majoribio katika Wilaya ya Kinondoni na Shamba la miti Sao Hill.

145. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Wakala ulitoa elimu kwa umma kuhusu usimamizi na uhifadhi wa misitu na ufugaji nyuki. Elimu hiyo ilitolewa kuititia vipindi 41 vya redio na 54 vya televisheni. Njia nyingine zilizotumika ni maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Siku ya Kupanda Miti, Kutundika Mizinga, na Siku ya Mazingira Kitaifa ambapo nakala 30,000 za machapisho zilitayarishwa na kusambazwa.

146. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Wakala uliwezesha vikundi 257, taasisi 17 (shule, makanisa na misikiti) na watu binafsi 84 katika wilaya 38 kuzalisha na kupanda miche ya miti takriban milioni 6. Aidha, mafunzo juu ya wajibu na majukumu ya uhifadhi na usimamizi wa misitu, yalitolewa kwa kamati 70 za maliasili za vijiji.

147. Mheshimiwa Spika, Usimamizi na uhifadhi wa misitu na nyuki nchini, unakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo, mifugo, makazi na uchimbaji wa madini. Aidha, kuna fikra kuwa maeneo ya misitu yaliyohifadhiwa kisheria yametengwa kwa ajili ya matumizi mengine ya baadaye (malisho, kilimo na makazi) taswira inayosababisha

kuongezeka kwa maombi ya kumegwa maeneo ya misitu. Changamoto nyingine ni uvunaji na usafirishaji haramu wa mazao ya misitu na utegemezi mkubwa wa misitu kwa ajili ya matumizi mbalimbali hususan nishati ya kupikia na mbao.

148. Mheshimiwa Spika, Ongezeko la mahitaji ya malighafi za misitu hususan magogo kwa ajili ya mbao limesababisha ugumu wa kugawa kiasi kidogo kinachoruhusiwa kuvunwa kila mwaka. Kwa kipindi kirefu Wizara imekuwa ikuza malighafi kutoka katika mashamba ya miti kwa njia ya kutoa vibali. Utaratibu huu umesababisha malalamiko mengi toka kwa wadau na makundi ya kijamii.

149. Mheshimiwa Spika, Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wakala umefanya mapitio ya njia ya kugawa malighafi kutoka katika mashamba ya miti ya Serikali. Aidha, Wakala umefanya tathimini ya viwanda vya misitu nchini kwa lengo la kujua idadi na uwezo wa viwanda hivyo kuchakata magogo. Matokeo ya mapitio hayo yanaonesha kuwa utaratibu wa vibali kwa kiasi kikubwa unasababisha kutoa vibali kwa wadau wasio na sifa za kutosha. Katika mazingira hayo, yameibuka makundi ya walanguzi wa vibali ambao huuza vibali hivyo kwa wale waliowekeza kwenye viwanda vya uchakataji. Matokeo yake ni kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na kumuathiri mlaji wa mwisho; kufungwa kwa viwanda vingi; na kuathiri ajira.

150. Mheshimiwa Spika, Katika kukabili changamoto hiyo, kuanzia mwaka 2017/2018 vibali vya uvunaji kutoka kwenye mashamba ya Serikali vitatolewa kwa waliowekeza kwenye viwanda vya uchakataji vilivyoahakikiwa. Viwanda vitakavyohusika ni vile vikubwa, vya katni na wajasiriamali wadogo wenye misumeno maarufu kama 'dingdong'.

151. Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, Wizara inawahimiza wajasiriamali wadogo wanaotumia 'dingdong' kuungana na kubadili teknolojia hiyo ndani ya mwaka mmoja. Hatua hii itaongeza ufanisi na kupunguza upotevu wa malighafi za misitu. Aidha, utaratibu wa kutoa

vibali kwa wenge viwanda tu inalenga kuvivezesha viwanda kufanya kazi muda mrefu kwa mwaka na hivyo kuendelea kuchangia katika pato la Taifa na kutoa ajira.

152. Mheshimiwa Spika, Athari za uharibifu wa misitu ambazo zinajitokeza ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi, kuenea kwa hali ya jangwa na kuongezeka kwa mmomonyoko wa ardhi na mapomoko ya milima. Uharibifu wa vyanzo vya maji pia umeongezeka na kusababisha kukauka kwa mito mikuu wakati wa kiangazi; kuongezeka kwa matukio ya moto kwenye misitu ambayo husababisha uharibifu wa misitu na kupotea kwa bioanuwai.

153. Mheshimiwa Spika, Katika kukabiliana na changamoto hizo Wakala utaendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za misitu na ufugaji nyuki kwa kushirikiana na wadau. Aldha, utaongeza kasi ya upandaji miti katika mashamba ya miti ya Serikali; kuhamasisha upatikanaji na matumizi ya nishati mbadala, kuendelea kuwaondoa wavamizi wa misitu ya hifadhi; kuimarisha mipaka ya hifadhi, kudhibiti uvunaji haramu na kuhamasisha upandaji miti. Vilevile, Wakala utaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu usimamizi wa misitu na matumizi endelevu ya mazao ya misitu.

154. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Wakala utaandaa mipango ya usimamizi ya misitu ya hifadhi 31, kufanya mapitio ya mipango 23 na kukamilisha mipango mipy 17. Misitu 28 na hifadhi za nyuki saba zitatangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Aidha, Hifadhi za misitu ya mikoko zitafanyiwa tathmini ya kujua kiwango cha uharibifu, kupanda hekta 734 zilizoharibiwa na kuweka alama za kutoa tahadhari katika mipaka. Vilevile, kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shirika la Kimataifa la ardhi oevu itatekeleza mradi wa usimamizi endelevu wa mikoko katika bonde la Mto Rufiji.

155. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Wakala utasafisha mipaka ya misitu yenye kilomita 6,427, kuweka *beacons* 2,603, mabango 1,252 na kufanya soroveya kwenye

mipaka ya misitu ya hifadhi 126 yenyе kilomita 585. Aidha, barabara zenye kilometra 2,194 zitasafishwa katika mashamba ya miti na kutengeneza nyingine kilometra 181. Vilevile, kilometra 5,123 za barabara za kuzuia moto katika misitu ya asili na mashamba zitasafishwa.

156. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, maeneo ya utalii ikolojia katika Misitu ya Hifadhi ya Mazingira Asilia yatatunzwa kwa kusafisha njia za asili zenye urefu wa kilomita 279. Aidha, kilometra 67 za barabara za msituni zitasafishwa; kambi 20 za kupumzikia wageni na minara mitatu ya kuona mandhari itakarabatiwa; na kambi moja ya kupumzikia wageni itajengwa katika Msitu wa Hifadhi wa Uzungwa.

157. Mheshimiwa Spika, Katika jitihada za kuimarisha uhifadhi na kukuza utalii ikolojia Wakala utaendelea na hatua za kupandisha hadhi misitu ya Uvinza (Uvinza), Itulu Hill (Sikonge) na Mwambesi (Tunduru) kuwa misitu ya hifadhi ya mazingira asilia. Aidha, Wakala utaendelea kuboresha miundombinu katika maporomoko ya Mto Kalambo yaliyoko Mkoani Rukwa ili yatumike kwa shughuli za utalii.

158. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018 Wakala utapanda miti katika hekta 8,800; kupalilia mashamba ya miti hekta 29,505; kupogolea hekta 6,263 na kupunguzia miti hekta 3,500. Aidha, Wakala utaongeza eneo la shamba la miti ya misaji (teak) Mtibwa, kwa kuongeza sehemu ya misitu ya Pagale (hekta 12,000) na Magotwe (hekta 700) ili yopo Wilaya ya Mvomero katika Mkoa wa Morogoro. Vilevile, itaaniszha mashamba mapya matatu. Mashamba hayo ni Buhigwe (hekta 800) na Makere (hekta 30,000) yaliyopo Mkoani Kigoma, na shamba la Biharamulo (hekta 30,000) katika Mikoa ya Geita na Kagera.

159. Mheshimiwa Spika, Matukio ya moto kwenye misitu yameendelea kuwa changamoto katika uhifadhi. Katika kukabiliana na changamoto hii, vijiji 378 vinavyozunguka mashamba ya miti vitashirikishwa katika kampeni ya kuzuia moto. Wakala pia utakarabati minara 19 ya kufuatilia moto

msituni. Elimu ya ugani itaendelea kutolewa sambamba na kuandaa mipango ya usimamizi wa moto kwa kushirikiana na jamii hususan mikoa ya Kusini. Vile vile, umoja wa kukabiliana na moto (*Fire Associations*) kwa wakulima wa miti Kanda ya Nyanda za Juu Kusini utaananzishwa. Wakala pia utatoa mafunzo kwa watumishi 40 namna ya kutambua, kuchambua na kutafsiri taarifa za moto kutoka kwenye mtambo wa satelaiti unaong'amua matukio ya moto.

160. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018 Wakala utaendelea kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa misitu ya asili kwa ushirikiano na wadau. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya siku-doria 19,616 na ufuatilaji wa klintelijensia; kufanya ukaguzi na udhibiti wa biashara ya mazao ya misitu katika vizuia vyote; kuandaa mfumo wa teknolojia ya "*Radio Frequency Identification*" wa kufuatilia mwenendo wa biashara ya mazao ya misitu. Aldha, Wakala utaendelea kushirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya katika kukabiliana na changamoto za uvamizi katika hifadhi za misitu na utatuzi wa migogoro.

161. Mheshimiwa Spika, Ili kudhibiti biashara haramu ya mazao ya misitu kupitia Bahari ya Hindi, Wizara yangu inashirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvumi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ushirikino huu unazingatia Sheria ya Misitu ambayo inakataza kusafirisha magogo na mkaa nje ya nchi. Hatua hii ni muhimu kwa sababu magogo na mazao mengine ya misitu ni malighafi muhimu kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza viwanda vya ndani.

162. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018 Wakala utaendelea kuimarisha kikosi cha kuzuia uharibifu wa misitu (*Forest Surveillance Unit - FSU*) sanjari na azma ya Wizara ya kuanzisha mfumo wa Jeshi Usu litakalowajibika kusimamia maliasili zote. Wizara inaendelea kuimarisha ushirikiano wa Kikanda katika kudhibiti biashara haramu za mazao ya misitu zinazofanyika mipakani. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza makubaliano na nchi jirani za Zambia, Msumbiji, Kenya, Madagascar, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kupitia ushirikiano huu Wakala utaendelea kushirikiana na

taasisi za nchi hizo na shirika la hifadhi za viumbe hai duniani la WWF ili kutengeneza mfumo wa kutambua mazao ya misitu kwa kutumia vihasaba (*DNA identification*).

163. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018 Wakala utaongeza udhibiti wa biashara holela ya mkaa. Aidha, Wakala utaendelea kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala kama gesi ambayo sasa inapatikana maeneo mengi nchini. Wakala utaendelea na jitihada za kuvutia wawekezaji katika eneo la nishati hasa utengenezaji wa bidhaa kama 'Briquettes' na 'mkaa poa'. Mfano wa uwekezaji huo ni kiwanda cha *Arti Energy* kilichopo Bagamoyo na kiwanda cha kampuni ya *Tractors Ltd* kinachojengwa katika wilaya Mufindi, Iringa. Kiwanda hicho cha Mufindi kinategemea kuzalisha mkaa kwa jina la biashara la "Mkaa Endelevu" na kuzalisha hadi tani 35 kwa siku kwa kutumia mabaki ya viwandani na masalia ya uvunaji katika misitu ya Sao Hill. Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wanaojihuisha na utafutaji na utengenezaji wa nishati mbadala.

164. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Wakala utaandaa mkakati wa kuendeleza ufugaji nyuki; kuwezesha uandaaji wa mwongozo wa usimamizi wa Hifadhi za Nyuki nchini na kukamilisha kutangaza hifadhi saba za nyuki za Serikali Kuu na nne za Serikali za Vijiji. Aidha, sampuli 60 za asali zitakusanywa na kufanyiwa uchambuzi wa kuanisha mabaki ya kemikali ili kulinda afya za walaji. Vilevile, Wakala utatoa mafunzo ya uzalishaji bora wa mazao ya nyuki kwa wafugaji wa nyuki 727 na vikundi 27 vya ufugaji nyuki. Kazi nyiningine zitakazofanyika ni kutoa mafunzo ya mfumo wa ufuatiliaji wa asali (Honey traceability system) yatakayotolewa kwa wadau 80 na mafunzo ya kutengeneza mizinga bora yatakayotolewa kwa mafundi seremala 55.

165. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018 Wakala utanunua viwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Meneja wa Wilaya saba; utajenga ofisi 13 na nyumba 74 za watumishi; na kukarabati ofisi nane na nyumba 17 za watumishi. Vile

vile, Wakala utaongeza vitendea kazi kama magari, pikipiki na boti ili kuimarisha doria na ulinzi wa misitu.

166. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018 Wakala utaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu uhifadhi wa misitu na ufugaji nyuki kupitia maonesho ya Sabasaba, Nane nane, Siku ya Kupanda Miti na Kutundika Mizinga Kitaifa, Siku ya Mazingira Duniani na Siku ya Utumishi wa Umma. Aidha, Wakala utaendelea kuwaelimisha wananchi kwa kuchapisha na kusambaza nakala 9,000 za majarida ya aina mbalimbali, kurusha vipindi 32 vya televisheni na 52 vya radio.

167. Mheshimiwa Spika, Katika kuboresha ukusanyaji wa maduhuli, Wakala utafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vituo vya kukusanya maduhuli, kusimamia uuzwaji wa miti kwa njia ya mnada na makubaliano binafsi. Aidha, mfumo wa kielektoniki utafungwa katika vituo vya kukusanya maduhuli na kutoa mafunzo kwa wakusanya maduhuli katika kanda saba na mashamba 12. Vilevile, wakala utaendelea na matumizi ya EFD katika kukusanya maduhuli. Katika mwaka 2017/2018, Wakala umekadiria kukusanya shilingi billioni 118.4.

5.2.3 Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania

168. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania (TTSA) umepewa majukumu ya kuzalisha na kusambaza mbegu bora za miti na vipandikizi vingine kwa ajili ya uendelezaji wa mashamba ya miti hapa nchini na kuza nchi za nje. Wakala unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Wakala Sura 245, Sera za Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 na Sheria za Misitu Sura 323 na Sheria inayolinda mimea ya mwaka 1997 (Plant Protection Act sura Na 13). Wakala una vituo vinne vya kanda vilivyopo Morogoro, Iringa, Lushoto na Shinyanga.

169. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Wakala wa Mbegu za miti umekusanya tani 14 za mbegu za miti ikilingalishwa na tani sita zilizokusanya mwaka 2015/2016. Jumla ya tani saba zinazoweza kupandwa kwenye maeneo

ya zaidi ya hekta 500,000 zimeuzwa kwa shilingi milioni 648.4. Aidha, Wakala umezalisha miche 300,000 ikilinganishwa na 150,000 mwaka 2015/2016. Hadi Machi 2017, Wakala umeuza miche 158,000 kwa wadau mbalimbali. Vilevile, Wakala umeendelea kutunza vyanzo 35 vya mbegu za miti na kuanzisha vyanzo viwili vya mbegu bora za miti aina ya mikaratusi (*Eucalyptus grandis* na *Eucalyptus tereticornis*); na kutambua na kusajili vyanzo vipyta 20 vya mbegu za miti ya aina mbalimbali.

170. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, Wakala wa Mbegu za miti umepata changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchakavu wa vitendea kazi, na uhaba wa wataalamu katika maeneo ya utambuzi wa mimea. Katika kukabiliana na changamoto hizo Wakala utaainisha fursa za kuongeza mapato ya ndani ili kuweza kujidesha. Aldha, Wakala utaendelea kuboresha vitendea kazi na kuwapatia mafunzo watumishi waliopo pamoja na kuajiri wataalamu wa fani husika.

171. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Wakala umekadiria kukusanya tani 20 na kuza tani 17 za mbegu bora za miti zenyet thamani ya shilingi milioni 850. Aidha, Wakala utazalisha na kuza miche 2,200,000 ya miti yenye thamani ya shilingi milioni 700. Vilevile, majaribio ya namna ya kukusanya na kuhifadhi aina nane za mbegu za miti yatafanyika. Vyanzo 50 vya mbegu bora kutoka misitu ya hifadhi na mashamba ya miti vitaainishwa. Wakala utaanisha vyanzo viwili vya mbegu za miti katika maeneo ya Kanda ya Ziwa na kaskazini na kuanzisha na kutunza eneo la hekta 100 la miti aina ya *Pinus patula*, *Pinus caribaea*, *Pinus tecunumanii*, *Eucalyptus saligna* na *Eucalyptus grandis* iliyoboreshwa. Wakala pia utaendelea kutunza vyanzo vyake 29 vya mbegu kwenye maeneo mbalimbali nchini.

172. Mheshimiwa Spika, Wakala utaendelea kujitangaza na kutafuta masoko ya mbegu za miti kwa kutumia mtandao na machapisho mbalimbali. Katika kutekeleza kazi hiyo, nakala 1,300 za jarida la mbegu kwa ajili ya masoko ya ndani na 200 kwa ajili ya masoko ya nje zitachapishwa.

Aidha, tovuti ya wakala wa mbegu za miti yenye anuwani www.ttsa.go.tz itaendelea kuboreshwa. Ili kurahisisha upatikanaji wa mbegu kwenye Kanda ya Ziwa, Wakala utaimarisha kituo cha kusambaza mbegu za miti kilichopo Shinyanga mjini kwa ajili ya mikoa ya Kagera, Musoma, Mwanza, Geita, Simiyu, Shinyanga, Kigoma na Tabora. Vile vile, Wakala utaendeleza ushirikiano na Sekta Binafsi kwa lengo la kupata mawakala wa kusambaza mbegu bora za miti kwenye maeneo yaliyo mbali na vituo vilivyopo.

5.2.4 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania

173. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) imepewa jukumu la kufanya na kuratibu utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi ya teknolojia bora za uendelezaji wa misitu. Wizara imeendelea kutumia matokeo ya utafiti wa misitu na ufugaji nyuki ili kufanya maamuzi sahihi kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya mazao ya misitu.

174. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Taasisi ilikamilishwa utafiti wa umri sahihi wa kuvuna miti ya Misindano na Misaji unaozingatia uwekezaji (*economic rotation age*). Kufuatia hatua hii, Taasisi inaandaa mwongozo wa kitaalamu (*Technical Order*). Aidha, utafiti kuhusu uzalishaji wa miche bora ya miti ya Msaji, Mkongo, Mvule na Mkangazi kwa kutumia teknolojia ya tishu (*tissue culture*) unaendelea. Shamba mama la miti bora ya Msaji limeanzishwa katika shamba la miti Mtibwa kwa ajili ya kukusanya vikonyo vya kuotesha. Vilevile, TAFORI imefanikiwa kuotesha vikonyo vya miti bora ya Mkongo, Mvule na Mkangazi kwenye bustani.

175. Mheshimiwa Spika, Kufuatia taarifa ya kukauka kwa miti ya kupandwa katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Taasisi imefanya utafiti ili kubaini chanzo halisi cha kukauka kwa miti katika eneo hilo. Utafiti umebaini kuwa miti ya Misindano iliyopandwa kwenye shamba la miti Mbizi lilitopo Wilayani Sumbawanga, inakauka kutokana na udongo kukosa madini ya boroni.

176. Mheshimiwa Spika, Baadhi ya miti ya kigeni inalalamikiwa kutumia kiasi kikubwa cha maji na kusababisha kukauka kwa baadhi ya vyanzo vya maji. TAFORI imejenga uwezo wa kupima kiwango cha matumizi ya maji katika miti, hivyo itasaidia kuelekeza miti inayofaa kupandwa kwa kuzingatia hali halisi ya maeneo.

177. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Taasisi itaendelea kutafiti na kuzalisha miche bora ya miti ya kigeni na ya asili kwa kutumia vikonyo (*cuttings*) na tishu (*tissue culture*). Miche inayozalishwa kwa njia hizni haina mzizi mkuu hivyo inaweza kupunguza matumizi ya maji chini ya ardhi. Katika jitihada za utafiti wa kuzalisha miche bora, Taasisi itaimarisha vitalu vyake vya miti viliwyopo Morogoro, Kwamarukanga (Korogwe) na Kongowe (Kibaha). Aidha, Taasisi itaendelea kufanya utafiti kuhusu kiwango cha maji kinachotumika kwenye mashamba ya miti ya kupandwa ili kupata takwimu sahihi za matumizi ya maji kwa aina mbalimbali za miti inayopandwa nchini. Vilevile, utafiti wa athari zinazosababishwa na moto na uchungaji wa mifugo kwenye uoto wa asili utafanyika. Taasisi itaendelea na utafiti kubaini umri sahihi wa kuvuna miti ya Misindano na ubora wa mbaao kutoka katika mashamba ya miti ya Rubare (Bukoba vijijini), Rubyia (Ukerewe) na Buhindi (Sengerema).

5.2.5 Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki

178. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Chuo cha Misitu Olmotonyi (Arusha); Chuo cha Viwanda vya Misitu (Moshi); na Chuo cha Ufugaji Nyuki (Tabora) vimeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Diploma na Cheti. Aidha, vyuo hivi vimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na ushauri kulingana na mahitaji ya wadau.

179. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI) kimefanya mapitio ya mitaala ili kuhuisha ithibati kulingana na matakwa ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundji (NACTE). Chuo kimeendesha mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi 593. Aidha, mafunzo ya muda mfupi kuhusu moto na

upandaji miti yamefanyika katika mkoa wa Iringa; na mafunzo ya usimamizi shirikishi wa misitu yamefanyika katika mikoa ya Pwani na Kigoma. Jumla ya washiriki 91 walipata mafunzo hayo. Kazi za maendeleo zilizotekelawa ni ukarabati wa nyumba nane za watumishi; na kuendeleza ujenzi wa ukumbi wa mihadhara na bweni la wasichana.

180. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI), kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 98, kati yao 88 ni wa Cheti na 10 ni wa Diploma. Aidha, kazi za ukarabati wa darasa moja, mabweni na ununuvi wa magodoro na vitanda zimetekelawa. Vilevile, kazi ya ujenzi wa maktaba ya Chuo inaendelea.

181. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Chuo cha Ufugaji Nyuki (BTI) kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 160 katika ngazi ya Cheti na Diploma. Aidha, kozi nne za mafunzo ya muda mfupi zimefanyika kwa vikundi vinne vyenye jumla ya washiriki 52.

182. Mheshimiwa Spika, Vyuo vya mafunzo ya misitu na ufgaji nyuki vinakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu na uhaba wa vifaa vya kufundishia. Katika kukabiliana na changamoto hii Wizara itaendelea kukarabati miundombinu na kuboresha vifaa vya kufundishia. Aidha, Wizara itaendelea kufuatilia uidhinishwaji wa muundo wa utumishi kwa wakufunzi wa vyuo vya misitu na ufgaji nyuki nchini.

183. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018 Vyuo vya Misitu na Ufugaji Nyuki vitaendelea kutoa mafunzo kwa kudahili jumla ya wanafunzi 700 kwenye vyuo vya Misitu Olmotonyi (450); Viwanda vya Misitu (100); na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (150). Aidha, Chuo cha Misitu Olmotonyi kitanunua magari mawili na samani za hosteli mpya ya wasichana. Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora kitaendelea na awamu ya pili ya matengenezo ya mfumo wa kuvuna maji ya mvua; kukarabati darasa na nyumba za kituo cha mafunzo kwa vitendo Igombe; kununua vifaa vya maabara, kukamilisha mapitio ya mitaala

na kununua kompyuta 10. Chuo cha Viwanda vya Misitu kitaendelea na ujenzi wa maktaba pamoja na ununuzi wa basi na vifaa vya kufundishia.

5.2.6 Mfuko wa Misitu Tanzania

184. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) ulianzishwa kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa fedha ili kuwezesha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu. Mfuko wa Misitu Tanzania una jukumu la kuwezesha wadau wa sekta ndogo ya misitu na ufugaji nyuki kwenye uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa misitu na ufugaji nyuki katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

185. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017 Mfuko wa Misitu Tanzania ulikadiria kupata shillingi billioni 6.3 na hadi kufikia Machi 2017, shillingi billioni 3.2 sawa na asilimia 51 zilipatikana. Katika kuwezesha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu, Mfuko umetoa ruzuku kwa miradi 135 inayoendelea na miradi 104 mipya. Aidha, Mfuko umewezesha Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania kuchapisha nakala 5,000 za Mwongozo wa Upandaji Miti Tanzania ili kuhakikisha kuwa wadau wa misitu wanapata miongozo stahiki ya upandaji miti na kuwezesha uanzishwaji wa mashamba matatu ya kuzalisha mbegu bora za miti yenye hekta 15. Mfuko pia umeiwezesha TAFORI kununua kifaa cha kupima matumizi ya maji kwenye miti na kuanzisha mashamba ya majaribio ya utafiti yenye hekta 100.

186. Mheshimiwa Spika, Mfuko umewezesha hatua za awali za ujenzi wa maktaba katika Chuo cha Viwanda vya Misitu Tanzania. Ujenzi wa Maktaba hiyo utaboresha utoaji wa mafunzo katika chuo. Aidha, katika kuwezesha elimu kwa jamii, Mfuko umewezesha uandaaji wa vipindi 24 vya redio, vipindi vinne vya televisheni na uchapishaji wa jarida la "Misitu ni Mali". Vilevile, Mfuko umewezesha kufanyika kwa upembusi yakinifu ikiwa ni hatua za awali za kuwezesha uanzishwaji wa mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kuboresha ukusanyaji wa maduhuli ya misitu.

187. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Mfuko utatoa ruzuku kwa miradi 218 inayoendelea na miradi 102 mipyä; utaendelea kuwezesha ujenzi wa maktaba ya Chuo cha Viwanda vya Misitu Tanzania na ujenzi wa jengo la ofisi za Chuo cha Misitu Olmotonyi. Mfuko pia utaboresha kitalu cha miti kinachotumika kutoa mafunzo kwa vitendo katika Chuo cha Misitu Olmotonyi. Aidha, Mfuko utaendelea kuwezesha uchapishaji wa nakala 4,000 za jarida la "Misitu ni Mali" na kusambazwa, kwa lengo la kutoa elimu kwa umma. Mfuko kwa kushirikiana na TFS, utaandaa mpango wa kuanzisha kiwanda cha kuboresha na kuongeza thamani ya mazao ya nyuki. Vilevile, Mfuko utawezesha kununua magari 10 na pikipiki 14 kwa ajili ya TFS, vyuo vya mafunzo, na TAFORI.

5.2.7 Miradi ya Maendeleo

188. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza miradi ya maendeleo katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa mazao ya misitu, kujenga uwezo wa taaluma, kuwezesha jamii kushiriki kwenye usimamizi wa misitu, kuimarisha mtandao wa misitu asilia na kutunza bioanuai.

5.2.7.1 Programu ya Panda Miti Kibiashara

189. Mheshimiwa Spika, Programu hii inatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na Finland, ikiwa na lengo la kupunguza umaskini kwa kuwashamasisha wananchi kupanda miti kibiashara. Programu hii imetekelawa katika Mikoa ya Njombe, Iringa, Ruvuma na Morogoro. Aidha, imewezesha kuanzishwa vikundi 120 vyenye wanachama zaidi ya 8,000 na kupanda miti bora zaidi ya hekta 10,000. Vilevile, programu imewezesha kuanzishwa kwa mtaala wa kufundisha elimu ya misitu katika vyuo vya VETA; kuanzisha vikundi 28 vya VICOBA pamoja na kuanzisha kituo cha mafunzo ya muda mfupi ya usimamizi misitu na viwanda vya misitu kilichopo Mafinga mjini.

190. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018 Mradi utatekelezwa katika wilaya za Mufindi, Kilolo, Njombe, Makete, Ludewa, Songea na Kilombero. Kazi zitakazofanyika ni kuwezesha vikundi 120 kupanda jumla ya hekta 4,000 za miti; kufanya aina nane za utafiti kuhusu misitu binafsi; kuendeleza na kuendesha mafunzo ya muda mfupi katika kituo cha mafunzo Mafinga; kuwezesha wanafunzi 30 kupata mafunzo VETA kwa mwaka mmoja. Programu pia, itawezesha ubadilishanaji uzoefu kati ya vijiji na wadau wengine kupitia ziara za mafunzo, kuandaa na kusambaza seti kumi za vifaa vya mawasiliano; na kuwezesha shughuli za uzalishaji mali kwa kaya 100 zinazojihusisha na upandaji miti.

5.2.7.2 Mradi wa Kuimarisha Mtandao wa Hifadhi ya Misitu kwa Utunzaji wa Bioanuai Tanzania

191. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuimarisha Mtandao wa Hifadhi ya Misitu kwa Utunzaji wa Bioanuai Tanzania (Enhancing the Forest Nature Reserve Network for Biodiversity Conservation in Tanzania) unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na UNDP. Mradi unatekelezwa katika Misitu ya Hifadhi za Mazingira Asilia 12 kwa kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa hifadhi hizo na kuboresha miundombinu ya hifadhi ili kukuza utalii na ustawi wa ikolojia.

192. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, misitu ya hifadhi asilia mipya nane imetangazwa kwenye gazeti la serikali, mipaka ya misitu hiyo imesafishwa na kuwekewa *beacons* na mipango ya usimamizi wa misitu 12 imekamilika. Magari mapya matano yamenunuliwa na kazi ya ujenzi wa ofisi sita za wahifadhi na vituo (Ranger posts) 15 imeanza.

193. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2017/2018 Mradi utaendelea na ujenzi wa ofisi sita za Misitu ya Hifadhi za Mazingira Asilia (Chome, Magamba, Minziro, Mkingu, Uzungwa na Magamba) pamoja na vituo 15 katika hifadhi hizo. Aidha, utaandaa na kutekeleza makubaliano ya

usimamizi wa pamoja (Joint Forest Management); utaimarisha miundombinu ya utalii ikolojia; na kutangaza vivutio vya utalii katika hifadhi 12 za Mazingira asilia.

5.2.7.3 Mradi wa Kuwezesha Jamii Katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu na Mabadiliko ya Tabia Nchi

194. Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuwezesha jamii katika usimamizi shirikishi wa misitu na mabadiliko ya tabia nchi (Empowering Communities through Training on PFM, REDD+ and Climate Change Initiatives – ECOPRC) unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Norway. Mradi huu upo chini ya Usimamizi wa Chuo cha Misitu Olmotonyi na unatekelezwa kwa pamoja na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), Taasisi ya *Regional Community Forestry Training Centre for Asia and Pacific* (RECOFTC) ya Thailand na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine. Katika mwaka 2016/2017, mradi uliwezesha Halmashauri za Wilaya na NGO's kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Hewa Ukaa na Ukataji Miti (MKUHUMI) na Mabadiliko ya Tabianchi; kuboresha miundombinu ya Chuo cha Misitu-Olmotonyi; na kuendeleza programu hiyo katika wilaya za Bagamoyo, Kilombero, Kiteto na Same.

195. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Mradi utaendelea kuboresha miundombinu ya Vyuo vya Misitu; kujenga uwezo wa watumishi wa Halmashauri za Wilaya na Taasisi zisizo za Kiserikali katika kutoa huduma za mipango na shughuli za Usimamizi Shirikishi wa Misitu, MKUHUMI, mabadiliko ya tabianchi; na kurekodi vipindi 100 vya radio katika Wilaya za Bagamoyo, Kilombero, Kiteto na Same.

5.2.7.4 Mradi wa Kujenga Uwezo wa Vyuo vya Misitu na Nyuki Nchini

196. Mheshimiwa Spika, Mradi wa kujenga uwezo wa vyuo vya Misitu na Nyuki nchini unatekelezwa kwa fedha za ndani. Mradi unalenga kujenga uwezo wa taasisi za mafunzo na utafiti zilizopo chini ya Idara ya Misitu na Nyuki kutekeleza

majukumu yao. Mwaka 2016/2017, kazi iliyofanyika ni kuendelea na ujenzi wa Maabara ya Nyuki, Njiro. Katika mwaka 2017/2018, mradi utaendelea kuboresha miundombinu ya taasisi.

5.3 Sekta Ndogo ya Utalii

197. Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Sekta ndogo ya Utalii ni kuendeleza utalii nchini na kuhakikisha inachangia ipasavyo katika Pato la Taifa. Majukumu hayo hutekelezwa kwa ushirikiano na sekta nyininge za umma na binafsi. Katika kutekeleza majukumu yake, Sekta hiyo inaongozwa na Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 na Sheria ya Utalii Sura 29.

198. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni maarufu duniani kwa utalii wa vivutio vyta wanyamapori, kupanda Mlima Kilimanjaro na kutembelea maeneo yenye masalia ya binadamu wa kale katika Bonde la Olduvai. Ubora wa kiikolojia wa Hifadhi zetu za Taifa, hali ya amani na utulivu uliopo nchini, utawala bora, mazingira mazuri ya uwekezaji na ukarimu wa Watanzania, vimekuwa chachu ya ustawi wa sekta ya Utalii hapa nchini. Hivi sasa juhudini zinafanya kwa kuainisha maeneo ya fukwe kutoka pwani ya Tanga hadi Mtwara ili yatumike kuendeleza shughuli za utalii wa fukwe. Napenda kuchukua fursa hii kuwaomba wadau wawekeze katika hoteli katika fukwe zetu za Bahari ya Hindi na maziwa makuu na kuendeleza michezo ya kwenye maji (water sports).

199. Mheshimiwa Spika, Mapato ya Utalii yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2016 mapato kutokana na utalii yalikuwa Dola za Marekani bilioni 2 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 1.9 zilizopatikana katika mwaka 2015. Ongezeko la mapato hayo limetokana na kuongezeka kwa watalii wa nje ambao katika mwaka 2015 walikuwa 1,137,182 na katika mwaka 2016 walikuwa watalii 1,284,279.

200. Mheshimiwa Spika, Juhudi kubwa zimefanywa ili kupanua wigo wa vivutio vyta utalii kwa kuhamasisha

wananchi kuanzisha na kuendeleza miradi ya utalii wa utamaduni. Miradi hiyo imeongezeka kutoka 60 mwaka 2015 hadi kufikia miradi 66 kwa mwaka 2016.

201. Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya Utalii inajumuisha Idara ya Utalii, Bodi ya Utalii Tanzania na Chuo cha Taifa cha Utalii.

5.3.1 Idara ya Utalii

202. Mheshimiwa Spika, Jukumu kuu la Idara ya Utalii ni kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Utalii, kanuni na miongozo inayosimamia maendeleo ya Utalii nchini. Aidha, Idara inaratibu utekelezaji wa Sera hizo kitaifa katika mamlaka za Serikali za Mitaa katika nyanja za maendeleo ya Utalii.

203. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Mapitio ya Sera ya Utalii yamefanyika na kazi inayoendelea ni kukusanya maoni ya wadau. Aidha, Wizara imeendelea na kazi ya kupanga huduma za malazi na chakula katika daraja za ubora kwa viwango vya katil ya nyota moja hadi tano. Huduma za malazi na chakula 203 zimekaguliwa katika mkoa wa Dar es Salaam.

204. Mheshimiwa Spika Kati ya huduma zilizokaguliwa, huduma 53 zilipata nyota ifuatavyo; nyota tano (1) nyota nne (2) nyota tatu (13) nyota mbili (31) na nyota moja (6). Aidha, huduma za malazi 18 ambazo hazikufikia kiwango cha kupata nyota moja zilipewa hadhi ya kuthibitishwa (*approved facilities*). Huduma 132 hazikufuzu kwa kiwango kinachotakiwa. Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kuwezesha huduma ambazo hazikufuzu ziweze kuboreshwa kufikia kiwango kinachotakiwa.

205. Mheshimiwa Spika, Faida ya kuweka huduma za malazi katika daraja za ubora ni kuwezesha wageni kufahamu viwango vya ubora wanavyotarajia kupata, wenye huduma za malazi kupata urahisi wa kujitangaza kibiashara na Serikali kuweza kufuatilia utoaji wa huduma

kulingana na vigezo vya ubora. Kupitia Bunge lako Tukufu ninawashauri wenye nia ya kuwekeza katika huduma za malazi na chakula, kutumia vigezo vya ubora vinavyopaswa kuzingatiwa kuanzia hatua za ujenzi hadi utoaji huduma. Vigezo hivyo vinapatikana Wizarani na wataalamu wako tayari kutoa ushirikiano pale watakapohitajika.

206. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa ushirikiano na UNDP kupitia Mradi wa Kuimarisha Mtandao wa Maeneo Yaliyohifadhiwa Ukanda wa Kusini (SPANEST) na sekta binafsi imewezesha mafunzo ya muda mfupi kwa watoa huduma 333 katika fani za huduma za malazi, mapishi na vinywaji kutoka mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe na Songwe. Mafunzo hayo yaliyotolewa kupitia Chuo cha Taifa cha Utalii yalikusudia kuboresha huduma zitolewazo kwa watalii na wateja wengine mbalimbali. Kazi hii itaendelea kwa mikoa mingine nchini ili kuinua viwango vya utoaji huduma katika tasnia ya ukarimu.

207. Mheshimiwa Spika, Wizara imekusanya maduhuli yanayotokana na ada za leseni za biashara za utalii ambayo yameongezeka kutoka shilingi bilioni 4.1 (mwaka 2015) hadi bilioni 5.6 (mwaka 2016) likiwa ni ongezeko la asilimia 36. Ongezeko hilo limetokana hasa na matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa usajili na utoaji leseni na ongezeko la kampuni zinazotoa huduma ya utalii kutoka 1,087 (2015) hadi 1,244 mwaka 2016.

208. Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio hayo maendeleo ya sekta ya utalii nchini bado yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti, mfumo wa malipo wa fedha taslimu badala ya kadi za kibenki za malipo (Visa, Amex, Mastercard), idadi ndogo ya huduma za malazi, mtazamo hasi wa jamii kwa wahudumu wa tasnia ya ukarimu na huduma hafifu zitolewazo, gharama za juu za huduma za utalii, na shirika letu la ndege kutokuwa na safari za moja kwa moja kutoka masoko makuu ya utalii, mabadiliko ya tabianchi yanayotishia uwepo na ubora wa vivutio vya utalii.

209. Mheshimiwa Spika, Katika kukabili changamoto hizo, Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa sekta ya utalii inaendelezwa na kuimariswa kwa kuainisha vivutio vipyta vyta utalii na kuendeleza vilivyopo; kuvutia uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi; kuboresha huduma na kujenga weledi na uaminifu kwa watoa huduma wa sekta ya utalii, kuhakiki ubora wa huduma za ukarimu na utalii pamoja na kutangaza utalii.

210. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2017/2018, Wizara itaweka msisitizo katika kutangaza utalii katika nchi ambazo zimeendelea haraka kwa siku za hivi karibuni, kama Uyahudi, China na Urusi.

211. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka, 1999 na Kanuni za kusimamia vyuo vinavyotoa Mafunzo ya Utalii na Ukarimu. Aidha, itaendelea kukusanya na kuchambua takwimu za utalii na kufanya ukaguzi kwa wafanyabiashara; kubaini vivutio vipyta vyta utalii katika mikoa ya Mbeya, Mwanza, Geita, Manyara, Mara na Kigoma; na kuandaa na kushiriki maonesho mbalimbali ya utalii ndani na nje ya nchi. Vilevile, Wizara itaendelea kupanga huduma za malazi katika daraja za nyota kwa mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Tanga na Mwanza; na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa watoa huduma 500 katika fani ya Utalii na Ukarimu.

212. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuibua vyanzo vipyta vyta mapato na kuendeleza vivutio vyta utalii ili kupanua wigo wa kukusanya maduhuli. Aidha, itaimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa maduhuli; kuhamasisha uwekezaji katika biashara za utalii; na kuimariswa ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

5.3.2 Bodi ya Utalii Tanzania

213. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) imepewa jukumu la kutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi. Jukumu hilo linatekelezwa kwa mujibu wa Sheria

ya Bodi ya Utalii Na. 364 ya mwaka 1992 iliyopitiwa upya mwaka 2002.

214. Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Utangazaji Utalii 2012 – 2017 ambao kwa sasa unafanyiwa mapitio, umeainisha masoko ya utalii na mbinu za kuyafikia. Katika mwaka 2016/2017, Bodi ilishiriki maonesho 11 na kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania. Maonesho hayo ni WTM (Uingereza), ITB (Ujeruman) MITT (Urusi), COTTM (China), INDABA na WTM – Africa (Afrika Kusini), Dutch Expo (Uholanzi), OTM (India), ATM na MICE ARABICA (Dubai) na The Pearl of Africa Expo (Uganda). Aidha, Bodi inaendelea kuandaa mikakati mahususi ya utangazaji utalii katika masoko makuu ya nchi za Uingereza, Ujeruman na Marekani.

215. Mheshimiwa Spika, Katika juhudzi za kupanua wigo wa vivutio vya utalii na kutangaza utalii wa historia na malikale, Bodi kuititia onesho la kimataifa la utalii liliofanyika nchini Ujeruman (ITB) mwezi Machi, 2017, ilionyesha kielelezo cha nyayo za zamadamu wa laetoli za miaka million 3.6 iliyopita pamoja na picha za wanyama na ndege wa kale. Kielelezo hicho kilivutia watu wengi kutembelea banda la Tanzania ili kujua chimbuko la historia ya binadamu. Aidha, Bodi ya Utalii kwa kushirikiana na Makumbusho ya Taifa imeandaa kielelezo kipyga cha tembo wa zamani walioishi katika Bonde la Olduvai miaka million 1.5 iliyopita ikiwa ni juhudzi za kutangaza utalii wa historia na malikale.

216. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017 Bodi iliwezesha wataalam wanne wa mifumo ya TEHAMA kupata mafunzo kwa vitendo katika Bodi ya Utalii Dubai na RETOSA. Mafunzo hayo yatawezesha kuanzishwa kitengo maalum cha kutangaza na kuvutia watalii kwa njia ya mtandao. Mfumo huo utawezesha mteja kuwasiliana moja kwa moja na mtoa huduma na hivyo kutoa fursa ya ushawishi kwa wageni kutembelea Tanzania.

217. Mheshimiwa Spika, Bodi kuititia mradi unaotekelizwa kwa ushirikiano na USAID na UNDP imetengeneza tovuti ya Utalii ya Tanzania yenye anuani

www.tanzaniatourism.com. Aidha, imeandaa programu inayojulikana kwa jina la “Application” inayopatikana katika vyombo nya mawasiliano nya simu na kompyuta kwa lengo la kuimarisha utangazaji wa utalii kwa gharama nafuu. Tovuti hiyo itawezesha watalii kupata taarifa za vivutio na kununua huduma kwa urahisi.

218. Mheshimiwa Spika, Ili kukuza utalii wa ndani, Bodi imeshiriki maonesho ya utalii na matukio ya hapa nchini. Maonesho hayo ni Saba Saba, Nane Nane, Wili ya Utalii Duniani, Karibu Travel and Tourism Fair, Kili Fair, Serengeti Cultural Festival, Hydom Tourism Festival, Karibu Kusini na Onesho la Utalii Nyasa. Aidha, ilishiriki Kumbukumbu ya Vita vya Maji Maji, Songea na tukio la kupatwa kwa Jua ambalo lilionekana vizuri zaidi katika mji wa Rujewa Wilayani Mbarali. Kupitia maonesho na matukio haya, Bodi ilitoa elimu juu ya utalii wa ndani na kugawa vipeperushi na majarida ya vivutio nya Utalii nya Tanzania.

219. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii imeshirikiana na vituo nya televisheni na redio nchini katika kurekodi na kurusha vipindi nya utalii. Vituo hivyo ni pamoja na TBC Redio na Televisheni (Hifadhi zetu, Ijue Hifadhi ya Ngorongoro); Channel Ten (Utalii wa ndani); Clouds TV (Kipindi cha 360 Talii na TTB); Star TV (Ijue Hifadhi ya Ngorongoro); na ATN (kupitia vipindi nya michezo na matangazo ya biashara katika Uwanja wa Taifa Dar es Salaam). Aidha, Bodi imeshirikiana na “wanablogs” maarufu hapa nchini katika kutangaza utalii kupitia mitandao ya kijamii.

220. Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua nafasi hii kuvishukuru vyombo vyote nya habari viliviyotangaza utalii wa Tanzania kwa uzalendo wao. Naendelea kuwahimiza Watanzania wengi kuendelea kuhamasika na kushiriki katika utalii wa ndani.

221. Mheshimiwa Spika, Serikali imetumia fursa ya ujio wa viongozi mbalimbali walitembelea Tanzania kuingia makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya utalii. Viongozi waliohusika ni kutoka China, Falme za Kiarabu (UAE),

Morocco, Uturuki, Ethiopia na Afrika Kusini. Vile vile, Serikali imeimarisha ushirikiano na nchi ya Ethiopia katika nyanja za uchumi ikiwemo kusafirisha watalii wanaokuja nchini. Napenda kuchukua fursa hii kuyashukuru mashirika yote ya ndege yanayofanya safari zao hapa nchini kwa mchango wao mkubwa katika maendeleo ya sekta ya utalii. Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Shirika la ndege la Ethiopia (Ethiopian Airlines) kwa kuwa mshirika mkubwa wa maendeleo ya sekta ya utalii tangu Shirika hilo lilipoanza safari zake hapa nchini zaidi ya miaka 40 aliyopita.

222. Mheshimiwa Spika, Katika juhudzi za kukuza biashara na soko la China, Bodi imeratibu ziara ya waandishi wa habari wa Kituo cha Televisheni cha "*China Anhui*" chenye watazamaji zaidi ya milioni 800. Wanahabari hao wamewasili nchini mwezi huu wa Mei, 2017 na watatembelea Pori la Akiba Selous, Kisiwa cha Pemba na Hifadhi ya Ngorongoro. Kufuatia ziara hiyo, kipindi maalum kwa jina la "*Our Venture in Tanzania*" kitarushwa hewani ili kuvutia watalii kutoka China kutembelea Tanzania.

223. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2016 Bodi imeratibu ziara ya wapiga picha wa Kampuni ya Filamu ya "Polyphon" pamoja na wacheza sinema wa tamthilia ya "Traum Schiff" kutoka Ujerumani. Picha za filamu na tamthilia hiyo zimepigwa katika maeneo ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na Bonde la Ngorongoro. Picha hizo zilirushwa kwenye Televisheni za Ujerumani kuanzia mwezi Aprili, 2017. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na sekta binafsi, imetengeneza jarida la utalii kwa lugha ya Kijerumani (Tansania Der Traum von Afrika); na majarida, vipeperushi, na filamu fupi (DVD) kwa lugha ya Kifaransa. Vilevile, jumla ya nakala 10,000 za jarida hilo pamoja na majarida na vipeperushi mbalimbali 9,650 vya lugha ya Kiingereza vilisambazwa ndani na nje ya nchi.

224. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii imeingia makubaliano ya ushirikiano na Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) katika kutangaza utalii. Kufuatia makubaliano hayo jarida la ATCL liitwalo "Safari Njema" (inflight magazine) limeanzishwa kwa lengo la kutoa habari za vivutio vya utalii

wa Tanzania na usafiri wa anga. Nakala 2,000 zimechapishwa na kuwekwa kwenye ndege za ATCL. Aidha, jarida hilo itaendelea kuchapishwa kila robo mwaka.

225. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa utalii; ilifanikisha ziara ya watalii 200 kutoka Marekani ambao walitembelea hifadhi za Mikumi na Saadani mwezi Desemba, 2016. Watalii hao walifika nchini kwa kutumia meli ya kitalii iitwayo *Silversea Cruise Ship*.

226. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Bodi itaendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Bodi itaweka mabango makubwa (Billboards) katika maeneo ya mpakani ya Namanga na Tunduma; viwanja vya ndege KIA, JNIA, Songwe na Mwanza. Aidha, Bodi itaweka matangazo ya utalii kwenye vituo vya mabasi ya mwendo kasi Dar es Salaam; na matangazo ya kielektroniki (LED Screen) katika maeneo muhimu yaliyopo Makao Makuu, Dodoma.

227. Mheshimiwa Spika, Bodi itatoa semina ya utalii na huduma kwa mteja kwa wafanyakazi wa mashirika ya ndege na viwanja vya ndege ili waweze kuvitangaza vivutio vya utalii wa Tanzania. Aidha, Bodi inaandaa mikakati ya utangazaji utalii mahsus kwa masoko ya Israel, Morocco, China, Ethiopia na Uturuki kwa mujibu wa mikataba ya ushirikiano iliyosainiwa katika mwaka 2016/2017. Bodi itaratibu onesho la tatu la kimataifa liitwalo *Swahili International Tourism Expo (SITE)* litakalofanyika Dar es Salaam mwezi Oktoba 2017 na kushiriki kwenye maonesho ya *Karibu Travel and Tourism Fair* na *Kili Fair* yaliyopangwa kufanyika mwezi Juni 2018.

228. Mheshimiwa Spika, Bodi itaendelea kuhimiza utalii wa ndani kupitia matangazo ya Redio na Televisheni, kutoa ushauri wa kitaalam katika vikundi 65 vya utalii wa kitamaduni na kuhamasisha uanzishaji wa vikundi vingine hasa katika Kanda za Kusini, Magharibi na Ziwa. Aidha, Bodi itaendelea kutangaza utalii kupitia wadau wa sanaa na michezo.

5.3.3 Chuo cha Taifa cha Utalii

229. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) kilianzishwa kwa Sheria ya Wakala za Serikali Sura 245 kupitia Tamko la Kuanzisha Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii la mwaka 2003. Jukumu la Chuo ni kutoa mafunzo, utafiti na huduma za ushauri katika fani za ukarimu na utalii katika ngazi ya Cheti na Diploma. Aidha, chuo kinatoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau wa sekta ya Utalii.

230. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 155 katika ngazi ya Cheti na Diploma na 164 walihitimu katika fani ya Utalii na Ukarimu. Aidha, Chuo kiliendesha programu ya uanagenzi (apprenticeship) kwa washiriki 100. Programu ya Uanagenzi inatolewa kwa ushirikiano baina ya Wizara, Shirikisho la Vyama vya Utalii (TCT), Chama cha Wamiliki wa Hoteli Tanzania (HAT) na Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa ufadhilli wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Norway (NORAD).

231. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Chuo kimeendelea kuwa mwanachama hai wa Chama cha Vyuo vitoavyo mafunzo ya Ukarimu na Utalii Duniani (International Association of Hotel Schools) chenye jumla ya wanachama 140. Kupitia chama hiki Chuo kimepata fursa ya kushiriki katika makongamano na vipindi vya kitaaluma. Kutokana na ushiriki wake Chuo kimepata uzoefu wa kitaaluma na kuanzisha ushirikiano na vyuo vingine ndani na nje ya nchi.

232. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2017/2018 Chuo kitadahili wanafunzi wa Cheti na Diploma 315, wanagenzi 200 na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 420. Aidha, maandalizi ya mitaala ngazi ya 4, 5 na 6 katika Uendeshaji wa Matukio (Event Management) yatafanyika.

5.3.4 Tozo ya Maendeleo ya Utalii

233. Mheshimiwa Spika, Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy - TDL) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utalii ya mwaka 2008 kifungu 59 na kuanza kutumika

rasmi mwaka 2013. Lengo la TDL ni kuendeleza na kusimamia ubora wa huduma za utalii, kujenga uwezo wa watumishi pamoja na kununua vitendea kazi, kutangaza utalii, mafunzo katika tasnia ya utalii, na utafiti. Hadi Machi 2017 shilingi billioni 5.6 zimepokelewa kutoka TANAPA na NCAA.

234. Mheshimiwa Spika, Kazi zilizofanyika kuititia TDL ni kusaidia mapitio ya Sera ya Taifa ya Utalii, kubaini maeneo ya uwekezaji utalii ukanda wa Pwani, mafunzo kwa watoa huduma katika huduma za malazi, chakula na vinywaji kwa mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe, ukarabati wa miundombinu katika Chuo cha Taifa cha Utalii na utangazaji wa utalii. Kwa mwaka 2017/2018, TDL itaendelea kusaidia kazi za maendeleo ya utalii, mafunzo ya utalii na utangazaji utalii.

5.3.5 Miradi ya Maendeleo

5.3.5.1 Mradi wa Ujenzi wa “Theme Park”

235. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Wizara itatekeleza Mradi wa Ujenzi wa “Theme Park” kwenye eneo la hekta 10,000 katika mwambao wa Bahari ya Hindi jijini la Dar es Salaam. Mradi huu utatoa fursa ya huduma mbalimbali kama vile mapumziko, burudani na michezo; kumbukumbu za kihistoria, hoteli zenyet hadhi, migahawa, maduka na bustani ya wanyama kupatikana mahali pamoja.

236. Mheshimiwa Spika, Mradi wa “Utalii House Phase II” unahuksu kuendeleza ujenzi wa ofisi za Bodi ya Utalii zilizopo kwenye mtaa wa Laibon, Oysterbay Dar es Salaam. Kwa mujibu wa makubaliano, Serikali ya Marekani imejenga awamu ya kwanza na Serikali ya Tanzania ina jukumu la kujenga awamu ya pili. Katika mwaka 2017/2018, kazi zitakazofanyika ni kuandaa michoro na kumtafuta mkandarasi.

5.3.5.2 Mradi wa Kusimamia Maliasili na Kuendeleza Utalii wa Ukanda wa Kusini

237. Mheshimiwa Spika, Wakati nawasilisha bajeti ya Wizara yangu 2016/2017, nilitoa taarifa hapa Bungeni kuwa Wizara yangu inafanya maandalizi ya Mradi wa Kusimamia Maliasili na Kuendeleza Utalii wa Ukanda wa Kusini unaoitwa Resilient Natural Resource Management for Tourism and Growth (REGROW). Mradi huu utatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Mradi huu wa miaka mitano utaanza kwa awamu ya kwanzza kuanzia mwaka 2017/2018 na utatekelezwa katika hifadhi za Pori la Akiba la Selous, Hifadhi za Taifa za Ruaha, Mikumi na Udzungwa na maeneo ya jirani.

238. Mheshimiwa Spika, Mradi unalenga kuongeza ubora wa vivutio vya utalii kwa kuimarisha miundombinu ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege na kambi za watalii; kuboresha usimamizi wa maliasili hususan rasilimali za maji katika Mto Ruaha Mkuu na kurejesha hali ya mto huo kutiririka mwaka mzima; na kuongeza faida za kiuchumi kwa jamii zinazoishi kandokando ya hifadhi hizo kwa kuimarisha shughuli za utalii wa utamaduni, shughuli za kujiongezea kipato kupitia kilimo na kujenga uwezo wa vijana wa maeneo hayo kushiriki katika biashara za utalii. Mradi utachangia kufikia lengo la watalii milioni 8 na dola za Marekani bilioni 20 kila mwaka kufikia mwaka 2025.

5.4 Sekta Ndogo ya Malikale

239. Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya Malikale imepewa majukumu ya kuandaa, kusimamia na kudurusu sera, sheria, kanuni na miongozo kuhusu urithi na utamaduni wa Taifa. Sekta ya Malikale inatekeleza majukumu haya kwa kuzingatia Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997; Sera ya Malikale ya mwaka 2008; Sheria ya Malikale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281. Sekta ndogo ya Malikale

inajumuisha Idara ya Mambo ya Kale na Shirika la Makumbusho ya Taifa.

5.4.1 Idara ya Mambo ya Kale

240. Mheshimiwa Spika, Idara hii imepewa majukumu ya kutayarisha na kusimamia Sera, Sheria, kanuni na miongozo ya kuendeleza na kutangaza urithi na utamaduni wa Taifa. Aidha, Idara inahusika na kutafiti, kutambua, kuhifadhi, kulinda, kuendeleza na kutangaza urithi na utamaduni wa Taifa.

241. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Malikale Sura 333 haitoi fursa kwa wadau kushiriki katika uhifadhi na uendelezaji wa malikale. Aidha, hajizingatia suala la uwekezaji katika kuendeleza malikale, pamoja na urithi wa malikale usioshikika na ule uliopo katika maji. Wizara inafanya mapitio ya Sheria hiyo ili iendane na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimazingira.

242. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya mji wa Mtwara-Mikindani na wadau wengine imekarabati Boma la Mikindani lenye umri wa zaidi ya miaka 100; gofu la kihistoria lillotumika kutoza ushuru wakati wa Utawala wa Mjerumani; nyumba aliyoishi Dr. Livingstone; na nyumba aliyoishi Gavana wa Kijerumani.

243. Mheshimiwa Spika, Wizara imepima na kuweka mipaka ya mji wa kihistoria wa Mikindani. Maeneo ya kihistoria ya mji huo yameainishwa na kuoneshwa kwenye ramani ya mji kwa ajili ya kutangazwa kuwa urithi wa Taifa. Aidha, Wizara imeandaa mwongozo na sheria ndogo kwa ajili ya uhifadhi na matumizi endelevu ya Mji wa Mikindani kwa lengo la kuimarisha uhifadhi wa mji huo.

244. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Mkoa wa Iringa na Chuo Kikuu cha Iringa kupitia mradi wa "Fahari Yetu" uliofadhliliwa na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya imekarabati Boma la Mjerumani lillojengwa mwaka 1900 na

kulifanya kuwa Makumbusho ya Mkoa wa Iringa na Kituo cha Utamaduni. Ukarabati wa Boma hilo, umewezesha kuwepo kwa Makumbusho ya Mkoa, maduka ya zawadi, studio ya muziki wa asili, na mgahawa ndani ya jengo hilo.

245. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya utafiti wa malikale kwa lengo la kubaini, kuhifadhi na kufanya matumizi endelevu ya rasilimali za malikale. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imefanya tafiti 13 kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje kwa lengo la kuhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za malikale. Utafiti huo umefanyika katika mikoa 16 nchini ambayo ni Lindi, Iringa, Tanga, Arusha, Mbeya, Manyara, Kilimanjaro, Tabora, Dar es Salaam, Njombe, Dodoma, Mtwara, Morogoro, Mwanza, Pwani na Katavi.

246. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Wizara imegundua nyayo nyingine za zamadamu na wanyama zenyenye umri wa miaka milioni 3.6 katika eneo la Laetoli, Mkoani Arusha. Ugunduzi huo umefanya maeneo yenye nyayo kufikia matatu ambayo ni Laetoli (2) na Engaresero (1). Vilevile, katika Mkoa wa Ruvuma Wilaya ya Mbanga, tarafa ya Mburi Wizara imebaini uwepo wa Jiwe la Mburi na unyayo kwenye jiwe hilo unaofanana na wa binadamu. Jiwe hilo linatumika kwa shughuli za kimila. Aidha, utafiti umebaini uwepo wa mapango ya Matiri yaliyopo Kindimba Juu na Kindimba Chini ambayo yalitumika kujificha wakati wa vita vya Majimaji.

247. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mjumbe wa Kamati ya UNESCO ya Urithi wa Dunia kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2015 hadi 2019 na pia ni makamu mwenyezekiti wa Kamati ya Urithi wa Dunia kwa kipindi hicho. Wizara imeshiriki mkutano wa 40 wa Kamati ya Urithi wa Dunia uliofanyika Istanbul, Uturuki mwezi Julai, 2016. Katika Mkutano huo, Tanzania ilipewa muda wa mwaka mmoja kufuatilia utekelezaji wa vigezo vya uhifadhi wa magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara na kuwasilisha taarifa UNESCO. Taarifa ya utekelezaji kuhusu maeneo hayo ambayo

yalikuwa hatarini kutoweka na baadaye kurejeshwa katika Orodha ya Urihi wa Dunia imeandaliwa na itawasilishwa katika mukutano utakaofanyika Oktoba, 2017.

5.4.2 Mfuko wa Mambo ya Kale

248. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mambo ya Kale ulianzishwa kwa sheria Na. 22 ya mwaka 1979 ukiwa na majukumu ya kuhifadhi na kufanya utafiti juu ya malikale. Kazi zilizotekelawa katika mwaka 2016/2017 ni kufanya ukarabati wa majengo ya kale, kuwezesha utafiti mbalimbali, kupima na kuweka mipaka ya mji wa kihistoria wa Mikindani na kukusanya milioni 811.9. Katika mwaka 2017/2018, Mfuko unakadiria kukusanya shilingi milioni 825. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kujenga kituo cha taarifa cha Mbozi, utafiti, na uendelezaji wa vituo vya mambo ya kale.

249. Mheshimiwa Spika, Kutokana na uwepo wa Malikale nchi nzima, kuna changamoto ya ufinyu wa bajeti na watumishi kuweza kuzifikia na kuzihifadhi kikamilifu. Aidha, kuna uharibifu wa malikale unaoendelea ikiwa ni pamoja na ubomoaji wa majengo na uvamizi wa maeneo ya kihistoria. Vilevile, kuna miundombinu isiyoridhisha katika maeneo mengi ya kihistoria; ushiriki mdogo wa jamii katika uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za urithi wa utamaduni; na jamii kutothamini na kutunza rasilimali za malikale.

250. Mheshimiwa Spika, Katika kukabiliana na changamoto zilizopo, Wizara itaendelea kurekebisha Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na kuendelea kuhamasisha jamii kutambua thamani na umuhimu wa Malikale. Aidha, Wizara itaimarisha na kuboresha mazingira katika uhifadhi na uendelezaji wa Malikale kiutalii. Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo jumuiya za kikanda na kimataifa katika uhifadhi, uwekezaji na uendelezaji wa maeneo ya Malikale. Vilevile, itaendelea kujenga uwezo wa kiutendaji katika nyanja za uhifadhi, utafiti na uwekaji wa kumbukumbu za malikale na kuhamasisha halmashauri na taasisi nyingine kuajiri Wataalam wa Mambo ya Kale.

251. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuhifadhi, kuboresha na kuendeleza maeneo ya malikale na kukuza utalii. Wizara itajenga kituo cha kumbukumbu na taarifa cha Amboni, banda la kutolea mihadhara na njia za waenda kwa miguu katika Magofu ya Kaole na uzio katika Magofu ya Kunduchi. Vile vile, Wizara itakarabati jengo la Makumbusho la Caravan Serai na jengo la Afya Tabora; kuandaa makisio ya kuboresha mandhari ya Kituo cha Kumbukumbu ya Dr. Livingstone yaliyopo Ujiji na Kituo cha Mji Mkongwe kilichopo Bagamoyo.

5.4.3 Shirika la Makumbusho ya Taifa

252. Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa lilianzishwa kwa Sheria Sura 281 na limepewa majukumu ya kutafiti, kuhifadhi, kukusanya, kuonesha na kuelmisha umma kuhusu urithi wa utamaduni wa asili wa Taifa. Aidha, Shirika linaonesha na kuelezea chimbuko na maendeleo ya binadamu, historia na utamaduni wa Taifa la Tanzania.

253. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Shirika limeboresha maonesho katika makumbusho zake kwa kubadili vioneshwa, mipangilio ya maonesho na maeleo ya vioneshwa (captions). Jumla ya maonesho 24 yamefanyika, kati ya hayo 14 ni ya kawaida (kwenye ofisi za makumbusho), tisa ya jukwaani na moja la uwanjani ambalo liliifanyika kwenye Viwanja vya Maonesho ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba). Mionganoni mwa maonesho yaliyofanyika yalihusisha wasanii wa sanaa za kazi za mikono na jukwaani ili kuwapa fursa ya kuonesha, kutangaza na kukuza sanaa na utamaduni wa Mtanzania.

254. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Shirika limehifadhi mikusanyo na nyaraka mbalimbali. Mikusanyo 1,242 imesajiliwa na taarifa zake kuhifadhiwa kwenye nakala laini (soft copy). Aidha, Shirika limeendelea kuhifadhi mikusanyo hiyo kwenye vyumba maalum na kuipanga kitaalaam.

255. Mheshimiwa Spika, Shirika limefanya jumla ya tafiti 12, kati ya hizo tafiti tisa ni za mikusanyo iliyohifadhiwa kwenye makumbusho na tatu ni kwenye maeneo ya *akiolojia*, *paleontolojia* na *ethonographia*. Baadhi ya tafiti hizo zilizofanyika katika bonde la Olduvai, Laetoli na Kilwa zimegundua masalia ya mifupa ya tembo waliopotea (extinct) miaka milioni 1.5 iliyopita. Aidha, zimebaini masalia ya zamadamu na wanyama na zana za mawe za miaka milioni 1.8 iliyopita. Ugunduzi huu umeongeza fursa ya Tanzania kuendelea kutambulika kimataifa kuwa ndiyo chimbuko la binadamu na kuongeza idadi ya vivutio vya utalii wa utamaduni.

256. Mheshimiwa Spika, Shirika linashirikiana na Makumbusho mbalimbali za Ujeruman, Hispania, Kenya na Uganda katika kubadilishana taaluma na uzoefu katika masuala ya makumbusho. Ushirikiano huo unahusisha baadhi ya mikusanyo kuazimishwa kwa lengo la kuoneshwa kwenye makumbusho hizo. Shirika limetumia fursa hiyo kutangaza vivutio vya utalii wa utamaduni na historia vilivyopo nchini.

257. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2016/2017, Shirika limekarabati nyumba tatu za jamii ya Wasukuma, Wasambaa na Wapimbwe na kujenga upya nyumba ya Wahaya ili kuhifadhi, kulinda na kuendeleza utamaduni na ujuzi wa ujenzi wa nyumba za jadi. Shirika limeandaa tamasha la Utamaduni wa Mtanzania liliofanyika Kijiji cha Makumbusho Dar es Salaam kwa kushirikisha jamii ya Wanyasa. Aidha, Shirika linakamilisha mpango wa matumzi endelevu ya ardhi ya Kijiji cha Makumbusho.

258. Mheshimiwa Spika, Tarehe 27 Februari, 2017 Familia ya Hayati Dr. Rashid Mfaume Kawawa maarufu kama *Simba wa Vita* ilikabidhi Wizara nyumba iliyopo Bombambil Songea, nyaraka na vifaa mbalimbali alivyokuwa akivitumia enzi za uhai wake ili itumike kama sehemu ya Makumbusho ya Taifa. Wizara inatoa shukrani za dhati kwa familia ya Mzee Kawawa kwani hii itakuwa ni Tunu ya kuenzi mchango wake mkubwa wa kuitumikia Tanzania kwa umahiri na uaminifu

mkubwa. Kumbukumbu hii itakuwa ni kielelezo na ukumbusho kwa kizazi cha sasa na cha baadae.

259. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/2017, Shirika limeratibu Maadhimisho ya Kumbukumbu ya miaka 110 ya Vita vya Maji Maji kwa ushirikiano na uongozi wa Mkao wa Ruvuma, Wazee wa Mila za Wangoni na wadau wengine. Maadhimisho hayo yenye lengo la kuwakumbuka na kuwaenzi mashujaa wa Vita vya Maji Maji yalitumika pia kutangaza fursa za utalii zilizoko mikoa ya kusini.

260. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2016/2017, Shirika liliadiria kukusanya jumla ya shilingi milioni 581 kutohana na viingilio, kukodisha kumbi, migahawa na duka la zawadi. Hadi Machi 2017, Shirika limekusanya jumla ya shilingi milioni 602.7 ambazo ni sawa na asilimia 104 ya lengo.

261. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, Shirika limekabiliana na changamoto kadhaa ikiwemo upungufu wa rasilimaliwateru na fedha. Aidha, Shirika linakabiliwa na upungufu wa vitendea kazi yakiwemo magari, kompyuta, na uchakavu wa miundombinu. Shirika litaajiri watumishi tisa na kuendelea kushirikiana na wadau wa ndani na nje ili kukabiliana na changamoto hizo.

262. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Shirika litaendelea kuboresha maonesho na kuhakikisha usalama wa mikusanyo, kutangaza Makumbusho na vivutio vya utalii. Aidha, Shirika litafanya uratibu wa Tamasha la Utamaduni wa Tanzania kwa kushirikisha jamii ya watu wa Mkao wa Lindi. Vilevile, litaibua tafiti na kazi za kishauri za machapisho, kuendeleza ushirikiano wa Kitaifa na Kimataifa, na kujenga upya nyumba za jadi na utamaduni kwa mpangilio wa ramani ya Tanzania katika Kijiji cha Makumbusho.

6.0 MASUALA MTAMBUKA (URATIBU, RASILIMALIWATU NA MADUHULI)

263. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2016/2017, Wizara imewezesha watumishi 57 kuhamia Dodoma ikiwa ni

utekelezaji wa mpango wa Kitaifa wa Serikali ya Awamu ya Tano. Aidha, Wizara imeendelea kuwawezesha watumishi wanoishi na VVU na UKIMWI waliojitokeza kwa kuwapatia fedha za kununulia lishe.

264. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuwawezesha watumishi wanoishi na VVU na UKIMWI kupata fedha kwa ajili ya virutubisho. Aidha, Wizara itafanya tathmini ya hali halisi ya VVU, UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukiza na kuandaa mpango mkakati wa kupambana na magonjwa hayo. Vilevile, jumla ya watumishi 223 watahamishiwa makao makuu Dodoma kwa awamu mbili.

265. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kusimamia masuala ya maslahi na ustawi wa watumishi katika maeneo ya ajira, mafunzo, nidhamu, maadili na afya kwa watumishi. Aidha, itaimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA katika ukusanyaji mapato, utoaji leseni za biashara ya utalii na mazao ya maliasili. Vilevile, itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa ada na tozo na itaunganisha mifumo yote ya TEHAMA ya Taasisi za Wizara na pia kuziunganisha na mifumo mingine. Sanjari na hatua hizo, mafunzo yatatolewa kwa wakusanya maduhuli na kuimarisha ufuatiliaji na tathmini. Utaratibu huu utaongeza na kuimarisha ukusanyaji na usalama wa mapato ya Serikali.

7.0 SHUKURANI

266. Mheshimiwa Spika, Niruhusu sasa niwashukuru Mheshimiwa Mhandisi Ramo Makani (Mb), Naibu Waziri; Meja Jenerali Gaudence S. Milanzi, Katibu Mkuu; na Dr. Aloyce K. Nzuki, Naibu Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kunisaidia kuongoza Wizara. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara, Vitengo, Mashirika, Taasisi, Wakala na watumishi wote kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kikamilifu. Kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wenyeviti na

Wajumbe wa Bodi za Mashirika na Taasisi za Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kunishauri kuhusu usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Mashirika na Taasisi.

267. Mheshimiwa Spika, Ninawashukuru kwa dhati mke wangu mpenzi Kudra Maghembe na watoto wetu kwa upendo, uvumilivu, nguvu na faraja wanazonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kulitumikia Taifa. Nimekuwa na majukumu mengi na wakati mwingine kukosa muda wa kuwa pamoja nao, hivyo kwa namna ya pekee nathamini sana mchango wao.

268. Mheshimiwa Spika, Napenda kuwashukuru wadau wote kwa ushirikiano walioonesha katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Villevile, natoa shukrani kwa Asasi za Kiraia na zisizokuwa za Kiserikali na sekta binafsi kwa mchango wao walioutoa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

269. Mheshimiwa Spika, Kipekee napenda kuzishukuru nchi, mashirika na taasisi mbalimbali kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Canada, China, Finland, Korea Kusini, Marekani, Norway, Ubelgiji, Ujeruman, Uswisi na Jumuiya ya nchi za Ulaya. Mashirika na taasisi ni pamoja na AWF, AWHF, BTC, FAO, FZS, GEF, GIZ, ILO, ICCROM, ICOM, ICOMOS, IUCN, KfW, NORAD, PAMS Foundation, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, World Bank, na WWF.

8.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018

270. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2017/2018, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi **148,597,946,000** kwa matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kati ya fedha hizo, shilingi **96,794,662,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **51,803,284,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

271. Mheshimiwa Spika, Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha shilingi **58,572,687,000** za Mishahara na shilingi **38,221,975,000** za Matumizi Mengineyo. Aidha, Fedha za maendeleo zinajumuisha shilingi **34,803,284,000** fedha za ndani na shilingi **17,000,000,000** fedha za nje.

272. Mheshimiwa Spika, Napenda kuhitimisha kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya: www.mnrt.go.tz

9.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo moja muhimu hapa. Waheshimiwa Wabunge, wanachama na wapenzi na mashabiki wa Timu ya *Simba Sports Club*, Taifa Kubwa wanaombwa kukutana hapo *Canteen* mara tu baada ya kuahirisha Bunge saa saba mchana. (*Makofii*)

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili.

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuleta taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fasili ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016

inataja majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na utalii kuwa ni:-

(a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii;

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ilio chini ya Wizara hii;

(c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hii; na

(d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu mengine yaliyoorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2016 imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa bajeti ya Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa, tarehe 21 hadi 23 Machi, 2017, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Aidha, kati ya tarehe 29 hadi 31 Machi, Kamati ilichambua Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa Fungu Na. 69.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inatoa maelezo ya mambo manne yafuatayo:-

(a) Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa maendeleo na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ikijumuisha makusanyo ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2016/17; upatikanaji wa Fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017; matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017;

pamoja na mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

(b) Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; ukijumuisha makisio ya makadirio ya makusanyo ya mapato kwa mwaka wa fedha 2017/2018; Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018; na mambo mengine muhimu yaliyojiteza wakati wa kuchambua na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

(c) Tutakuwa na maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

(d) Hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ulijikita zaidi katika makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha za matumizi mengineyo (*OC*) na fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Njia zilizotumika ni pamoja na kuangalia hali halisi ya makusanyo ya maduhuli, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Februari na Machi, 2017 na majadiliano yaliyofanyika yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ilitarajiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha Shilingi bilioni 116.4 kutoka katika vyanzo vifuatavyo: Idara, shilingi bilioni 4.1; Mifuko, shilingi bilioni 42.8; na shilingi bilioni 69.5 kutoka katika taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia Februari 2017, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 92.17 sawa na asilimia 79.2 ya kiwango kilichokadiriwa kukusanywa kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa makusanyo mpaka Februari, 2017 ni wa kuridhisha na kwa mwenendo huu hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara itaweza kufikia malengo ya ukusanyaji wa maduhuli yake na hatimaye kuchangia vizuri zaidi kwenye pato la Taifa. Jedwali la mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli ya Wizara kwa Idara, Mifuko, Tozo na Taasisi za Wizara limeambatishwa kama kiambatisho Na. 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya sh.135,797,787,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kiasi hiki cha fedha kinajumisha shillingi bilioni 118 za matumizi ya kawaida na shillingi bilioni 17.7 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Uwiano na utolewaji wa fedha hizo za mishahara, miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo hadi kufikia Februari, 2017 unaoneshwa kwenye jedwali Na. 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na uchambuzi katika jedwali kama inavyooneshwa hapo juu, Kamati imebaini kuwa mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo haridhishi. Hali hii inaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2016/2017; kwa mujibu wa kanuni ya 98(1) (2) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 Kamati ilifanya ziara ya kukagua miradi miili tu chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Miradi hiyo ni *Kilombero and Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management Project (KILORWEMP)* Na. 4809 na mradi unaojulikana kama *Support to Private Forest Plantations and Value Chains in Tanzania (PFP)*, Na. 4647 iliyopo Kilombero Mkoani Morogoro. Matokeo ya ukaguzi wa miradi hiyo kwa ufupi ni kama yafuatayo:-

(a) *Kilombero and Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management Project (KILORWEMP)*: Mradi huu unatekelezwa

kwa ushirikiano kati ya Serikali yetu na Ubelgiji. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi uliidihiinishiwa jumla ya shilingi bilioni mbili, lakini hadi kufikia Machi, 2017 kiasi cha shilingi milioni 397 tu kilipokelewa na kutumika kwa ajili ya usimamizi endelevu wa ekolojia ya ardhi oevu ya Bonde la Kilombero na Mto Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa mradi huu unategemea zaidi fedha za wafadhili kutoka nje hali inayoathiri utekekelezaji wa mradi kwa ujumla wake. Hata hivyo, kiasi cha fedha kilichotolewa kutekeleza mradi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hakitoshelezi kutekeleza mradi kwa ufanisi. Kwa ujumla, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi huu.

(b) *Support to Private Forest Plantations and Value Chains in Tanzania:* Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Finland. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, sh. 2,638,460,000/= ziliidihiinishwa. Hadi Februari, 2017 sh.756,021,900/= zilitolewa na kutumika kwa ajili ya kuanzisha mashamba ya miti kwa wakulima wadogo (*outgrowers*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi huu Kamati ilibaini kutokuwepo kwa uwazi wa fedha zinazotolewa kutekeleza mradi, kwa kuwa wafadhili hupitisha fedha zao kwa kampuni binafsi ya *Kilombero Valley Teak Company*. Kamati inashauri kuwa mikataba kati ya wafadhili na Serikali; wafadhili na *Kilombero Valley Teak Company*; na *Kilombero Valley Teak Company* na wakulima wadogo (*Outgrowers*) iwekwe wazi ili haki na wajibu wa kila mdau vifahamike ipasavyo. Aidha, Kamati inapendekeza Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ishirikishwe katika kuanzisha vikundi vyatya wakulima wadogo kwa lengo la kuratibu na kufuatilia maendeleo yao.

Maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa Kamati kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha ni kufanya tathimini halisi ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaokwisha ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuishauri Serikali ipasavyo katika bajeti ya mwaka wa fedha unaofuata. Kutokana na hali ilioonekana katika ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi na kutokana na Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2016/2017 Kamati ina maoni yafuatayo:-

(a) Utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi kutokana na kasi ndogo ya upatikanaji wa fedha. Hadi kufikia Februari, 2017 miradi mingi haikuweza kupata fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hali hii haina tofauti na bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016.

(b) Serikali kutotenga fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na kutegemea wafadhili kutoka nje kunaathiri mwenendo mzima wa utekelezaji wa miradi na kusababisha miradi kutokamilika ipasavyo na kuwa miradi endelevu, hususan mfadhili atakapomaliza muda wake wa ufadhili. Kwa mfano, katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017 kiasi cha shillingi bilioni 15.7 ni fedha za nje kutoka kwa wadau wa maendeleo na shillingi bilioni mbili ni fedha za ndani. Kwa mtazamo huo, bado fedha za ndani ni kidogo zikillinganishwa na fedha za nje. Kamati inaishauri Serikali ipunguze utegemezi na kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati, utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi, kwani Kati ya miradi 11 iliyopangwa kutekelezwa ni miradi minne tu ndiyo iliyotengewa fedha za ndani na kat i ya hiyo, ni mradi mmoja tu ndiyo uliopelekewa kiasi kidogo cha fedha zilizoidhinishwa. Miradi mingine iliyotengewa fedha za ndani hadi kufikia Februari, 2017 haikupelekewa fedha yoyote. Kwa utaratibu huu, Serikali haiwezi kufikia malengo yake kama ilivyokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa orodha ya miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha na kutekelezwa hadi kufikia Februari, 2017 unaonekana katika kiambatisho Na. 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017; wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilioa maoni, mapendekezo na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa yapo mapendekezo yaliyofanyiwa kazi kikamilifu, mengine yanayoendelea kufanyiwa kazi, lakini yapo mapendekezo ambayo hayakufanyiwa kazi kabisa na Kamati itaendelea kutoa ushauri katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha miundombinu ya utalii hususan barabara, huduma za maji na umeme ambavyo vimeendelea kuvutia watalii wengi kutembelea vivutio vya utalii na kuongeza idadi ya watalii hapa nchini. Aidha, Serikali inaendelea na maboresho na upanuzi wa viwanja vya ndege kama J.K. Nyerere kilichopo Dar es Salaam, Kiwanja cha Ndege Mbeya, Mwanza, Mtwara, Kigoma na *KIA* ambavyo vitasaidia kuvutia mashirika ya ndege kutua na kuongeza idadi ya watalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jithada zake za kufufua Shirika la Ndege la Taifa (*ATCL*) na kuliwezesha kununua ndege zake lenyewe. Tunaamini kufufuka kwa shirika hili kutachangia kuongezeka kwa watalii watakaosaidia kukuza biashara ya utalii na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii imeridhishwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kusimamia rasilimali za misitu hususan katika jithada za kuongeza vitendea kazi kama magari, pikipiki na boti kwa lengo la kuimarisha doria

na kudhibiti uvunaji haramu wa mazao ya misitu unaofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitekeleza ushauri wa Kamati kwa kuchukua hatua za kubainisha maeneo mapya yenye vivutio vyta utalii katika Mikoa ya Singida, Katavi, Rukwa na Tabora kwa lengo la kuendeleza vivutio hivyo ili vivutie watalii na kuongeza pato la Taifa. Kamati inashauri kuwa zoezi hili liwe endelevu katika mikoa mingine hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya utalii inahitaji ushindani mkubwa utakaosaidiwa na ubunifu wa aina mbalimbali hususan matangazo. Japokuwa matangazo haya ni gharama, inasikitisha kuona kwamba Serikali imeendelea kutoa fedha kidogo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kitalii ambazo hazitoshelezi kutengeneza matangazo yanayokidhi au kuendana na ushindani. Kwa mfano, bajeti ya kutangaza utalii Tanzania ni ndogo ikilinganishwa na bajeti ya kutangaza utalii katika nchi kama Afrika Kusini na Kenya. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuongeza fedha kwa Bodi ya Utalii ili iweze kutangaza vivutio vyetu vyta utalii ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018; Kamati imeridhishwa na vipaumbele na malengo ya kazi za Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Hata hivyo, vipaumbele, malengo na mipango hiyo itakamilika na kuinua pato la Taifa kama makusanyo yatakusanya kama ilivyokusudiwa na mgao wa fedha za matumizi utakuwa ni wa kuridhisha kwa lengo la kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2017/2018; makisio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018; katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi 23,041,862,881/= kutoptera na vyanzo vyta idara ya

Utawala na Rasilimali Watu, Idara ya Utalii na Taasisi zilizo chini yake. Kati ya makadirio hayo, Idara zitakusanya sh.11,731,056,881/= na Taasisi zitakusanya sh.11,310,806,000/=. Kiasi cha makadirio ya makusanyo haya ni pungufu ya shilingi bilioni 93.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 116.4 zilizokadiriwa kukusanya mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu huu wa mapato unatokana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (*TFS*) kujitegemea na hivyo kupeleka makusanyo yake moja kwa moja kwa Msajili wa Hazina. Ni mapendekezo ya Kamati kwamba Serikali ihakikishe inatafuta vyanzo vipyta na mbinu bora zaidi za ukusanyaji wa mapato ili kuongeza mapato ya Sekta ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Wizara ya Maliasili na Utalii inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya sh.148,597,946,000/=. Kati ya fedha hizo sh.96,794,662,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh.51,803,284,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa ujumla bajeti inayoombwa imeongezeka kwa shilingi bilioni 12.8 sawa na asilimia 9.4 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, bajeti ya maendeleo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 17.7 mwaka 2016/2017 hadi shilingi bilioni 51.8 kwa mwaka 2017/2018. Ongezeko hili linatokana na bajeti ya fedha za miradi ya maendeleo kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hairidhishwi kabisa na mwenendo wa Serikali wa kutotenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2017/2018. Masuala hayo ni pamoja na uvamizi wa maeneo ya uhifadhi. Hifadhi hizi zimevamiwa na binadamu kwa shughuli za makazi, malisho ya mifugo, uwindaji haramu wa wanyamapori kwa ajili ya biashara, kitoweo na uchimbaji wa madini ndani ya hifadhi uliopelekea

uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na kuongezeka kwa migogoro ya ardhi kati ya Mamlaka za kutunza hifadhi na wananchi wanaozunguka hifadhi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na migogoro hiyo, Kamati inaishauri Serikali kutafuta njia sahihi za kuweza kumaliza migogoro ya ardhi kati ya Mamlaka za Hifadhi na wananchi wanaozunguka hifadhi. Aidha, uandaliwe mpango maalumu wa matumizi ya ardhi utakaoainisha maeneo ya hifadhi na mipaka yake na maeneo kwa ajili ya malisho na shughuli nyingine za binadamu kwa lengo la kuwawezesha wafugaji kutumia maeneo hayo ipasavyo na siyo kuvamia maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mgongano wa kisheria kati ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori inayokataza sehemu ya ardhi ya vijiji kujumuishwa katika eneo lolote la Pori Tengefu, hasa likiwemo Pori Tengefu la Loliondo. Kamati inaishauri kuwa ni vyema utafiti ufanyike na sheria zinazogundulika kuwa zimepitwa na wakati na zenye kuleta ukinzani na kuongeza migogoro ya ardhi zifanyiwe marekebisho kwa lengo la kumaliza migogoro ya mipaka katika hifadhi zetu. Aidha, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wafanye zoezi la uhakiki wa mipaka ya maeneo ya hifadhi hasa katika maeneo yote yenye migogoro ya mipaka ili kuweza kumaliza migogoro iliyopo katika hifadhi na wananchi wanaopakana na hifadhi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na Taasisi zisizo za Kiserikali (*NGO's*) zaidi ya 25 ambazo zote zimejikita katika masuala ya utalii, uhifadhi na utetezi wa wananchi katika Pori Tengefu la Loliondo hususan katika Tarafa moja tu ya Loliondo. Taasisi hizi nyingi zinamilikiwa na wanasiasa na kufadhiliwa na taasisi za Kimataifa ambazo Kamati haina uhakika na lengo la taasisi hizo kufadhili uhifadhi nchini mwetu kwa kuwa ni washindani wetu katika biashara ya utalii na uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Kamati imegundua kuwa *NGO*'s hizi zilizo nyingi kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikichangia mgogoro unaoendelea katika eneo hili baina ya Serikali na wananchi kwa kuwapotosha wananchi juu ya wajibu wao kwa uhifadhi na Serikali yao. Kamati inashauri Serikali kuzifuta *NGO*'s zote zinazofanya shughuli zake katika Pori Tengefu la Loliondo na kusajili chache kwa masharti na vigezo vyta kulinda na kuhifadhi rasilimali za nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na sintofahamu ya matumizi ya ardhi pamoja na masharti maalum yanayotakiwa katika mapori yetu hasa kwa wawekezaji na wananchi wanaozunguka hifadhi na mapori tengefu. Kamati inaishauri Serikali kuweka wazi masharti ya uwekezaji na uwindaji katika maeneo ya mapori na hifadhi zetu kwa lengo la kuondoa migogoro inayoendelea hususan katika Pori Tengefu la Loliondo na jamii inayozunguka hifadhi na mapori mengine yenye migogoro ya aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na uharibifu wa vyanzo vyta maji katika hifadhi zetu unaosababishwa na wafugaji kupeleka mifugo katika hifadhi kwa lengo la kutafuta maji na malisho ya mifugo. Uharibifu huu umeendelea kujitokeza zaidi katika Hifadhi ya Ngorongoro na Pori Tengefu la Loliondo. Kamati inaishauri Serikali kuchimba visima, mabwawa na malambo katika vijiji vyote vinavyozunguka hifadhi na Pori Tengefu kwa lengo la kuzuia wafugaji kupeleka mifugo yao katika vyanzo vyta maji vilivyo po katika hifadhi hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na uharibifu wa misitu. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti ujangili wa misitu ili kuinusuru na kuiepusha nchi yetu na madhara yatokanayo na uharibifu wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na ongezeko la watu na mifugo katika hifadhi hususan Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wanaosababisha kuongezeka kwa gharama

za matumizi yanayotolewa na Mamlaka ya Hifadhi na kupelekea Mamlaka hii kubeba mzigo mkubwa na gharama kubwa kuliko ilivyokadiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kupitia upya na kuirekebisha Sheria liyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kuwa imepitwa na wakati. Aidha, ufanyike utafiti wa faida na athari za uhifadhi mseto unaoendelea katika hifadhi hii ili kutafuta namna bora ya kutatua migogoro iliyopo kwa lengo la kuendeleza hifadhi katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la migogoro ya mipaka limeendelea kuwa changamoto katika hifadhi zetu. Migogoro hiyo ni kati ya wananchi na mamlaka za hifadhi inayopelekea chuki na uhasama baina ya wananchi na wahifadhi na hata kuharibiwa kwa maliasili zillzomo kwenye hifadhi. Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi washirikiane katika kuhakiki mipaka katika maeneo yote yenye migogoro. Elimu itolewe kwa wananchi na viongozi wa vijiji kuhusu umuhimu wa hifadhi kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Hii itasaidia kuondokana na migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya Taarifa ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naomba niwasilishe maoni na mapendekezo ya Kamati kwa sekta mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kuongeza pato la Taifa kupitia Sekta ya Maliasili na Utalii, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea kusimamia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sheria na kanuni zake pamoja na

kutekeleza dhima ya Wizara ya Maliasili na utalii katika kulinda na kusimamia uhifadhi wa maliasili katika nchi yetu.

- Kufanya utafiti wa kutosha juu ya kodi ya Ongezeko la Thamani katika huduma za utalii iliyoanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017;
- Kuongeza kasi ya uwekezaji kikamilifu katika miundombinu kama maji, barabara na vyoo katika maeneo ya Uhifadhi; na
- Kuongeza kasi katika kufanya utafiti juu ya miundombinu ya utalii na toshelezo la utalii (*Visitor satisfaction*) kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali zinazotokana na utalii kwa lengo la kuboresha Sekta ya Utalii na kuongeza idadi ya watalii hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Wanyamapori; kwa kuwa katika kuliingizia Taifa mapato zaidi upo uwiano wa moja kwa moja kati ya ubora wa Sekta ya Maliasili na Utalii na Sekta ya Wanyamapori, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo kwa ajili ya kuboresha Sekta ya Wanyamapori:-

- Kushirikiana na Mamlaka husika kubaini mbinu za kupunguza vifo vya wanyamapori wanaokufa kwa kugongwa na magari katika barabara zinazokatiza katika hifadhi zetu;
- Kuongeza juhudi na mbinu za kisasa katika kutokomeza ujangili na biashara haramu ya wanyamapori ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo na kujenga uwezo wa kupambana na ujangili pamoja na kuimarisha doria za mara kwa mara;
- Serikali iharakishe mchakato wa kufanya maamuzi yenye tija ili kuweza kuokoa gharama ambazo Serikali inaingia kwa kumtunza Faru Fausta ambaye amewekwa katika uangalizi maalum kutokana na maradhi aliyonayo na umri wake mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Malikale; malikale ni rasilimali za urithi wa Taifa tangu enzi za Wahenga wetu. Hivyo Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuongeza mapato na kuinua sekta ya Malikale:-

- kuongeza ubunifu kwa kupanua wigo wa maeneo ya utalii kwa kutengeneza maeneo ya fukwe kuwa vivutio vya utalii; na
- Kupima na kuweka mipaka katika maeneo ya malikale ili kuzuia uvamizi na uharibifu katika maeneo yenye malikale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba taarifa yangu yote iingizwe kwenye *Hansard*, kama Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Misitu na Nyuki; Idara ya Misitu ni muhimu katika kuhifadhi mazingira, kurekebisha mfumo wa hali ya hewa, kupunguza mabadiliko ya tabia nchi, kuhifadhi bioanuai, pamoja na kuhifadhi vyanzo vya maji. Kufuatia fursa hizi, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuinua Sekta ya Misitu na Nyuki:-

- kuimarisha ulinzi katika misitu hapa nchini ili isivamiwe na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu kama uvunaji haramu, ufugaji, uchromaji mkaa usio endelevu na kilimo zinazopelekea hali ya rasilimali ya miti kuwa duni;
- Kusimamia sera, sheria na kanuni pamoja na kuandaa mikakati maalum ya kupambana na matukio ya moto katika misitu; na
- Kuongeza rasilimali watu katika Taasisi ya Utafiti wa Misitu (*TAFORI*) kwa lengo la kuiwezesha Taasisi hiyo kuanzisha na kusimamia majaribio ya utafiti ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Kamati inaamini ushauri wake utazingatiwa ili kuisaidia Serikali kutekeleza mipango ya maendeleo na kuinua utalii kwa faida ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na Naibu wake Mheshimiwa Mhandisi Ramo Makani pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara hii. Kamati inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuipa Kamati ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Ndugu Dickson Bisile, Ndugu Gerald Magili, Ndugu Haika Mtui, Ndugu Elieka Saanya na Ndugu Jane Ndulesi pamoja na wafanyakazi wote wa Bunge kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama yalivowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,
MALIASILI NA UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA
WA 2016/2017; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA
KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

1.0 UTANGULIZI

1.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

1.2 **Mheshimiwa Spika**, Fasili ya 7 (1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 inataja majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na utalii kuwa ni:-

- (a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii;
- (b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyochini ya wizara hii;
- (c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za wizara hii; na
- (d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

- 1.3 **Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu mengine yaliyoorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 98(1),(2), ya kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2016 imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa bajeti ya wizara inazosimamia. Naomba kutoa taarifa kuwa tarehe 21 hadi 23 Machi, 2017 Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Aidha kati ya tarehe 29 hadi 31 Machi, Kamati ilichambua Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa- fungu **69**.
- 1.4 **Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa maelezo ya mambo manne yafuatayo:-
- (a) Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa maendeleo na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ikijumuisha; -
- (i) Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka wa fedha 2016/17;
- (ii) Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- (iii) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- (iv) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017
- (b) Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; ukijumuisha.
- (i) Makisio ya Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

- (ii) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
 - (iii) Mambo mengine muhimu yaliyojitekeza wakati wa kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.
- (c) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.
 - (d) Hitimisho

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MAJUKUMU YALIYOTEKELEZWA

2.1 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA

BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ulijikita zaidi katika makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Njia zilizotumika ni pamoja na kuangalia hali halisi ya makusanyo ya maduhuli, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Februari na Machi 2017, na majadiliano yaliyofanyika yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vyta Kamati.

2.2 UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

2.2.1 Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ilitarajiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha Shilingi **116,448,268,664** kutoka katika vyanzo

vifuatavyo;- Idara **shilingi 4,136,781,818**, Mifuko **shilingi 42,777,620,308** na **shilingi 69,553,866,538** kutoka katika taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia Februari 2017, ilikusanya jumla ya shilingi **92,179,811,000** sawa na asilimia **79.2** ya kiwango kilichokadirwa kukusanywa kwa mwaka. Mwenendo wa makusanyo mpaka Februari 2017 ni wa kuridhisha na kwa mwenendo huu hadi kufikia mwisho wa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara itawenza kufikia malengo ya ukusanyaji wa maduhuli yake na hatimaye kuchangia vizuri zaidi kwenye pato la Taifa. Jedwali la mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli ya Wizara kwa Idara, Mifuko, Tozo na Taasisi za Wizara limeambatishwa kama **Kiambatisho na 1.**

2.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

2.3.1 Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya **shilingi 135,797,787,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kiasi hiki cha fedha kinajumisha **shillingi 118,051,105,000** za matumizi ya kawaida na **shilingi 17,746,682,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Uwiano na utolewaji wa fedha hizo za mishahara, miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo hadi kufikia februari 2017 unaonyeshwa kwenye **jedwali Na. 1**

Jedwali Na.1 Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida, Miradi ya Maendeleo na Mishahara

NA	MAELEZO	FEDHA ZILIZOIDHINISHWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017	FEDHA ZILIZOTOLEWA HADI FEBRUARI, 2017	ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA
1	Mishahara & Matumizi Mengineyo	135,797,787,000	56,946,079,705	42%
2	Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	2,000,000,000.00	156,688,000.00	8%
3	Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo	15,746,682,000.00	14,514,026.628	82%

Chanzo:Taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Malasili na Utalii 2016/2017

- 2.3.2 Mheshimiwa Spika**, Kulingana na uchambuzi katika jedwali kama inavyoonekana hapo juu, Kamati imebaini kuwa mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi. Hali hii inaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo ipasavyo.
- 2.4 UKAGUZI WA BAADHI YA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017**
- 2.4.1 Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa kanuni ya 98¹ ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 Kamati ilifanya ziara ya kukagua miradi miwili tu chini ya Wizara ya Maliasili na utalii. Miradi hiyo ni *Kilombero and Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management Project (KILORWEMP)* namba 4809 na mradi unaojulikana kama *Support to private forest plantations and value chains in Tanzania-PFP*, namba 4647 iliyopo Kilombero mkoani Morogoro. Matokeo ya ukaguzi wa miradi hio ni kama yafuatayo:-

(a) Kilombero and Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management Project (KILORWEMP)

Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali yetu na Ubelgiji. Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi uliuhinishiwa jumla ya **Tsh 2,080,000,000** hadi kufikia Machi 2017 kiasi cha **shilingi 397,000,000** kilipokelewa na kutumika kwa ajili ya usimamizi endelevu wa ekolojia ya ardhi oevu ya Bonde la Kilombero na mto Rufiji. Kamati ilibaini kuwa mradi huu unategemea zaidi fedha za wafadhili kutoka nje hali inayoathiri utekelezaji wa mradi kwa ujumla wake. Hata

¹ Kanuni ya 98(1)& (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016

hivyo kiasi cha fedha kilichotolewa kutekeleza mradi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hakitoshelezzi kutekeleza mradi kwa ufanisi.

Kwa ujumla Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi huu.

Aidha, Katika Hifadhi ya Jamii ya ILUMA inayoendeshwa chini ya mradi wa **KILOWEMP** Kamati ilibaini kutokuwepo kwa kanuni zinazosimamia rasilimali za misitu na wanyamapori katika hifadhi hii. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utungaji wa kanuni katika Hifadhi ya Jamii ILUMA ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa Rasilimali za Misitu na Wanyamapori.

(b) Support to private forest plantations and value chains in Tanzania- PFP

Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Finland na Tanzania. Katika Mwaka wa fedha 2016/2017 **shilingi 2,638,460,000** ziliidhinishwa. Hadi Februari 2017 **shilingi 756,021,900** zilitolewa na kutumika kwa ajili ya kuanzisha mashamba ya miti kwa wakulima wadogo (outgrowers). Katika mradi huu Kamati ilibaini kutokuwepo kwa uwazi wa fedha zinazotolewa kutekeleza mradi, kwa kuwa wafadhili hupitisha fedha zao kwa kampuni binafsi ya Kilombero Valley Teak Company. **Kamati inashauri kuwa mikataba kati ya wafadhili na Serikali, wafadhili na Kilombero Valley Teak Company na Kilombero Valley Teak Company na wakulima wadogo (Outgrowers) iwekwe wazi ili haki na wajibu wa kila mdau vifahamike ipasavyo.** Aidha Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ishirikishwe katika kuanzisha vikundi vyta wakulima wadogo kwa lengo la kuratibu na kufatilia maendeleo yao.

2.5 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

2.5.1 Mheshimiwa Spika, Msingi wa Kamati kukagua miradi ya maendeleo iliyo tengewa fedha ni

kufanya tathimini halisi ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kutekeleza miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuishauri Serikali ipasavyo katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaofuata. Kutokana na hali ilioonekena katika ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi na kutokana na Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ilitengewa fedha kwa mwaka 2016/2017² Kamati ina maoni yafuatayo:-

(a) Utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi kutokana na kasi ndogo ya upatikanaji wa fedha.Hadi kufikia Februari 2017 miradi mingi haikuweza kupata fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hali hii haina tofauti na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016.

(b) Serikali kutotenga fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na kutegeMEA wafadhili kutoka nje kunaathiri mwenendo mzima wa utekelezaji wa miradi na kusababisha miradi kutokamilika ipasavyo na kuwa miradi endelevu hususan mfadhili atakapomaliza muda wake wa ufadhili. Kwa mfano katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kiasi cha **Shillingi 15,746,682,000** ni fedha za nje kutoka kwa

wadau wa maendeleo na **Shillingi 2,000,000,000** ni fedha za ndani. Kwa mtazamo huo bado fedha za ndani ni kidogo zikilinganishwa na fedha za nje. Kamati inaishauri Serikali ipunguze utegemezi kwa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

(c) Serikali kutopeleka fedha katika miradi kwa wakati kunaathiri mwenendo mzima wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa taarifa za miradi unaonyesha kuwa hata kwa miradi iliyotengewa fedha za ndani haikupelekewa f edha kwa wakati kama

²Taarifa ya Wizara ya Maliasili na utali kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, iliyowasilishwa katika Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa Bajeti ya Mwaka 2016/2017

ilivyokusudiwa. Aidha kwa ile miradi iliopelekewa fedha kiwango kilichotolewa ni kidogo sana, hadi kufikia februari 2017,Wizara ilipokea kiasi cha **shilingi 156,688,000** fedha za ndani na **shilingi 24,357,338,628** fedha za nje, kiwango cha fedha za ndani kilichotengwa hakiridhishi kukidhi utekekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ukamilifu.

2.5.2 Mheshimiwa Spika, Kutokana na uchambuzi uliofanywa na kamati utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi. Kwani Kati ya **miradi 11** iliyopangwa kutekelezwa ni **miradi 4 tuu** ndio iliyotengewa fedha za ndani na kati ya hiyo ni **miradi 1** tuu ndio ulipelekewa kiasi kidogo cha fedha zilizoidhinishwa.Miradi mingine iliyotengewa fedha za ndani hadi kufikia februari 2017 haikupelekewa fedha yoyote³. Kwa utaratibu huu Serikali haiwezi kufikia malengo yake kama ilivyokusudia.

Mwenendo wa orodha ya miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha na kutekelezwa hadi kufikia Februari 2017 unaonekana katika **kiambatisho Na.2**

2.6 UTEKELEZAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

2.6.1 Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilitoa maoni, mapendekezo, na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii.Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa yapo mapendekezo yaliyofanyiwa kazi kikamilifu, mengine yanayoendelea kufanyiwa kazi, lakini yapo mapendekezo ambayo hayakufanyiwa kazi kabisa na Kamati itaendelea kutoa ushauri katika taarifa hii.

³ Kwa mujibu wa Randama ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2016/17, miradi ambayo haikupelekewa fedha ni Utalii House Phase II (miradi Na-6367II),Theme park (miradi Na-5202),Capacity

Building in Game reserves and Anti-Poaching Unit in Tanzania (miradi Na -4810)

- 2.6.2** **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha miundombinu ya utalii hususan barabara, huduma za maji na umeme ambavyo vimeendelea kuvutia watalii wengi kutembelea vivutio nya utalii na kuongeza idadi ya watalii hapa nchini.
- Aidha Serikali inaendelea na maboresho na upanuzi wa viwanja nya ndege kama **J.K. Nyerere kilichopo Dar es Salaam**, kiwanja cha ndege Mbeya, Mwanza, Kigoma na KIA ambavyo vitasaidia kuvutia mashirika ya ndege kutua na kuongeza idadi ya watalii nchini. Kipekee Kamati inampongeza Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jithhada zake za kufufua Shirika la ndege la Taifa (ATCL) na kuliwezesha kununua ndege zake lenyewe. Tunaamini kufufuka kwa shirika hili kutachangia kuongezeka kwa watalii watakaosaidia kukuza biashara ya utalii na kuongeza pato la Taifa.
- 2.6.3** **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kusimamia rasilimali za misitu hususan katika jithhada za kuongeza vitendea kazi kama magari, pipipiki na boti kwa lengo la kuimarisha doria na kudhibiti uvunaji haramu wa mazao ya misitu unaofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu.
- 2.6.4** **Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitekeleza ushauri wa Kamati kwa kuchukua hatua za kubainisha maeneo mapya yenye vivutio nya utalii katika mikoa ya Singida, Katavi, Rukwa, na Tabora kwa lengo la kuendeleza vivutio hivyo ili vivutie watalii na kuongeza pato la Taifa. **Kamati inashauri kuwa zoezi hili liwe endelevu katika mikoa mingine hapa nchini.**
- 2.6.5** **Mheshimiwa Spika**, Biashara ya utalii inahitaji ushindani mkubwa utakaosaidiwa na ubunifu wa

aina mbalimbali hususan matangazo (*Promotion*). Japokuwa matangazo haya ni gharama inasikitisha kuona kwamba Serikali imeendelea kutoa fedha kidogo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kitalii ambazo hazitoshelezi kutengeneza matangazo yanayokidhi ili kuendana na ushindani. Kwa mfano bajeti ya kutangaza utalii Tanzania ni ndogo ikilinganishwa na bajeti ya kutangaza utalii kwa nchi kama Kenya na South Afrika. **Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuongeza fedha kwa Bodi ya Utalii ili iweze kutangaza vivutio vyetu vya utalii ndani na nje ya nchi.**

3.0 MPANGO WA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

3.1 Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- a) Kuboresha mifumo ya ukusanyaji Maduhulii;
- b) Kuendeleza na kutangaza utalii;
- c) Kuimarisha uhifadhi wa Maliasili na Malikale kwa kushirikisha wadau; na
- d) Kudumisha na kuboresha ushirikiano wa Kikanda Kitaifa, na kimataifa.

3.2 Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na vipaumbele na malengo ya kazi za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Hatahivyo, vipaumbele, malengo na mipango hiyo itakamilika na kuinua pato la Taifa kama makusanyo yatakusanya kama ilivyokusudiwa, na mgao wa fedha za matumizi utakua ni wa kuridhisha kwa lengo la kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

4.0 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

4.1 Makisio ya Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

4.1.1 **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi **23,041,862,881/=** kutokana na vyanzo vya Idara ya Utawala na rasilimali watu, Idara ya Utalii, na Taasisi zilizo chini yake. Kati ya makadirio hayo, idara zitakusanya shilingi **11,731,056,881** na taasisi zitakusanya shilingi **11,310,806,000**. Kiasi cha makadirio ya makusanyo haya ni pungufu ya shilingi **93,406,405,783/=** ikilinganishwa na shilingi **116,448,268,664/=** zilizokadiriwa kukusanya wa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Upungufu huu wa mapato unatokana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kujitegemea na hivyo kupeleka makusanyo yake moja kwa moja kwa msajili hazina. **Ni mapendekezo ya Kamati kwamba Serikali ihakikishe inatafuta vyanzo vipyta na mbinu bora zaidi za ukusanyaji wa mapato ili kuongeza mapato ya Sekta ya Maliasili na Utalii.**

4.2 Makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

4.2.1 **Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Maliasili na Utalii inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 148,597,946,000**. Kati ya fedha hizo shilingi **96,794,662,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 51,803,284,000/=** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa ujumla bajeti inayoombwa imeongezeka kwa **shilingi 12,800,159,000** sawa na asilimia **9.4** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017. Aidha bajeti ya maendeleo imeongezeka kutoka shilingi **bilioni 17,746,682,000** mwaka 2016/2017 hadi shilingi **bilioni 51,803,284,000** mwaka 2017/

2018. Ongezeko hili linatokana na bajeti ya fedha za miradi ya maendeleo kuongezeka.

- 4.3 **Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi kabisa na mwenendo wa Serikali wa kutotenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha hata kwa ile miradi inayoidhinishiwa fedha za ndani hazipelekwi kabisa, na kama zikipelekwa hazipelekwi kwa wakati na kusababisha m dororo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kupeleka kwa wakati fedha zote zinazoidhinishwa ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- 5.0 **MASUALA MENGINE MUHIMU YALIYOJITOKEZA WAKATI WA KUCHAMBUA NA KUPITISHA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HII KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

5.1 **Uvamizi wa Maeneo ya Hifadhi na Mapori Tengefu.**

- 5.1.1 **Mheshimiwa Spika**, kulikua na masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii, Maswala hayo ni pamoja na uvamizi wa maeneo ya uhifadhi katika Hifadhi ya Ngorongoro na Pori Tengefu la Loliondo. Hifadhi hizi zimevamiwa na binadamu kwa shughuli za makazi, malisho ya mifugo, uwindaji haramu wa wanyamapori kwa ajili ya biashara, kitoweo, na uchimbaji wa madini ndani ya hifadhi uliopelekea uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na kuongezeka kwa migogoro ya ardhi kati ya Mamlaka za kutunza hifadhi na wananchi wanaozunguka hifadhi hizo. Ili kuondokana na migogoro hiyo **kamati inaishauri Serikali kutafuta njia sahihi za kuweza kumaliza migogoro ya ardhi kati ya Mamlaka za Hifadhi na wananchi wanaozunguka hifadhi**, Aidha uandaliwe mpango maalumu wa matumizi ya ardhi utakaoainisha maeneo ya hifadhi na mipaka yake na maeneo kwa ajili ya malisho na shughuli nyingine za binadamu kwa lengo la kuwawezesha wafugaji

kutumia maeneo hayo ipasavyo na sio kuvamia maeneo ya hifadhi.

- 5.1.2** **Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na mgongano wa kisheria kati ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori⁴ inayokataza sehemu ya ardhi ya vijiji kujumuishwa katika eneo lolote la Pori Tengefu, likiwemo Pori Tengefu la Loliondo wakati tayari katika eneo la Pori hilo kulikuwa na vijiji vilivyokuwa vimeanzishwa kisheria tangu wakati wa ukoloni na kulindwa chini ya Sheria ya Ardhi ya Viji Na. 5⁵ na Sheria ya Serikali za Mitaa Tawala za Wilaya⁶, Vijihi hivyo ni pamoja na Ololosokwan, Soitsambu, Oloipiri, Olorien, Maaloni, Arash, Malambo na Piyaya.

Kamati inashauri kuwa ni vyema utafiti ufanyike na sheria zitakazogundulika kuwa zimepitwa na wakati na zenye kuleta ukinzani na kuongeza migogoro ya ardhi zifanyiwe marekebisho kwa lengo la kumaliza migogoro ya mipaka katika hifadhi zetu.

Aidha Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wafanye zoezi la uhakiki wa mipaka ya maeneo ya hifadhi hasa katika maeneo yote yenye migogoro ya mipaka ili kuweza kumaliza migogoro iliyopo kati ya hifadhi na wananchi wanaopakana na hifadhi hizo.

- 5.1.3** **Mheshimiwa Spika**, Kumekuwepo na Taasisi zisizo za kiserikali (NGO's) zaidi ya 25 ambazo zote zimejikita katika masuala ya Utalii, Uhifadhi na utetezi wa wananchi katika Pori Tengefu la Loliondo. Taasisi hizi nyingi zinamilikiwa na wanasiwa na kufadhiliwa na taasisi za Kimataifa ambazo Kamati haina uhakika na lengo la taasisi hizo kufadhili uhifadhi nchini

⁴ Sheria namba 12 ya Mwaka 1974

⁵ Sheria ya Ardhi ya Vijihi namba 5 ya Mwaka 1999

⁶ Sheria ya Serikali za Mitaa, Tawala za Wilaya namba 7 ya Mwaka 1982

mwetu kwa kuwa ni washindani wetu katikabiashara ya utalii na uhifadhi. Hata hivyo Kamati imegundua kuwa NGO's hizi kwa kiasi kikubwa zimekua zikichangia mgogoro unaoendelea katika eneo hili baina ya Serikali na wanachi kwa kuwapotosha wananchi juu ya wajibu wao kwa uhifadhi na Serikali yao. **Kamati inashauri Serikali kuzifuta NGO's zote zinazofanya shughuli zake katika Pori Tengefu la Loliondo na kusajili chache kwa masharti na vigezo vya kulinda na kuhifadhi rasilimali za nchi yetu.**

- 5.1.4 **Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na sintofahamu ya matumizi ya ardhi pamoja na masharti maalumu yanayotakiwa katika mapori yetu hususan kwa wawekezaji na wananchi wanaozunguka hifadhi na mapori tengefu. **Kamati inaishauri Serikali kuweka wazi masharti ya uwekezaji na uwindaji katika maeneo ya mapori na hifadhi zetu kwa lengo la kuondoa migogoro inayoendelea hususan katika Pori Tengefu la Loliondo na jamii inayozunguka hifadhi na mapori mengine yenye migogoro ya aina hii.**
- 5.1.5 **Mheshimiwa Spika** kumekuwepo na uharibifu wa vyanzo vya maji katika hifadhi zetu unaosababishwa na wafugaji kupeleka mifugo katika hifadhi kwa lengo la kutafuta maji na malisho ya mifugo.Uharibifu huu umeendelea kujitokeza zaidi katika Hifadhi ya Ngorongoro na Pori Tengefu la loliondo. **Kamati inashauri Serikali kuchimba visima, mabwawa na malambo katika vijiji vyote vinavyozunguka hifadhi/Pori Tengefu kwa lengo la kuzuia wafugaji kupeleka mifugo katika vyanzo vya maji vilivyopo katika hifadhi hizi.**
- 5.1.6 **Mheshimiwa Spika** kumekuwepo na mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na uharibifu wa misitu. **Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti ujangili wa misitu ili kuinusuru na**

kuiepusha nchi yetu na madhara yatokanayo na uharibifu wa misitu.

- 5.1.7** **Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na ongezeko la watu na mifugo katika hifadhi hususan Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wanaosababisha kuongezeka kwa ghamama za matumizi yanayotolewa na Mamlaka ya Hifadhi na kupelekea Mamlaka hii kubeba mzigo mkubwa na ghamama kubwa kuliko ilivyokadiria. Kamati inashauri Serikali **kupitia upya na kuirekebisha Sheria liyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)** kwa kuwa imepitwa na wakati. Aidha ufanyike utafiti wa faida na athari za uhifadhi mseto unaoendelea katika hifadhi hii ili kutafuta namna bora ya kutatua migogoro iliyopo kwa lengo la kuendeleza hifadhi katika taifa letu.
- 5.1.8** **Mheshimiwa Spika**, Tatizo la migogoro ya mipaka limeendelea kuwa changamoto katika hifadhi zetu, migogoro hiyo ni kati ya wananchi na mamlaka za hifadhi inayopelekea chuki na uhasama baina ya wananchi na wahifadhi na hata kuharibiwa kwa maliasili zilizomo kwenye hifadhi.Kamati inashauri Serikali ifuatavyo:-
- (a) **TAMISEMI**, Wizara ya maliasili na utalii na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi washirikiane katika kuhakiki mipaka katika maeneo yote yenye migogoro.
 - (b) Vifanyike vikao vya ujirani mwema katika maeneo yenye migogoro ya mipaka kwa lengo la kuondoa chuki inayoendelea baina ya wananchi kwa wananchi na wananchi na wahifadhi.
 - (c) Kila wilaya waandae mipango ya matumizi bora ya ardhi na iainishe maeneo mbalimbali kama ya kilimo, malisho, n.k ili kuzuia

uvamizi na kupunguza migogoro kati ya wananchi na Mamlaka za hifadhi.

- (d) Elimu itolewe kwa wananchi na viongozi wa vijiji kuhusu umuhimu wa hifadhi kwa jamii na Taifa kwa ujumla hii itasaidia kuondokana na migogoro isiyo ya lazima.

SEHEMU YA TATU

6.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

6.1 Mheshimiwa Spika, Baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya Taarifa ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naomba niwasilishe maoni na mapendekazo ya Kamati kwa sekta mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

6.2 SEKTA YA UTALII

6.2.1 Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kuongeza pato la Taifa kuititia Sekta ya Maliasili na Utalii, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kusimamia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania⁷sheria na kanuni zake pamoja na kutekeleza dhima ya Wizara ya Maliasili na utalii katika kulinda na kusimamia uhifadhi wa maliasili katika nchi yetu kwa lengo la kuongeza pato la taifa litokanalo na utalii;

(b) Kufanya utafiti wa kutosha juu ya kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika huduma za utalii iliyoanza kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwani kumekua na mgongano wa taarifa mbili tofauti zinazotoka kwa Watoa huduma za utalii na Wizara ya Maliasili na Utalii;

⁷Ibari ya 27(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inamtaka kila mtanzania kulinda na kusimamia maliasili za Nchi ya Tanzania

Kwa upande wa Wadau wanaotoa huduma za kitalii wanadai kuwa utoaji wa kodi hio umepunguza idadi ya watalii na kuongeza gharama za uendeshaji wa makampuni yanayojihusisha na biashara ya utalii, wakati kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa nyakati tofauti imekua ikiripoti kuwa utozaji wa kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) katika Utalii haujaathiri kwa namna yoyote sekta hiyo zaidi ya kuongezea Serikali mapato.

Kwakuwa Kamati haijaweza kujiridhisha na ukweli kuhusu athari ya VAT kwenye huduma ya Utalii, na kwakuwa ukinzani huu unaweza kuathiri sekta hii muhimu, Ni vyema Bunge lako tukufu llijadili suala hili na ikiwezekana Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akakague athari ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika sekta ya utalii na kulishauri Bunge ipasavyo ili kuondokana na tofauti hii inayojitokeza.

(c) Kuongeza kasi ya uwekezaji kikamilifu katika miundombini kama maji, barabara, na vyoo katika maeneo ya hifadhi.

(d) Kufanya marekebisho katika sera, sheria na kanuni zinazosimamia uhifadhi wa wanyamapori pamoja na mapori yetu zilizopitwa na wakati kwa lengo la kuongeza ustawi wa hifadhi kwa manufaa ya nchi yetu;

(e) Kusimamia Chuo cha Taifa cha Utalii kwa lengo la kupata wataalamu wenyе sifa na vigezo watakaokidhi haja ya soko la ajira katika sekta ya utalii;

(f) Kuhamasisha sekta binafsi katika kuboresha mahotelii ili kupandisha madaraja ya ubora wa hotel kwa lengo la kupata makusanyo ya huduma za hotel yanayostahili kuongeza pato kiuchumi;

(g) Kuangalia uwezekano wa kuipatia Makumbusho ya Taifa gawio la fedha zinazokusanya na mfuko wa kuendeleza utalii kupitia Tourism Development Levy ili zitumike kuendeleza Malikale na vivutio vingine vya utalii;

(h) Kupeleka fedha zote zilizoidhinishwa katika bodi ya utalii (TTB) ili bodi hii iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, hususan katika kuongeza kasi ya ubunifu kwenye kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi ili kuendana na ushindani uliopo katika sekta ya utalii.

(i) Kuongeza kasi katika kufanya utafiti juu ya miundombinu ya utalii na toshelezo la utalii (*Visitor satisfaction*) kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali zinazotokana na utalii kwa lengo la kuboresha sekta ya utalii na kuongeza idadi ya watalii wengi hapa nchini.

(j) Kusimamia mipaka na maeneo ya mapori kwa lengo la kutatua migogoro iliyopo na inayoweza kujitokeza kwa lengo la kunusuru ikolojia, kulinda mazalia ya wanyama, mapito ya wanyama pamoja na vyanzo vya maji kwa ajili ya kuendeleza hifadhi na utalii nchini.

6.3 SEKTA YA WANYAMAPORI

6.3.1 Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa katika kuiingizia Serikali mapato zaidi upo uwiano wa moja kwa moja kati ya ubora wa sekta ya maliasili na utalii na sekta ya wanyamapori, kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo kwa ajili ya kuboresha sekta ya wanyamapori:-

a) Kuongeza juhudzi na mbinu za kisasa katika kutokomeza ujangili na biashara haramu ya wanyamapori hii ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa kupambana na ujangili pamoja na kuimarisha doria za mara kwa mara.

b) kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori walio hatarini kutoweka kama faru na tembo. Aidha ulinzi uimarishwe katika kudhibiti usafirishaji wa pembe za ndovu katika bandari zetu na viwanja vya ndege.

c) Kushirikiana na Mamlaka husika kubaini mbinu za kupunguza vifo vya wanyamapori wanaokufa kwa

kugongwa na magari katika barabara zinazokatiza katika hifadhi zetu.

d) kuongeza juhudii katika kusimamia sheria na taratibu ipasavyo kwa kuwashughulikia kikamilifu wote watakaokutwa na hatia ya ujangili wa wanyamapori hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kesi za ujangili zinasikilizwa haraka na kutoa adhabu kali kwa watakaokutwa na hatia.

e) Kuimarisha ulinzi katika ghala la kuhifadhia nyara za Taifa (Ivoryroom), hii ni pamoja na kuweka kamera za usalama, vifaa vyta kugundua moto (Fire detectors), na kutoa mafunzo ya mara kwa mara ya kujikinga na kupambana na janga la moto katika ghala la kuhifadhia nyara.

f) Kufanya utafiti kwa kuzingatia mikataba iliyopo kuhusu namna ya uhifadhi wa nyara za Taifa na kutafuta suluhu ya kudumu kwa kuwa idadi ya nyara inaongezeka siku hadi siku na ghala limekua likihifadhi nyara hizo tangu miaka ya 1960.

g) Kutenga bajeti ya kutosha kwa taasisi za mafunzo na utafiti zilizo chini ya idara ya wanyamapori kama Mweka, TAWIRI, TAWA ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

h) Kufanya utafiti wa kutosha katika sheria za wanyamapori zinazoruhusu mchanganyiko wa wanyamapori binadamu na mifugo kuishi mahali pamoja kwa lengo la kutatua changamoto ya wanyama wakali wanaoshambulia binadamu, mifugo, na mashamba yao.

i) Kutafuta mbini mbadala ya kupambana na changamoto ya maangamizi ya mbwa mwitu wanaovamiwa na kuuawa na jamii hata pale ambapo matukio ya uvamizi wa mifugo yao haujatokea. Hii hutokea hususan katika Pori Tengefu la Loliondo na Hifadhi ya Ngorongoro kutohana na kukosekana kwa gharama zinazopaswa kulipwa kama kifuta machozi.

j) Kuchukua tahadhari kwa kutoa elimu kwa jamii ilio hatarini katika maambukizi ya magonjwa yanayoweza kuwapata wanyamapori kama homa ya bonde la ufa (*Rify Valley Fever*), kimeta na kifua kikuu.

k) Serikali iharakishe mchakato wa kufanya maamuzi yenyе tija ili kuweza kuokoa gharama ambazo Serikali inaingia kwa kumtunza **Faru Fausta** ambaye amewekwa katika uangalizi maalumu kutokana na maradhi aliyonayo na umri wake.

6.4 SEKTA YA MALIKALE

6.4.1 **Mheshimiwa Spika**, Malikale ni rasilimali za urithi wa taifa tangu enzi za wahenga wetu. Rasilimali hii ikiboresha ipasavyo itachochea utalii na kuchangia ukuaji wa uchumi na kukuza sekta ya elimu hapa nchini. Hivyo basi Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuongeza mapato na kuinua sekta ya Malikale:-

a) Kuainisha vivutio vyatya malikale pamoja na kuviendeleza, sambamba na kuimarisha ulinzi, kukarabati na kutunza maeneo yenyе majengo ya Malikale kwa lengo la kuuenzi utamaduni wetu na kuvutia watalii kutoka katika maeneo mbalimbali nchini;

b) Kuendelea kukuza utalii wa ndani kwa kuyatangaza maeneo ya Malikale ndani na nje ya nchi kama vivutio vyatya utalii na maeneo ya kujifunza historia ya nchi yetu;

c) Kuongeza ubunifu kwa kupanua wigo wa maeneo ya utalii kwa kutengeneza maeneo ya fukwe kuwa vivutio vyatya utalii; na

d) Kupima na kuweka mipaka katika maeneo ya malikale ili kuzuia uvamizi na uharibifu katika maeneo yenyе Malikale.

6.5 MAKUMBUSHO YA TAIFA

- 6.5.1 Mheshimiwa Spika**, Makumbusho ya Taifa ni moja ya idara muhimu yenye kutunza kumbukumbu na historia ya taifa kwa ujumla kabla na baada ya kupata uhuru.Ni kivutio cha utalii na ni kielelezo muhimu katika kuinua kiwango cha elimu nchini. Cha kusikitisha zaidi Serikali inaisahau idara hii muhimu hivyo Kamati inaikumbusha Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuinua idara hii:-
- a) Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya ukarabati wa maeneo ya makumbusho ya Taifa.
 - b) Kutangaza Makumbusho ya Taifa kama kivutio sambamba na vivutio vingine vya utalii; na
 - c) Kuhamasisha wananchi kuitambua, kuithamini na kuitembelea makumbusho ya Taifa kama hatua ya kukuza utalii wa ndani pamoja na kuongeza uelewa wa historia ya nchi yetu.
 - d) Kuendeleza Makumbusho ya Taifa kwa kujenga vivutio mbalimbali kama vile maduka, vyoo, migahawa kwa lengo la kuinua utalii na kuwavutia watalii wengi kutembelea.
 - e) Kuboresha kijiji cha makumbusho cha Kijitonyama kwa kujenga nyumba za makabila ya watanzania kwa malighafi halisi kutoka katika mikoa yanakotoka makabila husika ili kuleta kumbukumbu na uhalisia wa makabila yote yaliyopo nchini Tanzania.

6.6 SEKTA YA MISITU NA NYUKI

- 6.6.1 Mheshimiwa Spika**, Idara ya misitu ni muhimu katika kuhifadhi mazingira, kurekebisha mfumo wa hali ya hewa, kupunguza mabadiliko ya tabia nchi, Kuhifadhi bioanuai, pamoja na kuhifadhi vyanzo vya maji. Pamoja na hayo, idara hii ikitunzwa kikamilifu

itachangia ongezeko la ajira na kupunguza umaskini. Kufuatia fursa hizi Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuinua sekta ya misitu na nyuki; -

(a) Kuimarisha ulinzi katika misitu hapa nchini ili isivamiwe na shughuli za kibinadamu zisizoendelevu kama uvunaji haramu, ufügaji, uchomaji mkaa usio endelevu na kilimo zinazopelekea hali ya rasilimaliya miti kuwa duni;

(b) Kuandaa mipango endelevu kwa ajili ya makazi ya watu hasa katika miji mikubwa inayozunguka hifadhi na ile inayokuwa kwa kasi, hii itasaidi miji kutopanuka kiholela na kuvamia misitu ya hifadhi kwa ajili ya makazi ya watu;

(c) Kuhakiki na kusimamia mipaka ya misitu hasa ile iliyopo karibu na miji ili misitu imilikiwe na kuendeshwa klutaratibu, kwakuwa ikibaki bila uhakiki inakuwa vichaka na kuonekana kama mapori yasiyokuwa na wamiliki wala faida hivyo kuleta ushawishi wa kumegwa kwa ajili ya shughuli nyingine;

(d) Kumaliza migogoro iliyopo baina ya hifadhi za misitu na jamii zinazozunguka hifadhi, kwani misitu mingi imevamiwa kwa shughuli za kibinadamu kama kilimo, ufügaji, makazi, uchimbaji madini na ukataji miti kwa ajili ya biashara na matumizi ya nyumbani;

(e) Kusimamia sera, sheria na kanuni pamoja na kuandaa mikakati maalumu ya kupambana na matukio ya moto katika misitu;

(f) Kutenga fedha za kutosha kuziwezesha Taasisi zilizo chini ya idara hii, hususan Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) na Chuo cha Misitu Olmotony kutekeleza majukumu yake kikamilifu;

(g) Kuongeza rasilimali watu katika Taasisi ya utafiti wa misitu (TAFORI) kwa lengo la kuziwezesha taasisi kuanzisha na kusimamia majoribio ya utafiti ipasavyo;

(k) Kutenga fedha za ruzuku (OC) kwa taasisi kwani upungufu mkubwa wa fedha toka Serikalini unapelekea taasisi kufanya tafiti zinazotokana na malengo ya wahisani tuu; na

(i) Kuziwezesha maabara za utafiti zilizopo chini ya TAFORI na TTSA kupata vifaa vipya vinavyoendana na sayansi na teknolojia kwa lengo la kuiwezesha taasisi kufanya tafiti kikamilifu.

(j) Kuchukua hatua madhubuti na za haraka kudhibiti athari kubwa zinazoweza kuletwa na maadui wa nyuki kama kupe (aina ya Varroa) wanaoshambulia nyuki na kupelekea sekta kuwa hatarini kupoteza mapato yatokanayo na mazao ya nyuki.

(k) kutenga bajeti ya kutosha kwa Serikali za vijiji, Serikali za mitaa pamoja na Halmashauri ili kuwawezesha kusimamia misitu ipasavyo ikiwa ni pamoja na kukabiliana na janga la uharibifu wa misitu. Aidha Serikali iwahamasishé wadau wote wanaohusika na usimamizi wa misitu nchini ili waweze kuungana katika kutekeleza jukumu la utunzaji wa misitu ipasavyo.

(l) Kusimamia mkakati wa upandaji miti kitaifa kwa kila Wilaya na kuhamasisha wanachi kutumia nishati mbadala ili kuondokana na utegemezi mkubwa wa misitu kama chanzo kikuu cha nishati. Hii ni pamoja na kutunga sheria ndogo zitakazowalazimisha wananchi kupanda na kutunza miti kwa lengo la kuinua sekta ya misitu nchini.

(m) Kutoa mafunzo yanayohusu kuanzisha na kuendeleza misitu kwa wananchi wanaozunguka misitu ya hifadhi kwa lengo la kuimarisha ushiriki wa wananchi katika uhifadhi wa misitu na hifadhi za nyuki.

7.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na ushauri wa Kamati

kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Kamati inaamini ushauri wake utazingatiwa ili kuisaidia Serikali kutekeleza mipango ya maendeleo na kuinua utalii kwa faida ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika Napenda kumshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe, Prof.Jumanne Abdallah Maghembe (Mb) na naibu wake Mhe, Mhandisi Ramo Makani (Mb) pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara hii.

Kamati inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuipa Kamati ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadiryo ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Atashasta Nditiye, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Kemirembe Lwota, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Atupele Fred Mwakibete, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Devota Minja , Mb "
5. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb "
6. Mhe. Jaffar Sanya Jussa, Mb "
7. Mhe. Joshua Samwel Nassari, Mb "
8. Mhe. Khalifa salim Suleiman, Mb "
9. Mhe. Dr. Godwin Aloyce Mollel, Mb "
10. Mhe. Magdalena Hamis sakaya, Mb "
11. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb.
12. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb"
13. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb "
14. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb "
15. Mhe. Risala Kabongo, Mb "
16. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb "
17. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb "
18. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb "
19. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb "
20. Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mb "

- | | | |
|-----|---------------------------------|---|
| 21. | Mhe .Omari Abdallah Kigoda,Mb | " |
| 22. | Mhe. Richard Mganga Ndassa,Mb | " |
| 23. | Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb | " |
| 24. | Mhe.Neema William Mgaya, Mb | " |
| 25. | Mhe. Salma Mohamed Mwassa, Mb | " |
| 26. | Mhe. Nappe Moses Nnauye, Mb | " |

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Ndg Dickson Bisile, Ndg Gerald Magili, Ndg Haika Mtui, Ndg Elieka Saanya na Ndg Jane Ndulesi pamoja na Wafanyakazi wote wa Bunge kwa kuihudumia kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii.Mwisho namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Eng. Atashasta J.Nditiye, (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII

23 Mei, 2017

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kufuatana na taarifa yao, kuna baadhi ya maneno machache sana kwa mujibu wa *ruling* ya Spika, yametolewa na Msemaji ameshapewa taarifa. Kwa hiyo, ukurasa wa 25 wa A4 ambayo Mheshimiwa Matiko unaisoma, uzingatie. Kwa Wajumbe ambao wana kitabu hiki cha Upinzani taarifa yao itakuwa ni ukurasa wa 21. Naomba maelekezo hayo yatekelezwe.

Sasa nakuita rasmi Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwenye Wizara hii. (*Makofii*)

MHE. ESTHER N. MATIKO - MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2017/2018, yanayotolewa chini ya Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(9), Toleo la Mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema nisimame mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa familia yangu, wananchi wangu wa Tarime Mjini kwa upendo wao mkubwa wanaonionesha na nitazidi kuwatumikia kwa uadilifu mkubwa sana ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mboge kwa kuendelea kuwa imara. Vilevile, natoa pongezi kwa viongozi wa UKAWA hususan kwa viongozi wa Chama cha Wananchi (*CUF*) kwa kuendelea kuwa wamoja hata pale ambapo imeonekana kuna baadhi ya watu wanataka kuwayumbisha kwa maslahi yao binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi, namshukuru Naibu Waziri Kivuli, Mheshimiwa Cecilia Pareso kwa kazi nzuri alioifanya na kutoa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kuandaa hotuba hii. Natoa pongezi kwa Wabunge wenzangu wa Upinzani kwa kuendelea kuwa wavumilivu, wenye busara na zaidi kuendelea kuwa na umoja na mshikamano katika kutekeleza wajibu wao wa kuishauri Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizi, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, lakini kabla ya kuwasilisha, naomba kufanya marekebisho kidogo kwenye ukurasa wa 15 sehemu ya 10 ambapo kuna neno " WMA" litaondoka liingie neno la "TAWA" kuhusiana na Mkurugenzi ambaye amekuwa akitaimu nafasi ile kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imebeba mambo yafuatayo:-

- Kwanza hali ya Sekta ya Utalii nchini;
- Mgogoro sugu wa Loliondo;
- Uanzishwaji wa usimamizi wa *Wildlife Management Areas (WMAs)*;
- Migogoro baina ya vijiji na Hifadhi ya Wanyamapor;
- Athari za ongezeko la kodi katika sekta ya utalii nchini;
- Kuanzishwa bustani wa wanyama katika msitu wa Pande, Ruaha *National Park*;
- Serikali kushindwa kuvumbua vivutio vipyaa ya utalii;
- Vazi la Taifa na manufaa yake katika Sekta ya Utalii;

- Ushirikishwaji wa *Diaspora* katika kutangaza utalii;
- Tathmini ya uthibiti wa biashara ya pembe za ndovu; Sekta ya Wanyamapori na biashara ya uwindaji nchini;
- Ugawaji wa maeneo ya hifadhi bila kuzingatia taratibu za kulinda wanyamapori na misitu;
- Zuio la matumizi ya mkaa, kilio kwa wananchi;
- Ufugaji wa nyuki; na
- Uchambuzi wa bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgogoro sugu wa Loliondo ni mgogoro uliodumu kwa takriban miaka 30 sasa. Ni mgogoro uliogharimu maisha ya Watanzania wengi kutoka katika jamii ya wafugaji waishio katika bonde la Loliondo. Mgogoro huo umechochewa na pande tatu zinazosigana kwa maana ya Serikali, Wawekezaji na wananchi wanaoishi katika eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya mgogoro wa Loliondo; miaka ya 1980 mpaka 1993 Mfalme kutoka nchi za Kiarabu alikuja Tanzania yeche na familia yake kwa shughuli za uwindaji wa wanyamapori. Mwaka 1992 walipokuja nchini walifanya uwindaji mkubwa zaidi ambao haukuwahi kutokea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jarida la *New York Times* la tarehe 13 Novemba, 1993 liliandika kushtushwa na uwindaji huo wa kutisha wa wanyama kama Duma na Mbwa

Mwitu ambao wapo katika hatari ya kutoweka; vilevile gazeti la Mfanyakazi la tarehe 20, Januari, 1993 lilichapishwa likiwa na kichwa cha habari "*Tanzania inavyoliwa na Waarabu.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfalme na familia yake kupitia kampuni ya *OBC* walipewa kibali cha uwindaji kwa miaka kumi na aliyekuwa Waziri wa Utalii wa wakati huo Abubakar Mgumia kinyume na Sheria za Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974 na Sheria ya Mashirika ya Umma Na. 17 ya mwaka 1969 ambayo iliyataka makampuni binafsi walete wageni nchini kupitia Shirika la Umma la wakati huo ambalo ni *Tanzania Wildlife Corporation (TAWICO)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na masharti hayo ya kisheria, kampuni hii ilipewa mkataba wa kumiliki ardhi ya vijiji sita vilivyo ndani ya hifadhi ya Loliondo. Mkataba huo ultiwa salni na Marehemu Richard Punye aliyekuwa Mbunge pamoja na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Abubakar Mgumia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa Mkataba huo uliwekwa saini kinyume cha sheria kama nilivyoelezea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kampuni ya *OBC* kumilikishwa ardhi kilichochea kuongezeka kwa mgogoro kati ya kampuni hiyo na wananchi, ambapo wananchi wengi walichomewa maboma na walinzi wa kampuni hiyo mwaka 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hiyo vijiji vilivyoathirika na uchomaji wa makazi yao, viliamua kuunda Kamati ya Wajumbe 13 walitumwa kuonana na aliyekuwa Mheshimiwa Rais wa wakati huo Jijini Dar es Salaam. Japokuwa hawakufanikiwa kuonana naye lakini walikutana na Mwandishi wa Habari Jenerali Ulimwengu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madai ya wanakijiji hao, walizungumzia ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu uliofanywa na mwekezaji huyo, ucharibifu wa mazingira, ukiukwaji wa haki za wanyama na kujenga majengo makubwa ndani ya hifadhi, karibu kabisa na Mto

Olasai ambapo ni kinyume cha Sheria za Uhifadhi. Majengo hayo yaliyojengwa wakati huo mpaka sasa yapo na Serikali haijachukua hatua yoyote pamoja na kujengwa kinyume na utaratibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, aliye kuwa Waziri wa Maaliasili na Utalii, Bi. Zakiah Meghji alitoka hadharani na kuwapinga vikali Wajumbe hao kuititia habari iliyochapishwa tarehe 11 Aprili, 2000 kwenye gazeti la *The Guardian*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Desemba, 2005 mwekezaji huyo aliongezewa vijiji vingine viwili na kufanya jumla ya idadi ya vijiji vinane ambavyo alipewa kumiliki ardhi yake katika shughuli za uwindaji. Hii ni kwa mujibu wa barua namba DC/NGOR/C.15/5/120 ilioandikwa na aliye kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro Ndugu Jowika Kasunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa mgogoro kati ya mwekezaji na wananchi ambao uligharimu maisha ya wananchi wengi na mifugo yao, mwaka 2009 aliye kuwa Mbunge wa Ngorongoro Ndugu Kaika Telele aliamua kuleta jambo hilo ndani ya Bunge. Turejee *Hansard* ya tarehe 11 Julai, 2009. Pamoja na Mbunge huyo kuzungumzia sana mgogoro huo, mpaka sasa hakuna suluhu iliyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2010, aliye kuwa Spika wa Bunge, aliamuru Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuunda Tume kwenda kuchunguza mgogoro huo wakati huo, lakini pia haikuweza kuwa mwarobaini wa mgogoro huo. Hata hivyo, aliye kuwa Waziri Mkuu wa wakati huo aliunda Kamati ya Mawaziri sita akiwemo aliye kuwa Waziri wa Utalii kulifuatilia suala hilo mnamo tarehe 8 Februari, 2010. Kamati ile nayo haikuzaa matunda na mpaka leo Serikali hii ya Awamu ya Tano haijaweza kuwa na mwarobaini wa mgogoro huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi majuzi tu mwezi Februari, 2017, Waziri Mkuu alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Arusha kufuatilia mgogoro huu ambao umedumu kwa muda

mrefu. Timu hii ya Mkuu wa Mkoaa imetumia mamilioni ya shilingi kama ilivyo kwa timu na Tume nyingi ambazo zimewahi kuundwa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Timu hii ya Mkuu wa Mkoaa wa Arusha iliwasilisha mapendekezo yake ambapo wakati huo huo Waziri wa Maliasili na Utalii tayari alikuwa amekwisha kufanya maamuzi juu ya mgogoro huu ambapo alitoa kauli ya kutenga eneo la kilometa za mraba 4,000 kwa ajili ya pori tengefu la Loliondo na kuamuru kwamba eneo la kilometa za mraba 2,500 zilizokuwa zimechukuliwa na wawekezaji zirejeshwe kwa wananchi ili kuendelea kulinda ikolojia ya Serengeti ambayo sasa ipo hatarini. Pia aliagiza *TANAPA* kuweka mipaka katika eneo hilo la hifadhi ili kuzuia mifugo inayoharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mgogoro wa Loliondo ni suala la muda mrefu, limegubikwa na tuhuma mbalimbali za rushwa, usiri, utapeli; na ukitazama kwa undani jambo hili utagundua ujasusi mkubwa wa kiuchumi unaofanywa na Mataifa mengine dhidi ya Taifa letu kuitia hifadhi zetu na hazina ya wanyamaporii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka majibu dhidi ya tuhuma zinazowakabili wawekezaji wa kigeni katika Bonde Tengefu la Loliondo wanaojishughulisha na shughuli za uwindaji na utalii ambapo Serikali zilizopita zimekuwa zikitofautiana kimtazamo juu la suala hili kama ifuatavyo:-

- Jeshi la Wananchi wa Tanzania kutoa ulinzi katika kampuni binafsi ya uwindaji na utalii tofauti na ilivyo kwa makampuni mengine ya uwindaji na utalii nchini;

- Uwepo na majengo ya kudumu katika eneo la mapitio ya wanyamaporii kwenye Bonde Tengefu la Loliondo kinyume na Sheria za uhifadhi;

- Uwepo wa lkulu ya Mfalme katika mapito hayo ya wanyamapor;
- Uwindaji wa wanyama usiozingatia haki za wanyamapor;
- Ukiukwaji wa Sheria za Uhifadhi wa Wanyamapor;
- Ukiukwaji wa Sheria ya ugawaji wa vitalu vya uwindaji ndani ya Bonde hilo;
- Ukiukwaji wa Sheria za Mawasiliano ambapo Kampuni ya *OBC* inayojinasibu kuwa mshirika wa *Zantelbado* inatoa huduma ya mawasiliano ya simu ya *Etisalat ya United Arab Emirates* kinyume na Sheria za Mawasiliano;
- Uwepo wa uwanja mkubwa wa ndege katika eneo la mapitio ya wanyamapor;
- Ukiukwaji wa sheria za vijiji na ardhi za vijiji;
- Ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu ikiwemo mauaji, uchomaji wa maboma, vitisho kwa wanahabari wa mgogoro huu kutoka ndani na nje ya nchi; na
- Tuhuma za rushwa kwa viongozi mbalimbali katika Sekta ya Utalii hasa wanaoshughulikia mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudi matumizi ya fedha nyingi na rasilimali za nchi ambapo tume mbalimbali zinazogharimu mamillioni zimeundwa bila mafanikio yoyote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na suluhisho la kudumu kuhusu mgogoro wa Loliondo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Serikali kuja na kauli moja kuhusiana na mgogoro wa Loliondo badala ya matamko ya kisiasa yanayokinanza na kauli za kubezana kwa watendaji wa Serikali kama zile alizozitoa Mkuu wa Mkoa wa Arusha katika mukutano wake na wanahabari wakati akitoa taarifa ya utendaji wa Serikali ya robo mwaka.

Mfano, kwa mujibu wa Gazeti la Mwananchi la tarehe 2 Februari, liliolobeba kichwa cha habari "RC Gambo ampinga Waziri Maghembe mgogoro wa Loliondo", ni ushahidi tosha kuwa Serikali haina malengo ya pamoja katika kutatua mgogoro kwani Mkuu wa Mkoa alisema tamko lillilotolewa kuhusiana na mgogoro huu ni maoni tu. Tukumbuke kuwa, tamko la Waziri ni suala linalohitaji utekelezaji na sio maoni kama alivyosema Mkuu huyu wa Mkoa. (*Makofii*)

(ii) Kwa kuwa Waziri aliahidi katika Tamko lake kurudisha kwa wananchi eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 2,500 kwa ajili ya wananchi na mifugo yao, hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa, ni vyema sasa eneo hilo likachimbwa mabwawa makubwa ya maji kwa ajili ya kusaidia mifugo na kupata maji ya uhakika na kuepusha wanavijiji kurundikana karibu na maeneo ya mto na pia kulinda ikolojia ya eneo hilo la wanyamapor. (*Makofii*)

(iii) Serikali itenge eneo lenye malisho itasaidia pia kuondoa tabia ya wanavijiji kwenda kwenye eneo la hifadhi ili pia kulinda mifugo dhidi ya magonjwa yanayotokana na wanyamapor kwani madhara yake ni makubwa kwa mifugo hiyo na pia ni hatari kwa afya za binadamu. (*Makofii*)

(iv) Serikali itoe majibu kwa tuhuma zinazoikabili Kampuni ya *OBC* pamoja na Serikali kama ilivyoelezwa kwenye historia ya mgogoro huu.

(v) Serikali ifanye uchunguzi wa mifugo katika vijiji hivyo kwani kuna malalamiko kuwa nchi jirani pia zinaingiza mifugo yake katika eneo hilo la Loliondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji na usimamizi wa *Wildlife Management Areas (WMAs)*. Kumekuwa na tatizo kubwa la ujangili ambapo umeathiri kwa kiasi kikubwa uwepo wa wanyamapori wa aina mbalimbali katika nchi yetu jambo ambalo pia kwa kiasi kikubwa limeathiri sekta ya utalii kwa ujumla. Ni wazi kuwa mtandao huu wa ujangili umefanya na watu wenye uwezo mkubwa kiuchumi na pengine kwa kushirikiana na watu wenye madaraka kisiasa au katika vyombo vya dola. Katika kupambana na tatizo la ujangili kulianzishwa kitu kinachoitwa *Wildlife Management Areas (WMAs)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo makuu ya kuanzishwa kwa WMAs ilikuwa ni:-

(i) Kushirikisha wigo mpana wa wananchi katika kuhifadhi wanyamapori;

(ii) Kuimarisha ulinzi wa wanyamapori nje ya maeneo rasmi ya uhifadhi; na

(iii) Wanavijiji kunufaika moja kwa moja na manufaa yatokanayo na matumizi endelevu ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, WMAs ni motisha kwa jamii ili kuendeleza wanyamapori na kulinda mazingira katika maeneo ya uhifadhi nchini. Kushirikisha jamii katika mpango huu ni njia mbadala inayoruhusu ubunifu katika mipango ya kulinda na kudumisha shughuli za uhifadhi. Mfano, ni hivi karibuni vijiji katika Wilaya ya Simanjo wamekubali kutenga ardhi ya vijiji kwa hiari yao ili sasa shughuli za utalii ambazo ni sehemu za lkolojia ya Tarangire ziweze kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kujenga hoteli za kitalii na kusitisha shughuli za ufungaji na kilimo katika maeneo hayo ili kulinda mazalia ya nyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uanzishwaji wa kisheria wa *WMAs* bado kanuni za uendeshwaji na mgawanyo wa mapato baina ya vijiji husika na Serikali kuu hazifuatwi ipasavyo. Jambo hili limekuwa likiibua migogoro ya mara kwa mara baina ya wanavijiji na *TANAPA*. *WMAs* zimekuwa na changamoto kubwa hasa katika mfumo wa utozaji kodi na magawanyo wa mapato. Hii ni kutokana na Serikali kuchukua kiasi kikubwa cha fedha kinachotokana na mapato ya utalii kwenye *WMAs* na hivyo kushindwa kutekeleza shughuli za ulinzi wa wanyamapori na kushindwa kufanya shughuli za kuwaletaa wanavijiji maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachukua 55% ya mapato yatokanayo na uwindaji na kuiachia *WMA* 45%. Vijiji vingi vinategemea mapato ya uwindaji kuliko utalii wa picha. Pamoja na hilo, Serikali imekuwa ikikusanya mapato yote ya utalii, yaani mapato ghafi, ambapo mapato hayo hupelekwa kwenye Mamlaka ya *TAWA* yenye akaunti *BoT*na fedha hizo huombwa tena kupelekwa *WMA* husika. Hii imechelewesha fedha kufika kwenye *WMA* hizi na fedha hizo wakati mwingine hazifiki kwa ufasaha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Serikali haijatia saini kanuni za uendeshaji wa *WMAs* zilizofanyiwa mapitio mwaka 2012. Mpaka sasa Serikali haijatoa sababu zozote ni kwa nini kanuni hizo hazijatiwa saini mpaka leo. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri yafuatayo:-

(i) Kupunguza masharti ya uanzishaji *WMAs* kwa jamii;

(ii) Kuwe na ufanuzi na utaratibu wa ugawanaji mafao katika *WMAs*, ili kuhakikisha kuwa asilimia 70% ya mapato kutoka *WMAs* inabaki ngazi ya vijiji kama ilivyoanishwa kwenye kanuni; (*Makofii*)

(iii) Kuhakikisha kuwa Serikali za vijiji zinapewa maamuzi ya kisheria kulingana na uwekezaji katika *WMAs*, ikiwa ni pamoja na kuamua ni kampuni zifiyanje shughuli

za kitalii katika maeneo yao na Serikali ibaki na usimamizi wa jumla na maelekezo ya kisera tu;

(iv) Maeneo ya *WMA* syaoanishwe na maeneo ya ardhi ya misitu ya vijiji ili jamii wapate manufaa ya juu kutokana na maliasili katika ardhi za vijiji;

(v) *WMAs* zilipwe fedha zake moja kwa moja kutoka kwa wawekezaji ili *WMAs* hizi ziweze kulipa mgao wa mapato kwa Serikali Kuu na Halmashauri za Wilaya;

(vi) Serikali iharakishe kutia saini kanuni zilizofanyiwa mapitio kama sehemu ya makubaliano kati ya Wizara ya Maliasili na Wadau wa Hifadhi yaliyofanyika tarehe 2 na 3 Julai, 2015;

(vii) *WMAs* ziweze kujengewa uwezo ili kuweza kuijendesha vizuri;

(viii) Mtazamo wa kisera unahitajika na elimu kwa wananchi kuhusiana na malengo ya *WMAs*; na

(ix) Serikali iweze kumthibitisha Mkurugenzi wa *TAWA* ambaye amekaimishwa nafasi hiyo kwa takribani miaka miwili sasa ili kuongeza ufanisi katika utendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro baina ya vijiji na hifadhi za wanyamapori. Kumekuwa na mgogoro mingi na ya muda mrefu baina ya vijiji na Mamlaka ya Hifadhi. Migogoro hii imekwenda mbali zaidi na katika maeneo mengine kusababisha vifo na familia nyingi kuathirika vibaya kutokana na operesheni za kamatakamata kwa wananchi katika maeneo ambayo yanapakana na hifadhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Mbarali ambapo kumekuwa na mgogoro uliodumu kwa takribani miaka nane baada ya Serikali kuamua kuongeza eneo la hifadhi kwa kuingia kwenye vijiji 21 ambavyo hutumiwa na wananchi kwa ajili kujipatia chakula na shughuli zingine za kiuchumi. Wananchi wa maeneo hayo

wameishi katika eneo hilo kwa miaka mingi kabla ya ukoloni kuwepo katika nchini yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa wananchi hawa sio wavamizi kama inavyoelekezwa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa kwa sasa wananchi wa vijiji hivi wamekataliwa kuendeleza miundombinu katika eneo hilo. Pamoja na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu uliopita Rais alipokwenda Mbarali alitoa ahadi kwa wananchi ya kujenga barabara ya lami Mbarali kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa mazao yao kwenda viwandani na tayari barabara hiyo imejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wananchi wa maeneo hayo kupongezwa kwa killimo kizuri tena kilichoingatia utunzaji wa mazingira leo wanaondolewa katika maeneo yao kwa sababu ya upanuzi wa hifadhi ambapo miaka iliyopita walishawahidi tena kusogezwa kwa sababu ya upanuzi wa hifadhi hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuja na majibu kuhusiana na mgogoro huu wa wananchi na hifadhi ambazo wananchi wamekuwa wakiishi katika maeneo yao kwa muda mrefu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupata sababu za kwa nini Wizara inapingana na ahadi ya Rais ya kuwasaidia wananchi wa Mbarali ambao hutegemea kilimo ili kuwasaidia katika usambazaji wa mazao ya chakula nchini ikizingatiwa kuwa kutokana na shughuli hizo wameweza kutoa ajira zaidi ya 30,000 na wanachangia uwepo wa viwanda vikubwa 42 na *magodown* makubwa zaidi ya 56. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maliasili na utalii. Athari ya ongezeko la kodi katika sekta ya utalii nchini. Suala la mlundikano wa kodi kwa wafanyabiashara katika sekta ya utalii sio geni. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikilizungumzia jambo hili mara kwa mara kutokana na jinsi

linavyowaumiza wadau wa sekta ya utalii nchini pamoja na wananchi wengine wanaotegemea shughuli za utalii katika kujipatia riziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Kambi ya Rasmi Upinzani wakati wa Mkutano wa Bajeti wa mwaka wa fedha 2016/2017, ilizungumzia suala la ongezeo la kodi la VAT na ikaonesha madhara makubwa yanayoweza kujitokeza endapo Serikali itapandisha kodi hii kwa ghafla. Pamoja na uchambuzi huo uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Serikali ili amuru wafanyabiashara hao kulipa kodi hiyo mara moja na jambo ambalo limewasababishia wafanyabiashara hao hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuyumba kwa biashara ya utalii nchini na pia ongezeko kubwa la kodi, wafanyabiashara hao walilazimika kupunguza wafanyakazi na hivyo Serikali ilikosa kodi ya mapato inatokanayo na mishahara ya wafanyakazi (*PAYE*). Aidha, baadhi ya wamiliki wa makampuni na hoteli wamelazimika kuuza hoteli na makampuni yao kwa sababu ya usumbufu kwa wageni kwani wengi walilazimika kuchangia ongezeko hilo la kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, kuna takribani zaidi kodi 36 ambazo wafanyabiashara wa utalii nchini wanalazimika kulipa. Hizi ni baadhi tu ya kodi katika sekta ya utalii nchini. Mlundikano huu wa kodi hasa kwa wafanyabishara wazawa ni taswira tosha kwa wananchi wetu kujua kwamba ni namna gani Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi inavyowakamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Gazeti la Mwananchi la tarehe 4 Februari, 2016 katika Makala ya Uchumi yenye kichwa cha habari kuwa "Wingi wa Kodi Unavyoua Utalii Tanzania" limeleeza kwa kina utafiti uliofanywa na Dkt. Hawa Eve Sinare unaoonesha ili mfanyabiashara wa utalii Tanzania aweze kulipa kodi, kutimiza masharti ya leseni na malipo mengineyo inamlazimu kutumia takribani saa 2,000 kwa mwaka. Hii ni kutokana na wingi wa masharti ya

wafanyabiashara wa ndani na nje katika sekta ya utalii ikilinganishwa na sekta nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Tanzania ina takribani makampuni 1,050 yanayofanya biashara ya utalii, lakini ni kampuni 300 tu ndiyo zilizoweza kutimiza masharti ya kulipa kodi kutokana na wingi wa kodi na mfumo mzima wa ulipaji kodi. Ni jambo la ajabu kabisa na ni rahisi zaidi kulipa faini kwa kosa la kufanya biashara kinyume na sheria kuliko kutekeleza masharti ya ulipaji kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuziangalia upya kodi zinazowaumiza wafanyabiashara ya utalii nchini, lakini pia Serikali haina budi kuanzisha '*one stop centre*' kwa ajili ya malipo ya kodi katika sekta ya utalii kwani kumekuwa na usumbufo mkubwa kwenye ulipaji. Vilevile Serikali iondoe mkanganyiko katika kudhibiti usajili unaojirudiarudia bila sababu katika kampuni za usajili nchini, hii ni kwa sababu kati ya kodi 36 zinazolipwa kodi 12 ni za usajili na leseni peke yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa bustani ya wanyama katika Msitu wa Pande. Pori la akiba lijulikanalo kama Msitu wa Pande limekuwa ni msitu wenye historia ya kipekee na ya kutisha sana kutokana na mauaji mbalimbali yanayofanyika ndani ya msitu huo. Msitu huu uliopo takribani kilometra 25 kutokea Jiji la Dar es Salaam kuelekea Bagamoyo ni msitu wenye wanyama wadogo wadogo na mimea ya kipekee ambayo haipatikani katika maeneo mengine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 ndani ya Bunge hili Mheshimiwa John Mnyika aliwahi kuuliza swalii la nyongeza kuhusiana na ahadi ya Serikali katika kuuendeleza msitu ili uwe sehemu ya utalii kama sehemu ya matumizi bora ya misitu ambapo ahadi hii ya kuufanya msitu huu kuwa sehemu ya utalii ni ahadi ya Serikali ya muda mrefu na Serikali ilishawahi kutangaza zabuni ambayo mpaka leo haijulikani ilipotelea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mheshimiwa Naibu Waziri, alijibu kama ifuatavyo:-

"Nimponeze Mheshimiwa Mnyika kwa mtazamo chanya wa kwamba anakubaliana na dhana nzima ya matumizi bora ya maeneo ya misitu; hapingani na dhana nzima ya Serikali kuhusiana na kuifanya misitu iwe ni rasilimali ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya maslahi ya jamii. Kuhusu suala la kwamba kuna ucheleweshaji kama ambavyo amesema, nataka nimtoe wasiwasi kwamba, historia inatukumbusha tulipotoka, mahali tulipo na inatuwezesha kuona kule ambako tunakwenda. Nataka Mheshimiwa Mnyika akubaliane tu na rai yangu kwamba, tumetoka tulikotoka, mipango imekuwepo, lakini awamu hii mipango hii ninayoizungumzia ni ya uhakika na kwamba awamu hii nataka anipe muda wa mwaka mmoja tu, halafu aweze kuona katika eneo hilli kutafanyika ni".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yaliyokuwa ni majibu ya swali mwaka 2015. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kutoa mfano wa nchi ya Kenya ambapo Jiji la Nairobi kuna Msitu wa Karura (*Karura Forest*) ambao umekuwa ni kivutio kwa wakazi wa Nairobi na wageni wanaotembelea nchi hiyo. Msitu huu wa Karura umekuwa ukichangia uhamasishaji na utangazaji wa shughuli za utalii nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kushauri kuwa ni wakati muafaka sasa Serikali kuanzisha bustani ya wanyama katika Msitu wa Pande na hivyo kuwa sehemu ya utalii kwa wananchi wa Mkoa wa Dar-es-Salaam pamoja na watalii wengine wanaotembelea nchi yetu. Bustani hii inaweza kuwa sehemu ya wananchi kuwa na maeneo ya kupumzika mwishoni mwa mwaka au wiki lakini vilevile inaweza kuliongezea pato Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kushindwa kuvumbua vivutio vipyta vya utalii. Kwa miaka mingi sasa Serikali yetu imekuwa ikitegemea mbuga za wanyama, milima, bahari, uchongaji wa vinyago na kutembelea

malikale kama sehemu kuu za utalii katika nchi yetu. Serikali imejifunga katika vivutio hivyo nilivyorejea japo kuna utalii wa aina nyingi ambao unaweza kuongeza pato la Taifa na kuwaleta wananchi maendeleo binafsi na kwa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya hivi karibuni kumekuwa na kauli mbalimbali za kutaka kujua katikati mwa Tanzania ni wapi ili kuweka alama itakayotumika kama sehemu ya kihistoria na sehemu ya utalii wa nchi yetu. Katika vyanzo mbalimbali vya habari vinaonyesha kuwa katikati mwa Tanzania ni kijiji cha Sukamahela kilichopo Kata ya Solya, Wilayani Manyoni, Mkoani Singida. Hii ni kutokana na uwepo wa chuma kilichopo kijijini hapo kinachosadikiwa kuwa ndipo eneo rasmi la katikati ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na taarifa hizo za Kijiji cha Sukamahela, vyanzo vingine vinaonesha kuwa Kitongoji cha Darajani, Kijiji cha Chisinzisa, Kata ya Sasilo, Tarafa ya Nkonko Wilayani Manyoni ndipo eneo la katikati mwa Tanzania. Katika Makala ya Gazeti la Mwananchi Januari, 2015 lilieleza kwa kina aina ya vipimo mbalimbali vilivyotumiwa na Serikali ya Ujerumani wakati wa ukoloni na vipimo vilivyofanyika na Serikali ya Tanzania chini ya mpima ardhi wa Singida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuwa na wataalam wa kufanya tafiti kwenye vivutio vipyta vya utalii nchini. Kitendo cha Serikali kuendelea kukumbatia vivutio vilevile ambavyo matokeo yake ni yaleyale, ni kitendo cha kuendelea kudidimiza sekta ya utalii nchini. Bajetti inayotengwa na Serikali ni lazima iweke kipaumbele katika kufanya utafiti ili kuweze kuwepo na vivutio vyenye tija ambavyo vitafikika kwa urahisi na vitawezwa kuwawutia watalii wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuna vivutio vingine ambavyo vikiwekezwa vinaweza kuleta manufaa makubwa. Mfano, Mkoani Kilimanjaro katika Wilaya ya Same kuna Mlima wa Shengena ambao ni maarufu kwa ufugaji wa ngo'mbe

wa asili ambao huitwa kwa miluzi na wanajichunga wenye na kuna uwanda mzuri kwa ajili ya watalii kufanya *camping*; kuna Ziwa Kenyabasa kule Kagera ambalo ni ziwa la maajabu kutoka kwenye chungu; kuna kimondo cha Mbozi; maajabu ya Mto Kiwira - mto huingia ndani ya shimo dogo la miamba; maji moto yaani *hot spring* katika Kijiji cha Chemka huko Wilaya ya Hai; *hot spring* Mkoani Mbeya; kuna udongo unahama (*shifting and sand dunes*) Mkoani Manyara ambapo eneo hilo halijatangazwa ipasavyo; Makumbusho ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kule Butiama; maporomoko ya maji ya Mto Rusumo na muonekano mzuri wa Ziwa Chala. Tuna vivutio vingi sana ambavyo Serikali ingeweza kuwekeza na kuvitangaza, tungeweza kuongeza watalii na kuongeza pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji wa *diaspora* katika kutangaza utalii. Biashara yoyote inahitaji matangazo ili iweze kufanya vizuri zaidi. Katika kufanya matangazo haya, mbinu mbalimbali zinaweza kutumika. Hapa nchini Bodi ya Utangazaji wa Vivutio vya Utalii imekuwa ikikumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo changamoto za kifedha katika kufanya maonesho mbalimbali, kutoa machapisho na matangazo kwa njia ya elektroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa, ni wakati sasa wa kuwa na Kitengo cha Utalii cha *Diaspora* ambacho kitafanya kazi kutangaza vivutio vyetu ikiwemo vivutio vipyta ambavyo vitatambuliwa. Pamoja na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa ni wakati sasa wa kuhamasisha *diaspora* ili waweze kufanya *investment* katika sekta ya utalii, hii ni pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kuweza kuwekeza zaidi katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Hotuba yangu yote kwa ukamilifu iweze kuingia kwenye *Hansard*. Naomba Serikali kwa kweli iweze kuifanya kazi na kuleta majibu kwa faida ya Tanzania yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho...

MWENYEKITI: Mpeni maji jamani.

MHE. ESTHER N. MATIKO – MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, *I don't need maji.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Mpaka sasa sekta nyingi hazifanyi vizuri kutokana na mapato hafifu yanayokusanya na Serikali hali inayosababisha hali mbaya ya uchumi wetu. Pamoja na hilo sekta hii ya maliasili na utalii inaweza kuwa mkombozi katika kuchangia uchumi, hususan miradi ya maendeleo, endapo tu Serikali itaamua kuweka kipaumbele na kuhimiza wawekezaji kwenye sekta ya utalii kwani matokeo yake yanaweza kuwa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani haitasita kuendelea kuishauri Serikali kwa kuwa, hii ni nchi yetu sote na endapo tutanyamaza basi ni hakika lori hili tulilolipanda linaweza kumshinda dereva na sote tukajikuta shimonii. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuja na majibu kwa maswali na hoja ilizohoji na pia kuufanya kazi ushauri uliotolewa kujenga Taifa lenye tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo tutashindwa kusema kwa kushauri au kukosoa, basi tujue wazi kuwa tutakuwa tumeamua kuua Taifa hili. Kuwanyima wenye akili mbadala kusema maana yake ni kuwalazimisha Watanzania kuwaza kwa namna moja inayofanana, jambo ambalo litahatarisha amani ya nchi na ukiukwaji mkubwa wa utawala bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere alisema kwa maneno haya, naomba kunukuu:-

"Tuweke utamaduni wa kudhibiti viongozi wetu kama wanavunja sheria ya nchi. Tusiogope, tukianza kuwa waoga, I promise you, mtatawaliwa na dictators, I promise you. Ninyi Wabunge mkiogopa na mkisema mzee wanakuwa wakali! I promise you, you will be under dictatorship." (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno haya yenye busara ya hali ya juu ya muasisi wa Taifa hili, basi tujifunze kupokea maoni mbadala hata kama hayatufurahishi, kwani kufanya hivyo tunaisaidia nchi yetu na tutakuwa tunaishi yale aliyoyasema Mwalimu Nyerere kwa vitendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante.

**HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI
MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAUS MATIKO KUHUSU BAJETI
YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA
MWAKA WA FEDHA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA
MWEZANI**

(Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016)

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara hii muhimu. Aidha, napenda kutoa pole kwa Bunge lako kwa kuondokewa na wapendwa wetu Marehemu Samwel John Sitta aliyekuwa Spika wa Bunge la Tisa , Marehemu Hafidhi Ali Tahir aliyekuwa Mbunge wa Dimani na Marehemu Dr. Elly Marco Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, Kipekee kabisa napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa familia yangu kwa upendo wao mkubwa wanaonionyesha. Napenda kuwaambia kuwa wao ni faraja kubwa katika maisha yangu na kila siku ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu ili aendelee kuwapa ulinzi. Pia, nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Tarime mjini kwa ushirikiano wao na upendo wanaonionyesha. Bado nitazidi kuwatumikia ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbewe (Mb) kwa kuendelea kuwa imara hata pale alipopata misukosuko ambayo mahasimu waliamini ingemrudisha nyuma katika kupigania demokrasia nchini.Vilevile, nitoe pongezi kwa viongozi wa UKAWA hususani kwa viongozi wa Chama cha Wananchi CUF kwa kuendelea kuwa wamoja hata pale ambapo imeonekana kuna baadhi ya watu wanataka kuwayumbisha kwa maslahi yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, zaidi nimshukuru Naibu Waziri Kivuli wa Wizara hii Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso kwa kazi nzuri aliyoifanya na kutoa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kuandaa hotuba hii. Nitoe pongezi kwa Wabunge wenzangu wa Upinzani kwa kuendelea kuwa wavumilivu, wenye busara na zaidi kuendelea kuwa na umoja na mshikamano katika kutekeleza wajibu wao wa kuishauri serikali. Nipende kuwatia moyo tu kwa kutumia maneno haya kutoka kwa Obrien anasema “ **I've learned that fear limits you and your vision. It serves as blinders to what may be just a few steps down the road for you.The journey is valuable, but believing in your talents, your abilities, and your self-worth can empower you to walk down an even brighter path. Transform fear into freedom-how great it that?**”Kwa tafsiri isiyo rasmi, *nimejifunza kwamba woga ni kikwazo kwangu na kwa maono yangu. Ni kama upofu kwa kile kilicho hatua chache tu mbele yangu. Safari hii ni ya thamani, amini katika kipaji chako, uwezo wako na thamani yako itakusaidia katika njia iliyonyoofu. Geuza hofu yako kuwa ukombozi wako.*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu sasa naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa kuanza na nukuu ya Theodore Roosevelt kuhususiana na utatuzi wa matatizo ya uhifadhi wa maliasili zetu alisema” ***The conservation of natural resources is the fundamental problem.Unless we solve that problem it will avail us little to solve all others***”.

2.0 MASUALA MTAMBUKA KATIKA SEKTA YA UTALII NCHINI

2.1 HALI YA SEKTA YA UTALII NCHINI

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikitamani kuona sekta ya maliasili na utalii ikiwa ni moja ya sekta ambazo huchangia mapato mengi ya nchi na pia kuchangia katika kuboresha huduma mbalimbali za kijamii. Hata hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuonesha masikitiko yake kutokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa sekta hii tofauti na matamanio yake.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kuna matatizo makubwa katika sekta ya utalii. Japokuwa takwimu zinaonyesha kuwa sekta hii inakuwa kwa takribani asilimia 11 tangu mwaka 2015-2016 kama ilivyoelezwa na Wizara kuititia kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Pamoja na takwimu hizo, ni ukweli usiopingika kuwa sekta ya utalii inaporomoka kwa kasi sana.

Mheshimiwa Spika, tafiti na habari kutoka katika vyanzo mbalimbali zinaonyesha kuwa wafanyabiashara wengi wenye hoteli za kitalii wamefunga hoteli zao kutokana na kupungua kwa watalii na hivyo kukosa wateja. Kuna kampuni mengi ya Utali ambayo tayari yamepunguza wafanyakazi kutokana na kupungua kwa idadi ya watalii nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wageni wanaokuja nchini kuititia makampuni makubwa ya kigeni ambapo wateja wake ni wale wenye uwezo mkubwa kifedha wamepungua, na hata hivyo, wale wanaokuja wanakimbilia katika hoteli zenye bei ya nafuu kutokana na kuongezeka kwa gharama za utalii nchini jambo ambalo limezua malalamiko mengi kutoka kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, katika ripoti ya Wizara ya mwaka 2016 ilionyesha kuwa Idadi ya watalii wa kimataifa kwa mwaka 2015 ilikuwa ni Watalii 504,711 ikilinganishwa na

mwaka 2016 ambapo idadi ya ilikuwa watalii 519,582 waliingia nchini. Takwimu hizi ni kinyume na takwimu zilizotolewa katika randama iliyowasilishwa kwenye kamati ya ardhi, maliasili na utalii fungu 69 ambapo idadi ya watalii wa kimataifa waliotembelea nchini mwaka 2016 inaonekana kuwa ni watalii 1,284,279 ikilinganishwa na watalii 1,137,182 mwaka 2015. Takwimu hizi pia ni tofauti na ile yiliyotolewa kwenye randama ya Wizara fungu 69 ukurasa wa pili kwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, mkanganyiko huu wa takwimu ni ushahidi tosha kuna walakini katika kauli zinazotolewa kuhusu idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu. Pamoja na hilo, kuongezeka kwa fedha za kigeni kutoka dola 1,901.9 mwaka 2015 mpaka dola 2,073 mwaka 2016 inaweza kuwa sio sababu ya kuongezeka kwa watalii pekee kama ambavyo serikali inaamini. Ongezeko hilo la fedha za kigeni katika sekta ya utalii inaweza kuchangiwa pia na idadi ya siku ambazo wageni hukaa hapa nchini na aina za huduma au bidhaa wanazonunua wakiwa nchini.

Mheshimiwa Spika, tutambue kuwa sio kila mgeni aliyeorodheshwa uhamiaji ni mtalii. Maana halisi ya mtalii *ni mtu yoyote anayesafiri au kutembelea eneo fulani kwa sababu za burudani au mapumziko (a person who is travelling or visiting a place for pleasure)*. Hii ni kwa mujibu maana halisi ya utalii kimataifa. Wapo wageni wengi wanaoingia nchini kwa shughuli mbalimbali zikiwemo za uwekezaji, biashara na shughuli mbalimbali za kijamii. Pamoja na hayo, serikali itambue kuwa tumefikia katika hatua mbaya ya kichumi na hivyo ni lazima kuboresha sekta hizi nyeti za kiuchumi ili kujinasua. Kuna msemo usemao “*the deaf believe there is nothing wrong but the hearing believe something needs to be fixed*” ikiwa na maana kwamba kiziwi haoni tatizo, ila anayesikia anaamini kuna jambo ambalo haliko sawa na linahitaji ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kama sehemu mbadala ya serikali, inaona tatizo kubwa katika takwimu za ukuaji wa sekta ya utalii kama

nilivyoonesha japokuwa serikali inaona kuwa sekta hii inakwenda vizuri. Sababu kubwa ni kuwa akili zinazotengeneza matatizo katika taifa haziwezi kamwe kuwa sehemu ya kutafuta suluhihisho. Hivyo, Kambi Rasmi ya upinzani inaitaka serikali kufanya upya tathimini ya ukuaji wa sekta ya utaifi badala ya kuonyesha wingi wa takwimu usio na tija kwani kufanya hivyo, hakusaidii ukuaji wa sekta hii.

2.2 MGOGORO SUGU WA LOLIONDO

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa Loliondo ni mgogoro uliodumu kwa takribani miaka 30 sasa. Ni mgogoro uliogharimu maisha ya Watanzania wengi kutoka katika jamii ya wafugaji waishio katika bonde la Loliondo. Mgogoro huo umechochewa na pande tatu zinazosigana ikiwa ni upande wa wawekezajli, serikali na wananchi wanaoishi katika eneo hilo.

Historia ya mgogoro wa Loliondo

Mheshimiwa Spika, Miaka ya 1980 mpaka 1993 Mfalme kutoka nchi za kiarabu alikuja Tanzania yeye na familia yake kwa shughuli za uwindaji wa wanyamapori. Mwaka 1992, walipokuja nchini walifanya uwindaji mkubwa zaidi ambao haukuwahi kutokea. Katika jarida la New York Times la tarehe 13 Novemba, 1993 liliandika kushtushwa na uwindaji huo wa kutisha wa wanyama kama Duma na Mbwa Mwitu ambao wapo katika hatari ya kutoweka. Vilevile gazeti la Mfanyakazi la tarehe 20, Januari 1993 lilichapishwa likiwa na kichwa cha habari "*Tanzania inavyoliwa na Waarabu*"

Mheshimiwa Spika, Mfalme na familia yake kupitia kampuni ya Otterlo Business Corporation Ltd (OBC) walipewa kibali cha uwindaji cha miaka kumi na aliyekuwa Waziri wa Utalii wa wakati huo Abubakar Mgumia kinyume na Sheria za wanyama pori namba 12 ya mwaka 1974, na Sheria ya Mashirika ya Umma namba 17 ya mwaka 1969 ambayo iliyataka makampuni binafsi walete wageni nchini kupitia shirika la Umma la wakati huo ambalo ni Tanzania Wildlife Corporation (TAWICO).

Mheshimiwa Spika, pamoja na masharti hayo ya kisheria, kampuni hii ilipewa mkataba wa kumiliki ardhi ya vijiji sita vilivyo ndani ya hifadhi ya Loliondo. Mkataba huo uliotiwa saini na Marehemu Richard Koillah Punye aliye kuwa Mbunge pamoja na aliye kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Abubakar Mgumia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa Mkataba huo uliwekwa saini kinyume cha Sheria kama nilivyo eleza.

Mheshimiwa Spika, Kitendo cha kampuni ya Otterlo kumilikishwa ardhi kilichochea kuongezeka kwa mgogoro kati ya kampuni hiyo na wananchi, ambapo wananchi wengi walichomewa maboma na walinzi wa kampuni hiyo mwaka 2000. Kufuatia hali hiyo vijiji vilivyoathirika na uchomoja wa makazi yao viliamua kuunda kamati ya wajumbe 13 waliotumwa kuonana na aliye kuwa Mheshimiwa Rais wa wakati huo Jijini Dar es Salam. Japokuwa hawakufanikila kuonana nae walikutana na mwandishi Jeneral Ulimwengu.

Mheshimiwa Spika, katika madai ya wanakijji hao walizungumzia ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu uliofanywa na mwekezaji huyo, uharibifu wa mazingira, ukiukwaji wa haki za wanyama na kujenga majengo makubwa ndani ya hifadhi na karibu kabisa na mto Olasai ambapo ni kinyume cha sheria za uhifadhi. Majengo hayo yaliyojengwa wakati huo mpaka sasa yapo na serikali haijachukua hatua yoyote pamoja na kujengwa kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo aliye kuwa Waziri wa Maaliasili na Utalii Bi. Zakiah Meghji alitoka hadharani na kuwapinga vikali wajumbe hao kupitia habari iliyochapishwa tarehe 11 April, 2000 kwenye gazeti la The Guardian.

Mheshimiwa Spika, Desemba, 2005 mwekezaji huyo aliongezewa vijiji vingine viwili na kufanya jumla ya idadi ya vijiji nane ambavyo alipewa kumiliki ardhi yake katika shughuli za uwindaji. Hii ni kwa mujibu wa barua namba DC/NGOR/C.15/5/120 ilioandikwa na aliye kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro ndugu Jowika Kasunga.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa mgogoro kati ya mwekezaji na wananchi ambao uligharimu maisha ya wananchi wengi na mifugo yao, mwaka 2009 aliyekuwa Mbunge wa Ngorongoro Ndugu Kaika Telele aliamua kuleta jambo hilo ndani ya Bunge (rejea hansard ya tarehe 11,Julai 2009). Pamoja na Mbunge huyo kuzungumzia sana mgogoro huo mpaka sasa hakuna suluhu iliyopatikana.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2010, aliyekuwa Spika wa Bunge, aliamuru kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuunda tume kwenda kuchunguza mgogoro huu wakati huo lakini pia haikuweza kuwa muarobaini wa mgogoro huu. Hata hivyo, aliyekuwa Waziri Mkuu wa wakati huo aliunda kamati ya Mawaziri sita akiwemo aliyekuwa Waziri wa Utalii kufuatilia suala hilo mnamo tarehe 08 Februari 2010, kwenye kikao cha ndani cha Chama cha Mapinduzi. Kamati ile nayo haikuzaa matunda na mpaka leo serikali hii ya awamu ya tano haijaweza kuwa muarobaini wa mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, ni hivi majuzi tu mwezi Februari 2017, Waziri Mkuu alimuagiza Mkuu wa Mkoa wa Arusha kufuatilia mgogoro huu ambao umedumu kwa muda mrefu. Timu hii ya Mkuu wa Mkoa imetumia mamilioni ya shilingi kama ilivyo kwa timu na Tume nyingine nyingi zilizopita katika kufuatilia mgogoro huu. Timu hii ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha iliwasilisha mapendeleko yake ambapo wakati huohuo Waziri wa Maliasili na Utalii tayari alikuwa amekwisha kufanya maamuzi juu ya mgogoro huu ambapo alitoa kauli ya kutenga eneo la kilometra za mraba 4,000 kwa ajili ya pori tengefu la Loliondo na kuamuru eneo la kilometra 2,500 zilizokuwa zimechukuliwa na wawekezaji zirejeshwe kwa wananchi ili kuendelea kulinda ikolojia ya Serengeti ambayo sasa ipo hatarini.Pia aliagiza TANAPA kuweka mipaka katika eneo hilo la hifadhi ili kuzuia mifugo inayoharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, suala la Mgogoro wa Loliondo ni suala la muda mrefu lililogubikwa na tuhuma mbalimbali za rushwa, usiri, utapeli, na ukitazama kwa undani jambo hili utagundua ujasusi mkubwa wa kiuchumi unaofanywa na

mataifa mengine dhidi ya taifa letu kuitia hifadhi zetu na hazina ya wanyama pori katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka majibu dhidi ya tuhuma zinazowakabili wawekezaji wa kigeni katika Bonde tengefu la Loliondo wanaojishughulisha na shughuli za uwindaji na utalii ambapo serikali zilizopita zimekuwa zikitofautiana kimtazamo juu la suala hili kama ifuatavyo;

- Jeshi la Wananchi wa Tanzania kutoa ulinzi katika kampuni binafsi ya uwindaji na utalii tofauti na ilivyo kwa makampuni mengine ya uwindaji na utalii nchini.
- Uwepo na majengo ya kudumu katika eneo la mapito ya wanyamapori kwenye bonde tengefu la Loliondo kinyume na sheria za uhifadhi.
- Uwepo wa lkulu ya mfalme katika mapito hayo ya wanyamapori.
- Uwindaji wa wanyama usiozingatia haki za wanyamapori
- Ukiukwaji wa sheria za uhifadhi wa wanyamapori.
- Ukiukwaji wa Sheria ya ugawaji wa vitalu vya uwindaj ndani ya Bonde hilo.
- Ukiukwaji wa sheria za mawasiliano ambapo kampuni ya OBC inayojinasibu kuwa mshirika wa Zantel bado inatoa huduma ya mawasiliano ya simu ya Etisalat ya United Arab Emirates kinyume na sheria za mawasiliano.
- Uwepo wa uwanja mkubwa wa ndege katika eneo la mapitio ya wanyamapori
- Ukiukwaji wa sheria za vijiji na ardhi za vijiji.

- Ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu ikiwemo mauaji, uchomaji wa maboma , vitisho kwa wanahabari wa mgogoro huu kutoka ndani na nje ya nchi
- Tumeshuhudia matamko mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi na hata yale ya watu binafsi.
- Tuhuma za rushwa kwa viongozi mbalimbali katika sekta ya utalii hasa wanaoshughulikia mgogoro huu.
- Tumeshuhudi matumizi ya fedha nyingi na rasilimali za nchi ambapo tume mbalimbali zinazogharimu mamilioni zimeundwa bila manufaa yoyote.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na suluhisho la kudumu kuhusu mgogoro wa Loliondo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kufanya yafuatayo;

o **Kwanza**, serikali kuja na kauli moja kuhusiana na mgogoro wa Loliondo badala ya matamko ya kisiasa yanayokinza na kauli za kubezana kwa watendaji wa serikali kama zile alizozitoa Mkuu wa Mkoa wa Arusha katika mukutano wa wanahabari wakati akitoa taarifa za utendaji wa serikali kwa robo mwaka. Mfano; kwa mujibu wa gazeti la mwananchi la tarehe 02, Februari lilitobeba kichwa cha habari **RC Gambo ampinga Waziri Magembe mgogoro wa Loliondo**, ni ushahidi tosha kuwa serikali haina malengo ya pamoja katika kutatua mgogoro kwani Mkuu wa Mkoa alisema tamko lilitolewa kuhusu kumaliza mgogoro huu ni "**maoni tu**". Tukumbuke kuwa tamko la Waziri ni suala linalohitaji utekelezaji na sio maoni kama alivyosema Mkuu huyu wa Mkoa.

o **Pili**, kwa kuwa Waziri aliahidi katika tamko lake kurudisha kwa wananchi eneo lenye ukubwa wa kilometra za mraba 2,500 kwa ajili ya wananchi na mifugo yao , Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa; ni vyema sasa eneo hilo likachimbwa mabwawa makubwa ya maji kwa ajili ya kusaidia mifugo na kupata maji ya

uhakika na pia kuepusha wanavijiji kurundikana karibu na maeneo ya mto na pia kulinda ikolojia ya eneo hilo lenye wanyama pori.

o **Tatu**, Serikali kutenga eneo lenye malisho litasaidia pia kuondoa tabia ya wanavijiji kwenda kwenye eneo la hifadhi ili pia kulinda mifugo dhidi ya magonjwa yatokanayo na wanyamapori kwani madhara yake ni makubwa kwa mifugo hiyo na pia ni hatari kwa afya za binadamu.

o **Nne**, serikali itoe majibu kwa tuhuma zinazoikabili kampuni ya OBC pamoja na serikali kama ilivyoelezwa kwenye historia ya mgogoro huu.

o **Tano**, serikali ifanye uchunguzi wa mifugo katika viijiji hivyo kwani kuna malalamiko kuwa nchi jirani pia inaingiza mifugo yake katika eneo hilo la Loliondo. Katika hili Waziri anazo taarifa za kutosha juu ya malalamiko ya wananchi kwa sababu alikumbana na malamiko hayo katika ziara yake fupi aliyoifanya tarehe 25 Januari, 2017 Loliondo.

2.3 UANZISHWAJI NA USIMAMIZI WA WILDLIFE MANAGEMENT AREAS (WMAs)

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo kubwa la ujangili ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa uwepo wa wanyamapori wa aina mbalimbali katika nchi yetu jambo ambalo pia kwa kiasi kikubwa umeathiri sekta ya utalii kwa ujumla. Ni wazi kuwa mtandao huu wa ujangili umefanywa na watu wenye uwezo mkubwa kiuchumi na pengine kwa kushirikiana na watu wenye madaraka kisiasa au katika vyombo vya dola. Katika kupambana na tatizo la Ujangili kulianzishwa kitu kinachoitwa Wildlife Management Areas (WMAs).

Mheshimiwa Spika, malengo makuu ya kuanzishwa kwa WMA ilikuwa ni;

Kushirikisha wigo mpana wa wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori (kukasimisha majukumu ya uhifadhi wa wanyamapori kwa wananchi)

Kuimarisha ulinzi wa wanyamapori nje ya maeneo rasmi ya uhifadhi (yaani hifadhi za taifa, mapori ya akiba n.k)

Wanavijiji kunufaika moja kwa moja na manufaa yatokanayo na matumizi endelevu ya wanyamapori

Mheshimiwa Spika, tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990, vijiji vingi vimejihuisha na utalii kwa kutoa maeneo kwa makampuni binafsi katika ardhi zao ili waweze kupata sehemu ya mapato yanayotokana na uwekezaji kwa ajili ya kusaidla shughuli za kijamii. Makubaliano hayo yalisimamiwa na mikataba ya kisheria ikihakikisha vijiji na hal mashauri za wilaya wanapata mapato kutokana na utalii wa wanyamapori. Makubaliano hayo yalifanyika kisheria chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (1982) na Sheria ya Ardhi ya Vijiji (1999).

Mheshimiwa Spika, WMAAs ni motisha kwa jamii ili kuendeleza wanyamapori na kulinda mazingira katika maeneo ya uhifadhi nchini. Motisha hii inaweza kuwa na tija pale tu wananchi wanapopata elimu ya uelewa kuhusu thamani ya wanyamapori katika kukuza uchumi na kuchangia maendeleo katika sekta mbalimbali za kijamii ili kuepusha au kumaliza matatizo ya ujangili katika maeneo yanayozunguka hifadhi yanayofanywa au kuweza kufanywa na baadhi ya watu wasio waaminifu na hata wageni wanaohujumu nchi yetu kwa kufanya matukio haya ya ujangili.

Mheshimiwa Spika, kushirikisha jamii katika mpango huu ni njia mbadala inayoruhusu ubunifu katika mipango ya kulinda na kudumisha shughuli za uhifadhi. Mfano, hivi karibuni vijiji katika Wilaya ya Simanjo wamekubali kutenga ardhi ya vijiji kwa hiari yao ili sasa shughuli za utalii ambazo

ni sehemu ya lkolojia ya Tarangire ziweze kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kujenga hoteli za kitalii na kusitisha shughuli za ufugaji na kilimo katika maeneo hayo ili pia kulinda mazalia ya nyumbu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uanzishwaji wa kisheria wa WMAs bado kanuni za uendeshwaji na mgawanyo wa mapato baina ya vijiji husika na Serikali kuu hazifuatwi ipasavyo. Jambo hili limekuwa likiibua migogoro ya mara kwa mara baina ya wanavijiji na TANAPA.

Mheshimiwa Spika, WMA zimekuwa na changamoto kubwa hasa katika mfumo wa utozaji kodi na magawanyo wa mapato. Hii ni kutokana na serikali kuchukua kiasi kikubwa cha fedha kinachotokana na mapato ya utalii kwenye WMA na hivyo kushindwa kutekeleza shughuli za ulinzi wa wanyamapori, kushindwa kufanya shughuli za kuwaletaa wanavijiji maendeleo n.k

Mheshimiwa Spika, serikali inachukua 55% ya mapato yatokanayo na uwindaji na kuiachia WMA 45%. Vijiji vingi vinategemea mapato ya uwindaji kuliko utalii wa picha. Pamoja na hilo, serikali imekuwa ikikusanya mapato yote ya utalii (yaani mapato ghafi) ambapo mapato hayo hupelekwa kwenye mamlaka ya TAWA yenye akaunti BOT na fedha hizo huombwa tena kupelekwa kwenye WMA husika. Hii imechelewesha fedha kufika kwenye WMA hizi na fedha hizo hazifiki kwa ufasaha. Mfano; Kambi Rasmi ya Upinzani ya imepata taarifa kuwa WMA ya Burunge-Babati hukusanya takribani shilingi bilioni 6 lakini iliyorudi kwenye WMA ni milioni 800 tu kiasi kwamba maendeleo ya WMA hii yanakuwa ya kusuasua kwa kuwa wananchi hawanufaiki kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kubwa inayotokana na single entry. Hii ni sera ya TANAPA (TANAPA'' single entry policy) ambayo ni kinyume na malengo ya sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998. Single entry policy imesababisha wageni kupungua kwenye WMA ya Ikona na

nyingine nyingi. Wageni wengi hukwepa kulipa tozo hizi kwa sababu hazina tija.Utaratibu huu umedidimiza maendeleo ya WMA.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa serikali haijatia saini kanuni za uendeshaji wa WMA zilizofanyiwa mapitio mwaka 2012. Mpaka sasa serikali haijatoa sababu zozote ni kwa nini kanuni hizo hazijatiwa saini mpaka leo Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri yafuatayo:

1. Kupunguza masharti ya uanzishaji WMA kwa jamii

2. Kuwe na ufanuzi na utaratibu wa ugawanaji mafao katika WMA, ili kuhakikisha kuwa asilimia 70% ya mapato kutoka WMA inabaki ngazi ya vijiji kama illivoanishwa kwenye kanuni.

3. Kuhakikisha kuwa serikali za vijiji zinapewa maamuzi ya kisheria kulingana na uwekezaji katika WMA, ikiwa ni pamoja na kuamua ni kampuni zipo zifanye shughuli za kitalii katika maeneo yao na serikali ibaki na usimamizi wa jumla na maelekezo ya kisera tu.

4. Maeneo ya WMA yaoanishwe na maeneo ya ardhi ya misitu ya vijiji ili jamii wapate manufaa ya juu kutokana na maliasili katika ardhi za vijiji.

5. WMA zilipwe fedha zake moja kwa moja kutoka kwa wawekezaji ili WMA hizi ziweze kulipa mgao wa mapato kwa Serikali Kuu na Halmashauri za Wilaya.

6. Kusimamisha utaratibu wa single entry na tathimini ya athari zake ifanyike

7. Serikali iharakishe kutia (Under certificate of urgency) saini kanuni zilizofanyiwa mapitio kama sehemu ya makubaliano kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na wadau wa uhifadhi yaliyofanyika tarehe 2-3 Julai mwaka 2015.

8. WMA ziweze kujengewa uwezo ili kuweza kuijendesha vizuri

9. Mtazamo wa kisera unahitajika na elimu kwa wananchi kuhusiana na malengo ya WMA's.

10. Kumthibitisha Mkurugenzi wa WMA's ambae amekaimishwa nafasi hiyo kwa takribani miaka miwili sasa ili kuongeza ufanisi katika utendaji.

2.4 MIGOGORO BAINA YA VIJIJI NA HIFADHI ZA WANYAMAPORI

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro mingi na ya muda mrefu baina ya vijiji na mamlaka za hifadhi. Migogoro hii imekwenda mbali zaidi na katika maeneo mengine kusababisha vifo na familia nydingi kuathirika vibaya kutokana na operesheni za kamata kamata kwa wananchi katika maeneo ambayo yanapakana na hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Katika Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Mbarali ambapo kumekuwa na mgogoro uliodumu kwa takribani miaka nane baada ya serikali kuamua kuongeza eneo la hifadhi kwa kuingia kwenye vijiji 21 ambavyo hutumiwa na wananchi kwa ajili kujipatia chakula na shughuli zingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 serikali ilitoa maagizo kuwa wataalamu wa maliasili na wataalamu wa ardhi wapitimia mapendekezo ya wananchi ambayo kimsingi yalikuwa yanaelekeza ni wapi hasa serikali iweke mipaka kwa makubaliano na wananchi. Hata baada ya hatua hiyo, hivi karibuni limetokea jambo la ajabu ambapo serikali imeanza kuweka kwa siri mipaka ya hifadhi bila kuwashirikisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa maeneo hayo wameishi katika eneo hilo kwa miaka mingi kabla ya ukoloni kuwepo katika nchini yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini

kuwa wananchi hawa sio wavamizi kama inavyoweza kuelezwa na serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa kwa sasa wananchi wa vijiji hivi wamekataliwa kuendeleza miundombinu katika eneo hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa wananchi hawa ni wazalishaji wazuri wa chakula, lakini pamoja na hilo hivi karibuni maombi yao ya kutumia *pamp* kwa ajili ya shughuli za kilimo yamesitishwa jambo ambalo limesababisha hasara kubwa sana kwa wakulima kutokana na fedha nyingi walizozitumia katika ujenzi wa miundombinu ya mashamba yao kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa wakati wa kampeni wa uchaguzi mkuu uliopita Rais alipokwenda Mbarali alitoa ahadi kwa wananchi ya kujenga barabara ya Mbarali kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa mazao yao kwenda viwandani.

Mhehimiwa Spika, pamoja na wananchi wa maeneo hayo kupongezwa kwa kilimo kizuri tena Kilichozingatia utunzaji wa mazingira leo hii wanaondolewa katika maeneo yao kwa sababu ya upanuzi wa hifadhi wakati ambapo miaka iliyopita walishawahi tena kusogezwa kwa sababu ya upanuzi wa hifadhi hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuja na majibu kuhusiana na mgogoro huu wa wananchi na hifadhi ambapo wananchi wamekuwa wakiishi katika maeneo yao kwa muda mrefu. Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kutoa sababu za kwa nini Wizara inapingana na ahadi ya Rais ya kuwasaidia wananchi wa Mbarali ambao hutegemea kilimo ili kuwasaidia katika usambazaji wa mazao yao ya chakula nchini ikizingatia kuwa kutokana na shughuli hizo wameweza kutoa ajira zaidi ya 30,000 na wanachangia uwepo wa viwanda vikubwa 42 na magodown makubwa zaidi ya 56.

3.0 MALIASILI NA UTALII

3.1 ATHARI ZA ONGEZEO LA KODI KATIKA SEKTA YA UTALII NCHINI

Mheshimiwa Spika, suala la mrundikano wa kodi kwa wafanyabiashara katika sekta ya utalii sio suala geni. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikilizungumzia jambo hili mara kwa mara kutokana na jinsi linavyowaumiza wadau wa sekta ya utalii nchini pamoja na wananchi wengine wanaotegemea shughuli za utalii kujipatia riziki.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Kambi ya Rasmi Upinzani wakati wa mkuatano wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilizungumzia suala la ongezeo la kodi ya VAT na ikionyesha madhara makubwa yanayoweza kujitokeza endapo serikali itapandisha kodi hii kwa ghafla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchambuzi huo uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, serikali iliamuru wafanyabiashara hao kulipa kodi hiyo mara moja na jambo ambalo limewasababishia wafanyabiashara hasara kubwa. Kutokana na kuyumba kwa biashara ya utalii nchini na pia ongezeko kubwa la kodi; wafanyabiashara hao walilazimika kupunguza wafanyakazi na hivyo serikali ilikosa kodi ya mapato inayotokana na mishahara ya wafanyakazi (PAYE). Aidha, baadhi ya wamiliki wa makampuni na hoteli wamelazimika kuza hoteli na makampuni yao na kusababisha usumbufu kwa wageni kwani wengi walilazimika kuchangia ongezeko hilo la kodi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo kuna takribani zaidi kodi 36 ambazo wafanyabiashara wa utalii nchini wanalazimika kulipa wafanyabiashara wa utalii nchini. Kodi hizo ni kama ifuatavyo;

1. TALA License
2. EWURA tax 1% charged by TANESCO from October 2009
3. REA tax 3% charged by TANESCO from October 2009

4. VAT
5. Corporation Tax
6. Withholding Tax
7. Stamp duty
8. Occupational and Safety Health Authority compliance certificate (OSHA)
9. Park fees to tourists
10. Crew Park entry fee-Mountain climbing
11. Guides licence
12. Annual vehicle road license fees
13. Safety week stickers
14. Land rent
15. Property tax
16. NSSF
17. Skills and Development Levy
18. Municipal Service Levy (Kodi ya huduma 0.3% ya pato)
19. Bedding levy hotels
20. Concession Levy-hotels
21. Registration of vehicles
22. Import duty
23. Local Community fees
24. Bar license- hotel
25. Camping fees to TANAPA
26. Ngorongoro Crater service fees
27. Rescue fees -Mountain climbing
28. Excise duty of 0.15% charged by banks on payments
29. Tourism development levy introduced from October 2013
30. Business License fees paid to Ministry of Industry and trade
31. Residence permit fees
32. Radio license fees paid to TCC
33. Wildlife management fees
34. SUMATRA fees paid to surface and Marine Transport Regulatory Authority
35. Workman's compensation fund
36. Forest fees

Mheshimiwa Spika, hizi ni baadhi tu ya kodi katika sekta ya utalii nchini Tanzania. Mrundikano huu wa kodi hasa

kwa wafanyabishara wazawa ni taswira tosha kwa wananchi wetu kujua namna serikali ya awamu ya tano ya Chama cha Mapinduzi inavyowakamua.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa gazeti la mwananchi la tarehe 04 Februari, 2016 katika makala ya uchumi yenye kichwa cha habari kuwa "**Wingi wa kodi unavyoua utalii Tanzania**" limeleeza kwa kina utafiti uliofanywa na Dr. Hawa Eve Sinare unaoonyesha ili mfanyabiashara wa utalii Tanzania aweze kulipa kodi, kutimiza masharti ya leseni na malipo mengine inamlazimu kutumia takibani masaa 2,000 kwa mwaka. Hii ni kutokana na wingi wa masharti kwa wafanyabiashara wa ndani na nje katika sekta ya utalii ikilinganishwa na sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, Kwa sasa Tanzania ina takribani kampuni 1,050 zinazofanya blashtara ya utalii lakini ni kampuni 300 tu ndio zilizoweza kutimiza masharti ya kulipa kodi kutokana na wingi wa kodi na mfumo mzima wa ulipaji kodi. Ni jambo la ajabu kabisa kwani ni rahisi zaidi kulipa faini kwa kosa la kufanya biashara kinyume na sheria kuliko kutekeleza masharti ya ulipaji kodi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuziangalia upya kodi zinazowaumiza wafanyabiashara ya utalii nchini, lakini pia serikali haina budi kuanzisha 'one stop centre' kwa ajili ya malipo ya kodi katika sekta ya utalii kwani kumekuwa na usumbufu katika ulipaji. Vilevile serikali iondoe mkanganyiko katika udhibiti na usajili unaojirudia rudia bila sababu kutoka kampuni za usajili nchini. Hii ni kwa sababu katika kodi 36 zinazolipwa kodi 12 ni za usajili na leseni pekee.

3.2 KUANZISHA BUSTANI YA WANYAMA KATIKA MSITU WA PANDE

Mheshimiwa Spika, Pori la akiba lijulikanalo kama Msitu wa Pande limekuwa ni msitu wenyewe historia ya kipekee na ya kutisha sana. Msitu huu uliopo takribani kilometra 25 kutokea Jiji Dar es Salaam kuelekea Bagamoyo ni msitu

wenye wanyama wadogo wadogo na mimea ya kipekee ambayo haipatikani katika maeneo mengine yoyote.

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA SPIKAJ]

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 ndani ya Bunge hili Mheshimiwa John Mnyika aliwahi kuuliza swali la nyongeza kuhusiana na ahadi ya serikali katika kuuendeleza msitu ili uwe sehemu ya utalii kama sehemu ya matumizi bora ya misitu ambapo ahadi hii ya kuufanya msitu huu kuwa sehemu ya utalii ni ahadi ya serikali ya muda mrefu na serikali ilishawahi kutangaza zabuni ambayo mpaka leo haijulikani ni nini kilichoendelea.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kama ifuatavyo: “ *nimpongeze Mheshimiwa Mnyika kwa mtanzamo chanya wa kwamba anakubaliana na dhana nzima ya matumizi bora ya maeneo ya misitu;hapingani na dhana nzima ya serikali kuhusiana na kufanya misitu iwe ni rasilimali ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya maslahi ya jamii;kuhusu suala la kwamba kuna ucheleweshaji kama ambavyo amesema;nataka nimtoe wasiwasi kwamba historia inatukumbusha tulipotoka,mahali tulipo na inatuwezesha kuona kule ambako tunakwenda.Nataka Mheshimiwa Mnyika akubaliane tu na rai yangu kwamba tumetoka huko tulikotoka,mipango imekuwepo lakini awamu hii mipango hii ninayoizungumzia ni uhakika na kwamba awamu hii nataka anipe muda wa mwaka mmoja tu,halafu aweze kuona katika eneo hili tunafanya nini*”.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo yaliyokuwa majibu ya serikali mwaka 2015, japo jambo hili limezungumziwa muda mrefu hata kabla ya mwaka 2015. Hii inaonyesha kwamba serikali ya Tanzania inazungumza na kutoa ahadi lakini haitekelezi inayoyazungumza. (*The government of Tanzania talks the talk but it doesn't walk the walk*). Kutokana na tabia ya serikali kutoa majibu mepesi yasiyo na utekelezaji, mpaka

leo hakuna jitihada zozote zilizofanyika ili kuhakikisha utekelezaji wa ahadi ya serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kutoa mfano wa Nchi ya Kenya ambapo katika jiji la Nairobi kuna Msitu wa Karura (Karura forest) ambao umekuwa ni kivutio kwa wakazi wa Nairobi na wageni wanaotembelea nchi hiyo. Msitu wa Karura umekuwa ukichangia uhamasishaji na utangazaji wa shughuli za utalii nchini Kenya.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali ya CCM kujisahihisha katika hili, kwani nchi haijengwi kwa maneno bali matendo. Ifike mahali sasa majibu na ahadi za serikali ziweze kutekeleza kwani tabia ya serikali kushindwa kutekeleza ahadi kunazidi kuchelewesha maendeleo ya taifa hili. Ni muhimu sasa serikali ikawa na wivu wa kimaendeleo kwa taifa lake na watu wake. Kambi Rasmi ya Upinzani inatamani kuona kila kiongozi wa serikali akijikita kwa dhati katika kutatua changamoto za kimaendeleo na sio kujikita katika siasa pekee..

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kushauri kuwa ni wakati mwafaka sasa serikali kuanzisha bustani ya wanyama katika Msitu wa Pande na hivyo kuwa sehemu ya utalii kwa wananchi wa Mkao wa Dar es Salaam pamoja na watalii wengine wanaotembelea nchi yetu. Bustani hii inaweza kuwa sehemu ya wananchi kuwa na maeneo ya kupumzika mwishoni mwaka au wiki na hivyo kuliongezea taifa mapato.

3.3 RUAHA NATIONAL PARK

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya wanyama ya Ruaha ni hifadhi yenye historia kubwa na ilianza kutambulika zaidi mwanzoni mwa mwaka 1877 pale ambapo iliingia rasmi katika machapisho mbalimbali. Hifadhi hii inauwanda mzuri sana wenye wanyama wengi.Ni moja ya hifadhi kubwa zaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki

Mheshimiwa Spika, bado serikali haijaitangaza hifadhi hii muhimu kwa ukanda wa kusini (Southern circuit). Idadi ya watalii wanaofika katika ukanda huu wa kusini ni wachache na hiyo yote inasabishwa na kukosekana kwa matangazo ya kutosha ili kuvutia watalii wengi kutembelea hifadhi hii.

Mheshimiwa Spika, bodi ya utalii nchini (TTB) iko taabani kutokana na wingi wa madeni inayoikabili na pia bajeti yake ni ndogo sana jambo linaloipelekea TANAPA na NCAA kuchangia gharama za maonyesho mbalimbali ndani na nje ya nchi. Iwapo TTB inashindwa kujiendesha tunategemea vivutio hivi vitawea vipi kutangazwa?

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kuzunguka hifadhi ya Ruaha hayana hoteli nyingi zenyet hadhi za kimataifa. Mpaka sasa kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wafanyabiashara na wadau wa utalii kwani kuna hoteli inayotegemewa katika eneo hilo ambayo hutoza gharama kubwa sana jambo ambalo wageni wengi hushindwa kutembelea eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na hilo usafiri mkubwa unaotegemewa ni wa ndege ndogo ambapo gharama yake ni kubwa. Kwa kuwa serikali imeshindwa kuendeleza eneo hili la hifadhi ili wageni waweze kutembelea kwa wingi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutengeneza barabara ili wageni wanaotembelea eneo hilo waweze kutumia usafiri wa barabara. Mheshimiwa Spika, Endapo barabara hii itatengenezwa basi wageni wanaotembelea hifadhi hii wanaweza kutembelea mpaka mbuga ya Mikumi kwa urahisi zaidi baada ya kuboresha miundombinu ya barabara ya hifadhi hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasitiza kuwa serikali ipunguze msusuru wa kodi kwa wafanyabiashara katika sekta hii ili sasa makampuni binafsi yaweze kuwekeza katika eneo la hifadhi ya Ruaha na hifadhi nyingine zilizopo Southern circuit ikiwa ni pamoja na kujenga hotel zenyet hadhi ikiwa ni pamoja na lodge na camp site.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuandaa mpango mahususi wa kuwaalika wawekezaji **kwa vitendo** kutoka ndani na nje ya nchi ili sasa waweze kuzungumzia namna bora ya kuwekeza katika ukanda huo,lakini pia serikali iweze kuisaidia TTB ili itangaze vivutio hivi zaidi.

3.4 SERIKALI KUSHINDWA KUVUMBUA VIVUTIO VIPYA VYA UTALII

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi sasa serikali yetu imekuwa ikitegemea mbuga za wanyama, milima, bahari, uchongaji wa vinyago na kutembelea mali kale kama sehemu kuu za utalii katika nchi yetu. Serikali imejifunga katika vivutio hivyo nilivyoreje japo kuna utalii wa aina nyingine mwangi ambao unaweza kuongeza pato la nchi na kuwaaletea wananchi maendeleo binafsi na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kati ya nchi zilizofanikiwa sana katika utalii ni pamoja na nchi za Uingereza, Ujeruman, Uturuki, Italia, China, Hispania, Marekani na Ufaransa. Mfano, kwa mujibu wa habari mbalimbali zinazopatikana katika tovuti mbalimbali za utalii zinabainisha kuwa katika nchi ya Ufaransa takribani watalii milioni 83.7 walitembelea nchi hiyo kwa mwaka 2014 pekee. Ufaransa ni nchi inayotegemea sana jengo la mnara wa Eifel (Eifel tower), Kasri la mfalme (Palace of Versailles) n.k Nchi hii inategemea sana maeneo ya kihistoria katika taifa la Ufaransa. Hii ikiwa ni majengo ya kale, sanamu za kumbukumbu, makumbusho na sehemu za mito na fukwe.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yanaipatia ufaransa fedha nyingi za kigeni na yanachangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa la Ufaransa. Hapa kwetu Tanzania mambo ni yaleyale (business as usual). Tumeshindwa kutengeneza akili mpya za kufanya tafiti kwa kina kwenye vivutio vipya pamoja na kuongeza bajeti ya maendeleo ili tafiti ziweze kufanyika ipasavyo. Kutokana na sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeona ni wakati muafaka sasa wa kupendekeza mambo mapya na vivutio vipya vya utalii ili kuweza kuisaidia serikali.

Mheshimiwa Spika, miaka ya hivi karibuni kumekuwa na kauli mbalimbali za kutaka kujua katikati mwa Tanzania ni wapi ili kuweka alama itakayotumika kama sehemu ya kihistoria na sehemu ya utalii wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika vyanzo mbalimbali vya habari vinaonyesha kuwa katikati mwa Tanzania ni kijiji cha Sukamahela kilichopo kata ya Solya wilayani Manyoni mkoani Singida. Hii ni kutohana na uwepo wa chuma kilichopo kijijini hapo kinachosadikiwa kuwa ndipo eneo rasmi la katikati ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa hizo za Kijiji cha Sukamahela, vyanzo vingine vinaonyesha kuwa kitongoji cha Darajani kijiji cha Chisinjisa kata ya Sasilo, tarafa ya Nkonk'o Wilaya ya Manyoni ndipo eneo la katikati mwa Tanzania. Katika makala ya gezeti la Mwananchi la tarehe 25, Januari 2015 lilieleza kwa kina aina ya vipimo mbalimbali viliviyotumiwa na serikali ya Ujerumani wakati wa ukoloni na vipimo vipyta vilivyofanywa na serikali ya Tanzania chini ya mpima ardhi mkoani Singida.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua jithada mbalimbali zilizofanywa na waandishi wa habari na wadau wengine kutaka kujua ni wapi hasa eneo la kitovu cha Tanzania lilipo ili sasa waweze kusaidiana na serikali katika kutengeneza eneo hilo kuwa sehemu nzuri ya kihistoria na utalii badala ya ilivyo sasa kwani maeneo haya hayajatambuliwa rasmi na serikali.

Mheshimiwa Spika, Tukumbuke kuwa Mwalimu Nyerere aliwahi kujenga nyumba katika eneo la Sukamahhela ili kuwasaidia Wazee waliokosa makazi na kwa sasa hali ya makazi hayo sio nzuri hivyo wengi hulazimika kukaa kando kando ya barabara kwa ajili ya kuomba riziki kutoka kwa abiria na wasamaria wema wanaopita maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo mkoani Kilimanjaro katika Wilaya ya Same kuna Mlima ya Shengena ambaao ni maarufu kwa ufugaji wa ngo'mbe wa asili ambaao

huitwa kwa miluzi na wanajichunga wenyewe, kuna uwanda mzuri kwa ajili ya watalii kufanya camping, kuna ziwa Kenyabasa kule Mkoani Kagera ambalo ni ziwa la maajabu kutoka kwenye chungu,tuna kimondo cha Mbozi,maajabu ya mto Kiwira ambapo mto huingia ndani ya shimo dogo la miamba, maji moto (hot springs katika kijiji cha chemka wilaya ya Hai , hotsprings za Mkoani Mbeya, kuna udongo unaohama (shifting sand dunes) mkoani Manyara ambapo eneo hili halijatangazwa ipasavyo, makumbusho ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere mkoani Mara, maporomoko ya maji ya mto Rusumo, muonekano mzuri wa Ziwa Chala, tuna milima ya Kolero yenye historia na maajabu yake na mti wa maajabu ulioishi miaka zaidi ya 500 katika Wilaya ya Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuwa na wataalamu wa kufanya tafiti kwenye vivutio vipyta vya utalii nchini. Kitendo cha serikali kuendelea kukumbatia vituo vilevile ambavyo matokeo yake ni yaleyale ni kitendo cha kuendelea kuididimiza sekta ya utalii nchini. Bajeti inayotengwa na serikali ni lazima iweke kipaumbe katika kufanya tafiti ili kuwepo na vivutio vyenye tija ambavyo vitafikika kwa urahisi na vitaweza kuwavutia watalii wengi.

3.5 VAZI LA TAIFA NA MANUFAA YAKE KATIKA SEKTA YA UTALII

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa Tanzania imekuwa na mchakato usiokamilika wa kutafuta vazi la taifa. Jambo hili la muda mrefu limeshindwa kukamilika kutokana na kuwepo kwa siasa na ukinzani usio na tija katika kutafuta vazi litakalotuunganisha kama taifa moja. Tangu Mwezi Desemba, 2011 aliyekuwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo aliunda kamati maalum ya kutafuta vazi la taifa ambalo kamati nyingi zimeundwa baada ya hapo.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuzuka kwa maswali mengi katika mchakato huu wapo wananchi wengi

wanaojuiliza kwamba ikiwa serikali imeshindwa kupata vazi la taifa, huku wadau wa mitindo ya mavazi nchini wakifanya vizuri katika medani za ndani na nje ya nchi, Je, serikali inatuhakikishia vipi kuwa inauwezo wa kutoa kwa utoshelevu bajeti iliyotengwa katika Wizara hii?

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani zimeweza kujitambulisha vyema kutokana na mavazi yao. Nchi kama Rwanda ina vazi lake la asili lijulikanalo kama Mshana na nchi kama Uganda ina vazi lake lijulikanalo kama Gomesi au Busuuti n.k Hata baadhi ya nchi katika mataifa ya Ulaya, Asia, na kwengineko nao wanamavazi yao yanayotambulisha utaifa wao na yamekuwa sehemu ya kivutio kikubwa kwa watalii.

Mheshimiwa Spika, ni rahisi sana kwa taifa kuiga mambo mengi kutoka kwenye mataifa mengine lakini kamwe hakuna taifa linaloweza kuiga utambulisho na utamaduni wa mataifa mengine. *Kushindwa Kwa taifa kuwa na utambulisho wake Kwa kupitia watu wake, ni utajiri wa umaskini.*

Mheshimiwa Spika, Mchakato wa kupata vazi la taifa kama utambulisho na sehemu muhimu ya utamaduni hauwezi kufikia hitimisho kwa kupelekwa kwa wananchi kama ilivyoelezwa na Wizara ya Utamaduni na Michezo katika hitimisho la hoja ya Bajeti ya Wizara hiyo na kuachwa bila usimamizi maalumu na hamasa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuangalia upya mchakato huu, ifanye tathimini ya kina kuona ni kwa namna gani kuwepo kwa vazi la kitaifa kutaleta manufaa kwa nchi hususani katika sekta ya utalii nchini. Katika kulingalia hili serikali iwe na mpango wa hamasa na elimu kwa wananchi kuona umuhimu wa kuwa na vazi hilo kuliko ilivyo sasa ambapo serikali imejitoa katika suala hilo na kuwaachia wananchi wenyewe wakati imetumia fedha nyingi kuunda kamati kwa ajili ya suala hilo.

3.6 USHIRIKISHWAJI WA DIASPORA KATIKA KUTANGAZA UTALII

Mheshimiwa Spika, biashara yoyote inahitaji matangazo ili iweze kufanya vizuri zaidi. Katika kufanya matangazo hayo mbinu mbalimbali zinaweza kutumika. Kwa hapa nchini Bodi ya Utangazaji wa vivutio vya utalii nchini imekuwa ikikumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo changamoto za kifedha katika kufanya maonyesho mbalimbali, kutoa machapisho na matangazo kwa njia ya kieletroniki.

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa ni wakati sasa wa kuwa na kitengo cha utalii cha Diaspora ambacho kitafanya kazi ya kutangaza vivutio vyetu ikiwemo vivutio vipyta ambavyo vitatambuliwa. Pamoja na hilo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa ni wakati sasa wa kuhamashisha Diaspora investment kwenye sekta ya utalii. Hii ni pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kuweza kuwekeza zaidi kwenye sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hili Diaspora tourism na uhamasishwaji wa sekta binafsi hautawenza kuwa na mafanikio endapo serikali haitachukua hatua za makusudi katika kupunguza kero zilizopo kwa wafanyabiashara katika sekta utalii ikiwemo wingi na ugumu wa masharti katika kuanzisha na kuendesha biashara ya utalii nchini pamoja na orodha ndefu ya kodi katika sekta hii.

4.0 WANYAMA PORI

4.1 TATHIMINI YA UDHIBITI WA BIASHARA YA PEMBE ZA NDOVU

Mheshimiwa Spika, serikali, mashirika ya umma, sekta binafsi na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa zimekuwa zikipinga sana ujangili dhidi ya Ndovu unayofanywa na watu wasiolitakia mema taifa letu. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazoendelea kufanya bado mpaka sasa ujangili dhidi ya Ndovu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sensa iliyofanywa na Taasisi ya utafiti wa wanyamapori Tanzania (TAWIRI) kuwa Mwaka 1979 idadi ya Ndovu ilikuwa takribani Ndovu 316,300, mwaka 2006 idadi ya Ndovu ilikuwa 136,753, mwaka 2009 idadi izidi sana kupungua mpaka Ndovu 109,051 na mwaka 2015 imepungua zaidi ya asilimia 60 na kufikia idadi ya Ndovu 50,443.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la kusikitisha sana. Serikali imeshindwa kulinda rasilimali za nchi hii kwa vivu wa hali ya juu kiasi kwamba tangu mwaka 1979 serikali imeshindwa kabisa kuzuia biashara hii haramu japo kuna matamko mengi jambo ambalo linazua maswali mengi kuwa ni akina nani hasa wanufaika wa biashara hii haramu?.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, mwaka 2014, Tanzania illitia salni mpango wa kuwalinda Ndovu (Elephant Protection Initiative).Mpango huu ulizua uuzaji wa pembe za Ndovu kwa muda wa miaka kumi. Pamoja na hilo Tanzania kuna ghalaa ya meno ya Ndovu/Tembo yenye uzito wa tani laki moja na kumi na nane kwa mujibu wa BBC News 2014.

Mheshimiwa Spika, ghalaa hili linagharimu takribani dola 75,000 kwa mwaka sawa na shilingi 167,925,439.19 kwa exchange rate ya shilingi 2,239.01 ya tarehe 20, May 2017 lakini pamoja na hilo pendekazo la Tanzania kwa CITES mwaka 2009, serikali ilisema kuwa ghalaa la kuhifadhi meno hayo ya tembo limejaa na hivyo serikali itahitaji dola milioni moja kujenga lingine ambayo ni sawa na kiasi cha shilingi 2,239,005,855.82

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kufanya yafuatayo:

Kuzuia kabisa biashara ya meno ya tembo na sio kusitisha kwa kipindi cha miaka kumi pekee. Serikali itambue kusitisha biashara hiyo pengine ni kuwapumzisha tu majangili.Inachukuwa takribani miezi 22 kwa tembo mmoja kuzaa lakini ni kitendo cha dakika tu kumuua tembo mmoja.

· Mpaka sasa ghala linalotumika kuhifadhi meno ya tembo halina utaratibu mzuri wa kuhifadhi pembe zilizokamatwa. Na hivyo ni rahisi biashara hii kuendelea kufanyika kwa kutumia pembe zilizo ndani ya ghala hilo kwa nia haramu. Hii ni kutokana na uhifadhi wa hovyo unaofanyika ndani ya ghala hilo. Pembe hizi hazina alama maalumu na za kisasa ili kuweza kuzifuatilia kitakwimu na kwa makundi yao ya sifa za kisayansi.

· Mpaka sasa ghala hili linagharimu fedha nyingi sana huku wananchi wakiwa hawana huduma muhimu kama chakula, maji, nishati n.k. Fedha hizi pia zingeweza kabisa kutumika katika kuweka mazingira ya kudhibiti ujangili nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji ni kwa nini sasa serikali isiweze kuziteketeza pembe hizi kama walivyofanya Kenya, China n.k kwani kuyapeleka sokoni ni kutoa motisha kwa majangili kuendelea kujipenyeza katika biashara hii.

· Serikali ituambie mpaka mwaka huu wa 2017 kuna tani ngapi za pembe za Ndovu zilizo katika ghala hilo kwani takwimu nyingi zinaonyesha kiwango cha pembe hizi mpaka mwaka 2014 pekee.

4.2 SEKTA YA WANYAMAPORI NA BIASHARA YA UWINDAJI NCHINI

Mheshimiwa Spika, Wanyamapor ni rasilimali endelevu kwa Tanzania ukilinganisha na rasilimali zingine kama madini na mafuta. Jambo la muhimu katika sekta hii ni kuwa na sera pamoja na matendo yenye usimamizi endelevu wa wanyamapor na hivyo shughuli za kiuchumi zinazotokana na wanyamapor zitaendelea kukua na kupanuka kwa miongo mingi ijayo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na bahati hiyo ya kuwa na wanyama wengi, Tanzania ina Mtando mkubwa wa maeneo yaliyohifadhiwa yaani (Protected Areas) ambayo huchukua takribani asilimia 28 ya ardhi yote ya Tanzania. Kati ya asilimia hiyo, asilimia 4 ni hifadhi za Taifa (National parks),

asilimia 1 ni Hifadhi ya Ngorongoro (NCA), asilimia 15 ni Mapori ya Akiba (GRs) na asilimia 8 ni Mapori Tengefu (GCAs). Aidha, hifadhi za misitu takribani 150 huchukua asilimia 15 ya ardhi yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, dhana halisi ya uwindaji wa kitalii ina maana ya matumizi endelevu ya wanyamapori ambayo yana faida kiuchumi. Hii inajumuisha uchumi endelevu unaoendana na sera ya utalii kuhusu uwindaji kwa kiwango kidogo lakini chenye tija na kinachoweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wa taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hali halisi ilivyo sasa maeneo mengi ambayo uwindaji umekuwa ukifanyika kumekuwepo na kuripotiwa madhara makubwa kuliko faida. Hii ni kutokana na wanyama wengi kuuawa bila kuzingatia sheria, kuuawa kwa wanyama wadogo, kupotezwa kwa baadhi ya viumbe kwa njia za kibailolojia bila hata serikali kutambua na hii imetokea katika mataifa mengi duniani kwa sababu za kiuchumi na kisiasa (economic and political conspiracy).

Mheshimiwa Spika, ukiukwaji huu mkubwa wa sheria za uwindaji umefanyika sana hapa nchini na katika kumbukumbu Kambi Rasmi ya Upinzani iliyahi kuzizungumzia sana Kampuni za Uwindaji za Green Miles na OBC zilizokumbwa na baadhi ya shutuma hizi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa mpaka sasa wanyama kama DUMA (Cheetah), Faru, Tembo, Mbwa mwitu n.k wanaendelea kutoweka katika hifadhi zetu jambo linaloilazimu serikali kuagiza wanyama kutoka nje ya nchi kama vile Faru ili kusaidia uzalishaji wa wanyama hawa jambo ambalo linaigharimu serikali fedha nyingi kutokana na uzembe tu wa serikali kushindwa kulinda rasilimali zake, kuwakumbatia watendaji waovu na wabinafsi wanaotazama maslahi yao binafsi kuliko maslahi ya taifa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mifano ni gharama kubwa iliyotumika kumnunua Faru John na shilingi milioni 64 ambazo hutumika kila mwezi kumtunza Faru Fausta ambae haingizi pato lolote kwa sasa na jambo hili ni matumizi mabay ya fedha za umma na kukosa vipaumbele kama taifa .Tukumbuke fedha hizi zinatumika wakati mamilioni ya wananchi wa Tanzania hawana huduma za afya, uhakika wa upatikanaji wa chakula, kukosa shule zenyenye ubora na wanakabiliwa na shida kubwa ya maji, nishati ya umeme, bei ghali za bidhaa ikiwemo sukari na unga pamoja na matatizo mengine lukuki.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tuhuma za rushwa kwa wanaojishughulisha na biashara hii ili kupata vitalu vya uwindaji kwa muda mrefu. Katika mtandao wa Jamhuri ya tarehe 23 Mwezi August, 2012 ilizungumzia jambo hili kwa kina sana.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa katika utekelezaji wa Sheria Namba 5 ya mwaka 2009 inaelekeza kwamba kampuni za kigeni zisizidi asilimia 15 ya kampuni zote zinazogawiwa vitalu. Lakini mpaka sasa takribani asilimia kubwa ya kampuni zilizogawiwa vitalu zinamilikiwa na wageni.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa biashara ya uwindaji inayohusisha kusafirisha wanyama pori wakiwa hai ilipigwa marufuku rasmi kufuatia tamko la Waziri Mkuu Bungeni tarehe 18,Agosti 2011. Lakini pamoja na hilo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kufanya yafuatayo;

1. Kuitaka TAKUKURU ichunguze kwa kina kama kuna kampuni yoyote bado inasafirisha wanyama hai kwa siri wakiwemo wanyama wakubwa na wale watambaa kama vile mijusi,kenge, nyoka, tumbili , vipepeo n.k kwani hata hao walishakatazwa kufuatia tamko la Waziri wa maliasili na utalii mwaka jana.

2. Serikali ilite muswada Bungeni kuhusu sheria ya uwindaji ili Bunge lipate fursa ya kupertia na kuangalia upya namna nchi itakavyowenza kunufaika na biashara ya uwindaji, na vilevile kuangalia namna ya kuwalinda wanyama na viumbe vingine ndani ya hifadhi ili kuhakikisha hatupotezi kiumbe hai cha aina yoyote 'species'.

3. Serikali ifanye upembuzi yakinifu (thorough analysis) kuhusiana na faida na hasara za uwindaji, kiasi cha uwindaji kinachofanyika nchini ikilinganisha na idadi ya wanyama waliopo, ifanye tafiki kuhusiana na uwepo wa viumbe vipyta au kupotdea kwa baadhi ya viumbe katika mbuga zetu ili sasa taifa liweze kuamua kusitisha au kuendelea na biashara ya uwindaji wa wanyamapor na viumbe hai.

4.3 UGAWAJI WA MAENEKO YA HIFADHI BILA KUZINGATIA TARATIBU ZA KULINDA WANYAMAPORI NA MISITU

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro imetuhumiwa kugawa eneo la msitu wa asili katika kijiji cha Olchoniomelole kwa kampuni ya utalii inayojulikana kama Asilia. Kampuni hii inamiliki hoteli za aina mbalimbali kama lodges na campsite. Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali kutoka kwa wananchi wa eneo hilo wamelalamikia tabia ya Mamlaka ya NCAA kugawa kiholela maeneo ya hifadhi na huku kukiwa na tuhuma za rushwa dhidi ya mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuna lodge na campsite zaidi ya 30 zilizojengwa kandokando ya kingo za kreta ya Ngorongoro jambo ambalo linaweza kuathiri uhai wa kreta, ikolojia ya eneo la kreta pamoja na viumbe hai wanaopatikana ndani ya kreta.

Mheshimiwa Spika, Uharibifu huu unaofanywa ndani ya kreta unaharibu pia barabara za kuingia na kutoka ndani ya kreta kwa kuwa magari makubwa ya vifaa vyta ujenzi yanaingia ndani ya kreta mbapo kimsingi barabara hizi hazina uwezo wa kubeba magari makubwa yenye mizigo mara kwa

mara. Jambo hili sio tu limelalamikiwa na wananchi bali pia jumuiya za kimataifa zinazoshughulikia mazingira ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, zipo tuhuma za majina ya maafisa mbalimbali wanaotajwa kushiriki vitendo vya rushwa na kukosa maadili ya kazi.Ni dhahiri vitendo hivi visipo dhibitiwa vinaliingiza taifa katika hasara kubwa ikiwemo kuharibika kabisa kwa Ikolojia ya Ngorongoro ambayo ndio eneo pekee duniani ambapo binadamu wanaishi eneo moja na wanyamaporii.

Mheshimiwa Spika, Kitendo cha kuharibu Ikolojia hii kwa ujenzi wa majengo makubwa ya kudumu ni kitendo kinachopeleka kupungua kwa malisho na maji kwa wanyama na mifugo iliyopo ndani ya hifadhi hii kwani mpaka sasa idadi ya watu na mifugo ndani ya kreta inaongezeka sana.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kufanya yafuatayo:

1. Serikali kuchukua hatua za dharura ili kufanya uchunguzi wa tuhuma hizi, na pia kufanya tathimini ya ugawaji wa ardhi katika eneo la kreta.
2. Serikali ichunguze tuhuma za eneo la ardhi ya msitu lilitolewa kinyemela kwa kampuni ya Asilia, pamoja na makampuni mengine yaliyojenga hoteli mbalimbali kwenye Kingo za kreta. Vilevile, serikali iangalie kama maeneo hayo yalitolewa kisheria na kwa ukubwa ule ule uliopaswa kutolewa kwa kampuni hizo. Endapo maeneo hayo yalitolewa kisheria na yalifuata taratibu serikali ituambie je, kuruhusu ongezeko la ujenzi wa majengo ya kudumu kando kando ya kreta lina athari gani kwa Ikolojia ya kreta siku za usoni?
3. Serikali ichunguze tuhuma hizi za rushwa na utovu wa nidhamu ya maadili ya kazi zinazowakabili watendaji ndani ya Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro.

5.0 MISITU NA NYUKI

5.1 ZUIO LA MATUMIZI YA MKAA NA KILIO KWA WANANCHI

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Wakala wa Misitu nchini (TFS)ni kusimamia rasilimali za misitu ili ziweze kusaidia ustawi wa taifa kwa sasa na vizazi vijavyo. Hivyo hatuna budi kama taifa kulinda rasilimali za misitu kwa nguvu zote. Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga juhudhi za kutunza misitu ikiwa ni pamoja na kuwajengea wananchi utamaduni wa kupenda kupanda miti maeneo yanayozunguka mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, serikali imekuwa ikitoa matamko ya kukataza matumizi ya mkaa kwa miaka mingi. Japokuwa matakazo haya ya matumizi ya mkaa ni ya muda mrefu bado serikali hajjaweza kuja na nishati mbadala inayopatikana ili wananchi waweze kuipata kwa urahisi na kwa bei nafuu kulingana na hali halisi ya uchumi wa wananchi ili sasa wananchi hao waweze kuhamasishwa kuachana na matumizi ya mkaa ili kuokoa misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke ni serikali hii iliyowaaminisha wananchi kuwa tuna akiba kubwa ya gesi na hivyo gesi itapatikana kwenye kila nyumba kwa bei nafuu sana jambo ambalo sio kweli hata kidogo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa mpaka sasa bei ya gesi ni ghalii kwani mtungi ambao unaweza kutumiwa na familia yenye matumizi ya wastani ni gesi ya shilingi 50,000/- kwa mtungi wa kilo 15 tu kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mkoani Dodoma serikali kupitia kwa Waziri wa Wizara hii ilitoa katazo la kusafirisha mkaa kutoka Wilaya moja kwenda nyingine na kunukuliwa na gazeti la Mwananchi la tarehe 11, April 2017 lenye kichwa cha habari "***Mwisho Julai kusafirisha mkaa***" lilieleza kuwa mkaa utaruhusiwa kuchomwa na kuuzwa ndani ya Wilaya husika tu.

Mheshimiwa Spika, kauli hii sio tu imeshangaza umma lakini pia **inawagawa Watanzania**. Ni kauli ambayo isipoangaliwa kwa kina inaweza kuleta shida kwenye jamii. Tujiulize, wananchi wanaoishi Wilaya za mijini au katika ya majiji wao watachoma vipi mkaa na watachomea wapi?

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa ni Watanzania wachache wenye uelewa wa kutosha kuhusiana na makaa ya mawe. Ni ukweli usiopingika wapo Watanzania wengi ambao hawajawahi kuona makaa ya mawe. Japokuwa serikali imetoa kauli ndani ya Bunge hili kupitia Wizara ya nishati na Madini tarehe 18 Mwezi, 2017 kuwa serikali ina hazina kubwa ya makaa ya mawe ila ukweli ni kuwa makaa ya mawe yanakayochimbwa nchini yanatumika zaidi katika shughuli za uzalishaji viwandani kuliko majumbani. Vyombo vinavyotumiwa kwa matumizi ya kupikia na Watanzania walio wengi ni vyombo ambavyo haviwezi kuhilmili moto wa makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kufanya utafiti wa kina kuhusiana na matumizi ya makaa ya mawe majumbani kwani nchi nydingi duniani hutumia makaa haya kwa ajili ya matumizi ya viwandani tu. Je, athari zake kiafya ni zipi hasa kwa watakao tumia kwa ajili ya kuchoma nyama, mahindi na vyakula vingine vinavyohitaji moto wa moja kwa moja (direct heat).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa vyombo mbalimbali vya habari wakiwemo viongozi wa serikali wenye mamlaka na suala hili kulizungumzia hadharani suala la kukataza matumizi ya mkaa jambo la kushangaza ni kuwa mnamo tarehe 19/05/2017 katika mitandao mbalimbali ya kijamii ilisambaa taarifa kwa umma kutoka kitengo cha Habari na Mawasilino kwa Umma cha Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) likipinga kauli iliyotolewa kuhusiana na katazo la usafirishaji na matumizi ya mkaa. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujuua kama kweli taarifa hiyo ilitoka katika kitengo hicho kwani mnamo tarehe 10 April 2017 Mheshimiwa Waziri tayari alikuwa ametoa taarifa rasmi kwa umma katika mkutano wa 24 wa Baraza la Wafanyaakazi katika sekta ya

maliasili na utallii katika ukumbi wa LAPF-Dodoma. Serikali ituambie kauli rasmi ya serikali kuhusiana na matumizi ya mkaa ni ipi?

5.2 UFUGAJI WA NYUKI

Mheshimiwa Spika, kazi ya ufugaji wa nyuki ni kazi ambayo imeweza kuwasaidia Watanzania wengi kunyayua kipato chao hususani miaka ya hivi karibuni. Hii ni kutokana na wengi kujitahidi kutafuta njia za kuanza kufuga nyuki kwa njia ya kisasa ziadi.

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto nyingi katika sekta ya ufugaji wa nyuki kutokana kukosekana kwa masoko ya uhakika, serikali kutokuchukua jitihada za makusudi za kutangaza asali inayotoka Tanzania katika masoko ya kimataifa, na zaidi serikali kutokutenga bajeti ya kutosha hasa katika kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Nyuki. Mpaka sasa mapitio ya Sera hii yameshindwa kukamiliha kutokana na uhaba wa fedha.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linashangaza sana. Tukumbuke kuwa serikali ya Chama cha Mapinduzi kuititia Waziri Mkuu aliyejita ilijipambanua kwa ufugaji bora wa nyuki lakini jitihada zile alizozionyesha Waziri Mkuu aliyejita ni sawa ameondoka na jitihada zile. Hii ni kutokana na serikali ya sasa kutojali sekta ya ufugaji wa nyuki. Jambo hili linatia mashaka kwani inaonekana kila kiongozi anakuja na jambo lake la kipaumbele na pale anapoondoka jitihada zake nazo zinatupwa kapuni. Ni vyema serikali itambue serikali ni taasisi na sio mtu hata akiondoka yale mazuri yanayofanywa yapaswa kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuthibitisha jambo hili kwa mujibu wa Randama ya Wizara Jedwali namba 9, ukurasa wa 68 serikali imetenga shilingi milioni 200 tu kutoka vyanzo vya ndani tena kwa ajili ya kujenga uwezo. Huku fedha nyingine zikitegemea wahisani kutoka Norway, Belgium na Finland. Yaani bajeti ya sekta ya misitu na nyuki ni bajeti ya wahisani tu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuangalia upya sekta hizi zinazochangia kukuza pato la familia na kutafuta namna bora zaidi ya kuwezesha sekta hizi kwani zinagusa moja kwa maisha ya Watanzania wengi. Mheshimiwa Spika, Uchumi wa viwanda utaweza kukua endapo uchumi huo utaweza kugusa maisha ya wananchi moja kwa moja. Hivyo basi, sekta hizi zipewe kipaumbele ukiwa ni pamoja na kuwa na viwanda vidogo vidogo vya kusaidia uhifadhi wa asali pamoja na ufungashaji wa asali unaoendana na viwango vya kimataifa (parkaging).

6.0 UCHAMBUZI WA BAJETI YA WIZARA

Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 fungu 69, Jedwali namba 10 Wizara hii imetengewa jumla ya shilingi **51, 803, 284,000** tu kama fedha za maendeleo ambapo kati ya fedha hizo zilizotengwa **17,000,000,000** ni fedha za wahisani kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni wizara nyeti inayochangia sana fedha za kigeni. Ni Wizara inayotoa ajira na inachangia uchumi wa nchi. Kupewa fedha ndogo za maendeleo kiasi hicho maana yake ni kuwa shilingi ya Tanzania inakuwa katika hatari ya kuzidi kuperomoka. Mpaka sasa dola moja ya kimarekani (1 USD) **ni sawa na shilingi 2,239.01** ikilinganishwa na shilingi 2,144.27 mwaka 2015, na 2,170.44 mwaka 2016 kwa mujibu wa gazeti la Mtanzania la tarehe 4 April 2017.

Mheshimiwa Spika, serikali kuendelea kushindwa kuza huduma za utalii nje ya nchi na vilevile kushindwa kuwasaidia wafanyabiashara katika sekta ya utalii na hoteli kwa kuhakikisha kuwa inakuwa na masharti nafuu katika usajili ili ikupunguza wingi wa kampuni bubu ambapo mpaka sasa kati ya kampuni 1,050 ni kampuni 300 tu ndio zilizokidhi vigezo vya usajili, kwa sababu hiyo ni wazi kuwa sekta hii haitaweza kuongeza tija kwenye uchumi wetu. Na pia kupunguza kodi zisizo za lazima kwa wafanyabiashara ili

waweze kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuzingatia vigezo vyatika na kutoa huduma za kisasa ili kuvutia watalii wengi zaidi ni jambo litakaloisadia sekta hii kufanya vizuri zaidi balada ya kuendelea kuwa na bajeti tegemezi kutoka kwa nchi wahisani.

7.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa sekta nyngi hazifanyi vizuri kutokana na mapato hafifu yanayokusanywa na serikali kwa hivi sasa hali inayopelekea hali mbaya ya uchumi wetu. Lakini pamoja na hilo sekta hii ya Maliasili na Utalii inaweza kuwa mkombozi katika kuchangia uchumi hususani miradi ya maendeleo endapo tu serikali itaamua kuweka kipaumbele kuhimiza uwekezaji kwenye sekta ya utalii kwani matokeo yake yanaweza kuwa makubwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upizani haitasita kuendelea kuishauri serikali kwa kuwa nchi hii ni yetu sote na endapo tutanyamaza basi ni hakika lori hili tulilolipanda linaweza kumshinda dereva na sote tukajikuta shimonii

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuja na majibu kwa maswali na hoja ilizohoji na pia kuufanya kazi ushauri uliotolewa ili kujenga taifa lenye tija. Pale ambapo tutashindwa kusema kwa kushauri au kukosoa, basi tujue wazi kutakuwa tumeua taifa hili .Kuwanyima wenye akili mbadala kusema maana yake ni kuwalazimisha Watanzania kuwaza kwa namna inayofanana jambo ambalo litahatarisha amani ya nchi na ni ukiukwaji mkubwa wa utawala bora. Mwalimu Nyerere alisema maneno haya “**tuweke utamaduni wa kudhibiti viongozi wetu kama wanavunja sheria ya nchi, tusiogope! tukianza kuwa waoga, I promise you! Mtatawaliwa na dictators. I promise you!, ninyi wabunge mkiogopa ogopa na mkisema Mzee wanakuwa wakali I promise you, you will be under dictatorship**”. Kwa maneno haya yenye busara za hali ya juu za muasisi wa Taifa hili basi ijifunze kupokea maoni mbadala hata kama hayaifurahishi kwani kufanya hivyo

kutaisaidia nchi yetu na tutakuwa tunayaishi yale aliyoyasema Mwalimu Nyerere kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba kuwasilisha.

.....
ESTHER NICHOLAUS MATIKO (Mb)

Msemaji Mkuu Kambi Rasmi ya Upinzani -

Wizara ya Maliasili na Utalii

23 Mei 2017

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza kuchangia na ataanza Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni. (*Makofii*)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia katika Wizara hii. Nianze tu kwa kuipongeza Wizara, Waziri, Mheshimiwa Profesa Maghembe; Naibu Waziri, Mheshimiwa Injinia Ramo na watendaji wote wakiongozwa na Katibu, Mkuu Meja Jenerali Milanzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakinia pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wa nchi yetu kwa kuwateua hawa lakinia kwa kulinda maliasili ya nchi yetu na kuonesha kwamba ana nia nzuri ya kuendeleza utalii kwa kununua ndege ambazo zitakuwa zinatoa watalii maeneo mbalimbali na kuwaleta hapa kwa ajili ya kuongeza mapato ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze leo kwa kutumia hotuba zote hizi mbili ya Waziri na Kamati, yote ambayo tulitegemea kusema humu ndani hasa mimi naona wamezungumzia maeneo mengi. Nianze kwa kuangalia kitabu cha hotuba ya Waziri, ukurasa wa 17, ibara 36 wanasesma:-

"Dhana ya ushirikishwaji jamii katika uhifadhi wa wanyamaporilianzishwa kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanashiriki katika uhifadhi na kunufaika kwa mujibu wa Sera ya Wanyamaporiyamwaka 2007".

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye maeneo yangu ya Bunda na kwa bahati mbaya lugha inakuwa tofauti nikisema tembo inakuwa kosa basi niseme ndovu. Nimshukuru Waziri katika msimu wa kilimo wa mwaka jana na mwaka huu wametusaidia kuleta magari na askari ili kuzuia ndovu wasije kwenye maeneo ya makazi ya watu na kula mazao yao. Nina ombi maalum kwa Waziri kwamba kwa sasa wakulima wale wamelima sana na mazao yao yako kwenye hatua nzuri, kwa mwezi wa Tano, Sita na Saba watusaidie kupeleka magari na askari wa wanyamaporili wananchi waweze kuvuna kwa msimu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu hiki cha hotuba ukurasa wa 19, ibara ya 39 inasema, jumla ya shilingi milioni 567.5 zimelipwa kwa wananchi ambapo shilingi milioni 504 ni kifuta jasho. Miogoni mwa Wilaya zilizolipwa hizo hela ni Bunda, nikushukuru Waziri kwa sababu amewakumbuka watu wa Bunda kwa Vijiji vya Unyari na Kiumbu. Mheshimiwa Naibu Waziri alifika Kijiji cha Maliwanda ambacho kimeathiriwa sana na wanyamaporilakini kwa bahati mbaya katika malipo haya hawakupata na Kijiji cha Sarakwa. Nilishaenda Ofisi kwao wakaniahidi kwamba watafanya marekebisho na hawa watu watapata malipo yao ya kifuta jasho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo nzungumzie hili la kifuta jasho. Mwaka jana katika hotuba hii ya bajeti tumezungumzia marekebisho ya kanuni za wanyamaporikuhusu kifuta jasho. Wanasema kutoka kwenye mpaka, mpaka kwenye eneo ambalo ni kilomita tano kutoka kwenye mpaka ambao wananchi na wanyamaporilanaishi, mwananchi atakayeliwa mazao yake zaidi ya kilomita tano analipwa shilingi laki moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuseme ndovu amekula mazao kilomita arobaini kutoka eneo la mpaka analipwa shilingi laki moja kwa heka moja. Iko sheria pale kwamba kama umelima heka arobani halafu ndovu wamekuja kwenye shamba lako wamekula heka arobaini unalipwa heka tano tu kwa shilingi laki moja. Kwa lugha nyingine unalipwa shilingi laki tano, kwa heka 40 unalipwa heka tano tu heka 35 inakuwa sadaka. Sasa ni vizuri tukaangalia namna gani ya kurekebisha sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia kwenye kitabu hiki namna gani watu wanaozunguka wanyamapori wananaufaikana nao. Katika eneo langu la Unyari miaka mitatu iliyopita ndovu walivunja jengo la watoto na akina mama wajawazito. Tukajitahidi kujenga jengo hilo na Serikali ikaahidi kwamba itaezekwa na kufanya *finishing*. Niishukuru Wizara imetoa shillingi milioni 50 jengo lile linaendelea vizuri lakini alipokuja Waziri wa Afya amesema jengo lile kwa sababu tumelijenga vizuri liwe kituo cha afya. Kwa sababu ya sera yetu, nafikiri Mheshimiwa Waziri ni vizuri sasa akatusaidia hela nyingine kwa sababu inahitajika pale shilingi milioni 50 nyingine ili kubadilisha maeneo yale yote yawe kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba tutasaidiana katika jengo hilli ili kiwe kituo cha afya na ikiwezekana hata kama litaitwa Profesa Maghembe siyo mbaya ili mradi tu umetutengenezea eneo limekuwa zuri zaidi kwenye maeneo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo ya mipaka kati ya viji kumi na tano na Pori la Akiba la Grumeti. Mgogoro huu ni wa muda mrefu, tumesema sana na tunafikiri ile Kamati iliyoundwa ya Wizara tatu itafika kwenye eneo letu na kuweza kuangalia mipaka hii. Ipo hoja kwamba mwaka 1994 wakati eneo hilo linachukuliwa kutoka *open area* kuwa *game reserve* (pori la akiba), wananchi hawakushirikishwa. Kwa hiyo, tunafikiri kuwa sasa ni muda muafaka kuangalia mipaka hiyo na Kamati imesema ili tuweze kujua ukweli uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi ni kwamba wakati hilo pori la akiba linachukuliwa ambalo maarufu kule kwenye maeneo yangu kama Kawanga kulikuwepo na malambo mawili yaliyochimbwa na wananchi kwa ajili ya kunywesha mifugo. Yale malambo mawili sasa wanyamapori ndio wanakunywa maji lakini sisi huku chini hatuna maji ya kunywa. Mheshimiwa Waziri anajua mpaka wetu ni Mto Rubana, sasa watu wakienda katika maji yale wanafukuzwa kwa sababu wakivuka Mto Rubana tu wameenda porini. Kwa hiyo, tulifikiri ni muhimu sana Serikali kuja kuangalia namna ya kuchimba malambo upande wa pili ili ng'ombe wawe wanapata maji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia kero ya mipaka ambayo ni ya muda mrefu lakini kuna vijiji vya Mgeta, Tingirima, Kandege na vyenyewe havikupata huu mgao wa kifuta jasho. Ni vizuri sasa tukaona ni namna gani wanawenza kuzingatiwa, lakini Maliwanda ni kijiji cha kwanza kuzingatiwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilitaka nichangie hayo, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante na uko umuhimu umuandike kwa maandishi maana vijiji hivyo ni vingi. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda nikushukuru sana kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niungane na msemaji wa kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na wataalam wao kwa kuweza kuandaa bajeti hii ambayo wote tumeisikiliza hapa kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii ni nyeti sana. Nadhani kama Waheshimiwa Wabunge

tunatakiwa tuiangalie kama moja ya Wizara ambazo zinaingiza mapato makubwa sana katika uchumi wa nchi yetu. Wizara hii jinsi ilivyo na inavyofanya kazi ina changamoto nydingi sana na hasa ukizingatia suala la utalii kwa mfano ndiyo sura ya nchi ndani na nje ya nchi yetu lakini kuna vitu ambavyo havijakaa sawa. Kwa maana gani? Kwa maana kwamba kunapaswa kuwa na uwialinishaji kati ya wageni wanaoingia nchini na watu walioko hapa nchini, watu wanaokuja kufanya shughuli hapa nchini na sisi Watanzania tulioko hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yakiunganishwa vizuri na yakifanyika vizuri yatachochea nchi yetu kupata watalii wa kutoka na kuongeza kipato kwa ajili ya matumizi ya Watanzania. Bajeti yetu hii kwa mfano Mheshimiwa Waziri kasema hapa kwamba kwa mwaka 2015/2016, Wizara hii iliweza kuchangia zaidi ya billioni 1.9 dola za Kimarekani na mwaka huu unaokwisha wa 2016/2017 imechangia zaidi ya dola billioni mbili, ni hela nydingi sana hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna ukiritimba mkubwa sana mtu anapokuja hapa Tanzania anakutana nao. Mtalii anapoingia hata pale *airport*, watu wa Idara ya Uhamiaji wanavyowapokea wale wageni, lugha wanayoitumia si lugha ambayo inapaswa kutumika kwa kukaribisha wageni. Kuna haja sana Mheshimiwa Waziri wa Utalii, ajaribu kuongea na hizi Idara ikiwezekana washirikiane kwa karibu zaidi na wawape fursa ya kutembelea vivutio mbalimbali ili wajue thamani ya kumpokea mgeni pale *airport* na kumpa *treatmentinayostahili* kwa sababu ni mgeni anayekuja kwa ajili ya kujenga nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ina changamoto nydingi, ina tozo kibao, tozo zaidi ya 36. Hizi kodi na tozo hazina afya au tija kwa ajili ya kujenga sekta hii. Kuna haja ya kuangalia namna ya kupunguza hizi tozo na kodi ili kusudi tuweze kupata mapato mengi zaidi kutokana na watu wanaokuja hapa nchini kwa ajili ya shughuli za kitalii au shughuli nydingine mbalimbali. Haya tunayoyasema hatujaanza leo hata jana tulishauri. Ningombaa sana

Wizara ya Fedha na Wizara ya Maliasili na Utalii wajaribu kukaa na kuona kodi na tozo zipi ziweze kuangaliwa upya. Hii itaongeza ufanisi wa kupata mapato makubwa zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina changamoto moja nyingine kubwa sana. Wizara hii imepelekea wafugaji katika nchi yao sasa kuonekana ni yatima kitu ambacho ni tatizo kubwa sana. Ukiangalia hivi mfugaji anapokwenda akaingiza mifugo ndani ya hifadhi au kwenye misitu na mtu anayekata misitu kwa ajili ya kuchoma mkaa na kadhalika ni nani mharibifu zaidi ya hara? Kila siku tunaona magunia ya mkaa zaidi ya milioni 50 yanaingia Dar es Salaam ambayo yanatokana na kukata miti ambaa ni uharibifu wa mazingira lakini mfugaji anaonekana ndio haramu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakati Mheshimiwa Waziri anakuja ku-*windup hotuba* yake tunataka tuone ni namna mfugaji katika nchi hii naye anapewa nafasi na kuthaminiwa. Kwa mfano kule Muleba, Mkuu wa Wilaya anasema kwamba amewapa *notice* wafugaji wahame, waende wapi hawa ni Watanzania. Pili, ukisema wahame ina maana kwamba waanze kutafutana wewe umetokea wapi, kila mmoja amfukuze mwenzake. Tutajenga *situation* ambayo siyo nzuri kwa ajili ya nchi yetu na tutaanza kuleta ubaguzi ambaa hauna tija yoyote kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hili suala la mifugo na hifadhi, ndio tunahitaji tuwe na hifadhi lakini naomba tuziangalie sheria. Kuna baadhi ya mashamba mengine yalikuwa ya mifugo sasa hayafanyi kazi, kwa nini tusiyakate yale mashamba yakatumika kwa ajili ya wafugaji kufugia mifugo yao na kutoka kwenye hifadhi? Hata hivyo, tujue kwamba idadi ya wananchi inaongezeka kila kukicha lakini ardhi haiongezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo ni lazima kuwe na mustakabali sasa wa kitaifa wa kuangalia kwamba tunahitaji kuhifadhi misitu na hifadhi zetu wakati huohuo wananchi nao wanahitaji kutumia mazao ya mifugo,

kufuga mifugo na kufanya kilimo chao, vinginevyo tutachochaea vurugu ambayo haina tija kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwepo na doria dhidi ya ujangili na biashara haramu ya nyara za Serikali. Hii maana yake ni kuwe na vikosi maalum visaidie kulinda hifadhi zetu hizi au maliasili yetu hii. Wenzetu siku hizi wana teknolojia mpaka kutumia zile ndege ambazohaziendeshwi na rubani (*drones*) na wana mpaka wale mbwa maalum wa kunusa, naomba tuongeze hiyo jitihada ili kusudi tuhifadhi na kulinda maliasili yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuitangaze Tanzania. Mimi nimefurahi juzi nilipanda ndege ya *Bombadier* wameweka kwenye ndege *air flying magazine* wameonesha baadhi ya picha na mahali vilipo na kuutangaza utalii wa nchi yetu, ni kitu kizuri sana. Tunapaswa tutoke pale tulipo, sasa tumepata ndege zetu lakini vilevile suala la kutangaza utalii nje ya nchi ubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Bodi ya Utalii (*TTB*) ipewe mamlaka na ipewe fedha kwa ajili ya kuendesha utalii nje ya nchi. Haiwezekani Ngorongoro wanaenda kutangaza kivyao, *TANAPA* kivyao, sijui nani kivyao, haiwezekani wote wanatoka Tanzania hawa. Hii Bodi ingewezeshwa, tena bahati nzuri imepata Mwenyekiti mzuri sana, *Advocate* Mihayo, ni wakili mzuri anajua vizuri sana haya mambo. Nina imani kabisa kwamba akiwezeshwa na Bodi ikiwezeshwa tutafanya kazi nzuri sana ya kuitangaza nchi yetu nje ya mipaka yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ambalo lipo na naomba kwenye kitabu chako ukurasa wa 19 umekosea sana, unasema wananchi walindwe na mali zao dhidi ya wanyama waharibifu, tuna tatizo la tembo wanaharibu mazao na mali za binadamu, lakini bado watu hawapati fidia inavyotakiwa. Tunaomba Wizara yako iunde kikosi maalum ambacho kitasaidia kwa ajili ya kuhifadhi na kuwalinda wananchi pamoja na mali zao. (*Makof*)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu chako una-refer kwamba Magu wanapata hicho kifuta jasho na kifuta machozi. Magu hawapakani na Hifadhi ya Serengeti isipokuwa ni Wilaya ya Busega, zamani ilikuwa ni sehemu ya Magu. Naomba rekodi za Mheshimiwa Waziri azibadilishe isomeke Busega badala ya Magu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna kuboresha miundombinu inayopakana na hifadhi, nimeshamwomba Mheshimiwa Waziri barabara ya Kijereshi naomba anisaide waitengeneze kwani inasaidia sana kuongeza idadi ya watalii wanaoingia Serengeti na iko Busega. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri hili uweze kulifanyia kazi ili kusudi sasa tuweze kuimba wimbo mzuri wa kuongeza watalii na kuongeza mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kuzingatia sana suala la Ushirikishaji wa Jamii katika Uhifadhi (*WMAs*)...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ryoba dakika tatu.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nina jambo moja. *WMA* ni sehemu ya ardhi ya vijiji kwa maana kwamba Serikali za Viji ni wananchi wao walikaa wakatoa hayo maeneo wakaunda *WMA* ili wanyamapor i wakiingia humo wao wawekeze wapate mapato. Ni vizuri Waziri afahamu sera na sheria ilioanzisha *WMA* ilikusudia nini, ilitaka kugatua madaraka kuyapeleka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *WMA* zimeundwa lakini mmeanza kuziua kwa kuanzisha kitu kinaitwa *single entry*. *Ikona WMA* ambayo ndio *WMA* kioo ambayo ina-*shine* kuliko

WMA zote, mmeiua. *Camps* zote na hoteli zilizokuwa zimewekeza kwenye ile WMA wameanza kuondoka kwa kukosa wageni. Mwaivaro ni *camp* ambayo ilikuwa inapata wageni 400 kwa msimu sasa hivi wameshuka mpaka 70. *Camps* nydingi pale zimeondoka kwa sababu ya *issue* ya *single entry*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Mheshimiwa Waziri afahamu kwamba ili uende *Ikona WMA* lazima utokee Arusha na ukitokea Arusha lazima u-cross *Serengeti National Park*, kwa ku-introduce mfumo wa *single entry* wageni hawaendi tena *Ikona WMA, you kill it*. Sisi tunasema ahsante, yeye aue tu lakini kwenye ardhi ile sisi tutafuga ng'ombe na tutalima tumbaku kwa sababu hawataki sisi tufanye *conservation*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuja hapa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji wa maeneo yanayounda *Ikona WMA*, wamekuja Madiwani na wajumbe wa WMA tukaenda mpaka kwa Mheshimiwa Waziri akasema ataishughulikia hii ya Serengeti ni *very unique*, baadaye akaniambia Kamati imekataa. Mimi nikachukua jukumu la kwenda kwenye Kamati ya Maliasili na Utalii hata hawana habari, sasa ni Kamati ipi ilikataa? Sasa mimi nataka leo kwa dakika hizi tatu ambazo nimepewa atakapokuja ku-wind-up aniambie yuko tayari kuangalia upya mfumo huu wa *single entry* au wapo tayari kuua hizi WMA?

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MARWA R. CHACHA: Kama msipopitia upya kanuni hizi zilizouna WMA, *you will kill it* na sisi hatuna shida tutachunga tu ng'ombe mle. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante mengine muandikie.

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Balozi Adadi, Mheshimiwa Risala Saidi Kabongo na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka.

Baada ya maneno haya, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa Hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Wakati wa kusitisha mchana nilimtaja Mheshimiwa Balozi Adadi, ajiandae Mheshimiwa Risala Saidi Kabongo.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza mchana huu. Kwanza napenda kuwashukuru sana Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kuweza kutuletea watalii wengi. Wizara hii ni muhimu sana ambayo inaingiza pato la Taifa kama alivyo sema mwenyewe Mheshimiwa Waziri kwenvye asilimia 21; asilimia 17.5 ikiwa utalii na misitu asilimia 3.9. Nitakuja kuongelea suala hilo baadaye lakini ningependa kuanza mchango wangu na Hifadhi ya Amani (*Amani Natural Reserve*). *(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Misitu ya Amani ni mikubwa sana na kama nilivyoongea kwenye mchango wangu mwaka jana ni misitu ambayo ina mambo mengi ndani yake. Ukiacha mambo ya miti yenyewe ambayo ipo pale pamoja na vivutio mbalimbali au *scenario* ambayo ipo au pamoja na vipepeo, maua na kila kitu ambavyo viko pale lakini ni *reserve* ambayo inatakiwa iangaliwe kwa uangalifu. Ni *reserve* ambayo inatupa chanzo cha maji kutoka Mto Zigi. Kwa hiyo, *reserve* hii sasa hivi ina hatari ya kuharibiwa na ina hatari ya hata chanzo cha maji kuharibiwa kabisa kwa sababu hivi karibuni tu maji ya Tanga yote yalikuwa ni tope. *(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudui zimefanyika kimko, Mkoo wa Mkoa amejaribu kupeleka watu kule kwa ajili ya kuzuia ukataji wa miti kwenye hifadhi hiyo. Mkoo wa Wilaya pamoja na Halmashauri tumekuwa tukipeleka Askari wa *Field*

Force lakini nguvu inakuwa ni ndogo. Ningeshauri ili kuweza *ku-preserve Amani Nature Reserve*, Mheshimiwa Waziri hawa Askari wa Wanyamapori ambao wapo kwa ajili ya kuangalia nafikiri wako pia kwa ajili ya kuangalia hifadhi zetu, tafadhalii ahamishe hata *unit* moja *immediately* vinginevyo hii *reserve* itapotea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *reserve* hii ni ya maana sana na iliwahi kulinganishwa kama ni moja ya maajabu ya dunia na mwanahistoria mmoja ambaye alikwenda kwenye Kisiwa cha Galapagos kule Ecuador Pacific. Sasa tutakapoachia *reserve* hii iweze kuharibika tutakuwa tumefanya makosa makubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu wakulima wangu wa Derema 1,128. Wakulima hawa wameshapewa maeneo kwenye shamba la Kibaranga lakini bado hawajahama. Kama nilivyosema kwamba bado wanahitaji kifuta jasho ambacho Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba atakiangalia, naomba akiangalie ili wakulima hawa waweze kuhama mara moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni kuhusu Mnada wa Miti ya Tiki. Mheshimiwa Waziri alikuja kuhudhuria Mnada wa Tiki pale Lunguza. Mnada huu umekuwa na malalamiko mengi sana kwani umekuwa ni kilio kwa wafanyakishara na wenye viwanda pale Muheza kwa sababu tangu hii *system* ya mnada imekuwa *introduced* kuna viwanda karibu kumi vimefungwa pale Muheza. Hii ni kwa sababu matajiri wanakuja pale na hawa wenye viwanda vidogo vidogo hawawezi kushindana na hawa matajiri, utakumbuka kwenye mnada uliopita tajiri mmoja alichukua karibu vitalu vyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri aangalie *system* hii ya mnada ijaribu kuboreshwa na kuangalia watu ambao wapo wanazunguka wanaangalia hizi hifadhi. Tiki zinapandwa vizuri sana, huyu Meneja wa Shamba la Lunguza Abdallah anafanya kazi nzuri sana na kila tiki inapokatwa unakuta amekwishapanda. Sasa

wafanyakazi na wakulima wanafanya kazi nzuri, itakuwa siyo busara wao kuwanyang'anya sasa kwa sababu hawa matajiri wanaponunua hivi vitalu wanapakia magogo yote wanakwenda kupasulia Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri aangalie ili hawa wazawa ambao wamefungua hivi viwanda pale waweze na wao kupata hizi tenda za kuweza kupasua haya magogo, vinginevyo itakuwa shida. Kwa sasa viwanda karibu kumi vimefungwa, wafanyakazi karibu 1,000 wale wanaokaa pale wamepoteza kazi. Kwa hiyo, ni lazima kuwawekea masharti, kama hao matajiri lazima wafungue viwanda pale ili wafanyakazi wa pale waweze kupata kazi ya kufanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilikwishamwomba Katibu Mkuu ni kwamba tunategemea barabara ile sasa hivi kuiweka lami, lakini pale kuna malighafi (*moram*) ambayo ipo kwenye msitu huu lakini ipo pemberi. *TANROAD* wameomba sana kutumia hiyo malighafi kwa ajili ya kutengenezea hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ombi hili liweze kuzingatiwa kwa sababu kipindi kijacho tumeshaingizwa kwenye mpango kwa ajili ya kuwekewa lami kipande kidogo. Naomba kabisa mfikirie tutumie hiyo moram ambayo ipo pale iweze kutengeneza barabara hiyo ya Amani. Barabara hii itasaidia sana kuleta watalii ambao wataongezeka ili kupanda kwenye Milima ya Amani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Mbuga ya Saadan ambayo ina upungufu sana wa wanyama. Mbuga hii sisi Muheza tuna *interest* nayo kwa sababu inapita Bagamoyo, Pangani na inatoboa mpaka Muheza inakwenda mpaka Amani. Sasa tulikuwa tunaomba waongezwe wanyama pale iweze kusaidia ili siku zijazo watalii watatoka Sadaan wanakwenda Pangani, Amani wanarudi Pangani kupumzika. Ni suala la muhimu sana ambalo naomba mzingatie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kwenye utalii. Kama nilivyosema, utalii unaingiza pato kubwa la Taifa lakini ukiangalia idadi ya watalii wanaoingia hapa nchini sasa hivi imeongezeka tuna milioni 1.2 ukilinganisha na mwaka jana ambayo ilikuwa milioni 1. Hata hivyo, bado idadi hii haitoshi kabisa ukiillinganisha na nchi nyingine. Kwa mfano, *Victoria Falls* Zimbabwe, pale ni hizo *falls* tu zenyewe lakini watalii ambao wanaingizwa pale ni wengi kuliko hawa wa kwetu, ni zaidi ya milioni 2.5 kama sikosei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu wa kujaribu kuongeza vivutio vya kuwafanya watalii waweze kuja kwa wingi na tumeona katika Afrika tupo kwenye namba 10 au 11. Kwa hiyo, bado tupo nyuma na tunahitaji kuongeza juhudili ili kuongeza watalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalii hawa unawaongeza namna gani? Kuna masuala ya matangazo (*advertisements*). Suala hili ni muhimu sana na ukiangalia hapa hela ambazo zimetolewa kwa ajili ya *advertisement* ni ndogo sana. Nakumbuka kuna wakati mimi nilikuwa *Denverkule Marekani* na nilifarijika sana nilipoona kwenye *TV* moja ya *Fox* wanaonesha *migration Serengeti* na baada ya ule mukutano Wazungu wengi sana walonesha *interest* ya kuja kuangalia hii *migration* huku Tanzania. Sasa *advertisement* kama zile zinasaidia sana, ni lazima tuweke umuhimu sana kwenye mambo ya *advertisements*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *advertisements* kuna masuala ya *tour operators*. *Tour operators* wamesahauliwa sana na siajona wakitajwa kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri. Hawa ndiyo watu wanaleta watalii, hawa ndiyo wanafanya mipango, *tour operators* ni watu muhimu sana. Ukiangalia kwa mfano hao *Victoria Falls* ambao wanaletewa watalii wengi sana, wengi wanatoka *South Africa* na Zimbabwe wamefungua Ofisi kule (*tour operator*), wengi wanawachukua wanawaleta mpaka wanajaa, ni vizuri sana tukawapa umuhimu watu hawa. (*Makofii*)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tu nilikuwa naangalia kwenye gazeti moja la wananchi kwamba *Kenya Airways* inatoa ndege mara tatu sasa hivi kutoka *Cape Town - Victoria Falls* – Nairobi. Ni muhimu sana kuangalia *tour operators* ambao tukijumuisha pamoja na *direct flights* ambazo ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri azipate, Wizara hii ina uwezo wa kununua au kukopa ndege yake ili kuwatoa watalii *direct*, watalii wanapenda *direct flights*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano kama Zanzibar, Zanzibar wanapata watalii wengi sana, lakini tatizo la Zanzibar sikumbuki sasa hivi kama wamesharekebisha ile mikataba yao ya zamani ambayo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Balozi. Mheshimiwa Risala ajiandae Mheshimiwa Lulida.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu katika nchi yetu. Kwanza, niipongeze hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo imetolewa na Waziri Kivuli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitazungumzia Hifadhi ya Mikumi ambayo imepitiwa na barabara kuu ya Tanzania – Zambia yenyе urefu wa kilomita 50 ambayo ilianzishwa mwaka 1964 kabla ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi. Barabara hii imekuwa na ongezeko la magari mwaka hadi mwaka. Kwa takwimu za mwaka 2012 idadi ya magari yalikuwa yanapita katika hifadhi ni 1,750 sawa na asilimia 60 ambayo yalikuwa yakipita kwenye kilomita 50 ndani ya hifadhi. Mwaka 2014 magari yaliongezeka hadi kufikia 1,991 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili ni kubwa na maoteo yanaonesha ifikapo mwaka 2025 magari yanayopita

katika Hifadhi ya Mikumi yanaweza kufika 4,699 kitu ambacho ni hatari sana kwa kukua kwa Hifadhi ya Mikumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna madhara ya kiikolojia ambayo yanaweza kutokea kwa magari hayo kupita ndani ya hifadhi. Pamoja na madhara hayo ya kiikolojia kuna ajali nydingi zinatokea ikiwa ni pamoja na vifo vyta wanyama na binadamu. Kumekuwa na ajali nydingi, nina takwimu kidogo hapa za mwaka 2011 - 2015. Nikiangalia katika takwimu zangu zinaonesha mwaka 2011 idadi ya vifo vyta wanyama ilikuwa 125 katika Hifadhi ya Mikumi lakini 2012 idadi ya wanyama waliogongwa ni 111, mwaka 2013 ni wanyama 132, mwaka 2014 ni wanyama 354 na mwaka 2015 ni wanyama 237.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa wale wanyama tu ambao wanaonekana barabarani lakini wanyama wengine wanagongwa wanaenda kufia ndani ya hifadhi. Kwa idadi hiyo kubwa ni lazima hatua zichukuliwe. Barabara hii imekuwa ni changamoto kubwa na hatua zisipochukuliwa basi tunaweza kupoteza uhai wa Hifadhi ya Mikumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwa Wizara. Wizara ya Maliasili na Utalii wanaweza kukaa na Wizara ya Miundombinu ili waangalie namna gani ya kuboresha barabara ya Melela – Kilosa - Mikumi yenye urefu wa kilomita 141.75 kwa kiwango cha lami ili tuweze kupunguza idadi ya magari ambayo yanapita ndani ya hifadhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kitu kingine ninachoweza kuishauri Wizara ni kufanya utafiti kwa nchi nydingine ambazo barabara zinapita ndani ya hifadhi na tunaweza kuona namna gani wao wanafanya na tuweze *ku-implement* kwenye nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ni kwa *TANAPA* kama wanaweza kutoa tozo za magari yanayopita hifadhini yaani kutoza magari badala ya abiria ili tuweze kupata mapato yanayotokana na magari yanayopita

hifadhini wakati tukiendelea kufanya tafiti mbalimbali kwenye nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yanayopotea kutokana na magari kupita kwenye barabara ya Mikumi ni makubwa sana. Tafiti za mwaka 2012 zinaonyesha hifadhi inapoteza shilingi bilioni 4.7 kwa tozo za abiria lakini Serikali inapoteza shilingi bilioni 1.4 kwa tozo kwa ajili ya magari. Kwa hiyo, ukiangalia ni fedha nyngi sana kama Wizara tungeweza kuzingatia kutoza hizi tozo basi tungeweza kupata mapato mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoke kwenye barabara ya Mikumi, niingie kwenye kimondo ambacho kipo Wilaya ya Mbozi katika Mkoa wa Songwe. Katika Mkoa wangu wa Songwe kuna kitu kinaitwa kimondo, sidhani kama Wabunge wengi wanakifahamu labda kwa kukisikia lakini ni kivutio pekee sana kwenye Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Kivutio hicho kina changamoto nyngi sana na kinasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Ukiangalia miundombinu katika kivutio kile hairidhishi, majengo ya Ofisi ni chakavu sana, kimondo kile hakina uzio ili kusaidia ukusanyaji wa mapato lakini pia vyoo haviridhishi hivyo kusababisha wageni wengi kutofika katika eneo lile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka katika mchango wangu uliopita nilisema kwamba eneo lile liboreshwe hata tuweze kuweka *camp site* ambazo wasafiri wanaokwenda nchi za Malawi na Zambia wanaweza kufanya *camping* katika eneo lile na tukaweza kuongeza mapato. Kwa hiyo, nashauri Wizara itenye fedha kwa ajili ya miundombinu ya eneo la kimondo ili kuweza kuvutia wageni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naunga mkono hoja ya kupunguza tozo kwenye biashara za utalii. Tozo zimekuwa nyngi sana kwenye Wizara hii na wafanyabiashara wengi wanakwama kutokana na tozo. Vilevile pamoja na tozo hizi hakuna *one stop center*ya kulipia hizi tozo ili wafanyabishara wawzeze kufanya biashara zao kwa urahisi. Hii inasababisha

hata uwekezaji wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kupungua sana na kusababisha wawekezaji kushindwa kuja kuwekeza katika mikoa yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kidogo utalii wa utamaduni na utalii wa fukwe. Utalii wa utamaduni umekuwa ni kivutio kikubwa sana kwa wageni wanaotembelea kwenye maeneo yetu ya uhifadhi. Unapotoka kwenye maeneo ya hifadhi, wageni wengi wamekuwa wakilazimika kwenda kwenye maeneo ya vijiji ili kuona utalii wa kitamaduni lakini utalii huu haujaboreshwa vizuri, hivyo huwafanya wageni wengi kutofurahia aina hii ya utalii wa utamaduni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna utalii wa fukwe, fukwe zetu nydingi bado hazijaboreshwa, sio nzuri, hazivutii. Kwa hiyo, tumekuwa tuna tatizo kubwa la wageni kutumia fukwe zetu, ni chafu, takataka ni nydingi, zinanuka na hazina huduma nzuri. Kwa hiyo, nadhani Wizara ijikite katika utalii huu ambaa pia wageni wengi sasa wanapochoka kuangalia wanyama wanapenda kuona utalii wa namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia hili suala la hawa wanaokwenda kufanya *field* kwenye hoteli za kitalii. Kumekuwa na changamoto kubwa sana ya vijana wetu kwenda kufanya *field*, imekuwa sasa ni mtindo wa kawaida kwa watu wengine hoteli kuwatumia vijana hawa kwa idadi kubwa kuwafanya kazi na baadaye kutokuwapa ajira. Imekuwa kama ni kawaida kwa wao kupewa kazi za *field* wanapomaliza wanachukua watu wengine lakini ukiangalia idadi ya watu wanaofanya *field* na idadi ya waajiriwa ni ndogo na kuwafanya vijana hawa kukata tamaa, kulipwa fedha kidogo na wengine hawalipwi wanaambiwa ni *field*. Kwa hiyo, vijana wetu hawa wamekuwa wakitumika sana kwenye hoteli hizi za kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara ije na sera au mpango wa kuona ni namna gani hawa vijana wanapomaliza vyuo wanapokwenda kwenye *field*, wangapi

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wanaajiriwa na wangapi wanaondoka. Kwa sababu inakuwa kama ni mtindo sasa wao kutumika tu kuwapatia faida wale ambao wana hoteli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani na nashauri muichukue na kuifanyia kazi. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Lulida, ajiandae Mheshimiwa Cosato Chumi na Mheshimiwa Mwanne Mcemba.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia katika hoja iliyopo Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza nataka niishukuru na kuipongeza timu ambayo ilisimamia kuhakikisha Tanzania *concession fee* inapita na kuifanya Serikali iweze kupata mapato. Nitataja kwa majina ni akina nani walismamia hiyo timu, ilikuwa chini ya Mwenyekiti wa Bodi iliyopita Ndugu Modestus Lilungulu, Mama Chijoriga, Ndugu Fumbuka, Mama Wilmo, Mheshimiwa Jenista Mhagama na mimi mwenyewe Riziki Lulida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtajiuliza kwa nini tumefikia hapo? Tanzania tulifikia mahali ambapo uchumi wetu ulikuwa nyuma, watu walikuwa hawataki kulipa tozo ambayo ni halali katika nchi hii. Tozo ya dola nane katika hoteli ni hasara kubwa katika nchi hii na uchumi mkubwa unakwenda kwa wawekezaji sisi wenyeewe Watanzania tunakosa mapato. Nilimwomba Waziri Mkuu ashirikiane na Wizara watufanyie semina, namshukuru juzi tumepeata semina ya kwanza, bado hajatosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hajatosha kwa vile watu wengi au baadhi ya Wabunge bado hawana uelewa. Ili kujenga uelewa kwa Wabunge wapya, kwanza watembezwe katika maeneo husika wajionee kiasilia. Leo

unaona mwenye hoteli anaotoza dola 500 anataka atoe dola nane lakini jiulize *TANAPA* ndiyo wanajenga barabara, wanapeleka maji, *TANAPA* na Ngorongoro ndiyo wao wanapeleka maaskari kutunza maeneo yale ili watalii wawe katika usalama. Je, mnaposimamia tozo hizi ziendelee kuwa kwao sisi wenyewe tuendelee kupata tabu, ni nini hicho? Maana yake hatujafunguka. Ili tufunguke, naomba tena tuje tufanyiwe semina mbalimbali ili watu wapate uelewa (*awareness creation*) kwa ajili ya Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha mwekezaji anaingia ndani ya mbuga, ana hoteli lakini anaingiwa na kigugumizi cha kutotaka kulipa kodi na anatumia mbinu zote mpaka kwenda mahakamani toka mwaka 2007 na ndiyo sasa hivi *concession fee* imeruhusiwa na tutalipa katika *fixed rate* ambapo uchumi wa nchi utaruka. Baadhi ya Wabunge mnasema tusilette hizi tozo, kwa falda ya nani? Tuna ajira ndani ya *TANAPA*, watoto wetu, ndugu zetu wanafanya kazi watapata wapi mishahara? Kuna *tour operators* ambao wanakuja kufanya kazi Tanzania na wana wafanyakazi, kama tozo hizi mnataka zirudi kwa upande wa pili hela hii itapatikana wapi? Ndiyo maana nasema tupewe semina tena ili kujenga uelewa wa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nizungumzie Mbuga kubwa ya Selous. Selous ni mbuga ya kwanza kwa ukubwa Afrika, lakini ni mbuga kubwa duniani lakini hakuna chochote kinachofanyika ndani ya Selous hata mapato hayaonekani. Kuna *corridor* ambayo inatoka Mozambique inakuja Tanzania, kila mwaka tembo, simba, chui na nyati wanakuja Tanzania, haijatangazwa hata siku moja, kila mwaka inatangazwa Mbuga ya Serengeti. Kwa nini mnaiacha Selous isitangazwe halafu mnaridhia kuwapa *percent* ndogo ya 17.2. Jamani tufike mahali tufunguke tuinue uchumi huu kwa kuiongezea pesa za *promotion* ili Selous ifanyi kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Selous na ukubwa wake lakini *two third* ya Selous ipo Mkao wa Lindi na Mwenyezi Mungu ameujalia Mkao wa Lindi kuna fukwe kubwa za bahari

kuanzia Lindi mpaka Mtwara. Kwa nini Selous isingefunguka ili ikasaidia uchumi wa kusini, Selous imefungwa. Ni uwindaji na ujangili kwa kwenda mbele matokeo yake tunapigania uchumi ambaao umefungwa na baadhi, sielewi kama ni makusudi au ni dhamira. Nataka kesho Waziri atakapokuja kufunga hoja yake aniambie kwa nini Selous haiwi *utilized*. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenda Liwale kwenye Selous yenye hakuna barabara, kutoka Nangurukuru kwenda Liwale mpaka Nachingwea ambayo Selous inachukua asilimia 2.3, hakuna barabara. Nataka Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano akishirikiana na Waziri wa Maliasili na Utalii watujibu kwa nini wameifunga Mbuga ya Selous isifanye kazi? Imefikia mahali tunajiuliza, tunataka uchumi endelevu na uchumi upo na wanakuja wageni wakileta fedha za kigeni lakini unaona ajabu Selous haitumiki. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia uchumi wa utalii ambaao uko ndani ya Tanzania na ukitalia Tanzania ni lazima na Zanzibar uitaje. Utalii huu Bara unaonekana lakini Zanzibar haionekani. Ili kuondoa umaskini ni lazima kuhakikisha maeneo yote haya mawili yanaendelezwa kiutalii. Maana yake mtalii anatoka Ulaya akiwa na *package* kuwa anaingia Serengeti, Ngorongoro anamalizia Zanzibar, kwa nini Zanzibar pesa hakuna, kwa nini Zanzibar wasifunguke na utalii huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo madogo kama Seychelles, ni nchi ndogo lakini utalii na uchumi wao ni mkubwa lakini Zanzibar imedorora. Lazima tuijilize kuna nini Zanzibar mpaka utalii wake uko mikononi mwa wajanja na Wazanzibari wenyewe inabidi wafunguke. Humu ndani kuna Wazanzibari, tumieni fursa yenu kuiona Zanzibar inakwamuka na utalii wa Zanzibar unafanya kazi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kupambana na Ujangili ndani ya Bunge, nataka kuzizungumzia *corridors*. Corridors kubwa za tembo Tanzania

moja ipo Rukwa (Rukwati) na nyingine ipo Niassa (Mozambique). *Corridor* ya Rukwa (Rukwati) ambayo inatokea Zambia inakuja mpaka Katavi haitangazwi, vilevile ya kutoka Mozambique kuja mpaka Tanzania haitangazwi matokeo yake wameingia wafugaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe taarifa, nikiwa na mwenzangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, tulikutana na kundi la ng'ombe, wale wafugaji wakiwa na silaha wanaingia ndani ya mbuga. Tukajiuliza wanakwenda kufanya nini ndani ya mbuga, kuna tembo, simba, faru na nyati, kuna harufu kubwa ya baadhi ya wafugaji kushirikiana na majangili. Hivyo, Wabunge mtapendelea ufugaji lakini mnashindwa kuelewa kuwa hao wafugaji sio wote ni wafugaji wengine wanatumika. Hivyo, elimu ya wafugaji itolewe na wenyewe wafunguliwe kuwa wengine wanatumika ndiyo maana unaona ujangili unaingia ndani ya mbuga kwa kupitia hao wafugaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sina mengi sana, nawashukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chumi, wajiandae Mheshimiwa Mwanne Mchemba na Mheshimiwa Kamala.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na pia niishukuru Wizara, watendaji kwa ujumla na niwashukuru zaidi kwa huu mzigo, nimeukuta pale kwenye *pigeon hole* yangu, una *documents* za kutosha, utaendelea kuniongezea ufahamu na kujihabarisha zaidi kuhusu Sekta hizi za Maliasili na Utalii, kwa hiyo, nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi, napenda mchango wangu u-base kwenye *statement* ifuatayo; kwamba *conservation has to take into consideration the livelihood of the people, so it is conservation with development*. Katika *thinking* za zamani ilikuwa inaonekana kwamba binadamu katika viumbi hai ndiye anayeongoza kwa uharibifu wa mazingira na masuala mazima ya hifadhi.

Baadaye *thinking* hizi zimeendelea kubadilika na kumfanya binadamu awe *part and parcel* ya kutunza mazingira na hifadhi zetu kwa namna ambayo itamfanya awe shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini binadamu alikuwa *destructive*? Kwa sababu kimazingira, kimahitaji, alikuwa analazimika kutafuta namna ya kujikimu lakini katika kutafuta namna ya kujikimu ikawa inamsababishia awe ni mharibifu wa mazingira. Ndiyo maana *conservation* ya sasa tunasema *conservation with development*, maana yake ni kwamba utunzaji wa mazingira lazima uendane na uzingatie pia maisha ya watu. Huwezi ukasema unatunza mazingira halafu maisha ya watu yanaendelea kuteketea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano. Juzi nilitoa kilio cha vinyungu hapa, huwezi ukasema maisha ya watu halafu unawazuila wasilime kitu ambacho ndiyo maisha yao au unawazuia wasifuge kitu ambacho ndiyo maisha yao. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema *conservation* lazima iwe *with development*, tusi-focus tu kwenye *conservation* tukaacha watu wanaanza kuangamia. Sasa tutakuwa tuna-*conserve* kwa ajili ya nani ili aweze kuishi? Kwa hiyo, msingi wa mchango wangu ningependa usimame katika msimamo au falsafa hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza na naanza kwa masikitiko kwa sababu mambo mengine ni ya kushangaza, lakini unashangaa halafu unaendelea mbele na safari na maisha. Mimi yanapokuja ya kusikitisha kutoka kwa wananchi wangu wa Mafinga hakika siwezi kukaa kimya, lazima niyasemee. Watu wa Iringa, Mafinga, Mufindi, Njombe na Kilolo, wanaongoza na wana mwamko mkubwa wa kupanda miti, ndiyo hiyo tunasema *conservation with development*, lakini kutoka kusikojulikana Serikali inakuja inaanza kutoa maelekezo ambayo kimsingi yanakwenda kinyume kabisa na hii tunayosema *conservation with development*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nina karatasi hapa na bahati nzuri Mheshimiwa Profesa Maghembe

nilionana naye, inaelezea uvunaji katika misitu ya jamii, watu binafsi na taasisi. Kipengele (b) kinasema, uvunaji utaruhusiwa mara baada ya ukaguzi wa miti kufanyika na kuthibitishwa na Afisa Misitu kuwa miti hiyo imefika kiwango cha kuvunwa. Afisa Misitu wa Wilaya au Meneja Misitu wa Wilaya atapima kipenyo cha mti kabla haujaangushwa. Mwananchi huyu ambaye amejipandia miti yake, ametafuta miche yeye kusikojulikana, leo hii anapangiwa lini avune mti wake. *This cannot be accepted at all!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtu anapokwenda kuvuna miti yake ana shida zake, mwingine mtoto amekosa mkopo anataka aende shule, mwingine ana mgonjwa hospitali anataka akamhudumie, wewe unamwambia kwamba eti kwanza mpaka Afisa Misitu aridhie. Kwanza hiyo capacity ya hao Maafisa Misitu, hata juzi tumelalamika hapa, je, hao Maafisa Misitu tunao wa kutosha wa kuweza kufanya hiyo kazi? Mtu yuko Mapanda, Usokani, Luhunga, Bumilayinga, Luganga, Afisa Misitu atawezaa ngapi kwenda kufanya kazi hiyo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo kama hili naomba baadaye Waziri anapohitimisha atupe msimamo wa Serikali. Hatuko tayari kupangiwa lini tuvune miti ambayo tumeipanda kwa nguvu yetu, sio miti ya Serikali, ile ni miti yetu na tunavuna sisi kwa shida zetu wenye. Juzi ilikuwa vinyungu, leo kwenye miti, yaani mnataka mpaka nione kazi ya Ubunge ni ngumu, hapana, sitakubali, jambo linalohusu maslahi ya wananchi wangu nawahakikishia nitawatetea mpaka mwisho. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye bei ya magogo, kwa nini sisi Taifa letu linawajali wawekezaji wa nje kuliko wa ndani? *MPM* wanauziwa magogo nusu ya bei, sisi wawekezaji wetu wa ndani wanauziwa kwa bei ya juu. Mheshimiwa Waziri mwaka jana ametoa maelezo ambayo bado hajani-*convince*, naomba mwaka huu anipe sababu, kwa sababu kama *point* ni *investor* na huyu wa ndani naye ni *investor*, naye anunue kwa nusu ya bei kama yule ambaye ametoka nje. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumzie kuhusu utalii. Mimi nimesema mara nyingi, utalii bila matangazo ni bure, nina takwimu hapa. Uganda ambao sisi tunaona kwamba si washindani wetu kwa sababu tu sisi tuna vivutio vingi kuliko watu wengine duniani baada ya Brazili, katika bajeti yao ya kutangaza mwaka jana wameweka dola milioni nane, Rwanda dola milioni 11, sisi dola milioni mbili, tutavuna kweli kutoka kwenye sekta hii? Kama hiyo haitoshi, maana nimelinganisha na Rwanda na Uganda, Kenya mwaka jana kwenye *Expo - Italy*, yale maonesho ya barabarani ya miezi sita, bajeti walio tenga ni *3.9 million dollar*, onesho hili moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bila kuwekeza kwenye kutangaza hatuwezi kuvuna, tutabaki tunajisifia sisi wa pili baada ya Brazil. Ni lazima tuiwezeshe *TTB* kwa vitendo. Kwa sababu ukienda hata kwenye *TDL* inasema kwamba kulingana na *GN.218*, *TANAPA* na Ngorongoro wataipa *TTB* asilimia tatu ya mapato au makusanyo yao, lakini sijui kama inaenda na kama inaenda sijui kama inafanya kilichokusudiwa. Naomba tuongeze nguvu katika jambo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya utalii lazima kwa namna yoyote *i-take into consideration* maoni ya wadau wengine na hasa sekta binafsi, vinginevyo itakuwa lawama hizi za *VAT*. Serikali inasema kwamba *VAT* haijakuwa na athari, wadau wanasema imekuwa na athari lakini kama wangehusishwa kutoka mwanzo maana yake ni kwamba wote tungakuwa *on the same boat*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mpango wa matumizi bora ya ardhi. Haya yote tunayoyasema ndugu zangu, Serikali peke yake haiwezi, katika kila jambo lazima ifanye ushirikishaji na inapogusa maisha ya watu lazima sisi viongozi wa kuchaguliwa tushirikishwe. Bila kuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi tutakuja wa vinyungu tutalalamika, atakuja Mheshimiwa Doto Biteko wa wafugaji atalalamika, atakuja mtu wa tembo atalalamika. Kwa hiyo,

kwa vyovoyote lazima tuwekeze katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Menyekiti, tumeambiwa juzi *population* ya Vietnam ni milioni 91, eneo lao ni 360,000 *square kilometers*, *population density* watu 255, sisi *per square kilometer* watu 57, Singapore *per square kilometer* watu 7,987 hawajawahi kugombana wala hawajawahi kudhuriana kwa sababu wamekuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi. Sasa ili hili lifanyike siyo tu la Mheshimiwa Profesa Maghembe peke yake, ni la Wizara ya Ardhi, ni la TAMISEMI, ni la Wizara karibu tatu au nne, tano. Kwa kufanya hivyo, tutaondokana na haya matatizo kwa sababu *square kilometers* ni zilezile lakini idadi ya watu inaongezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumuuliza Mheshimiwa Profesa Maghembe, hivi ile *Embassy Hotel* ni gofu tu hatuna mpango wowote? Namba mbili, yule mjisii aliyeko Ujerumani hatusemi kwamba arudi, je, hakuna namna ambayo sisi tunaweza tuka-*benefit* kutookana na yule Mjisii? Wajerumani naambiwa wako tayari kushirikiana na sisi kujenga *historical site* na hoteli pale mjisii alipotoka lakini je hatuwezi... (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwanne Mcemba ajiandae Mheshimiwa Kamala.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara hii kwa uchungu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kwa mara nikisimama hapa huwa nasikitika, nasikitika sana kwa kuusahau Mkoa wa Tabora. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya. Mheshimiwa Waziri mimi nina sababu ya kumpongeza. Mwaka 2006 alifanya kazi

ambayo Tabora hawatamsahau, nataka nimkumbushe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Chuo cha Nyuki Tabora, chuo hiki kiliondolewa kikapelekwa Arusha. Mwaka 2006 nilimwomba sana Mheshimiwa Waziri na mimi nilikuwa Mbunge na yeye wakati ule alikuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, akakubali akakirudisha. Pamoja na kurudisha mimi nikawa Mwenyekiti wa Bodii, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, tangu 2006 hakuna mabadiliko. Nilombwa sana ukarabati wa jengo la utawala ambalo lilikuwa na maabara ndani yake, jengo hilo limejengwa tangu 1949, kwa hiyo ujue umuhimu wa chuo hicho tangu Mkoloni. Mimi simlaumu, inawezekana wataalam nao wana matatizo na Tabora. Kupeleka Chuo cha Nyuki Tabora kulikuwa na sababu za msingi sio upendeleo, kule tunarina asali yaani sisi ni wafugaji kabisa wa nyuki na Tabora kuna miti ambayo inaitwa miombo ambayo ina maua mazuri, lakini nashangaa bado kinapigwa danadana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora kuna asali ya nyuki wadogo kwa hiyo wanapokitangaza Chuo cha Nyuki cha Tabora maana yake unatangaza na biashara ya asali lakini wameondoa, hakuna ukarabati wowote. Nimeangalia kwenye kitabu hapa. Mwaka jana ilitengwa shilingi milioni 500 lakini mwaka huu shilingi milioni 200 lakini ni pamoja na Chuo cha Misitu Arusha. Sasa hapo sijajua kama kweli Tabora watapata siyo rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la kusikitisha sana na ambalo linauma, tulikuwa na *TAWIRI*-Tabora, kituo cha wataalam wa utafiti kuhusu nyuki na mizinga ya kisasa yenye tija, nacho wamekiondoa wamekipeleka Arusha, hivi Waziri anajua hilo? Kwa hiyo, nimekuja mwaka huu nianze tena kumwomba kituo cha utafiti kirudi Tabora, hivi inawezekana? Nimwombe Mheshimiwa Waziri, namheshimu na najua kazi anayoifanya lakini kuionea Tabora nachukia sana, hiyo itasababisha na mimi nimchukie. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hilo tu mpaka gari imeondolewa imapelekwa Arusha, Waziri ana habari hiyo? Watafiti wa *TAWIRI* wako pale lakini wameondoa mpaka komputa. Mimi nilienda wakati ule kutembea nikakuta wanafunzi wa Arusha wanakuja kuchukua *practical* Tabora. Nikauliza swali humu ndani, hivi inakuwaje gharama hii, wanataka Arusha wanakuja Tabora? Wameacha kabisa na kikitangaza kwani miaka ile walikuwa wanakuja watu kutoka Ethiopia, Zimbabwe kujifunza sasa hivi wamewaondoa, sababu ni nini, hawaitaki Tabora? Leo nimwombe Waziri anisaidie kwa nini wanaidharau Tabora na kwa nini wanahamisha vitu viliviyowekwa Tabora kupeleka Arusha? Wote tuhamie Arusha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kitabu hiki hiki cha bajeti hela za ukarabati zimeenda Njiro lakini Tabora hakuna, ukisoma humu unaona kama ukarabati upo lakini haupo. Naomba Waziri akija kuhitimisha alizungumzie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna wazabuni wanadai hebu aangalie hilo ni haki yao lazima walipwe. Wanadai madai yao ya 2016, Waziri akisimama hapa lazima aseme kitu chenye uhakika, naomba afuatilie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nahamia Malikale kwenye suala zima la utalii. Watu wanaidharau Tabora lakini ina kumbukumbu nydingi. Ukizungumzia utalii Tabora kwamba haupo, zamani nilikuwa silalamiki sana kwa sababu miundombinu ilikuwa hakuna, leo Rais kaleta ndege kwa hiyo lazima niseme ili vile vivutio ambavyo wamevisema kwenye taarifa ya Kamati na yeye mwenyewe amesema kwamba tujitahidi ila sijui lugha ya kwenda kuongelea kutafuta watalii kwa sababu ingekuwa kama kuna sehemu ya kwenda kujifunza mimi ningeenda kutafuta watalii ili waende Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora kuna kumbukumbu ya Livingstone na Stanley na ukiongelea Tabora unaongelea na Kigoma-Ujiji, hivi navyo siyo vivutio hivyo? Tabora kuna eneo ambalo alikaa *Livingstone* walipokutana na *Stanley*

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wakitokea Kigoma eneo la Kuyara, nayo ni kivutio cha utalii. Nimwombe Waziri atume *delegation* yake iende ikaone halafu baada waitangaze. Pia *Livingstone* alikaa Ujiji karibuni miaka 27, njia aliyopita ni Tabora na aliacha alama. Jamani naomba niwarudisheni shule ili mjue historia ya Tabora. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora kuna majengo ya Wajerumani kama ilivyo Amboni (Tanga), kuna kumbukumbu ziko pale lakini nani atazisemea? Leo bajeti ya Wizara ya Maliasili imeanza leo na mimi naitangaza Tabora kama sehemu ya utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna njia ya watumwa kwa sababu ilikuwa watumwa wakitoka Kigoma wanakuja Tabora wanakwenda Bagamoyo. Juzi tulipokuwa kwenye semina, Tabora halmo kwenye hiyo kumbukumbu ya Malikale, sasa leo naitangaza Waziri aikumbuke. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hilo tu, tuna kumbukumbu nzito sana katika dunia hii ya Hayati Baba wa Taifa. Wanafunzi wanasoma shulenii lakini hata utalii wa ndani unatosha kuwapeleka Tabora. Baba wa Taifa alisoma *Tabora Boys*, akafundisha Mirambo lakini wakati wa kupigania usalama wa nchi na uhuru umeanzia Tabora, jamani hii nayo inataka mtu kwenda shule kwa ajili ya kuitangaza tu Tabora? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini uhuru huo ulisaidia pia kuwa na karata tatu za kuunda Serikali pale Tabora...

MBUNGE FULANI: 1958.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mwaka 1958, wenzangu wananiunga mkono, hiyo historia inatakiwa isomeke. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pale Tabora kuna shule ya msingi inaitwa *Town School*, ndipo alipokuwa anakutana

na Wanyamwezi wakarimu sana, wanamfundisha, anajificha... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kamala ajiandae Mheshimiwa Profesa Tibaijuka.

MHE. BALOZI. DKT. DIODORUS B. KAMALA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja muhimu iliyo mbele yetu. Hoja ya kwanza niliyonayo leo ni kuhusu Wakala wa Huduma za Misitu. Wakala huyu anajitahidi kufanya kazi yake na kwa kweli tatizo kubwa linalojitokeza ni kwamba kwa muda mrefu alikuwa likizo lakini baada ya kuhimizwa na baada ya Wakala huyu kwenye mipango yake kuona kwamba ni muhimu sasa waanze kuweka mipaka ya kuonyesha eneo lao lakini kubwa linalojitokeza hapa ni mabadiliko ya tabianchi, lazima sote tukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani Misenyi kwa muda mrefu sana hali ya hewa ilikuwa nzuri. Hakuna mtu aliyefikiria kuna sababu ya kwenda kulima kwenye maeneo ya matingatinga, hata hawa wenzetu wa huduma za misitu hawakuona umuhimu wa kubainisha mipaka kwa sababu kila mtu alikuwa na eneo la kutosha, kwa hiyo kulikuwa hakuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na mahitaji ya maeneo kuongezeka, sasa kila mmoja anajitahidi kuweka mipaka yake. Watu wa hifadhi wanajitahidi kubainisha mipaka ya maeneo yao kuonesha wanaanza wapi na wanaishia wapi lakini na wananchi pia wangependa wawe na maeneo ya kutosha ya kuchungia mifugo yao. Wananchi wanafuata maelekezo ya viongozi ambapo tumezoea inapokuja wakati wa ukame wanawahimiza waende kulima kwenye maeneo ya matingatinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia pale Wilayani Misenyi, kuna hifadhi inaitwa Lusina; hii inagusa Kata za Bugandika na Bugorora; kuna hifadhi inaitwa Kikuru; hii inagusa Kata za Buyango na Ruzinga, lakini pia kuna hifadhi nyingine kubwa tu inaitwa Minziro. Hifadhi zote hizi zina changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi na changamoto ya hawa wenzetu wa hifadhi kuanza kubainisha maeneo ya hifadhi zao na kwa kufanya hivyo unakuta wananchi wanaona wameingiliwa maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa ya Mheshimiwa Waziri utagundua kuna kipengele kinasema kuna vijiji 228, hii ni kwa nchi nzima na maeneo mengine, vipo ndani ya hifadhi na vijiji 157 vimeshasajiliwa. Sasa kama kwenye kitabu chake cha hotuba Mheshimiwa Waziri anatambua vipo vijiji 228 ndani ya hifadhi katika maeneo mbalimbali Tanzania na anabainisha kwamba vijiji 157 vimeshasajiliwa maana yake alichokuwa anajaribu kutueleza Mheshimiwa Waziri ni kwamba kuna migogoro hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ikishatokea kinachotakiwa ni kuitafutia ufumbuzi. Hatuwezi kuacha migogoro hii ikaendelea kwa sababu ukiacha na wewe unakuwa sehemu ya mgogoro. Kwa hiyo, nimwombe Profesa najua amebobeaa katika masuala haya, najua ana nia nzuri, najua wataalam wake kupitia hizi hifadhi za misitu wana nia nzuri pia basi tushirikiane kuhakikisha kwamba migogoro hii tunaipatia ufumbuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nishukuru wenzetu wa *TANAPA* kwa sababu nilipoteuliwa mara ya kwanza kuwa Balozi, maana kazi nyingine hizi hujasomea, nakumbuka baada ya kuteuliwa Mheshimiwa Rais akatuambia Ubalozi husomei nenda tu mtafanya kazi. Nikauliza wenzangu pale tunaanzia wapi? Tutakubaliana kwamba hebu tuwaombe *TANAPA* ambao wanasimamia hizi hifadhi watupe angalau mafunzo kidogo, tukienda nje huko basi tuweze kuitangaza Tanzania kwa sababu

huwezi ukatangaza kitu usichokijua. *TANAPA* wakatupangia *route* nzuri...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge.

MHE. BALOZI. DKT. DIODORUS B. KAMALA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* wakatupangia safari nzuri, tukaenda *Northern circuit* lakini pia wakatupeleka *Southern circuit*, tukatembelea Ruaha ni nzuri kweli kweli, tukaenda Katavi kule tukajifunza mambo mengi. Nakumbuka tulikuwa na Mabalozi mbalimbali, Mheshimiwa Balozi Batilda, Mheshimiwa Balozi Marmo, Balozi aliyeenda Msumbiji, Misri na Mabalozi wengine, kwa kweli tulijifunza vitu vingi kutokana na ziara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoenda kwenye vituo vya kazi tukajikuta kumbe kazi yetu kubwa ni kuitangaza Tanzania lakini huwezi kuitangaza Tanzania usiyojua, ziara ile kwa kweli ilitusaidia sana. Nachukua nafasi hii kuwashukuru *TANAPA* na kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Kijazi kwa sababu nilikuwa sijapata nafasi ya kurudi katika Bunge hili kushukuru. Kwa hiyo, nilienda, nilifanya kazi, nilijifunza na nimerudi na nawashukuru sana kwa kutupeleka maeneo hayo ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali Na.3 la kitabu cha Mheshimiwa Waziri linaonyesha *estimates* za maduhuli kwa mwaka 2015/2016 ni shilingi bilioni 25 lakini ukiangalia *estimates* za mwaka uliofuata ni sifuri. Sasa sijui ni makosa ya uchapaji, huwezi ukawa na makisio sifuri sijui nini kilitokea. Pia ukiangalia hata maduhuli upande wa wanyamapori ni shilingi bilioni 13 kwa 2015/2016, lakini ukiangalia mwaka unaofuata *estimate* ni sifuri. Nimwombe Mheshimiwa Waziri na watalam wapitie ili waweke rekodi vizuri ili vitabu viweze kueleweka isije ikaonekana kwamba mwaka huu unapata shilingi bilioni 25 mwaka unaofuata unapata sifuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa kazi ambayo wanaifanya najua

kutangaza utalii ni kazi ngumu. Niseme jambo moja, nimesikiliza kwa makini hotuba ya wenzetu wa upinzani, hili suala la Loliondo limechukua muda mrefu na naomba niseme tusipoangalia, hatutapata ufumbuzi kwa sababu kuna wadau wengi wanaoshiriki kwenye changamoto ile lakini nzuri na mbaya zaidi kuna na hela nyngi pia. Sehemu yoyote ikishakuwa na hela nyngi zinazunguka, usipokuwa makini huwezi kupata ufumbuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *OBC* inaongelewa sana lakini nyuma ya *OBC*kuna wadau wengine pia ambao na wao wanachochea mgogoro huu. Ukitumia nguvu nyngi kuzungumzia *OBC* ukasahau wengine kama Wamarekani na watu wengine, ndugu zangu ule mgogoro wa Loliondo utaendelea miaka mingi kwa sababu kuna hela zinazunguka na watu hela wanazihitaji na hakuna anayependa kusema kwamba kuna hela. Kwa hiyo, ule mgogoro tusipokuwa makini utaendelea miaka nenda miaka rudi, watakuja Mawaziri hapa, tutawajibisha, tutasema Waziri hapa umechukua mlungura ondoka, tutafanya kile na kile lakini Loliondo itaendelea kuwa Loliondo miaka nenda, miaka rudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa pale *Brussels*, ndani ya Bunge la Jumuiya ya Ulaya ilitolewa hoja nzito na Tanzania wakatuazimia pia, hoja ile ilikuwa inahu *land grabbing*. *Land grabbing* ni hoja mpya na ya kisasa ambayo wanasema unamnyang'anya mtu ardhi unaenda kutumia kwa maslahi yako au kwa vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ile ya *land grabbing* ilipokuja, Bunge la Jumuiya ya Ulaya likaiazimia, likaleta hoja, likasema Mheshimiwa Balozi jibu. Balozi kazi yako ya kwanza lazima utetee nchi yako, kwa hiyo, unapoambiwa jibu, majibu unayotakiwa kutoa ni yale ya kutetea nchi yako siyo jibu lingine. Nilipopitia zile hoja zilizotolewa ambazo ni nyngi sana kuzipitia kwa sababu hapa Tanzania tuna zaidi ya mashirika 70 yote yako Loliondo na kila shirika lina taarifa na kila shirika linaongelea kivyake kuhusu masuala ya *land grabbing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiacha tatizo tunaloliona Loliondo ndiyo wanasema kuna Loliondo nyingine kubwa inatengenezwa na Bunge la Ulaya limeshapitisha azimio. Tusipojpanga sasa, siku azimio likirindima ndani ya Bunge hili, ndugu zangu hatutaweza kupata majibu, tutaanza kutafutana mchawi ni nani, ndiyo maana nasema mapema ili tujipange. Yale majibu niliyotoa nikiwa Balozi, ukiwa Balozi unazungumza kama Balozi, nikija humu siwezi kuzungumza kama Balozi, nitazungumza kama Mbunge na hiyo itakuwa lugha tofauti kabisa, ndiyo maana nawaombeni ndugu zangu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Tibaijuka ajiandae Mheshimiwa Gibson Blasius Ole-Meiseyeki.

MHE. BALOZI. DKT. DIODORUS B. KAMALA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adimu. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuwapongeza kwa kazi nzuri ambayo mmeefanya, mimi sikuwepo nilipata changamoto za kiafya lakini *Alhamdulillah* sasa nimerejea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi mama hapa mimi kama Mbunge wa Muleba Kusini iliyopo katika Mkoa wa Kagera. Kama mnavyojua mapori ya hifadhi na sehemu ambazo zina mvua za kutosha ziko katika Mikoa ya Kagera na Geita, kwa kweli tuko katika hali ngumu. Mheshimiwa Waziri na timu yake nawapongeza lakini kwa sababu ni mwanafunzi mwenzangu, *research methodology* tulisoma wote, leo naomba aniruhusu niende kiutafiti. Nina nyaraka 10 (*annexes*) ambazo nitaomba Mheshimiwa Waziri azifanyie kazi asije akaniweka katika hali ngumu ya mimi kuondoa shilingi hapo kesho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii tuna migogoro ya wakulima na wafugaji, asilimia 28 ya nchi hii sasa hivi ni hifadhi. Mheshimiwa Profesa ambaye anafanya kazi nzuri, anatambua kabisa kwamba neno la Kiingereza la kutumia hapa ni *untenable*, kwamba hali hii haiwezekani kuendelea kama ilivyo *business as usual*, asilimia 28 ya Tanzania inaendelea kuwa hifadhi wakati watu hawana mahali pa kulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kinadharia, haiwezekani Wabunge wengi wamechangia hapa na wote tunaelekea huko haiwezekani, *something has to give way*. Haiwezekani kwa sababu watu wameongezeka, sasa naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba Mheshimiwa Waziri Nchemba tarehe 22 Desemba, 2015 mara baada ya kupewa jukumu la kuongoza Wizara ya Mifugo alikuja Ngara akakaa na wananchi, akaingia makubaliano, akaleta faraja, akatupa matumaini naomba nyaraka ya kwanza *appendix no. 1* Waziri airejee, sina muda wa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nyaraka hii, kilichotokea ni nini, Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye tunajivunia sana sisi akinamama, Samia Suluhu akaandika barua ambayo naomba niikabidhi kama *appendix no. 2* akiagiza kwamba mifugo iendelee kuwa pale ilipo mpaka hapo Serikali inajipanga. Sisi tukawaambia wananchi kwamba Serikali yetu sikivu inayoongozwa na Jemedari Dkt. Magufuli haiwezi kuwaacha wafugaji hoi, kwa hiyo barua ya Mheshimiwa Makamu wa Rais ipo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka *telegraphically*, tarehe 11 Oktoba, 2016 Mheshimiwa Waziri huyu Profesa ndugu yangu, akatoa tamko hapa akawaambia kwamba kulingana na maelekezo ngazi za juu basi wafugaji wabaki pale walipo, wakati anajipanga, naomba niikabidhi iko hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naogopa maana dakika kumi siyo nyingi lazima niende *telegraphically*. Sasa kilichotokea na kinachoendelea sasa hivi *from nowhere ile*

Kamati ya Serikali iliyoundwa ya kutafuta maeneo mbadala kwa ufugaji, mara wakaibuka kuwafukuza wafugaji kutoka kwenye mapori ya akiba. Hii ni *contradiction* kabisa na kwa kuokoa muda natoa nyaraka hapa kumsaidia Ndugu yangu Profesa Maghembe aangalie mambo yaliyojiri. Kwa sababu yeche na mwenzangu na jirani ya jirani yangu hapa Mama Kilango wanatoka Upareni. Nimeleta hapa picha za ng'ombe wa Ankole wanavyofanana wanapopita kwenye shamba, hakuna linalobaki. Huwezi kusema una- *support* kilimo kama mifugo itatolewa kwenye akiba kiholela huwezi, *it is not possible.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mkulima miezi sita amehangaika, lakini kundi la ng'ombe likipita *in five minutes* shamba limekwisha, kwa hiyo ndiyo hali halisi. Kwa hiyo, tatizo hili siyo tu la wafugaji ni tatizo la wakulima, kwa sababu wakulima wale ng'ombe watamaliza hayo mazao yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuokoa muda kinachofuata sasa, mapendekezo ya wafugaji wamekaa na Serikali, Mheshimiwa Waziri anajua hilo. Serikali kwa ujumla Serikali inayofanya kazi ya matumaini sasa inakuwaje hiki kitu kinatuhinda wakati tunakwenda kujenga *standard gauge* na vitu vingine vikubwa. Kwa hiyo, nataka kuweka hapa mapendekezo ya wafugaji wenyewe, *let us take it from the horse's mouth*, wafugaji wenyewe wanasemaje, wafugaji hawa wanatii Serikali, hawakaidi Serikali lakini hawawezi bila ardhi, kama huna ardhi huwezi kufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala la kuwapatia wafugaji ardhi, *appendix zinaendelea ninayo ya nane hapa ambayo na yenyewe Waziri ataifanyika kazi*. *Apppendix* hii inaonyesha kabisa mapendekezo na wafugaji wanavyohangaika, wana vijana makini, tunahangaika nao sisi, sasa inaonekana Mheshimiwa Waziri anakuwa mbali hawamfikii kwa urahisi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kama yote haya hayakutosha, tunavyozungumza sasa hivi wafugaji

wameporwa ng'ombe wao kwenye mapori. Kwa kumsaidia Waziri katika kuja kujibu kesho, mimi msimamo wangu unatoka kesho baada ya kusikia majibu na nyaraka zote hizi za Kiprofesa nilizoweka mezani hapa. Huyu siyo kwamba ni Profesa pia ni *my classmate, he knows what I am talking about*. Suala hili ni nyeti, suala hili ni la Usalama wa Taifa naomba lifanyiwe lifanyiwe kazi. Ng'ombe 2000 wameporwa maporini, mtu msanii mmoja anasema anaendesha eti mnada maporini. Sasa mnada nani ananunua ng'ombe porini? Wanauziana wao kwa wao, *It is totally unacceptable* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli haya mambo anataka tuseme ukweli, nami ninasimama hapa kwa imani kabisa kwamba Serikali haiwezi kushindwa kitu hiki. Mitandao ya Ma-game wapo kule kwenye mapori wanaendesha minada ya kisanii wanauziana wao, naomba Serikali, Mheshimiwa Waziri Serikali watuletee taarifa hawa ng'ombe wamewauza wamemuuzia nani na sasa hivi hao ng'ombe wapo wapi, maana yake itabidi wawapeleke, siyo wapo kwenye misitu hiyo hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema hivi sitaki *sensation* nimeleta *facts* hapa kwa imani kabisa kwamba Serikali itazifanya kazi. Kwa sababu, bila kufanya hivyo *you forget* kuzungumza mambo ya wakulima na wafugaji, viwanda vitatoka wapi, viwanda vyta ngozi kwa mfano, kama huna mifugo huwezi kuwa na viwanda vyta ngozi! kwa hiyo lazima tuwawezeshe wafugaji wetu, wakulima wamewasukuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hapa katika Jimbo langu watu wengi hata mifugo hawana, lakini jirani zangu kutoka Geita, kutoka Simiyu wako kule na ni Watanzania wana haki ya kuwa kule. Sasa wanaendesha propaganda oo, unajua yule Mama Tibaijuka ni Munyamulenge na yeche ana mifugo, maneno ya rejareja kutukatisha tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wenzetu Rwanda kule kwa Kagame ni ng'ombe 10 hakuna mchezo. Kule kwa Mseveni anauza maziwa Dubai, wenyewe wameshapiga hatua kwa nini, *because of land tenure*, wametoa maeneo ya kudumu kwa hiyo wana *Small Ranching Associations*. Hicho ndicho kilio chetu naomba Serikali itusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndio msimamo wangu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu twende *conceptually tuisupport* Serikali hii kwa kuleta *facts*, wale ambao wanalinda maslahi yao kwenye ma-game na kuniita majina, mimi hayo majina hayanitishi, yaani wanasema ukijaribu kutetea hoja wanasema huyu ana maslahi binafsi. Kwa hiyo, inakuwa *characterization* watu wengi wanaogopa. Watu wengi wanaogopa kusimamia jambo hili kwa kuogopa kwamba watasema hawa ndiyo wana mifugo, lakini nataka kusema kwamba tafadhalii sana hali ni tete, na ni suala la Usalama wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi za ufugaji tuondokane na migogoro; nimezungumzia Mkoa wa Kagera lakini *the same applied to* sehemu nydingi Tanzania nzima. Naomba kuwasilisha nashukuru sana, kesho ndiyo nitajua baada ya kumsikiliza Profesa mwenzangu kama naunga mkono hoja au naondoka na shillingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Gibson, jiandae Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

MHE. GIBSON B. OLE-MEISEYEKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, labda tu nirekebishe majina yangu kidogo, naitwa Gibson Blasius Ole -Meiseyeki, ni gumu kidogo jina la Kimasai hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, kwa sababu ya muda ni mfupi nitazungumza *in a bulletin form ili* Profesa pale aweze kunipata kidogo. Nina-*declare* tena *interest* kwamba

mimi ni mdau wa utalii wa zaidi ya miaka 15 ya utalii wa picha lakini ni mwekezaji pia kwa maeneo fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamezungumza na tulishauri Serikali kwenye bajeti mwaka jana kwamba *VAT is going to kill us* na hasa kwa namna ambayo Serikali ilikuwa imeileta, ililetta ghafla na ikaanza *implementation* pale pale. Kwa hiyo, ilituathiri na niseme tu kwamba *introduction* ya VAT ilishusha sana biashara yetu ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *statistics* ambazo Mheshimiwa Profesa pale ametupa, pengine ni wale Watalii ambaao wanakuja kusaka kazi Tanzania lakini siyo wale Watalii wa *Photographic Safari's* kama ambavyo tunawategemea. Wakati mwingine anapotuletea *record* atuambie wallokuja kutafuta kazi ni hawa ambaao wao wanawaita watalii na wale wanaokuja kwa lengo la kutembelea mbuga zetu watupe *recordzake* pia kwa sababu wanatupotosha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kuleta *VAT* biashara ya Utalii ilianguka na mbaya zaidi iliharibu sana *image* ya Taifa letu katika *forum* za Kimataifa. Mheshimiwa Waziri wao hasa ndiyo wanaorudisha nyuma jitihada za *TTB* nirekebishe kutoka mchango wangu wa mwaka jana, tumegundua kwamba *policy* za nchi ndizo zinazoshusha au zina-*demoralize* kazi nzuri ambayo *TTB* inafanya ya kuitangaza hii nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wageni wanapokuja hapa Tanzania hawawi *treated* katika ile namna ambayo inapaswa kuwa. *Hospitality* yetu ni *poor* sana pia tozo hizi ambazo ni za kuibuka ibuka halafu mnaanza ku-*implement immediately*, zinashusha *image* ya nchi Kimataifa. Wakienda kwenye *forum* mbalimbali za Kimataifa wataona jinsi gani ambavyo watu wa utalii wameizungumzia Tanzania, wameizungumzia *negatively*. Sasa hiyo inasababisha tena baadaye tuanze kutumia fedha zilezile ambazo

wamewanyang'anya kwenda kufanya utangazaji mwingine ili kuweza ku- *stabilize* wageni ambao wanatembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunapoleta tozo hizi tuwe na *grace period* maana VAT watu hawakuikataa lakini ku- *introduce* leo na kuanza ku -*implement* kesho that was a problem na anafahamu Mheshimiwa Profesa Maghembe alishapambana sana na waongoza utalii miaka ya nyuma mlivyokuwa mnabadiilisha rates katikati ya msimu. Wana-*introduce* wakati ule Ngorongoro *crater service fee*, wakataka ku- *impose immediately*, wakapambana na waongoza utalii wakabadilisha, lakini walipoleta VAT *this time* wali-*implement immediately*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ilituletea shida sana na ikalazimika kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Wawekezaji wakalazimishwa wao ndiyo walipe hizo fedha siyo kumchaji mteja ila makampuni ndiyo walitoa fedha mfukoni kuwalipa VAT. Wale watu mliwanyang'anya fedha kwa sababu hatukuwachaji *clients*, wako *sensitive*sana hawa waongoza utalii unapoleta mabadiliko ya gharama katikati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwelyekiti, nizungumzie pia suala la *entry fees* kama nilivyosema mimi ni Mwekezaji na ni muathirika, lakini hapa nazungumzia pia *in a National perspective* kwamba, *Introduction* ya *single entry*lengo lenu ilikuwa hasa kuwakandamiza wawekezaji wadogo ambao hawana ubavu wa kuwekeza ndani ya hifadhi. Kwa hiyo, mnawabeba wale wakubwa ambao wamewekeza hoteli zao kubwa ndani ya hifadhi, wanaenda kuwaminya wale wadogo wanyonge ambao wamewekeza kwenye vijiji vyetu na wanasaidia sana maendeleo kwenye vijiji kwa kuwalinda watu wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu waka-*review*tena hiyo *single entry system* kama alivyozungumza Mheshimiwa Marwa Ryoba asubuhi, inawaumiza sana na sasa hivi wale watu wote waliowekeza nje ya hifadhi wanashindwa kufanya

biasara. Kwa sababu imekuwa ni gharama sana kwenda kumlaza mgeni nje kuliko kumlaza ndani. Mjue kwamba hakuna mgeni wa utalii ambaye anapenda kulala nje ya hifadhi. Wamefanya hivyo tu ile ilikuwa ni mpango wa Serikali kwamba kwa sababu changamoto ya vitanda vyta kulala wageni ilikuwa ni kubwa sana miaka ya nyuma, Mheshimiwa Maghembe anakumbuka alikuwa ni Waziri wakati ule miaka ya 2000. Kulikuwa na changamoto kubwa ya vitanda vyta kulala wageni, kwa hiyo, kukawa na *a sort of kuwahamasisha* watu wajenge *tented lodges* nje ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wamejenga wamewekeza, *all of a sudden* wanafanya gharama iwe kubwa sana kuwalaza wageni kule nje au wana wa-equate, wanataka hao watu wawe na gharama zinazofanana, siyo sahihi. Hiyo kitu *ime-affect* sana uwekezaji hasa wa watu ambao wana mitaji midogo. Kwa hiyo, ningeshauri ni vema tukarudi kwenye zile tozo za masaa. Kwa sababu, haiwezekani mtu anayelalala ndani ya hifadhi alipe kidogo na yule anayelala nje alipe zaidi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia suala la Ikoma, kwa hiyo hebu waka-review hapo hizi *fees* ziwe *timely*, iwe ni kwa saa, kama ni masaa 12 iwe ni masaa 12 nje na ndani, kama ni masaa 24 iwe ni hivyo nje na ndani. Siyo kwamba anayelala nje alipe mara mbili, wanafahamu kabisa kwamba jiografia kama alivyosema mwenzangu asubuhi kwamba ili uweze kuingia Serengeti wengi wanatokea Arusha kuingia Serengeti, sasa anapitiliza kwenda kulala upande wa pili wa Serengeti maeneo ya Ikoma. Ameshalipa *park fees* unamwambia kesho akirudi tena akiingia kufanya *full day game drive* alipe tena *park fees* halafu akitoka akirudi tena kesho wakati anaenda Arusha analipa tena, hawa watu wanawabana sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala pia la leseni, wafanyabishara wetu wadogo wenye gari moja, gari mbili, wanawatoza leseni sawa na mwenye magari 400. Hayo nimeyasikia sana Arusha na tunaomba wawe wasikivu wanaposhauriwa. *TATO* ameongea na ninyi mara nyingi, siyo

sahihi kumtoza mtu leseni dola 2000 sawa na mwenye gari moja na mwenye magari 20 ama 200 wanatozwa *fee* ambayo ipo sawa, siyo sahihi. Kwa hiyo waingalie na hiyo, waje na utaratibu ambao utawatenganisha mwenye mengi aliye zaidi na mwenye magari machache aliye kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri pia kwenye Shirika letu la Ndege la ATCL badala ya kujaza zile *Bombardier* ifikirie pia kuleta ndogo kama *LET* zile za kubeba watu ishirini. Hizi ndege ndogo ndiyo zinaweza kusambaza watalii kwenye Mbuga zetu hizi nyingine ndogondogo zilizozunguka nchi hii. Ruaha, Mikumi, Katavi mpaka Gombe kule, lazima tuwe na *feeder planes* zile ndogo ambazo zinaleta watalii kutoka kwenye mbuga na kuleta kwenye viwanja vikubwa, hivyo ndiyo tunaweza kuwasambaza wageni katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naizungumza hii *based on my experience*, ni vigumu sana kumtoa mgeni Serengeti ukampeleka Ruaha, gharama za hizi ndege za binafsi ni ghali sana. Tungependa kama wangeweka ndege kama tatu hivi za Shirika la Ndege la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri ana-*wind up*, ningependa kujua pia ni namna gani alilishughulikia suala la mauaji ya wananchi wangu watano yaliyotekelezwa Arusha mapema mwaka huu. Nataka kujua walishiriki vipi na imefikia hatua gani na nini hatua zaidi ambazo zinachukuliwa kwa Askari wa Mheshimiwa Waziri ambao waliwauwa wananchi wangu watano kwa kuwapiga risasi kama wanyama mapema mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na *incidence* ya Januari watu wanne na mwezi Aprili aliuawa mtoto wa miaka 15 kwa kupigwa risasi nne mgongoni akiwa anaongoza ng'ombe watatu ambao walikuwa pembezoni mwa misitu ya Meru USA kule Arusha. Ningependa kufahamu kwamba walishiriki vipi na ni nini kauli rasmi ya Serikali hapa kuhusiana na mauaji hayo yaliyofanyika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni uvunaji wa misitu na mazao ya misitu kwa ujumla. Tunaomba waondoe *contradiction* iliyopo kutoka Wizara za Kilimo, Ardhi na Maliasili ya namna gani kilimo kinaweza kikafanyika nchini humu. Kwani kuna watu wana mashamba yenye mazao ya misitu miti, sasa mtu anataka kuendeleza shamba lake lakini ruhusa ya kuvuna miti inatoka kwenye Wizarani na kuna urasimu mkubwa sana kwenye ...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, wajiandae Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar na Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo nami nitoe mchango wangu katika Wizara ya Maliasili. Kwa imani yangu ni kwamba Mawaziri wa Wizara hii ni wasikivu, basi haya nitakayoyashauri hapa, pengine yakawa na tija kwao na kwa Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa kujielekeza kwenye Hifadhi ya Selous. Kama ambavyo alivyotangulia kusema mama yangu pale, kwamba asilimia 60 ya Selous iko Liwale. Nami nataka kuwapa historia ya Selous pengine Wabunge wenzetu hamuelewi hii ilikuwa kuwaje. *Founderwa hii hifadhi ya Selous alikuwa ni Fedrick Selous mnamo mwaka 1879. Mwaka 1905 ndipo hili eneo la Selous likatengwa kama eneo la uwindaji. Siyo hivyo tu mwaka 1922 ndipo eneo hili likahifadhiwa kama game reserve.* Mpaka mwaka 1982 UNESCO waliitambua hii kama Hifadhi ya Dunia, hiyo ni historia fupi ya Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sifa hizi zote zilizonazo Selous lakini lango la kuingilia Selous liko Morogoro. Kwa maana ya kwamba ukanda mzima ule wa Kusini kuanzia Rufiji mpaka Lindi hakuna lango la kuingilia Selous. Sasa wana Selous wale walioko Liwale ambao ndiyo

wahifadhi wa kwanza, mimi naamini kwamba wahifadhi wa kwanza wa hifadhi yoyote ile ni wale wanaozunguka hifadhi. Kwa hiyo, Wanaliwale au Wanalindi kwa ujumla wake ndiyo wahifadhi wa kwanza lakini hakuna lango la kuingilia Selous, kwa maana hiyo basi hakuna manufaa yoyote ambayo wanapata wale ya *direct* kwa watu waliopo pale Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri hebu aiangalie Selous na aangalie Kusini, mpaka leo hii Kusini hatuna hoteli ya kitalii wala hata barabara ya kufika kwenye hii hifadhi hatuna. Kama mpaka hata Wazungu nao wenzetu wanaithamini kwa kiwango hicho tunawezaje kushindwa hata kuweka barabara ya kuifikia hiyo Selous? Hili ni jambo la kusikitisha sana hasa kwa watu wa Kusini tunaoizunguka hii Selous. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nijielekeze sasa kwenye mamlaka ya Uvunaji wa Mali za Misitu (TFS). TFS ilivyoundwa na lengo lake na inavyofanya kazi, mimi kwa upande wangu naona ni kinyume chake. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale tuna misitu ya aina mbili, kuna msitu wa Nyera Kipelele huu msitu tumeurithi kutoka kwa wakoloni, kuna msitu wa Hangai, huu ni msitu wa vijiji. Msitu huu ni msitu ambao umechangiwa na vijiji kadhaa moja ya vijiji vichache ambavyo vimechangia msitu huu ni Kijiji cha Ngongowele, Mpigamiti, Mikunya, Lilombe, Kitogoro, Mtawango, Mtawatawa, Mitawa, Namakololo, Makirikiti na Kipule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wote wamechangia kuhifadhi hii misitu lakini kinachoshangaza kwenye Kamati ya uvunaji wa misitu hii, Mwenyekiti ni Mkuu wa Mkoa, Mwenyekiti wa Halmashauri hayumo kwenye Kamati ya Uvunaji, Mbunge wa Jimbo husika hayumo kwenye Kamati ya Uvunaji waliopo kwenye Kamati hii ni Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri, *OCD* na watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu hii imehifadhiwa na wanavijiji nami kama mwakilishi wa wanavijiji simo kwenye

Kamati ya Uvunaji, uvunaji huu unakwendaje? Namwomba sana Mheshimiwa Waziri hebu afikirie muundo wa hii Taasisi ya *TFS* na uvunaji wa *TFS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kwenye *TFS* Halmashauri tunapata asilimia tano ya kile kinachovunwa pale Halmashauri. Naomba sana hata wakati nachangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu nilisema naomba Mheshimiwa Waziri turejeshe hapa hiyo sera ya uundwaji wa *TFS* ili tuongeze angalau tufike hata asilimia 20 ili tunaozungukwa na ile misitu tuweze kunufaika na ile misitu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti katika nafasi hiyo ya *TFS*, elimu kwa sababu kuna Kamati za Vijiji ndiyo wanashughulika na mambo ya uvunaji wa hii misitu, lakini wale wanavijiji hawajapata elimu yoyote na wala hakuna semina yoyote inayowafikia. Matokeo yake kinachofanyika sasa mtu anapata leseni, anaenda kuvuna *cubic meter* 100 na anakata mti akikuta huo mti una pango anauacha, ili uweze kukamilisha mzigo wake maana yake unaacha jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanavijiji wale wanasaidiwa vi? Hakuna elimu yoyote wanayoipata kujua kwamba madhara yanayotokana na ile miti ambayo yule mwekezaji haitaki, ile miti anailipiaje, Halmashauri inapata nini? Matokeo yake Halmashauri tunapata jangwa tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msitu wa Nyera Kipelele ni msitu tumeurithi kutoka kwa wakoloni, mpaka leo hii *harvesting plan* ya msitu ule haijatoka. Nimekwenda pale nimepata kitabu cha mwongozo kinaitwa kitabu cha mwongozo wa uvunaji endelevu. Kitabu hicho kwenye Halmashauri kipo kimoja tu na nimekutajia vijiji zaidi ya 20 ambavyo vina hifadhi lakini kitabu cha mwongozo wa uvunaji endelevu kipo kimoja kwenye Halmashauri. Msitu wa Nyera Kipelele mpaka leo hauna *harversting plan* maana yake ni kwamba huu msitu haujaanza uvunaji, tumeurithi kutoka kwa wakoloni. Sasa hawa ambao wanazungukwa na huu msitu wanufaika na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nijielekeze kwenye Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (*TAWA*). Hii taasisi haina ushirikiano na Halmashauri zetu, kwa sababu leo hii wanasesma asilimia 25 ya mapato ya uwindaji wa kitalii yanaenda kwenye Halmashauri, huu ni mwaka wa tatu, mwaka wa nne, kila tukifungua kwenye Halmashauri pale kwenye mapato yetu haimo, hili pato halilingi. Nimefuatilia mpaka *TAWA*, nikawauliza kwanza nilitaka njue hii asilimia 25 ni ya nini? Sijapata majibu mpaka leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawa watu wa *TAWA* hawawezi kutoa ushirikiano, tena nilienda pale wakaniambia kwamba hii sisi siyo Wasemaji wa *TAWA* nenda kwa Katibu Mkuu. Nimefika kwa Katibu Mkuu wa Wizara sijapata majibu mpaka leo. Tunapata asilimia 25, asilimia 25 ya nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mambo ya utalii; utalii kwenye Halmashauri ya Liwale kuna boma la Mjerumani nilishalisema hapa, lile boma la Mjerumani ni moja ya kivutio cha utalii. Kwa sababu kumbukumbu yote ya vita ya Maji Maji ukitaka kuongelea leo lazima utalikumbuka lile jengo la vita ya Maji Maji. Vilevile tuna kivutio cha utalii kwenye kaburi la Mfaransa, watalii wanakuja kutoka Ujerumani wanakuja kuangalia pale, kila mwaka wanakuja kuhiji, lakini sisi wenyewe tumelala. Kuna kaburi la Bimkubwa wangu mmoja pale Ndapata, watu wanakwenda kuhiji pale lakini sisi wenyewe tumelala hivi vyote ni vivutio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Tanzania tupewe nini na Mwenyezi Mungu ili tuone kwamba tuko duniani. Kama watu wa nje wanaweza kutambua vivutio vyetu vya utalii sisi wenyewe tusivitambue. Mheshimiwa Waziri, najua ni msikiu najua hili ninalolisema ataliskia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba niongelee mgogoro wa Hifadhi ya Selous na Kijiji cha Kikulyungu. Mgogoro huu sasa hivi una zaidi ya miaka 10 na umeshapoteza maisha ya watu wanne, namwomba Mheshimiwa Waziri afanye analoliweza, afike Kikulyungu atumalizie huu mgogoro kati yetu na wahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze sasa katika mchango wa maendeleo unaotokana na hifadhi ya misitu. Mchango wa maendeleo pale kwetu wanasema kwamba ubao mmoja wana utoza sh. 400 kwenye Halmashauri ya Kijiji, gogo moja sh. 1000, hebu fikiria msitu ule unaohamishwa pale, sisi tunaambulia sh. 400! Kwa kweli Mheshimiwa Waziri hizi sheria tunaomba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar ajiandae Mheshimiwa Yahaya Omary Massare.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kwanza tumshukuru Mheshimiwa Rais, maana tusipomshukuru tutakuwa ni wezi wa fadhila. Mheshimiwa Rais katika Wizara hii ametoa mchango mkubwa sana kwa kuchukua jitihada zake za dhati kabisa kutafuta fedha na kuweza kununua ndege ambazo kwa kweli umekuwa mchango mkubwa sana kwa Wizara hii ya Utalii. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mheshimiwa Gibson pale rafiki yangu naye ameona kwamba mchango wa Mheshimiwa Rais katika kununua ndege ni mchango mkubwa sana kwake yeeye binafsi amesaidia sana kufanya *contribution* ili Wizara hii na yenye kwenye utalii ionekane machoni kwetu na watalii wa nje moja kwa moja na ndege nyingine zinakuja. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchango huu ningewomba rafiki yangu Maghembe ambaye ndiye Waziri, atambue mchango wa Mheshimiwa Rais, vilevile atengeneze nishani ya kumtambua Mheshimiwa kama Mr. Utalii namba moja baada ya hapo kila mwaka atakuwa anatengeneza nishani moja moja hii itakuwa nafasi mojawapo ya kumtangaza Mheshimiwa Rais na kuwatangaza wale wengine wote ambao watakuwa wanashiriki katika kutangaza utalii katika nchi yetu, yatakuwa

ni mashindano makubwa ambapo tutakuwa tunatambua vyanzo vipyta, hapo itakuwa ni sehemu ya matangazo, atashirikisha wanafunzi, atashirikisha wanavyuo na wanahabari vilevile. Mheshimiwa Maghembe asiogope, atumie jitihada zake kutangaza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo za Mheshimiwa Rais, kama Wabunge wenzangu walivyosema sekta ya utalii ni sekta ambayo ni pana sana, ili sekta hii iweze kufahamika au kama unataka kuanzia kwenye sekta ambayo ni mpya ni lazima azitambue maliasili zilizopo katika ardhi hii na akishatambua maliasili ardhi zilizopo katika ardhi hii ni lazima afanye tafiti. Akishafanya hizo tafiti hana jinsi nyingine ni lazima aingie ghamama kubwa sana ya kutangaza vivutio hivyo, ukishatangaza hivyo vivutio hapo ndipo utapata rasilimali na atapata fedha Mheshimiwa Maghembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Maghembe juzi wakati tunatoa mchango hapa mimi nilitoa mfano mmoja mdogo sana kuhusu kisiwa cha Kilwa. Katika mchango wangu mkubwa sana nitazungumzia Kisiwa cha Kilwa. Inawezekana watu wengi hawajui Kilwa maana yake nini, wanaskia tu kwamba kuna Kilwa Kipatimu, Kilwa Masoko, Kilwa Pande. Hayo maeneo yote yalikuwa ni kisiwa kimoja na kisiwa hiki kina maajabu sana. Kisiwa hiki kilinunuliwa na tajiri mmoja ambaye inasadikika kwamba alinunua kwa kipande cha nguo ambacho kilifunika kwenye vijiji vyote hivi na kile ambacho kilifunika paliitwa Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilwa zote saba au nane ni maeneo ambapo yule mfalme alikuwa anamilliki, hiyo historia ni nani ambaye anayefahamu kwa kweli, watu wengi hawaifahamu historia hiyo na kuna majengo katika hivyo visiwa pamoja na hayo maeneo kuna majengo ya Wajerumani ambayo namwomba Mheshimiwa Waziri akafanye tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nilizungumzia kwamba kuna magofu na visiwa zaidi ya 1000 ambavyo hata Waheshimiwa Wabunge humu ndani tukisema tugawane kila

mmoja atapata viwili viwili, haya ni maeneo mapya ya utalii, Mheshimiwa Maghembe aende kule akafanye tafiti hayo maajabu watu wayaone. Siyo ajabu hata Waheshimiwa Wabunge humu ndani wengine hawajui. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, Watalam wake wafanye tafiti za kina ili imsaidie ye ye mwenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ukienda Lindi Mjini, kuna eneo linaitwa Kitunda. Bahati nzuri nilikuwa nimekwenda kule kulikuwa na watu ambao wapo kule chini inasemekana kwamba wanatafuta fedha ya Wajerumani, na inasemekana kwamba kuna handaki ambalo liko ndani kama kilomita mbili ambapo Wajerumani walikuwa wanatembea chini kwa chini. Mheshimiwa sisi ambao tulikwenda kule tuliweza kuogopa, lakini Mheshimiwa Waziri nadhani akitumia watalaam wake ataangalia lile handaki lina nini ni sehemu moja ambayo ni nzuri sana ya klutallii ya vivutio, lakini kwa kuwa havijatambuliwa haviwezi kufahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka hapo nenda Mtwara moja kwa moja kule kuna maeneo ambako Stanley alikaa siku saba kule kuna nyumba, bahati nzuri nimeiona leo katika maandishi ya Mheshimiwa Waziri, lakini yale magofu yaliyopo pale Mtwara ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba yale magofu ambayo au na vile visiwa ambavyo viro kule Kilwa ambavyo watu wanaweza wakavirekebisha, tuwavutie wao hata kama wakitengeneza basi wakae navyo kwa muda mrefu na siyo kwenda kuwanyang'anya na kuwabugudhi wale. Kwa mfano, kulikuwa na yule Mama ambaye alikuwa amekuja pale akatengeneza kile kisiwa na akajenga hoteli akawa analeta watalii wake wasiopungua 70 hadi 80 na akawasomesha wanakijiji pale tusim-*discourage* sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ye ye anamiliki lakini maana yake baada ya hapo ile ardhi hawezi kuondoka nayo hebu Wizara ifanye utaratibu wa kuhakikisha kwamba hawa watu

ambao wanafufua au wanarekebisha hayo magofu, hayo magofu yanaendelea kubaki katika *structure* ya asili, *provided* hawachukui hatuna sababu ya kufunga biashara zao. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Utalii kama kuna mtu anaweza kutambua hivyo na anaweza akavitangaza hivyo na kuna watu wanafanya hizo *renovation* basi watambue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwangu pale kuna shimo linaitwa shimo la Mungu, shimo la Mungu hilo ukiangalia liko chini ni kama kilomita mbili hivi. Kwa hiyo, maana yake ukienda ukiangalia mara moja kama siyo mzoefu lazima mtu aje akushike mkono. Vilevile kuna njia ambayo walipita Wajerumani na kuvuka kwenda Msumbiji. Hawa Wajerumani walikuwa wametokea Msumbiji wakati wanafanya *research* wakafika pale na ndiyo maana waka-establish Willaya ya kwanza Tanzania ambayo ni ya Newala, lakini walikuwa wanafanya *research* katika lile shimo la Mungu. Namwomba Mheshimiwa Waziri aende akalibainishe hilo shimo la Mungu ili watu walifahamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani anayejua kwamba leo ukienda Zanzibar kuna Kisiwa cha Chumbe ambacho kuna kobe wakubwa ambapo watu wawili tunaweza tukapanda kama ngamia tukazunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais aliyejita alizungumza kitu kimoja '*ukitaka kula lazima uliwe*' asiogope kuliwa Mheshimiwa Maghembe! Aingize fedha, apeleke *proposal* mbona makusanyo ni makubwa? Ili hii sekta tuweze kuvuna fedha za kutosha ni lazima tuwekeze kwa kiasi kikubwa. Alikuwa ana maana ya kwamba tusiogope hasara ili tuje kupata faida na ndiyo maana alisema kwamba ukitaka kula ni lazima uliwe, maana yake wekeza mtaji mkubwa *then* utapata. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haingii akillini leo maeneo ya uwekezaji ya maajabu saba ya dunia yako Tanzania, nenda Ngorongoro *crater* nenda Serengeti. Serengeti kuna maajabu pale kutokana na *movement* ya wale wanyama

ambao wana-move kutoka eneo moja la juu kwenda sehemu nyingine, lakini ile kwa kweli ni maajabu lakini tunayatangaza kwa kiasi gani? Mheshimiwa Waziri apeleke habari kote Tanzania ili watu wazijue, duniani kote tusiogope hizo gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara huwa kwanza tuna-*risk*, tunaingiza fedha kwa kiasi kikubwa ndiyo baadaye tunakuja kupata, usitegemee kupata bila kuwekeza haiwezekani, hayo maajabu hayapo duniani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bodi pale kama tatu au nne, kuna *fees anazopipata* Mheshimiwa Waziri, kwa nini anatumia shilingi bilioni mbili kutangaza, kwa nini asichukue bilioni 20 tukapata bilioni 300. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge katika Wizara ambazo tunaweza tukapata fedha ni Wizara ya Maliasili na Utalii, fedha ipo nje, haihitaji kutumia gharama kubwa. Kwa hiyo, nimwombe sana, zile bodi tatu kwa nini zinakuwa nyingi vile? Kwa nini asiziunganishe kama vile tunavyofikiria kuunganisha mifuko? Aunganishe zile bodi apate bodi moja ambayo itakuwa inafanya kazi kwa ufanisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa kumalizia niongelee kuhusu utalii wa ndani. Kama vile ambavyo tumezungumza, haiwezekani utalii wa ndani Mheshimiwa Waziri akafanya peke yake. Suala la utalii ni kubwa. Naomba aunganishe nguvu na Wizara ya Habari vilevile na Wizara ya...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maghembe umemwelewa lakini, ukitaka kula lazima uliwe! (*Kicheko*)

Hana maana hiyo lakini. Mheshimiwa Massare na Mheshimiwa Bwanausi ajiandae. (*Makofi*)

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na taasisi inayoshughulika na kutoa asilimia 25 zinazotokana na fedha za wawindaji katika vitalu vya utalii katika maeneo yetu. Wilaya ya Manyoni tuna vitalu vya utalii lakini Manyoni kuna Halmashauri za Wilaya mbili, kuna Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na Halmashauri ya Wilaya ya Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vitalu 11 katika Wilaya yetu lakini vitalu saba viro katika Halmashauri ya Itigi na vitalu vinne tunashirikiana pamoja na Halmashauri Mama ya Wilaya ya Manyoni. *TAWA* tumewapelekea taarifa siku nyingi na mipaka wanajua, wamekuwa wakipeleka pesa za mgao zile asilimia 25 moja kwa moja kwa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni wakati Halmashauri ya Itigi ipo na akaunti zilishapelekwa kwao, lakini kumekuwa na kizungumkuti hatuelewi. Mpaka sasa hivi Halmashauri yangu ya Wilaya Itigi inaonekana inasuasua katika makusanyo ya ndani kwa sababu tu ya uzembe wa watu amba hawataki kuwajibika katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri awasiliane na hawa watu na anipe majibu mazuri, kwa nini watu wenye maeneo hawapelekewi pesa katika eneo lao. Tuna Halmashauri kamili na tunatakiwa pesa zile ziende kwetu. Hivi tunavyozungumza pesa za mwezi huu amba umekwisha hawajapeleka, lakini miezi ile iliyokwisha walipeleka milioni 128 katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na pesa za Itigi zikiwemo. Sasa ni kitu gani hawajui au hawataki, kama hawataki kutupa waseme tu basi ninyi mkae kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki na usawa huu Halmashauri kama ile tuanze kuhangaika wakati tuna kitu chetu pale. Naomba hawa wataalam, sasa sijui ni Mkurugenzi au ni nani kwenye hicho kitengo amweleze Mheshimiwa Waziri. Mimi nitalia na Mheshimiwa Waziri kwa nini sisi hatupati hizi pesa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuna vitalu nya utalii, tuna mbuga ya Rungwa, Muhesi lakini na mbuga ya Kizigo. Rungwa, Muhesi iko katika Jimbo langu na kuna changamoto kadhaa zinazotokana na wanyama hawa kuwemo katika maeneo yetu, wamekuwa wakivuka mipaka yao na kwa sababu wanyama hawana akili wanaingia maeneo ya watu na wanafika mahali wanaua watu wetu, lakini wanakula mazao ya wananchi ambayo wameyalima. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukitoa taarifa hapa katika Bunge hili, wapiga kura wangu wawili wamepotea, kwa hiyo nimepoteza kura za watu waaminifu kabisa, lakini wakati huo huo sasa tulitoa taarifa kwa Mheshimiwa Naibu Waziri hatua zilichukuliwa kidogo hazikuwa na uzito naomba mara nydingine tukiwapa taarifa kuna watu wa Rungwa pale, kuna kikosi kikubwa kabisa cha *KDU* pale Manyoni, hawachukui hatua hata kufika kwenye eneo la tukio kuwafukuza wale wanyama warudi katika maeneo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara hii wazingatie kuwa karibu na wananchi ambao wanawachunga wale wanyama lakini wanapodhuriwa basi wafike haraka na tutoe kifuta machozi hicho ambacho wamekianisha japo ni kidogo sana, lakini kifike kwa wakati, ili watu kabla hawajaanza kuchoka na kujisika huzuni kwamba Serikali yao inawatelekeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi katika Sekta ya Misitu. Wizara hii niipongeze kwa kazi nzuri ilizofanya lakini kuna upungufu kadha wa kadha. kuna baadhi ya Maofisa wao ni wala rushwa sana. Suala hili tumelisemea sana na

Mheshimiwa Waziri anajua, nilishamwona na nikamwambia, walishafikishwa hadi Mahakamani, wamekamatwa na rushwa katika *check point*, lakini viongozi wa pale *TFS* pale Makao Makuu waliamu kumtoa yule mtu pale. Badala ya kumtoa Mheshimiwa Waziri kamrudisha matokeo yake sasa lile eneo lote linanuka rushwa. Ni vizuri mtu anayetuhumiwa kwa rushwa akakaa nje ya mfumo wa makusanyo kodi au maduhuli kwa sababu tu atasababisha na ataambukiza, samaki akioza Mheshimiwa Waziri ataambukiza na yeze atanuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote samaki akioza katika tenga, anaweza akasababisha ukatupa tenga zima. Sasa ni vizuri ukawahi kutoa ili wale samaki wengine wazuri tuwapeleke katika masoko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kumekuwa na matukio machache ambayo Wizara hii lakini hasa wadau hawa wa *TFS* wamekuwa wakiyafanya, mengi ni ya kupongeza lakini kuna changamoto kadha kidogo. Bei ya *TIK*/katika minada kama hivi hapa majuzi juzi, katika mnada wa Mtibwa kulikuwa na shida lakini bahati nzuri Lunguza niwapongeze wamefanya vizuri, wameuza vizuri na wamepata bei nzuri, kwa hiyo wanaisaidia Serikali yetu katika kukusanya maduhuli, kuna changamoto kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnategemea viwanda vyta misitu vifanye kazi kwa maana viwanda vile vina matatizo sana ya *Saw Doctor*, hapa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 85 Chuo cha *Fitii* hajakipa uzito, hatuna *Saw-Doctor* kabisa nchi hii na wachache wale mnaozalisha wengi wanachukuliwa na Serikali. Sekta binafsi hii ambayo inategemewa ndiyo watakaokuwa wana- process haya mazao ambayo mnayaiza, hawana Ma- *Saw Doctor*. Je ni utaratibu gani mtatumia hao watu mnaowazalisha pale *Fitii* japo ni wachache, kwa sababu katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ameonyesha ni watu 80 tu na kitu hawafiki hata 100 kwa mwaka ambao anawazalisha katika soko la ajira, Serikali hao hao inawahitaji, na wengi wanapotoka *Fitii*/hawaajiriwi kama wataalam wa misumeno

matokeo yake wanarudi kuwa *Forester* na kazi kubwa wanapewa ya kukusanya maduhuli. Mheshimiwa Waziri ajitahidi kutuonyesha na wale wadau wa misitu wanapataje wataalam wanaozalishwa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa hivi hakuna chuo kingine mbadala cha kuzalisha *Saw Doctor*, katika nchi hii. Inafika mahali makampuni mengi wanaanza kuajiri wageni kwa sababu upande wa Serikali ikishawazalisha inawaajiri wao, lakini upande wa sekta binafsi hamna. Hatukatazi ajira kwa vijana wetu tunafurahia sana, wanapoajiriwa na soko kuu ambalo ni rasmi, lakini watoe basi fursa kwa watu ambao wanahitaji kupeleka vijana wao pale *FIT* basi gharama ziwe rafiki ili *Saw Doctor* kutoka katika viwanda binafsi nao waweze kuhudumiwa na chuo hiki ambacho ni cha umma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya mkaa, Serikali imekuwa ikizuia mkaa kutoka eneo moja kwenda lingine, wameanzisha magilio kama walivyosema, lakini haiwawezeshi wadau ambao wanataka kutengeneza hata mkaa mbadala. Mkaa mbadala unaotokana na nyasi, mkaa mbadala unaotokana na vumbi la mbao, yote hii Serikali haijaonesha dhamira ya dhati, inapozuia mkaa unaotokana na miti. Ni vizuri sasa basi tutafute katika Mfuko wa Misitu au mahali unapoona.

Mheshimiwa Waziri hata mimi akinewevesha nitazalisha mkaa, mimi ni mdau wa mazao ya misitu najua vizuri. Sasa watuwezeshe sisi wadau tuweze kuzalisha mkaa tuondokane na kukata miti. Wakati huu hakuna mbadala unaooneshwa, hata bei ya gesi bado siyo rafiki sana kwa wananchi wetu, wakulima wa vijijini. Watanzania walio wengi wanatumia mkaa tukiacha wale wa miji mikubwa tunatumia sisi wa vijijini pia. Sasa siyo rafiki, mtungi wa gesi unakaribia laki moja, Sh. 65,000 - 70,000 mpaka 90,000 ule mtungi mkubwa, sasa ni vigumu sana kwa mtu wa kawaida uweze kutumia. Tusaidieni sisi tuweze kusaidia hilo ambalo litatufika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ufugaji nyuki halijatiliwa maanani kabisa, Mheshimiwa Waziri amelizungumza juu juu, hakuna mizinga angalau anaweza akatupa; kila Mbunge akapata hata mizinga 100 tu akapeleka katika maeneo yake. Maeneo ya misitu tunayo mengi, ili tuondokane na umaskini huu. Katika Tanzania ya viwanda ameonesha kiasi kidogo cha nta kilichouzwa katika soko la nje, lakini Serikali inaweza ikawekeza na namna ya kuwekeza ni kidogo tu, ana wadau wengi, asaidie wananchi... (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bwanausi, wajiandae Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Maliasii na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kumpongeza sana Profesa Maghembe; Naibu Waziri, Injinia Makani; Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa kuanza kuonesha sura mpya ya Wizara na kuanza kuleta matumaini mapya kwa Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishauri Wizara, Mheshimiwa Waziri Profesa Maghembe na wenzake kwamba juhudzi zinazoendelea hivi sasa za kutatua migogoro walioyoikuta ziongezwe kasi ili kuwe na mahusiano mema kati ya Wizara na wananchi katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Pia niitahadharishe Wizara siyo vema kuanza kutafuta migogoro mpya kwenye maeneo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakala wanaoshughulika na mambo ya misitu wamepewa jukumu la kwenda kutathmini mipaka ya hifadhi za misitu, lakini nimwombe na kumkumbusha tu Mheshimiwa Waziri kwamba zoezi hili halikuwa limefanyika kwa zaidi ya takribani miaka 20 iliyopita,

kinachotokea hivi sasa ni baadhi ya maeneo kuanza kuzalisha migogoro kutokana na zoezi hili. Mheshimiwa Waziri nitolee mfano tu kwenye Jimbo langu la Lulindi tunayo hifadhi ya msitu ya Njawala, lakini tunavyo vijiji vinavyozunguka katika eneo hili, ambavyo Vijiji hivi nya Njawala, Mchoti na Mtona ni vijiji ambavyo viro tangu miaka 20 iliyopita, katika zoezi hili vijiji vile vinaambiwa vimo ndani ya msitu, sasa inaleta kero kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha basi ni vizuri kueleza wataalam wetu wasiende kuanzisha migogoro mipy. Nilipokuja katika Bunge hili nimemletea Mheshimiwa Waziri barua na wamenituma nimwombe Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge atembelee maeneo ya Jimbo la Lulindi ili akajionee hali halisi katika maeneo haya, naamini atanikubalia ili tukayasililize na kuyatatua matatizo haya tukiwa kule *site*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kulichangia ni tatizo kubwa sana la wanyama hatarishi na wanyama ambao wanawadhuru wananchi. Tangu niingie katika Bunge hili 2010 nimekuwa nikilalamika sana juu ya Wizara kutotilia maanani matatizo yanayotokana na mamba wanaoshambulia wananchi katika Jimbo langu la Lulindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuliwahi kufanyika utafiti kama miaka minne iliyopita na utafiti ulifanywa na wenzetu wa Wizara ya Maliasili, wakabaini kwamba katika Mto Ruvuma hasa eneo langu la Jimbo la Lulindi, mamba ni wengi zaidi ya 300 wapo katika eneo lile. Kulitolewa ahadi, ya kuwapunguza mamba wale lakini kwa masikitiko makubwa katika miaka minne tu wananchi wa Jimbo langu na Watanzania 35 wameshapoteza maisha na zaidi ya watu 50 wamekwishajeruhiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua tunayo Taasisi ya Utafiti ya Wanyamapor (TAWIRI), nichukue fursa hii kuilalamikia sana TAWIRI, najiuliza labda makao makuu yapo mbali sana na

Mtwara yako Arusha, katika kipindi chote cha Ubunge wangu sijawahi kuwaona *TAWIRI* wakija kutembelea maeneo yaliyoathirika katika Majimbo yetu. Kikubwa ambacho wanakatisha tamaa ni kwamba sisi tunasikiliza maelekezo yanayotolewa na Shirika la Wanyama Duniani kwamba lazima tuwalinde wanyama wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hebu awape matumaini wananchi wale ambao wanaishi kandokando ya Mto Ruvuma, vijiji hivi ni vijiji vya ulinzi, kuna Vijiji vya Mapili, Mduhe, Maparawe, Mkoo, Sindano na Mgwagule wananchi hawa katika kipindi chote hiki wameishi kwa maisha ya shida mno. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshafika ofisini kwa Mheshimiwa Waziri mara nydingi na tumezungumza, kwamba moja ya suluhisho la kuwasaidia wananchi wale ili wasiathirike na tatizo la mamba ni kupunguza idadi ya wananchi wanaokwenda kuchota maji na huduma zote za maji kutoka kwenye mto ule. Tunao mfuko hapa unaoshughulika na wanyama pori, tunayo mifuko mingi inayoshughulika na wanyama pori, inazo fedha, kwa nini Wizara isihakikisha kwamba inasaidia vijiji vile kupata maji ili tupunguze idadi ya watu wanaokwenda kutumia maji kutoka Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namfahamu Mheshimiwa Profesa Maghembe, Naibu Waziri *EngineerMakani* na Katibu Mkuu kwamba ni wasikivu sana, naamini atakapokuwa anahitimisha kwenye hotuba yake atawaambia ndugu zangu wale Lulindi ni jinsi gani Wizara yake itakavyolichukulia suala hili kwa uzito mkubwa na kuhakikisha katika bajeti hii ya 2017/2018, tunatenga fedha kwa ajili yakuchimba visima vinane kwenye vijiji hivi ili kuwasaidia wananchi wale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaacha kusema aliyosema aliyetangulia kutoa maoni yake. Mheshimiwa Waziri hili tamko tunalotaka kuendelea kupewa msisitizo la kuzuia mkaa

kutoka eneo moja kwenda lingine ni lazima litazamwe upya. Bado hatujafika wakati ambapo nishati mbadala zinaweza kutosheleza badala ya mkaa. Namwomba sana hili jambo la kuhifadhi misitu ni jambo muhimu sana, nakubaliana nalo sana kwa asilimia mia moja, lakini twende taratibu, kuagiza tu mamlaka zote zianze kuzuia mikaa kuingia mijini kwenda wapi, wakati mitandao ya gesi hatuja kamilisha, ni jambo ambalo hapana, hili jambo tutaonekana tunakurupuka na litaleta athari kubwa sana kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana kwa sababu hili jambo linagusa maisha ya wananchi wetu wengi wa vijiji na maisha ya wengi wa mijini, jambo hili lisitishwe mpaka pale ambapo tayari tutakuwa na nishati nyingine ambayo wananchi hawa wanaweza wakatumia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa sina tabia ya kupenda kugongewa kengele, naamini haya ambayo nimeambia Wizara, nimeambia Serikali na hasa kwa wananchi wale amba wanapoteza maisha, yatazamwe sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki cha mvua huwa hakuna matukio makubwa ya mamba kuwavamia wananchi, kwa sababu maji yamejaa, wako katikati ya maji marefu, lakini kuanzia Julai hadi Desemba kila siku tunapokea taarifa ya vifo vya wananchi. Mheshimiwa Waziri wale ni Watanzania sasa nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kuwaambia Watendaji kwamba, wakiwa wanang'ang'ania taarifa zinazotolewa na jumuiya ya Kimataifa... (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Owenya, wajiandae, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq na Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyozungumza utalii unachangia sana katika pato la Taifa, lakini wafanyabiashara katika sekta hii, niungane na wenzangu kusema kwamba tozo na kodi ni nyingi sana, ziko kodi 36 na nimeziambatanisha hapa naomba uzione ili wakati Kamati ya Bajeti inakaa wakati wa *Finance Bill* waangalie ni jinsi gani wanaweza wakazipunguza kodi hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba VAT haikuathiri watalii kuja nchini. Kwa mfano kabla ya VAT Ngorongoro Crater mwaka 2014 walikuja watalii 332,163, mwaka 2016 wamekuja watalii kuingia Crater 228,689, kuna pungufu ya 103,000, sasa kama wanabisha siyo VAT, basi wafanye uchunguzi ni kitu gani kinafanya watalii hawaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuko katika sekta, watalii wengi walikataa kulipa zile VAT. Sasa wao wanasesma watalii wameongezeka sijui hizi takwimu wanatoa wapi, sijui mnajumlishia na hao Wachina wanaokuja kujenga barabara huku, sielewi kwa kweli, naomba Waziri atueleze hizi takwimu anazitoa wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kodi nyingi sekta hii inakuwa vigumu sana kufanya matangazo, unakuta wafanyabiashara wana kodi nyingi lakini ni wao wao watengeneze vipeperushi, wajilipie *exhibition* lakini *TTB* haiwezeshwi. *TTB* mwaka 2016 waliomba shilingi bilioni 2.7 mpaka sasa hivi wamepata milioni 422, watafanyaje *advertisements?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuna masoko mapya kama Nchi za *Czech*, Ukraine, Yugoslavia na sehemu nyinginezo, wanataka kuja Tanzania lakini *TTB* ndiyo inayotakiwa iende ikatangaze vivutio vya Tanzania lakini wanashindwa, kuna vivutio vingi. Mathalani, Mkoa wa Kilimanjaro Kijiji cha Mrusunga, Kata ya Mbokomu, Moshi Vijijini, kuna mti mrefu mita 80 mti ule unakadirwa umekaa zaidi ya miaka 500, lakini Wizara ya Utalii hajafanya utafiti wowote, wanatakiwa waende wakaweke uzio pale ili

muuweke kati ya vivutio wageni wanavyokuja kutembelea Mlima Kilimanjaro, wakati wanangojea kupanda, wakati wa *climatization*, tuiweke kwenye *itinerary* Wazungu waweze kwenda pale waende wakapige picha na tunaweza kupata mapato. Wizara imekaa kimya sijui wanashubiri mzungu aje apige picha aseme ame-*discover* mti mrefu Afrika, wakati watafiti wako hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hivi vitu tuvifanye wenyeve na tuwe *proud* na nchi yetu wenyeve, tusingojee Wazungu waje hapa watuambie wame- *discover* Mlima Kilimanjaro wakati sisi tuko hapa na babu zetu walikuwa wanaokota kuni kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la wakulima na hifadhi *TANAPA*. Mfano, kuna wakulima wanaolima mpunga kule Mbarali wakulima hao wana vijiji 32, *TANAPA* inataka iende ikachukue vijiji vile ifanye hifadhi, lakini wameshaendelea wamejenga viwanda zaidi ya 46 wana ma-*godown* karibu 56, wana wafanyakazi zaidi ya 10,000, viwanda vile walivijenga kwa zaidi ya billioni 72, tayari wameshawekeza kwenye viwanda na Serikali wanasema Tanzania ya viwanda, sasa hivi wanataka kwenda kuwanyang'anya vile viwanda, sasa wataenda wapi, watafanya nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri nimeshazungumza naye na pia nilimwona Waziri Mkuu kuhusiana na suala hili. Naomba vile vijiji waviache waendelee na ile kazi tayari ni ajira iko pale, tayari viwanda viko pale, wawaache wafanye kazi, waende wakaendeleze hifadhi nytingine. Kuna hifadhi kama ya Selous inatakiwa kuendelezwa, Saadani inatakiwa kuendelezwa, sasa wanaenda kufukuza watu ambao tayari wana makazi, wana wafanyakazi, wana kila kitu, kwa nini wasiende huko ambako kunatakiwa kuendelezwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa nimekosea sana kama sitauongelea Mlima Kilimanjaro. Kila siku nimekuwa katika Bunge hili tangu tumeanza naongelea suala la *rescue*.

Rescue katika Mlima Kilimanjaro bado hairidhishi, unakuta mgonjwa anaugua kule juu, sijui ni kwa nini pamoja na mapato yote haya wanayopata kutoka Mlima Kilimanjaro wasinunue *helicopter* ya ku-rescue wagonjwa wanaopata matatizo kule mlimani ikiwa ni pamoja na ma-porter.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni shida mtu akipata ugonjwa kutoka Uhuru Peak mpaka ashushwe chini, akutane na gari ya *National Park* ile inayo-rescue unakuta ameshakufa, ni zaidi ya masaa kumi, lakini wakinunua *helicopter* yenye uwezo wa kuweza kushuka kule Shira wataokoa maisha ya watu na wale Wazungu wanaokuja wataona kwamba tunawajali pamoja na *Porters*, lakini sisi tumekuwa tukiwaleta kwa mikono, wanakufa, wanaenda kufanya uchunguzi kwa nini wamekufa lakini tatizo ni *rescue system* tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nimeulizia mara nyingi kuhusu vyoo, vyoo ni tatizo katika mlima wetu mmesema watu wanaenda ku-camp *crater* naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri wana-camp *crater* watajisaidia wapi? Mazingira tutayatunzaje? pale *crater* hamna choo, vile vyoo vilivyoko kwenye *camping roots* ni vya shimo, vimejaa, kila *Tour Operator* anajaribu kupeleka *chemical portable toilets*, lakini ile waste wanaipeleka wapi? Wanaenda kuimwaga kule kwenye yale mashimo ya *National Park* ya choo, lakini bado yamejaa, kwa hiyo bado yale mazingira Mlima unarudi pale pale kunazidi kuwa kuchafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba sana, hili suala la choo, kuna vile vyoo vya Wajerumani mlivyovileta vya kujaribu vimeishia wapi? Maana yake mnakuja hapa mmaongea maneno mazuri lakini hamtekelezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine tunacholalamika kule Kilimanjaro ni feesza *forest*. Mtu analipa *National park fee* mfano kule Umbwe, Longai na Lemosho, unalipa *forest fee* unalipa na *National Park fee*, unaenda mpaka Umbwe unafika Umbwe hakuna maji, inabidi warudi tena chini wanunue tena maji, zote hizi ni tozo tu zinazidi

sasa unakuta tunashindwa kufanya biashara kwa sababu ya hivi vitozo vidogovidogo. Kwa hiyo, naomba sana waliangalie hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine pamoja na mambo mengine ni lile suala la Faru Fausta, Faru Fausta anatumia fedha nyngi sana shilingi millioni 60 kwa mwezi ni fedha nyngi. Mnyama yule alizoea kutembea huru, hivi kwa nini msimuache afe *naturaly* kama anavyokufa tembo, anavyokufa simba lakini anakuwa ni chakula kwa ajili ya wale wanyama wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wanamtesa yule mnyama wanamfungia kwenye *cage*, ana vidonda, anateseka mnyama wa watu, kwa nini wasimuachie aende kwenye mbuga ili akafe *natural death* kama wanyama wengine, lakini mnamuweka pale mnampa madawa mnamtunza kuliko binadamu, *at the end of the day* lazima atakuja kufa tu. Kwa hiyo, wamwache afe kwa kifo chake cha kawaida, lakini siyo mumtunze pale na wakati tunahitaji fedha nyngi kwa ajili ya kutunza hifadhi zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, watu wamekuwa wakija sana *Northern Circuit*, nami niungane na wengine niombe sasa tuweke mkazo *Southern Circuit*. *Southern Circuit* kumekuwa ni *monopoly*, unakuta ni mtu mmoja amejenga hoteli kule, barabara sio nzuri sana kwa hiyo unakuta Wawekezaji wa ndani inawawia vigumu sana kwenda kuwekeza kule kama nilivyozungumza mwanzoni. *Licence* ni nyngi, *fees* ni nyngi, unakuta *Local Tour Operators* ni vigumu sana kwenda kuwekeza kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iweke mazingira wezeshi ili Watanzania nao waweze kwenda kuwekeza kule *Southern Circuit*, wajenge hoteli tuweze kuuza *Southern Circuit*, maana yake sasa hivi ukisema unaiuza *Southern Circuit* huwezi, unakuta ni zaidi ya dola 6,000. Mtu anataka apande mlima, atembee aende *Southern Circuit*, aende aka-*relax* Zanzibar, inafika karibu dola 12,000 au 15,000 watu hawawezi ku-*afford* hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujio wa watalii sasa hivi kuna *competition*, wenzetu Kenya wanapeleka *very cheap* kwa sababu ndege zao zinawaleta wageni *direct* mpaka Nairobi, kwa hiyo inakuwa ni rahisi kwa wao kuweza kuuza utalii Nairobi kwa bei rahisi kuliko ilivyo Tanzania... (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, jiandae Silafu Jumbe Maufi.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa nami nichangie hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote kwa kuandaaj bajeeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye biashara ya uwindaji. Inabidi ikumbukwe kwamba biashara hii ni biashara tofauti sana na biashara nyingine. Uwindaji wa kitalii ni shughuli ambayo ni starehe kwa watalii husika, hivyo basi ni dhahiri kwamba Watalii hawa wanapokuwa wamekuja kwa ajili ya uwindaji wa kitalii wanahitaji kuwa na mazingira ambayo yametunzwa vizuri na yako vema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna tishio kubwa sana la uvamizi wa mifugo katika mapori yetu mbalimbali au mapori ya akiba na hii imekuwa ni kikwazo sana kwa uwindaji wa kitalii na hata hii imesababisha asilimia 34 ya uwindaji wa kitalii ukaporomoka kati ya 2013 na 2017. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aone kwamba hii tunapoteza pato la Taifa, kwa hiyo ipo sababu ya msingi kabisa kwa Serikali kuona inafanya mkakati wa kuhakikisha kwamba mifugo haikai katika haya mapori ya akiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee kwamba kupoteza hii asilimia 34 ya vitalu kwa kweli Taifa linakosa mapato makubwa sana. Kwa mfano, Serikali inakosa mapato kwenye ile daraja la kwanza kabisa la vitalu US\$ 60,000, hii ni pesa ya kutosha sana. Sambamba na hilo kwenye *grade* ya pili tunakosa US\$ 30,000 na kadhalika na kadhalika mpaka *grade* ya tano ni US\$ 5,000. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla ione kwamba kweli hapa Serikali inakosa mapato kwa sababu tu ya mifugo kuingia katika mapori haya. Naomba nitoe shime kwamba lazima uwepo mkakati wa uhakika wa kuhakikisha kwamba mifugo haiingii katika mapori haya.(*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nibainishe kwamba kwa kuwa sekta ya utalii inaingiza asilimia 25 ya fedha za kigeni na kuchangia asilimia 17 ya pato la Taifa, hivyo naendelea kusititiza kwamba ni budi Serikali ikawa na mkakati endelevu wa kuhakikisha kwamba tunaweza kupata pato zaidi kwa kuboresha miundombinu iliyopo katika maeneo yote ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie sekta hiyo ya utalii hasa nishauri kwamba, sekta ya mifugo pamoa na Halmashauri zijiitahidi sana kusimamia Sera ya Mifugo kwa kutenga maeneo ili kusudi wafugaji waweze kupata maeneo yao waweze kuweka mifugo yao kule. Hii pengine inaweza ikasaidia mifugo isiingie katika hifadhi zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ni budi tuwe na takwimu sahihi za mifugo iliyopo katika nchi hii na kila mfugaji abainike kwamba ana mifugo mingapi. Pia wafugaji lazima wahamasishwe tu wafuge kwa tija ili mwisho wa siku Serikali iweze kupata mapato kwa kutokana na utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie suala la misitu katika mabonde na mito. Haina shaka kwamba tatizo la uharibifu wa mazingira binadamu ndiyo wahusika wakuu. Kwa hiyo, maeneo mengi sana

yameharibiwa, maeneo mengi sana yamekatwa miti na kadhalika hasa kwenye maeneo ya mabonde. Nashauri kwamba, Serikali pia ije na mkakati wa nguvu wa kuhakikisha kwamba maeneo yale ambayo ni ya mabonde yahifadhiwe na yapandwe miti mingi sana kwa sababu ile miti na maziwa ambayo yanakauka inatokana na ukataji miti, hivyo nilikuwa nashauri Serikali ilisimamie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba nisisitize tena suala la upandaji wa miti ili tuweze kukilinda kizazi hiki na kizazi kijacho, watoto wetu na wajukuu zetu na vitukuu wasije wakatulaumu kwamba sisi tulishindwa, kwa hiyo suala la udhibiti wa mazingira ni lazima lifanyike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba pia nichangie idara ya utalii ya mambo ya kale. Kuna mwenzangu mmoja ameshalizungumzia hili lakini nami naomba niongezee. Ili Taifa liweze kupata kipato ni budi Serikali yetu iendelee kutangaza vivutio vya utalii pamoja na malikale. Kwa mfano, katika maeneo ya fukwe, mapango, kuna mionganii mwetu ambao pia wamezungumzia kuhusu suala la mila na desturi za makabila mbalimbali, historia za viongozi, pamoja na mila za makabila na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, hapa kwetu Mkoani Dodoma Wilaya ya Kondoa kuna mapango ambayo michoro yake iko katika historia ya dunia. Je, Serikali imetangaza kiasi gani Wilaya hii ya Kondoa ili kusudi nayo iwe ni mojawapo ya kivutio cha watalii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzenzu wa Afrika ya Kusini, kuna utalii wa mila na desturi ambao unaendelezwa kule, sisi tuna zaidi ya makabila 120. Je, tumejiandaaje makabila haya nayo yaweze kuwa kivutio cha watalii? Tuna makabila mbalimbali, tuna Wamasai, tuna Wayao, tuna Wanyakyusa na mengine ambayo sikuyataja, wote hawa wana mila zao na desturi, hebu nasi tuone ni kwamba tunafanyaje kuhusu hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba pia niishauri Serikali ifanye utaratibu wa kutuma wataalam wetu katika maeneo mbalimbali ya Afrika na nje ya Afrika, kuona wenzetu wamewezaje kufanikiwa katika hili suala zima la utalii. Sisi tuna vivutio vingi sana sana duniani, lakini bado hatujaweza kuwavutia watalii kiasi hicho. Nashauri Serikali ingefanya utaratibu wa kuapeleka wataalam mbalimbali ili kusudi waje walete ujuzi kutoka maeneo hayo angalau na sisi itusaidie kupaisha sekta yetu ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nichukue fursa hii kushukuru sana na kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi amepata dharura hayupo, kwa hiyo anapewa Mheshimiwa Mipata ajiandae Mheshimiwa Catherine Ruge.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami niwe mmoja kati ya watu ambao wanapongeza maandalizi mazuri ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekuwa hodari kusikiliza matatizo ya wananchi hasa tunapomwendea sisi Wabunge ni muungwana. Nina hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Wilayani kwetu tuna mbuga inaitwa Rwamfi *Game Reserve*, mbuga hii imepakana na vijiji kadhaa na kabla ya mbuga hii hajakuwa Serikalini ilikuwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Kutokana na umuhimu wa uhifadhi tunaoujua tuliamua kuipeleka Serikalini, Serikali ikaitwaa ikaanza kuihudumia. Katika kipindi ambacho Serikali inahudumia tumezionna faida kwamba kwa kweli wanyama wameongezeka na mbuga inatunzika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto ambazo tunaziona kwa wahifadhi wenyewe, kwamba hawana vitendea kazi nya kutosha, hawana idadi ya watumishi wa kutosha na kwa maana hiyo tunaiomba Serikali iwalettee gari, maana yake nalionna pale gari bovu sana la muda mrefu, kwa hiyo haliwapi nafasi ya kufanya kazi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pamekuwa na migogoro baina ya mipaka na vijiji vinavyopakana. Kuna vijiji nya Kasapa, vijiji nya King'ombe, vijiji nya Mlambo, vijiji nya Ng'undwe, vijiji nya Mlalambo, Kizumbi, Kata, Namansi na vinginevyo. Vijiji hivi vimekuweko kabla hata ya kuanza kwa pori lenyewe, vijiji nya kiasili, lakini kwa sasa vinaonekana kwamba viko ndani ya pori na kwa hiyo kuna mgogoro tayari kwamba wahame nao, kwa hivyo hawana nafasi, hawana maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo Kamati ya Kitaifa ambayo imeshaundwa inatembea kila mahali, kwetu haijafika naomba wafike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilifika hata Ofisini kwa Waziri nilimwelezea juu ya mgogoro wa Kijiji cha Kasapa ambao ulipelekea wananchi kufyekewa mazao yao kwa kiwango kikubwa, zaidi ya hekta 20, kitu ambacho kwa mwaka huu ni shida kubwa sana hakuna chakula, ingawaje Waziri alinipa ushirikiano mkubwa na kuwaambia wahifadhi kwamba ni vizuri wawe wanawasiliana kuliko kuchukua hatua kali za namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, Mheshimiwa Waziri ameshaniahidi kwamba baada ya Bunge tutaenda huko ili kwenda kuiona hii changamoto. Namshukuru sana, bila shaka ataiangalia kwa makini na kuona jinsi inavyoweza kusuluuhishwa kwa vijiji vyote ni changamoto kubwa kwetu. Namna nzuri ya kuikabili changamoto ni kuangalia kama yapo maeneo ambayo yanaweza yakaachwa kwa wananchi kwa ajili ya kuendeleza shughuli za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo naiona katika Rwanza ni mpaka wake na Kalambo *ranch*. Kalambo ranchi ni ranchi ya Taifa na kuna *blocks* ambazo wamepewa wawekezaji, wawekezaji hawa katika eneo hilo hakuna mipaka inayoonekana wazi, kwa hiyo pemekuwa na migogoro ya hapa na pale, jambo ambalo linafanya wawekezaji hawa *wa-face* migogoro mingi na wahifadhi. Kwa hiyo, jambo zuri hapa ni kuweka mipaka iwe wazi ili wananchi hawa ambao wanalipa kodi ya Serikali wasibughudhiwe pia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni vivutio vyatya utalii. Wilayani kwetu hasa Jimbo la Nkasi Kusini kuna vivutio vyatya utalii vingi. Ukiwa kwenye mwambao mwa Ziwa Tanganyika kuna ukanda mzuri sana, kuna mawe mazuri ambayo yamepangika kwa namna yake na kuna visiwa vizuri ambavyo vikiendelezwa vinaweza vikawa ni utalii wa namna yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naishauri Wizara itembelee maeneo hayo ione utajiri uliopo ya utalii waone utajiri uliopo wa utalii ambao ukiendelezwa unaweza ukachangia sana. Siyo tu kwetu kwa Mkoa mzima kuna maeneo kama vile ukienda Kasanga kuna Ngome ya Bismarck, ikiendelezwa ile inaweza kuwa nzuri sana, kuna Kalambo *falls* ambayo sasa hivi nimeona kama Wizara inaizingatia, ikiendeleza inaweza ikaleta pesa nydingi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama unaenda Kala kuna eneo ambalo ilikuwa ni makazi ya Zwangendaba ambaye alikuwa maarufu sana katika historia ya Tanzania kutoka Kusini. Aliuawa maeneo hayo na kuna majengo ya Mjerumani pale ambaye ndiye alimdhhibit kwenye eneo hilo na alizikwa eneo hilo. Kwa hiyo, inaweza ikasaidia sana kwa watu wanaotaka kujua mambo ya kihistoria katika suala zima la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu sana katika maeneo ya utalii kwetu ni eneo la Kijiji

karibu na Mji wa Namanyere. Kuna maji moto ambayo yanatoka kiasi kwamba yakiendelezwa pale kijijini inaweza ikasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi niishauri Serikali, katika kuendeleza utalii nchini waangalie miji ambayo inawekeza katika ujenzi hasa ambayo ni ya kimkakati katika suala zima la utalii kama Mikoa ya Rukwa, Katavi na maeneo mengine. Majengo yanayojengwa pawepo na ushauri wa kitaalam wa kuangalia Halmashauri ambazo zinasimamia ujenzi ili angalau viwango viwe vinafikia ili changamoto ya mahali pa kufikia wageni ambaao wanajielekeza kwenye utalii isiwe ni changamoto inayokinzana na suala zima la utalii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba bado suala la mkaa kama wenzangu walivyolisema liangaliwe upya. Sasa hivi bado hatujawa na nishati mbadala ambayo inaweza ikakidhi mahitaji ya watu kwa sasa. Kwa hiyo, pamoja na uhifadhi na umuhimu wake, lakini pawepo na ustaarabu wa kuangalia jambo hili kwa umakini zaidi, vinginevyo tunaweza tukazua migogoro ambayo italeta shida kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Catherine Ruge, tunamalizia na Edwin Sannda.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wizara hii Mheshimiwa Ester Matiko kwa hotuba nzuri. Baada ya kusema hayo naombe niende moja kwa moja kwenye kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii ina mchango mkubwa sana katika maendeleo ya Taifa hili, ina mchango mkubwa katika pato la Taifa na imeweza

kuchangia asilimia 17.5 kwa maana ya *GDP*. Pia sekta hii inachangia ajira milioni moja na laki tano(1,500,000) katika nchi hii, kwa maana ajira laki tano za moja kwa moja lakini pia ajira milioni moja ambazo si za moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Sekta ya Utalii ni sekta ambayo inaliingizia Taifa letu fedha za kigeni. Asilimia 25 ya pesa za kigeni katika Taifa hili zinatokana na Wizara ya Maliasili na Utalii. Sekta hii ya Utalii ni sekta namba mbili katika kuvutia wawekezaji. Mwaka jana 2016 Sekta hii ya Utalii imeweza kuliingizia Taifa letu dola za Kimarekani bilioni 2.1. Kwa kutambua umuhimu, fursa na mchango wa Sekta ya Utalii katika kuwezesha na kuendeleza uchumi wa nchi yetu, ni dhahiri kabisa tunahitaji Sera Wezeshi na mikakati thabiti kuweza kuendeleza na kuboresha sekta hii ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji na wafanyabiashara wa Sekta ya Utalii wamekuwa wakikumbwa na changamoto nyingi, naomba niongelee utitiri wa kodi, ada, leseni na tozo mbalimbali katika sekta hii. Jambo la kusikitisha tozo, ada na leseni hizi hazilipiwi kwenye mamlaka moja, zimekuwa zikilipiwa kwenye mamlaka tofauti na hivyo kuwa kikwazo na changamoto kwa wawekezaji na makampuni yanayowekeza katika sekta ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niseme baadhi ya tozo na leseni mbalimbali na mamlaka mbalimbali zinazolipiwa gharama kwenye sekta hii. Utaambiwa uende *TRA ukalipe kodi*; nenda Wizara ya Maliasili na Utalii ukalipe leseni na ada; nenda *Marine Park Authority* ukalipe *concession fee*, nenda *Tanzania Civil Aviation Authority* ukalipe leseni ya huduma za anga na ukaguzi; nenda *SUMATRA ukalipe SUMATRA vehicle sticker*; nenda *TANAPA ukalipe motor vehicle guide fee*; nenda *Ngorongoro Conservation Area ukalipe NCAA vehicle fee*. Niombe Serikali iangalie ada, tozo na leseni ambazo zina tija katika sekta ya utalii ili kupunguza changamoto na usumbufu kwa wawekezaji katika sekta hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee katazo la matumizi ya mkaa na kilio cha wananchi. Naomba nieleweke, sipingi harakati za Serikali katika kulinda misitu yetu kwa utalii endelevu. Lakini, karibu kila mtu anatumia mkaa ikiwa ni pamoja na sisi baadhi ya Wabunge. Serikali hajaja na nishati mbadala ambayo inapatikana kwa urahisi na ambayo ni *affordable* kwa mwananchi wa kawaida *especially* vijijini, ambayo inaweza kumsaidia katika matumizi ya nyumbani. Kwa hiyo, niishauri Serikali iweze kuangalia ni jinsi gani inaweza kuja na nishati mbadala ili tuweze kumwezesha mwananchi wa kawaida aweze kumudu gharama za matumizi ya kupikia na taa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *option* ya gesi lakini *option* hii ni ghali sana. Mtungi wa kilo 15 ni shilingi 52,000, siamini mwananchi wa kawaida wa kijijini kule Serengeti ninakotoka mimi anaweza kumudu hii gharama. Pia kuna *option* ya makaa ya mawe, sijaona kwenye hotuba hii kwamba kuna utafiti wowote umefanyika ambaao unaonesha nishati ya makaa ya mawe hayana madhara kwa matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kwa maeneo ambayo ni ya wafugaji, kuna miradi imefanyika ya *biogas* kwa maana ya kutengeneza *biogas* kwa kutumia kinyesi cha ng'ombe, tuweze ku-*invest* katika hii *area* na ile miradi ambayo imefanywa na wafadhili. Kwa mfano, Serengeti kuna Kata ya Morotonga, Ring'wani kuna miradi imefanywa na wafadhili. Niombi Wizara ya TAMISEMI kwa kushirikiana na Halmashauri zetu kuona ni jinsi gani inaweza ikachukua hii miradi na kuiendeleza na kui-scale kwenye Wilaya zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Mkoa wa Mara ninakotoka. Mkoa wa Mara ni Mkoa ambaao una makabila mengi na wenye tamaduni tofauti. Wizara ya Maliasili na Utalii hajaweza kuwekeza kwenye fursa ya utalii wa tamaduni mbalimbali zinazopatikana katika Mkoa wa Mara. Niombi Waziri uweze kuangalia pia ni jinsi gani tunaweza kuwekeza kwenye tamaduni zinazotokana na

makabila mbalimbali badala ya kuangalia utalii wa wanyamapor peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 70 ya mbuga ya Serengeti iko Mkao wa Mara, lakini wananchi wa Mkao wa Mara wamekuwa wakiishi maisha ya kimaskini kama vile hii mbuga ya Serengeti haiko Mkao wa Mara. Ni asilimia 10 tu ya watu walioajiriwa Serengeti *National Park* wanatoka Mkao wa Mara. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anakuja kuhitimisha hotuba yako atuambie watu wa Serengeti na watu wa Mkao wa Mara ni sababu gani ni asilimia kumi tu ndiyo wameajiriwa katika Serengeti *National Park*, je, ni kwa sababu hatuna watu wenye uwezo ambao wanaweza kufanya kazi kwenye mbuga hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto ya wanyama wanaotoka mbuga ya Serengeti kuvamia vijiji vilivyo pembezoni ya mbuga ya Serengeti na kufanya uharibifu wa mali za wananchi ikiwemo mashamba, pia kuwadhuru wananchi na kusababisha vifo kwa baadhi ya wananchi ikiwa ni tembo, nyumbu na wanyama wengine wanaokula mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba kuna kifuta jasho na kifuta machozi, lakini kuna wananchi wa vijiji vinavyozunguka Wilaya ya Serengeti ikiwemo Pakinyigoti, Makundusi, Robanda ambao hawajalipwa toka mwaka 2005. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anakuja kuhitimisha hoja yake atuambie *compensation plan* ya hawa watu ikoje na watalipwa lini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hiyo kuna migogoro kati ya Askari wa Wanyamapor na wananchi wanaoishi pembezoni mwa mbuga ya Serengeti. Askari hao wamekuwa wakiwabambikia kesi wananchi wanaoingia kwenye hifadhi ama kwa kujua au kwa kutokujua kwa sababu hakuna mipaka inayoeleweka. Kinachonisikitisha ni kwamba wananchi hawa wamekuwa wakipelekwa Mahakama ya Bunda na siyo Serengeti wakati Mahakama ya Bunda ina uwezo sawa na Mahakama ya

Serengeti. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yako atuambie watu wa Serengeti ni kwa nini wanapelekwa Mahakama ya Bunda na siyo Mahakama ya Serengeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee *issue* ya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sannda.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza niende moja kwa moja kwenye ushauri, leo nitakuwa nafanya zoezi la ushauri tu kwa Wizara na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo kama linanishangaza kidogo, ninaposikiliza Wabunge wenzangu wote na ninapofuatilia hali halisi ya migogoro inayotokana na mwingiliano mkubwa kati ya maeneo ya hifadhi pamoja na maeneo ya makazi nashangaa sijaona kama jambo hili limewekewa uzito sana kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nilitegemea kwa kuwa hili ni tatizo kubwa sana lazima ungelizungumzia kwa kina sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu kila pori la akiba, kila eneo la hifadhi ni vurumai tu. Tumesikia madhara makubwa ya migogoro, tunesikia vifo, tunesikia wanyama wanadhirika ndiyo maana tunazungumzia habari ya kufanya mipango mizuri ya ardhi kwa ajili ya kuweza kutenga maeneo ya ufugaji, maeneo ya hifadhi na maeneo ya kilimo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona uzito unaostahili kwenye hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende mbele kidogo kwamba, tatizo hili limekuwa la muda mrefu sana, kila kwenye pori kelele ni hizo, miaka nenda, miaka rudi ni kero kubwa kweli. Hatuna budi tufike mahali sasa tuweze kupata

ufumbuzi wa kudumu kabisa wa migogoro hii baina ya maeneo ya hifadhi, mapori ya akiba, vijiji, maeneo ya wafugiaji na maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kitu kimoja, tufanye mpango mahsus wa kuwekeza kwenye elimu kwa mambo makubwa matatu. Elimu kwa maana ya mafunzo, hamasa na programu shirikishi. Kwanza kwa ajili ya kuimarisha mipaka, wakati wa kuimarishwa lazima tushirikishe wale wananchi vilevile. Tunapofanya wenyewe mwisho wa siku wananchi wanakuja kuona kwamba "aah, hawa walibadilisha mipaka" malalamiko mengi yamekuja maeneo ambayo wanasema mipaka ilikwishapimwa, zoezi la kuja kuimarisha na kuweka zile *beacon* limechukua muda mrefu. Serikali ilivyokuja kwa maana ya Wizara ilivyokuja walikwenda wenyewe, hawakushirikisha wale wananchi pale kiasi kwamba wananchi wanaona "aaah! hawa watu wametuvizia wakati hatupo wamekuja wameweka mipaka usiku" (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kuna tatizo au shida gani ya ku-*involve* wananchi wakati wa kwenda kuimarisha mipaka. Kwa nini tusitumie muda mwingi angalau kuwaunganisha na kuweza kufanya nao kazi pamoja ili kuepuka lawama hizi na migogoro huko mbele. Nisisitize sana wakati wa mazoezi ya kuimarisha mipaka, kwanza tusichukue muda mrefu, lakini wakati wa zoezi hili tushirikishe sana wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine katika mapato tunayoyapata kwenye hifadhi zetu. Tuwekeze kidogo kwenye elimu ya uhifadhi kwa wananchi. Wananchi nao waweze kuelewa kwa nini na wao wawe sehemu ya kulinda yale mazingira ambayo tumeamua kuyahifadhi, nao wanufaiki kwa namna moja au nyngine. Tukiwekeza kwenye elimu hiyo, vurumai itapungua, watu watazuia mifugo, wataacha shughuli za kibinadamu kwenda kwenye maeneo yaliyohifadhiwa itakuwa ni *win win situation*. Tumeweka kidogo na wao wanakaa kule wanajua kabisa kuna umuhimu, leo nimepata labda kisima cha maji pia, wakati

mwingine wamekuja watu wametupa mafunzo hapa kama wanakijiji, keshokutwa tumepata madawati, tumejengewa madarasa. Tujitoe kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu hapa mmoja alisema ukitaka kula ni lazima uliwe, lazima utoe hela ili uweze kupata manufaa. Naomba nisisitize sana kwenye elimu ya uhifadhi kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuwekeze kwenye elimu ya utii wa sheria bila shuruti kwa wananchi na kwa wale Askari wetu maana tumekuwa na kesi nyngi sana. Mara ya mwisho niliongea hapa kuhusiana na Wizara hii, kesi kubwa sana ya mauaji. Sasa tufanye utaratibu ambapo yule Askari anaji-*feel responsible* kumkamata mtu, amhoji vizuri, afuate taratibu mpaka yule mtu amtie kwenye mkono wa sheria, siyo anajichukulia sheria mkononi. Wananchi nao pia waweze kuelewa kwamba ninapokutana na labda wanyama wameingia huku kwetu sio naua tu au sio nafanyaje. Tuiti sheria bila shuruti, bila kuingia kule, bila ya kwenda kwenye hifadhi kufanya shughuli za kibinadamu, itatusaidia sana kupunguza hii migogoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la migogoro limekuwa ni kero kubwa ambayo bila ya kuiwekezea hivi hatutaweza kuimaliza kwa muda mfupi. Mheshimiwa Waziri, pia tufanye uwekezaji kwenye kutoa elimu ya ku *co-exist*. Wale watu wanaoshughulika na uhifadhi na wananchi waweze kuona umuhimu wa ku *co-exist* wao pamoja. Kila mmoja ni muhimu kwa mwenzio, siyo mmoja amuone, imefika wakati wanyama wanaonekana ni muhimu kuliko wanadamu, hatuwezi kwenda namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa ule mfano wa kijana aliyeuawa kwa ajili ya sukari guru, haiwezekani hata kama ameua mnyama gani, hebu tuone namna gani tunaweza tukaona kila mmoja kwa nafasi yake tunaweza tuka *co-exist*. Siku moja moja mwisho wa siku wakafikia wakaoana kati ya wahifadhi na wananchi kawaida wakawa wanakaa wanashirikiana kwa kila namna. Katika ufumbuzi ninaouuna

mkubwa wa hii migogoro, tuwekeze kwenye kutoa elimu katika nyanja aina hizo tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili nataka nizungumzie kwenye suala la utangazaji. Utangazaji wa vivutio vyetu, kwa kweli hatujawekeza vya kutosha. Wamezungumza Wabunge waliotangulia, huko tunaona wenzetu takwimu za watalii zinazidi lakini siyo bure, watu wame-*invest* kama kuna sera, kama kuna utaratibu wa kushirikiana na sekte binafsi kushirikiana na hizi wakala na taasisi mbalimbali tuweze kuongeza uwekezaji kwenye kutangaza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Waziri, ile michoro ya mapangoni ambayo iko kwenye historia sisi toka tuko wadogo tunaisoma, tunayo michoro zaidi ya 450. Wangapi wanajua hapa, wala haiko mbali, iko hapa Kondoa tu kwetu. Wangapi wanajua ile michoro, hatujai-*promote*, tumeiacha na ofisi ziko pale lakini hata rasilimali watu sijui kama inazingatiwa, kama watumishi wapo, yaani pako *dull* kwelikweli ni kana kwamba vivutio hivi havipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuwekeza, tunahitaji kujitoa ili tuweze kuvutia watalii wengi na tutaongeza kipato kupitia njia ya namna hii. Ni lazima *to-invest* ili wale watalii tunaotaka waje, watakuja kwa wingi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri napenda sana nizungumzie kuhusiana na uwekezaji hususan kwenye maeneo ambayo yapo, tunayajua kihistoria lakini tumeyaacha kama malikale zimelala, tumeandika kidogo sana kwenye hotuba yetu hapa. Inaonekana hata dhamira ya dhati ya *ku-promote* vivutio hivi ni kama haipo. Sasa huku kwenye kutenga fedha ndiyo kabisa, kuko kutupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa safari yetu tunayotaka kuboresha utalii, nafikiri kwa utaratibu huu tutakuwa tumekwama sana. Namwomba pale anapokuja kwenye majumuisho nategemea na naomba nisikie anatueleza nini kuhusiana na *investment* kwenye *promotion* ya vivutio vya utalii, malikale na mengineyo. Pia

atueleze vizuri mipango na programu zilizopo na uwekezaji ambao upo au anapanga kuuweka kwenye utatuzi wa migogoro hasa kwa njia hizi shirkishi. Kadri nilivyokuwa nimeelezea kwa maana ya kutoa elimu ya uhifadhi, kwa maana ya kutoa elimu ya kutii Sheria bila shuruti na kutokujichukulia sheria mkononi na pia kwa maana ya elimu ya *co-existence*, pamoja na programu shirkishi za kuwa-*engage* wananchi ili nao wajione kwamba ni sehemu ya uhifadhi na wasije kuwa wao ndiyo tatizo au changamoto zinazosababisha hii migogoro, badala yake wao wawe chanzo cha ufumbuzi na suluhisho katika kupata majibu ya migogoro hii ambayo imekuwa kero kubwa na inaleta madhara, inapoteza nguvukazi, watu wanakufa kila leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kondoa kuna mapori mawili, yote ni vurumal, karibu mara zote tunasikia huko watu wamekufa watano, mara amekufa mtu mmoja. Kila unapokuta pori la akiba au maeneo ya hifadhi ni vifo. Mheshimiwa Waziri tutavimaliza lini hivi, kweli kila siku tunazungumzia jambo moja tu la migogoro baina ya maeneo ya hifadhi? Tumeshindwa kabisa kupata ufumbuzi wa kudumu wa mambo haya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya kweli ipo katika hili? Mheshimiwa Waziri na...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wa siku ya leo wote wamekwisha. Nawashukuru sana kwa michango mizuri.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili

muhimu, Wabunge wanachama na washabiki wa Simba mnaarifiwa kuwasiliana na Mheshimiwa Rashid Shangazi mratibu wa tiketi za kuingia uwanjani fainali za *FA Cup* mwisho ni kesho.

Kutokana na ugeni huo mzito wa Kitaifa, Waheshimiwa Wabunge wanachama na wapenzi wa Simba *Sports Club* wanaandaa utaratibu wa kuipokea timu yao Simba *Sports Club* hapa Mjini Dodoma inayokuja kucheza fainali ya kombe la *FA* dhidi ya Mbao *FC* siku ya Jumamosi, tarehe 27. (*Makofi*)

Kutokana na ugeni huo mzito wa Kitaifa, Waheshimiwa Wabunge wanachama na wapenzi wa Simba *Sports Club* wanaombwa kuwasiliana na Kamati ya Uratibu wa mapokezi inayoundwa na Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mheshimiwa Rashid A. Shangazi, Mheshimiwa Godfrey W. Mgimwa, Mheshimiwa Cosato D. Chumi. (*Makofi*)

Tangazo hili pia linamhusu mdau mkubwa sana wa Simba Mheshimiwa Jaji Mihayo, Mwenyekiti wa *7TB* ambaye najua uko ndani umekaa upande wa kulia. (*Kicheko*)

Kawaida, Kibunge, likishapita jambo hakuna timu nyingine tena inahitaji kutangazwa humu. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpamgilio*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

(*Saa 1.45 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 24 Mei, 2017 Saa Tatuu Asubuhi*)